# BARAZA LA WAWAKILISHI

**HOTUBA YA KAMATI YA PAC KUHUSU RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

---

## ILIYOWASILISHWA
## KATIKA MKUTANO WA KUMI NA MBILI WA BARAZA LA WAWAKILISHI - ZANZIBAR

**OKTOBA, 2023**

## YALIYOMO

RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI ....................................5

1. UTANGULIZI ....................................5

1.1 ....................WAJUMBE NA SEKRETARIETI YA KAMATI YA PAC ....................................7

1.1.1 Waheshimiwa Wajumbe: ....................................7

1.1.2 Sekretarieti: ....................................7

1.1.3 Mgongano wa Maslahi: ....................................8

1.2 UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI ....................................8

UCHUNGUZI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2020/2021 ....................................10

2. MAUDHUI: ....................................10

MRADI WA KUENDELEZA ELIMU MBADALA AWAMU YA II (ALSD II) ....................................10

MRADI WA UJENZI NA UNUNUZI WA VIFAA KWA AJILI YA SKULI ZA SEKONDARI ZANZIBAR ....................................12

MRADI WA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KWA ELIMU (GPE II) ....................................13

3.0 ....................MRADI WA UIMARISHAJI WA ELIMU YA SEKONDARI ZANZIBAR (ZISP) ....................................20

MPANGO WA LISHE MASHULENI (HGSFP) ....................................24

MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA SEKTA ZA FEDHA NA MIPANGO MIJI ....................................26

MRADI WA MABORESHO YA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA ....................................26

(PFMRP) ....................................26

WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI ....................................33

MRADI WA KUSAIDIA SEKTA YA UCHUKUZI (TSSP) ....................................33

MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA SEKTA YA UCHUMI WA BULUU, KILIMO NA MAMBO YA KALE ....................................39

MRADI WA MAMLAKA YA UVUVI WA BAHARI KUU ZANZIBAR (SWIOFish 1 - GEF GRANT) ....................................39

MRADI WA MAMLAKA YA UVUVI WA BAHARI KUU ZANZIBAR (SWIOFish 1 - IDA) ....43

5.4 MRADI WA UHIFADHI WA ENEO LA KIHISTORIA LA MKAMANDUME PEMBA ....46

MRADI WA UJENZI WA JENGO LA MAMA NA MTOTO HOSPITALI YA CHAKE CHAKE - PEMBA ....................................61

UCHUNGUZI WA HOJA ZA MDHIBITI ZA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI MAALUM WA UHAKIKI WA MADENI YA WIZARA NA TAASISI ZA

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI 2021 ........................................................................90

4.7.1 WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA..................................90

4.7.2 IDARA YA MAKUMBUSHO NA MAMBO YA KALE ..........................................97

4.7.3 TAASISI YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA......................................98

KAMISHENI YA UTALII ........................................................................................99

4.7.5 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI ..............................................100

4.7.6 BARAZA LA MITIHANI ZANZIBAR ................................................................102

4.7.7 TAASISI YA ELIMU YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA KARUME.........................103

4.7.8 WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA...................................................................................................104

4.7.9 WAKALA WA SERIKALI MTANDAO (e-Government of Zanzibar) .....................104

4.7.10 SHIRIKA LA HUDUMA ZA MAKTABA ZANZIBAR ........................................106

4.7.11 WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR........................107

4.7.12 HOSPITALI YA MNAZIMMOJA ....................................................................108

4.7.13 BARAZA LA MJI KASKAZINI “B” ................................................................109

4.7.14 BARAZA LA MJI MKOANI PEMBA..............................................................111

Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC............................................112

4.7.15 OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR ..........................................................................................................112

4.7.16 WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI ..................................113

4.7.17 AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI .........................................117

4.7.18 WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI.....................................118

4.7.19 OFISI YA MKOA WA MJINI MAGHARIBI....................................................118

4.7.20 CHUO CHA MAFUNZO ..............................................................................120

4.7.22 KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA......................................................121

4.7.23 WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO. .....................121

4.7.24 WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO..........................122

UCHUNGUZI KUHUSU RIPOTI YA UKAGUZI WA FEDHA ZA MUUNGANO .............124

WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO ................................130

UCHUNGUZI WA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA YA BOHARI KUU YA DAWA KWA MWAKA 2020/2021 ..........................................................................147

UCHUNGUZI WA UKAGUZI WA RIPOTI YA MFUMO WA MISHAHARA YA SERIKALI (GOVERNMENT PAYROLL SYSTEM) KWA MWAKA 2020/2021..............................178

UCHUNGUZI WA UKAGUZI WA RIPOTI YA MFUMO WA UVIKO 19 (WIZARA YA AFYA) KWA MWAKA 2020/2021 ........................................................................190

UCHUNGUZI KUHUSU UKAGUZI WA RIPOTI YA TEHAMA KWA WAKALA WA SERIKALI MTANDAO (EGAZ) KWA MWAKA 2020/2021 ........................................264

MFUMO WA ZANMALIPO WA ZAMANI.................................................................264

MFUMO ZANMALIPO MPYA ........................................................................275

12.8.3 DOSARI KWENYE UDHIBITI WA JUMLA WA UENDESHAJI WA TEHAMA ....285

UKAGUZI MAALUM WA DAWA NA VIFAA TIBA KWA WIZARA YA AFYA USTAWI WA JAMII, WAZEE, JINSIA NA WATOTO ......................................................299

1.5.2 HADIDU REJEA NAMBA 1 .......................................................................299

1.5.3 HADIDU REJEA NAMBA 2 .......................................................................304

HADIDU REJEA NAMBA 3:..........................................................................310

1.5.8 HADIDU REJEA NAMBA 5 .......................................................................334

1.5.9 HADIDU REJEA NAMBA 6 .......................................................................338

1.5.10 HADIDU REJEA NAMBA 7 .....................................................................340

HITIMISHO ...............................................................................................345

**RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) YA BARAZA LA WAWAKILISHI - ZANZIBAR, KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

## 1. UTANGULIZI

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa chini ya Kanuni ya 107(1) ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020 ambapo pamoja na mambo mengine inajukumu kuu la kufuatilia na kuchunguza Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mara tu baada ya kuwasilishwa kwa Spika. Kiujumla, Kamati hufuatilia Ripoti hiyo kwa niaba ya Baraza na hatimae kuwasilisha Ripoti yake hususan katika mwezi wa Febuari au muda mwengine wowote ambao Kamati ya Uongozi ya Baraza itaamua kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 109(15) ya Baraza.

Katika kutekeleza matakwa ya Kanuni za Baraza, Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati ya PAC imefanikiwa kufanya uchunguzi wa vitabu vitatu vya Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufuatia uwasilishwaji wake uliofanywa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman mbele ya Baraza la Tisa, 2023.

Katika uchunguzi wa Vitabu vilivyowasilishwa, jumla ya Ripoti Tatu zilifuatiliwa na kuchunguzwa. Ripoti zenyewe ni:-

1. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi Maalum kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 iliyojumuisha Ripoti zifuatazo:-

    a) Ripoti ya Ukaguzi Maalum kuhusu mapato ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kwa Taasisi za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021;
    b) Ripoti ya Ukaguzi Maalum kuhusiana na Dawa na Vifaa Tiba kwa Wizara ya Afya;
    c) Ripoti ya Ukaguzi Maalum kuhusu Uhakiki wa Madeni ya Wizara na Taasisi za Serikali;

d) Ripoti ya Ukaguzi Maalum kuhusu Usimamizi wa Fedha za Muungano kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoka hazina; na
e) Ripoti ya Ukaguzi Maalum kuhusu Mashamba ya Mikarafuu, Ekari na Vitalu vya Miche ya Mikarafuu - Pemba.

2. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mifumo ya Tehema kwa mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 iliyojumuisha Ripoti zifuatazo:-

a) Ripoti ya Ukaguzi wa Mfumo kuhusu Mishahara ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021;
b) Ripoti ya Ukaguzi wa Mfumo kuhusu Kusimamia Daftari la Mali za Kudumu kwa mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2012; na
c) Ripoti ya Ukaguzi wa Mfumo kuhusu Uviko 19 kwa mwaka wa Fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2021.

3. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 iliyojumuisha Ripoti zifuatazo:-

a) Ripoti ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo wa Kusaidi Sekta ya Uchukuzi (TSSP) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021;
b) Ripoti ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kuhusu Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Zanzibar (SWIOFish GEF) Grant kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021;
c) Ripoti ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kuhusu Miradi ya Maendeleo Sekta ya Elimu kwa mwaka wa fedha unaishia tarehe 30 Juni, 2021;
d) Ripoti ya Ukaguzi wa Miradi ya Mendeleo kuhusu Sekta ya Fedha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021;

e) Ripoti ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kuhusu Ujenzi wa Mama na Mtoto kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021;

f) Ripoti ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kuhusu Mahanga kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 juni, 2021; na

g) Ripoti ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kuhusu Uvunaji wa Maliasili zisizorejesheka kwa mwaka fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021.

## 1.1 WAJUMBE NA SEKRETARIETI YA KAMATI YA PAC

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati hii imeundwa na Wajumbe Sita (5) kama ifuatavyo:

### 1.1.1 Waheshimiwa Wajumbe:

| Na. | Jina Kamili | | Cheo/Wadhifa |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Juma Ali Khatib | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed | - | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | - | Mjumbe |

Aidha, Katika utekelezaji wa kazi zake, Kamati imesaidiwa na Sekretarieti iliyoundwa na Maofisa Watatu (3) ambao ni Makatibu wa Kamati na Maofisa Saba (7) wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama wafuataao:

### 1.1.2 Sekretarieti:

| Na. | Jina Kamili | | Cheo/Wadhifa |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Said Khamis Ramadhan | - | Katibu |
| 2. | Ndg. Maryam Haji Ali | - | Katibu |
| 3. | Ndg. Adam Moulid Simai | - | Katibu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4. | Ndg. Nassor Mdachi Mwinyi | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti (Unguja) |
| 5. | Ndg. Robert Mwairo | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti (Mifumo) |
| 6. | Ndg. Juma Mohammed Juma | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti (Mifumo) |
| 7. | Ndg. Mussa Kadir Mussa | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti (Mifumo) |
| 8. | Ndg. Ramadhan Iddi Hassan | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti (Madeni) |
| 9. | Ndg. Maryam Ali Khamis | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti (Mifumo) |
| 10. | Ndg. Moh'd Suleiman Amour | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti (Pemba) |

### 1.1.3 Mgongano wa Maslahi:

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya PAC ilifuata matakwa ya Kanuni na Sheria za nchi zilizoelekeza uwekaji wazi Mgongano wa Maslahi kwa Wajumbe dhidi ya jambo linalojadiliwa ili kuepusha kujitokeza kwa upendeeo hususan wakati wa kufanya maamuzi na kusababisha uonevu au ubatilishaji wa haki. Kwa bahati nzuri, Katika majadiliano ambayo Kamati imeyafanya, hakujajitokeza aina yoyote ya mgongano wa maslahi.

## 1.2 UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya PAC imezingatia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo hutumika kuwa ni Hadudi Rejea, matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Sheria ya Kinga, Uwezo na Fursa za Wajumbe pamoja na Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020).

Kadhalika, Kamati kwa mara kadhaa ilikuwa ikifanya rejea ya Sheria Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Nambari 11 ya mwaka 2016,

Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nambari 12 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria nyengine za Zanzibar.

Sambamba na hilo, Kamati ilikutana na Watendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali zilizohusika na hoja zilizoibuliwa katika Ripoti ya Mdhibiti kwa kufanya mahojiano, kupitia vielelezo na hatimae kufanya ziara katika maeneo mbali mbali ili

Kushuhudia uhalisia wa majibu yaliyotolewa na Wizara au Taasisi husika. Aidha, Kamati kwa kuzingatia haja iliyokuwepo, ilifanya ziara katika maeneo husika na baadae ilifanya mijadala ya hoja mbali mbali.

Shughuli hizi zilifanyika ndani ya mizunguko mitatu kama ifuatavyo:

1. **Mzunguko wa Kwanza:** Ulianzia tarehe 27/03/2023 hadi 31/03/2023 - Pemba na kumalizia tarehe 3/4/2023 hadi 12/4/2023 - Unguja
2. **Mzunguko wa Pili:** Ulianzia tarehe 17/07/2023 hadi 21/07/2023 - Pemba na kumalizia tarehe 24/7/2023 hadi 02/08/2023.
3. **Mzunguko wa Tatu:** Ulianzia tarehe 7/08/2023 hadi tarehe 11/08/2023 - Pemba na kumalizia tarehe 21/08/2023 hadi tarehe 01/9/2023 - Unguja

**UCHUNGUZI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2020/2021**

**2. MAUDHUI:**

**MRADI WA KUENDELEZA ELIMU MBADALA AWAMU YA II (ALSD II)**

Mradi wa kuendeleza elimu mbadala awamu ya pili (Alternative Learning and Skills Development II - ALSD II) ni mradi uliofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ambao umesainiwa tarehe 12 Septemba, 2011 na kuanza utekelezaji wake rasmi tarehe 23 Machi, 2012 kwa Unguja na Pemba na ulitarajiwa kumalizaka tarehe 31 Disemba, 2020.

Lengo kuu la mradi huu ni kuongeza ajira kwa vijana na kuboresha upatikanaji wa elimu za amali ikiwemo ufundi na biashara unaohitajika katika soko la ajira. Mradi huu unatekelezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (MoEVT) Zanzibar kupitia kitengo cha uratibu wa Mradi (PCU) kwa ajili ya usimamizi na kuratibu shughuli za kila siku za mradi.

**Hoja Nambari: 3.1.1.2 Kuwepo kwa ongezeko la fedha za mradi shilingi 5,957,009,228**

Mradi wa ALSD II kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 uliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 5,423,960,019 ambapo imebainika kuwa kiasi cha shilingi 11,380,969,247 ziliingizwa na kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo na kupelekea kuwepo kwa ongezeko la shilingi 5,957,009,228 sawa na asilimia 110 ya fedha zilizoidhinishwa. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi yasiyoridhisha ya fedha pamoja na rasilimali za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mradi kuongeza umakini katika kufanya makisio ya matumizi ya fedha ili iendane na hali halisi ya gharama za Utekelezaji wa mradi. Mchanganuo wa ongezeko la fedha za mradi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 2: Kuwepo kwa ongezeko la fedha za mradi**

| Maelezo | Kiasi cha fedha kilicho kadiriwa (Tshs.) | Kiasi cha fedha kilichotumika (Tshs.) | Tofauti (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| Huduma ya Mshauri Elekezi kwa KIST, ZITOD na VTA | 38,705,920 | 151,194,500 | (112,488,580) |
| Ujenzi wa Skuli, Makunduchi Unguja | 1,866,414,670 | 3,345,835,079.9 | (1,479,420,409.91) |
| Ujenzi wa Daya Pemba | 1,798,895,074 | 4,737,701,507 | (2,938,806,433) |
| Ujenzi wa jengo la KIST | 204,556,558 | 212,471,344.92 | (7,914,786.92) |
| Ugavi wa vifaa kwa ajili ya Daya na Makunduchi | - | 89,448,848 | (89,448,848) |
| Vifaa vya ZITOD | 166,174,217 | 269,862,410.52 | (103,688,193.52) |
| Replenishment | - | 488,842,023 | (488,842,023) |
| Mchango wa Serikali | 1,349,213,580 | 2,085,613,533.43 | (736,399,953.43) |
| **Jumla** | **5,423,960,019** | **11,380,969,247** | **(5,957,009,228)** |

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara inathibitisha kiasi cha fedha zote zilizolipwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ni kwa mujibu wa taratibu na hakuna fedha ya ziada ambayo imelipwa. Kwani kulikuwa na bakaa ya fedha za bajeti ya nyuma kwa mwaka wa fedha 2019 - 2020 ambazo zinaendelea kutumika kwa mwaka mwengine unaofuatia mpaka mradi kukamilika.

Na kwa kipindi cha mwaka 2020/2021, Mradi wa ALSD II ulikuwa unamalizika na kufungwa Disemba 2020. Hivyo katika kipindi hicho kuna shughuli ambazo zilikwisha kamilika katika mwaka 2019/2020 lakini malipo yake yalikuwa bado hayajafanyika tukisubiri malipo hayo wahisani wafanyie kazi kwani malipo hayo ni "Direct payment". Vilevile kulikuwa na madeni ya mikataba ambayo ililipwa kupitia fedha za Serikali, fedha zote hizo ambazo zililipwa zilikuwa "Committed" na ilikuwa ndio wakati pekee wakulipa kabla Mradi haujafungwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba kuwepo kwa ongezeko la shilingi 5,957,009,228 limetokana na bakaa ya fedha za nyuma kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambazo ziliendelea kutumika kwa mwaka mwengine kama majibu yanavyojieleza. Hali hii inatokana na kuwa Wahisani au Wafadhili wa Mradi kutokuingiza fedha za mradi kwa wakati na kupelekea kuweko na bakaa za fedha. Hata hiyo kamati imekubaliana na majibu hoja ya Wizara.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri kuwe na utaratibu na miongozo maalum kwa wafadhili wa miradi katika utoaji wa fedha za miradi ili kuepusha fedha za miradi kutotumika kwa wakati.

**MRADI WA UJENZI NA UNUNUZI WA VIFAA KWA AJILI YA SKULI ZA SEKONDARI ZANZIBAR**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) Zanzibar imeingia mkataba na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi Barani Afrika (BADEA) kwa ajili ya kufanyia marekebisho mfumo wake wa elimu tarehe 1 Aprili, 2020 na unatarajiwa kumalizika tarehe 31 Machi, 2023. Mradi wa Ujenzi na Ununuzi wa Vifaa kwa Ajili ya Skuli za Sekondari Zanzibar (The Contruction And Equiping of Secondary Schools Projects) umetekelezwa kwa ajili ya ujenzi wa skuli za sekondari na usambazaji wa samani za Skuli na Mabasi ili kukidhi mahitaji ya elimu kwa umma. Mradi huo unajumuisha kazi za ujenzi wa skuli tatu katika maeneo ya Mfenesini Mjini Magharibi, Gamba kaskazini Unguja na kijiji cha Kifundi kisiwani Pemba, pamoja na ununuzi wa vifaa.

Lengo kuu la mradi huo ni kuifanya Zanzibar iweze kufikia mipango ya maendeleo endelevu kupitia katika nyanja ya elimu, ikiwa ni pamoja na utoaji wa fursa za elimu kwa wanafunzi wa maeneo yanayokabiliwa na upungufu wa Skuli za Sekondari.

**Hoja nambari 3.3.1.1: Ucheleweshaji wa kuidhinishwa kwa kibali cha Mshauri wa Michoro na Usanifu wa majengo**

Katika ukaguzi uliyofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebaini kuwepo wa ucheleweshaji wa ujenzi wa skuli tatu zilizotarajiwa kujengwa Mfenesini na Gamba kwa Unguja na Kifundi kisiwani Pemba chini ya usimamizi wa mradi wa BADEA II ambapo ujenzi huo ulitarajiwa kuanza mwezi wa Oktoba, 2021. Hali hiyo ilitokana na kucheweshwa kwa uhakiki wa kibali cha mshauri wa Michoro na Usanifu wa majengo jambo ambalo limepelekea kutotekelezeka kwa ujenzi wa skuli hizo kwa wakati.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu kuwa makini katika kusimamia vyema utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa wakati na kuelewa kwamba ujenzi ndio kiini chamkopo.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara ya Elimu na Mafunzo Amali inakiri mradi kuchelewa kuanza na sio kibali cha Mshauri Elekezi. Hii inatokana na kusababishwa Mfadhili (BADEA) kwa kuchelewa kutoa ruhusa ya kuendelea na Mradi (No Objection). Ripoti ya mwanzo ya kumtafuta Mshauri mbunifu wa michoro na kusimamia majengo ya skuli 3 ilifanyika tarehe 14/7/2020, ambayo ilikuwa na wabunifu 30 na kupatikana wabunifu wanane 8. Baada ya mapitio ikarudi na wabunifu 11. Na. ripoti ya pili ilikuwa 20/01/2021 na baada ya mapendekezo ya mfadhili kampuni 10 ndizo zilzofunguliwa kati ya 11. Makubaliano (Negotiation) ya Mbunifu yalifanyika 23/06/2021 na saini ya mkataba ni tarehe 30/08/2021. Michoro iliwasilishwa 2/12/2021.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa katika hoja hii kilicho sahihi ni ucheleweshaji wa ruhusa ya kuendelea na mradi ndio imechelewa hali hii imetoka na mfadhili wa BADEA kuchelewa kutoa ruhusa ya kuendelea na mradi na sio Ucheleweshaji wa kuidhinishwa kwa kibali cha Mshauri wa Michoro na Usanifu wa majengo kama mkaguzi alivo andika hoja hii.

Hata hivyo, Wizara ya Elimu imekiri kuchelewa kwa mradi kama majibu yanavyojieleza, kamati imeelezwa tatizo hili la kuchelewa kwa kukamilika kwa miradi litaendelea kwa sababu masharti ya wafadhili wa miradi BADEA huchelewa kutoa idhini ya kuendelea kwa mradi, kwani Wizara ya Elimu hawawezi kuendelea mpaka wapate document ya 'no option' ambayo inatoka kwa wafadhili BADEA wa Mradi ndio waendelee na utekelezaji wa mradi. Hata hivyo kamati baada ya kupata maelezo imeridhika na majibu.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri wafadhili wa Miradi ya Maendeleo kufuata taratibu na miongozo iliyopo katika mikataba hususan kipengele cha kupata ruhusa ya kuendelea na mradi ili kuepusha miradi kutokamilika kwa wakati.

**MRADI WA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KWA ELIMU (GPE II)**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imekuwa ikitekeleza Mpango wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu (Global Partnership for Education - GPE II) unaofadhiliwa na Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu na unasimamiwa na Ubalozi wa Sweden kama Wakala wa Ruzuku kuanzia mwaka 2014 hadi mwaka 2016, kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa elimu

kwa usawa na kuboresha umuhimu na ubora wa elimu katika sekta nzima yaelimu.

Utekelezaji wa Mradi wa awamu ya pili (GPE II) ulianza Julai, 2018 kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa elimu katika mfumo mzima kwa kuendeleza programu ya Elimu Jumuishi na kutoa elimu bora kwa wanafunzi wote wa Zanzibar, Mradi huu unatarajiwa kufanya kazi kwa muda wa miaka minne kuanzia Aprili, 2018 hadi tarehe 30 Juni, 2022.

**Hoja Nambari 3.3.3.1: Kukosekana kwa Ufanisi katika matumizi ya fedha**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2021 ukaguzi umebaini mradi ulikuwa na bakaa ya jumla ya USD 4,536.70 sawa na jumla ya shilingi 10,411,727 ambapo mradi huo ulibainika katika kipindi cha mwezi Agosti, 2020 ulipokea jumla ya USD. 2,000,000 sawa na shilingi 4,629,965,298 kutoka Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (SIDA).

Ukaguzi umebaini kuwa mradi haukuwa na ufanisi mzuri wa matumizi ya asilimia 100 ukilinganisha na shughuli zilizopangwa. Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu kufanya matumizi katika shughuli za mradi zilizopangwa kulingana na bajeti iliyoidhinishwa

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Shughuli nyingi ambazo zilipangwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 zilitekelezwa kwa baakaa iliobakia ni kutokana na kutokea kwa ugonjwa wa COVID 19 ambapo ilipelekea ugumu katika utekelezaji wake ndipo ikapelekea bakaa ya Tzs. 10,411,727.

Kwa sasa shughuli za bakaa ya fedha hizo zimekamilika kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Wizara imeweza kutumia fedha kikamilifu na bakaa iliyobakia kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikuwa ni fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa kupitia (review) Mitaala na matayarisho ya vitabu kwa ajili ya mitaala mipya.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC baada ya kupata maelezo ya kina imebaini kwamba sababu kubwa ya kutokuwa kwa ufanisi wa miradi ni kutoka na Ungonjwa wa COVID 19 ambao umepelekea shughuli nyingi za mradi zilizohusiana na mikusanyiko ya watu kutokutekelezeka kwa wakati uliopangwa kama ilivyoelezwa katika majibu ya Wizara. Kamati imeridhika na majibu ya hoja.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inapendekeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwa makini katika kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha za umma.

### Hoja nambari 3.3.3.2: Utekelezaji wa Mradi kinyume na bajetiiliyopangwa

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi umebaini utekelezaji wa shughuli za mradi haukuwa wenye kuridhisha ambapo jumla ya shilingi 5,200,680,444.97 zilitumika sawa na asilimia 56 ya matumizi ukilinganishwa na fedha iliyotengwa ya shilingi 9,231,818,700 kwa utekelezaji wa shughuli za mradi katika kipindi cha mwaka husika ambapo kunaweza kusababisha kutokufikiwa kwa malengo ya utekelezaji wa mradi kwa kulingana na wakati uliopangwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufanya usimamaizi wakina ili shughuli zote za mradi zilizokusudiwa zinatekelezwa kulingana na mpango wa bajeti ya mradi na kwamba fedha zote za mradi zilizopangwa zinatumika kama ilivyokususdiwa. Hali halisi ya utekelezaji wa mradi ni kama inavyoonekana hapo chini:-

**Jadweli Nambari 3: Utekelezaji wa Mradi kinyume na bajeti iliyopangwa**

| Na | Vipengele | Kiasi cha fedhakilicho kadiriwa (Tshs) | Kiasi cha fedha kilichotumika (Tshs) | Tofauti ya fedha (Tshs) | Tofauti ya asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Elimu ya awali na Msingi | 6,696,983,000 | 4,122,160,027 | 2,574,822,973 | 61.5 |
| 2. | Elimu Jumuishi | 1,900,291,700 | 782,495,212 | 1,117,796,488 | 41 |
| 3. | Usimam izi na Utawala | 634,544,000 | 296,025,206 | 388,518,794 | 46.6 |
| | **Jumla** | **9,231,818,700** | **5,200,680,445** | **4,081,138,255** | 56 |

### Majibu ya uongozi wa Wizara

Kiujumla katika kipindi cha mwaka kwa mwaka wa fedha 2020/2021 shughuli zilitekelezwa kwa mujibu wa fedha zilizopatikana kutoka kwa muhisani. Kutokana na changamoto zilizokuwepo kupitia Uviko19 uliathiri upatikanaji wa fedha za kuendeleza mradi huo kwani Uviko uliweza kuathiri uchumi wa dunia. Kwa hivyo, fedha iliyokadiriwa siyo iliyopatikana na kupelekea kuwepo kwa tofauti baina ya makisio na matumizi halisi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa kweli bajeti iliyopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi ya shilingi 9,231,818,700 haikutumika kama ilivyokisiwa,hali hii imetokana na kujitokeza kwa maradhi ya Uviko 19 na kupekelea shughuli nyingi za miradi kutokufanyika kwa wakati.kutokana na changamoto ya maradhi kamati imeridhika na majibu ya hoja

**Hoja nambari 3.3.3.3: Kutokuthibitika kwa matumizi yaliyobainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka ya shilingi 437,161,495**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 437,161,495 zilitumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali za mradi lakini ukaguzi haukuweza kuthibitisha matumizi yaliyoripotiwa katika taarifa ya fedha ya mwaka. Kufanya hivyo kunapelekea uwepo wa viashiria vya upotevu wa fedha na matumizi mabaya ya rasilimali za Umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuzingatia sheria, miongozo na kanuni zinazoongoza taratibu katika kufanya miamala ya fedha ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Fedha na Usimamizi na Rasilimali za Umma ya mwaka2016.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Baada ya kuidhinishwa kwa mpango kazi wa Mradi (Work Plan) baadhi ya shughuli hutekelezwa na Wakala wa Sida (Grant agent). Fedha za shughuli zinazowahusu Wizara huingizwa moja kwa moja kwenye Akaunti kwa matumizi ya utekelezaji wa shughuli hizo na nyaraka za utekelezaji wa shughuli huhifadhiwa katika Ofisi zao. Hata hivyo, uongozi umepokea ushauri kutoka kwa wakaguzi na tunaufatilia kupata nyaraka za ufafanuzi wa matumizi kwa ajili ya kumbukumbu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Baada ya kamati kupata maelezo yanayohusiana na hoja hii, Kamati imebaini kuwa fedha huingizwa moja kwa moja kwenye akaunti ya Wakala wa Sida na matumizi yote hufanyika Sida jambo ambalo limepelekea Wizara ya Elimu kukosa vielelezo na matumizi ya fedha hayo kwa kutofuatilia vielelezo hivyo.

Hata hivyo Kamati ilipatiwa vielelezo hivyo vikiwemo barua ya matumizi ya shilingi 52,755,000 kwa ajili ya kufanya mikutano ya kuwasilisha na kuimarisha mihutasari ya darasa la I - VII baada ya Wizara kuchukua juhudi za kufuatilia vielezo ili kupata uhalali wa matumizi ya fedha hizo na kamati imepatiwa na kudhipitisha uhalali wa matumizi na imeridhika na majibu.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kwamba wanafuatilia vielelezo vyote vya matumizi ya fedha inayoingia kwenye Wakala wa Sida, kwa vile Wizara ndio wahusika wa Mradi ili kuepusha kujitokeza kwa changamoto wakati wa ukaguzi hususan pale vielelezo vinapohitajika kwa ukaguzi.

**Hoja nambari 3.3.3.4: Kutotekelezwa kwa shughuli za Mradi zilizopangwa shilingi 267,372,900**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi ulipitia taarifa ya mpango mwaka wa 2020/2021 ya mradi wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu (GPE II) na kubaini baadhi ya shughuli za mradi zilizopangwa kwa mwaka husika hazikutekelezwa kwa mujibu wa bajeti ambapo kunaweza kuathiri mabadiliko ya bajeti katika bidhaa na bei za huduma pamoja na shughuli za mradi zilizopangwa kutokufanyika kwa wakati.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kwamba shughuli zote za mradi zinatekelezwa kwa wakati kwa mujibu wa kiasi cha fedha kilichokadiriwa. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 4: Kutotekelezwa kwa Shughuli za Mradi zilizopangwa**

| Na | Shughuli iliyopangwa kufanywa kwa mujibu wa Mpango kazi wa Mradi | Kiasi cha fedha kilichokadiriwa (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Warsha katika kila wilaya ili kushauriana na wadau kuhusu mfumo na mwongozo wa ECE | 29,346,000 |
| 2. | Siku 3 za mafunzo ya kazini kwa ADES, ARASS ikijumuisha mtaalamu wa PPE, washauri wa masomo, walimu wakuu na mkaguzi wa Mpango wa Maendeleo ya Kitaaluma. | 106,570,000 |
| 3. | Majaribio ya program ya Uongozi katika skuli kumi 10 | 750,000 |
| 4. | Kuchapisha Nakala 1600 za Mafunzo ya Usimamizi yaliyoratibiwa | 8,000,000 |
| 5. | Machapisho ya watu wenye mahitaji maalum (Printing the inclusive) | 27,091,000 |
| 6. | Mshauri kukagua na kufuata ufanisi wa mafunzo | 95,615,900 |
| **Jumla** | | **267,372,900** |

**Majibu ya uongozi ya Wizara**

Kwa kipindi cha utekelezaji wa bajeti ya Tsh. 267,372,900 kwa zote zilizoelezwa katika jadweli nambari 4, hazikufanyika kwa sababu zifuatazo:-

- Athari ya uwepo wa maradhi ya Uviko 19. Ambapo kulipelekea kusimamishwa kwa utoaji wa mafunzo kwa washiriki, ilikuepusha mkusanyiko wa watu.
- Machapisho hayakuweza kutolewa wala kutafuta mshauri wa kukaguwa mafunzo hayo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa kweli kulikuwa na baadhi ya shughuli za mradi wa ushirikiano wa Kimataifa (GPE 11) hazikufanyika kutokana na mripuko wa Maradhi ya Uviko 19 lakini kamati imebaini fedha zilikuwepo za mradi.

Kamati ilihoji kuhusiana na fedha shilingi 267,372,900 na kuelezwa kuwa zilitumika baada ya maradhi ya Uviko kupungua na shughuli zilifanyika kama zilivyopangwa katika utekelezaji na kupata fusra ya kukagua vielelezo. Kamati imeridhika na majibu.

**Hoja nambari 3.3.3.5: Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 141,136,290**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 141,136,290 zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ushirikiano wa kimataifa lakini vielelezo vya matumuzi hayo havikupatikana kwa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo husika.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo matumizi yasiyoridhishaya fedha za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Kifungu Nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

UkaguziunashauriuongoziwaWizarayaElimunaMafunzoyaAmalikuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika yanawekewa vielelezo na kuwasilishwa kwa ajili yaukaguzi.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kiasi cha shilingi 141,136,290 ni miongoni mwa fedha 437,161,495 Baada ya kuidhishwa kwa mpango kazi wa Mradi (Work Plan) baadhi ya shughuli hutekelezwa na Wakala wa Sida (Grant agent). Fedha za shughuli zinazowahusu wao huingizwa moja moja kwenye Akaunti kwa matumizi ya

utekelezaji wa shughuli hizo na hati za utekelzaji wa shughuli huhifadhiwa katiak ofisi zao. Hata hivyo uongozi umepokea ushauri kutoka kwa wakaguzi na tunafatilia kupata nyaraka za ufafanuzi wa matumizi kwa ajili ya kumbukumbu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa kulikuwa na kutokufahamiana baina ya Wizara ya Elimu na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwani kamati imebaini fedha ya shilingi 141,136,290 ni miongoni mwa fedha ya 437,161,495 kama majibu yanavojielezo ya Wizara.

Pia, Kamati imebaini fedha hungizwa kwenye akaunti ya Wakala wa Sida na kufanya matumizi yote ya mradi, koso lililofanyika kwa upande wa Wizara ya Elimu kutokufuatilia vilelezo vya matumizi ya fedha hizo ili kudhibitisha uhalali wa matumizi ya fedha hizo. Kamati ilikagua vielelezo hivyo na kuridhika navyo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ya inaishauri Wizara ya Elimu kuhakikisha kuwa fedha inayoingia kwenye akaunti ya Wakala wa Sida inafuatilia kwa makini ili kujua uhalali wa matumizi yanoyofanyika ikiwemo kupata vielelezo vyote vinavohitaji na kuepusha changamoto zisijitokeze wakati wa ukaguzi.

**Hoja nambari 3.3.3.6: Kutotumika kwa fedha za mradi kwa wakati uliopangwa shilingi 362,246,648.52**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa bakaa ya dola za kimarekani 156,410 mwishoni mwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambazo ni sawa na shilingi 362,246,648.52 zilizopaswa kutumika kwa ajili ya shughuli za utekelezaji wa mradi. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuchelewa kumalizika kwa mradi kwa wakati ambapo kunaweza kuathiri maendeleo ya mradi huo kutokana na uwezekano wa kupanda kwa bei za bidhaa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kwamba mpango kazi wa mradi unatekelezwa kulingana na bajeti ili kufikia lengo lililokusudiwa.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kwa kipindi cha utekelezaji wa bajeti ya Tsh. 362,246,648.52 zilibakia katika akaunti za mradi kwa sababu zifuatazo:-

- Uwepo wa maradhi ya Uviko 19. Ambapo kulipelekea kutotekelezeka kwa shughuli zilizopangwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika hoja hii kamati ya PAC imebaini kuwa kweli kulikuwa na ucheleweshaji wa kutotumika fedha kwa wakati kama ilivyoelezwa kwenye hoja. Baada ya kamati kupata maelezo ya kina imebaini kuwa maradhi ya Uviko 19 yamesababisha shughuli za mradi kutokutelezeka kwa wakati.

Hata hivyo Kamati ilihoji kuhusiana na muendelezo wa fedha na kuelezwa kuwa ilitumika kwa mwaka wa fedha mwengine na ilipata fursa ya kukagua baadhi ya vielelezo vya matumizi ikiwemo vocha namba 41/03 ya tarehe 18/3/2022 malipo ya shilingi 39,548,500 yakiwa ni malipo ya SIDA elimu ya maandalizi na msingi.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaishauri Wizara ya Elimu ishirikiane Mkaguzi anapofanya ukaguzi wake kwa kutoa maelezo ya kina kuhusiana na hoja husika ili kuepusha kujitokeza kwa baadhi ya hoja ambazo zinayo majibu.

## 3.0 MRADI WA UIMARISHAJI WA ELIMU YA SEKONDARI ZANZIBAR (ZISP)

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari Zanzibar (ZISP) umefadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (IDA) ambao unaboresha elimu ya Sekondari katika visiwa vya Zanzibar na kuweka mazingira mazuri ya kujifunzia na masomo yaliyokusudiwa.

Mradi huu unatarajiwa kuwanufaisha jumla ya watu 170,000 katika kipindi cha miaka mitano (5) ambapo walengwa Wakuu ni wanafunzi wa darasa la juu la msingi na sekondari ya chini pamoja na kuwanufaisha walimu, Walimu Wakuu na wafanyakazi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

**Hoja nambari 3.4.2.1: Ucheleweshwaji wa fedha kutoka kwa wafadhili dola za Marekani 5,009,650**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa usheleweshaji wa fedha za utekelezaji wa Mradi kutoka kwa wafadhili wa Mradi huo ambao ni Shirika la Maendeleo la Kimataifa-IDA ambapo jumla ya dola za Marekani 5,009,650 zilipokelewa tarehe 16 Disemba, 2020 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi wa ZISP jambo ambalo limepelekea baadhi ya shughuli za mradi kusita kwa muda wa miezi 6 kutokana na kutopatikana kwa fedha za utekelezaji wa mradi huo kwa wakati hali inayopelekea kuzorota kwa utekelezaji wa mradi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu kuwashauri wafadhili wa mradi wachukue juhudi ya kuhakikisha kwamba fedha zote zilizokusudi wa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi na kwa kuzingatia muda halisi uliopangwa zinapatikana kwa wakati ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Shughuli nyingi za Mradi hazikuweza kukamilishwa mpaka unamalizika mwaka wa fedha Juni 2021 kwa sababu fedha za utekelezaji wa shughuli hizo zilichelewa kuingizwa kutoka kwa Mfadhili kwa wakati Hata hivyo uongozi ulichukuwa jitihada za kufuatilia kwa karibu ili fedha ziingizwe kwa wakati ili shughuli ziweze kutekelezeka kama zilivyopangwa.Mradi umekamilika kwa mwaka 2021/2022.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa kweli kulikuwa na ucheleweshaji kwa uingizaji wa fedha za mradi hali iliyopelekea mradi kuchelewa kukamilika kama ilivyopangwa, aidha, Kamati imebaini kuwa wafadhili hawaingizi fedha kwa wakati, hata hivyo Maradhi ya Uviko 19 pia yamechangia mradi kuchelewa na hadi kamati inamaliza kazi zake mradi tayari umekamilika. Hivyo Kamati imeridhika na majibu ya Wizara.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaishauri Wizara ya Elimu na Amali kuhakisha kwamba miradi inakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa.

**Hoja nambari 3.4.2.2: Kukosekana kwa taarifa za matumizi ya fedha za mradi shilingi 697,564,125**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 697,564,125 zimelipwa kwa kutumia hati ya malipo yenye nambari 2/12 ya tarehe 21 Disemba, 2020 kwa ajili ya ruzuku katika madarasa ya Kidato cha kwanza, Kidato cha tatu na Kidato cha nne kwa skuli mbalimbali za Zanzibar lakini hadi ukaguzi unakamilika ripoti za matumizi ya fedha hizo hazikuweza kupatikana. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa upotevu wa fedha za Umma ambapo ni Kifungu Nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu kupitia wasimamizi wa mradi kuhakikisha kwamba katika kipindi chote cha utekelezaji wa mradi panakuwepo na matumizi sahihi ya fedha na rasilimali za Umma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni pamoja na miongozo mbali mbali ya fedha inayotolewa Kitaifa na Kimataifa ikiwa ni pamoja na kuongeza umakini katika uaandaaji wa ripoti mbali mbali zamradi.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kwa kipindi cha ukaguzi Skuli zilikuwa hazina utaratibu wa kutayarisha ripoti za fedha kuwasilisha Wizarani baada ya matumizi ya fedha. Baada ya kupata ushauri wa mkaguzi, wizara ilichukua jitihada ya kuwaelimisha viongozi wa Skuli na kuweza kutaarisha ripoti za matumizi kwa fedha zote wanazopatiwa

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa kweli Wizara ya Elimu ilikuwa haina utaratibu wa kuandaa taarifa au ripoti ya matumizi ya fedha za mradi ikiwemo mradi wa shilingi 697,564,125. Hata hivyo, Wizara imekiri kujitokeza kwa kosa hili na kufuata ushauri wa Mkaguzi wa kufanyiakazi na kupelekea kamati kupatiwa kwa baadhi ya ripoti ya matumizi ya fedha ikiwemo ripoti ya ripoti ya utekelezaji wa matumizi ya fedha. Kwa majibu hayo, Kamati imeridhika na hatua iliyochukuliwa na kukubaliana na majibu.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufuatilia taarifa za matumizi ya fedha za miradi kwa makini ili kuepusha viashiria vya upotevu wa fedha za umma na kupelekea rasilimali za nchi zitumike vibaya.

**Hoja nambari 3.4.2.3: Kutotumika kwa fedha za mradi kwa wakati uliopangwa USD 3,734.74**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa bakaa ya dola za Kimarekani 3,734.74 mwishoni mwa mwaka wa fedha 2020/2021 zilizopaswa kutumika kwa ajili ya shughuli za utekelezaji wa mradi. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuchelewa kumalizika kwa mradi kwa wakati ambapo kunaweza kuathiri maendeleo ya mradi huo kutokana na uwezekano wa kupanda kwa bei za bidhaa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kwamba mpango kazi wa mradi unatekelezwa kulingana na bajeti ili kufikia lengo lililokusudiwa.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Baadhi ya shughuli hazikuweza kukamilika kwa sababu fedha za utekelezaji wa shughuli zilichelewa kuingizwa kutoka kwa Mfadhili.

**Uchunguzi ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC baada ya kupata maelezo ya kina imebaini kuwa kweli Wizara ya Elimu haikutumia fedha kwa wakati uliopangwa kutokana na Mfadhili kuchelewa kuingiza fedha kwa wakati, hata hivyo kamati haikuridhika na majibu ya utekelezaji wa hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaishauri Wizara ya Elimu kuhakikisha fedha zinaingizwa kwa wakati uliopangwa kutoka kwa wafadhili ili kuepusha miradi isichelewe kukamilika na kupelekea kuzorota kwa maendeleo ya nchi.

**Hoja nambari 4.4.3.4: Dosari zilizobainika katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi Kituo Maalum chaSayansi**

Katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi wa kituo maalum cha sayansi kilichopo Mkwajuni Kaskazini Unguja kupitia mradi wa ZISP ukaguzi umebaini dosari mbalimbali kama ifuatavyo:-

- Kitokuzungushiwa uzio ili kuzuwia uvamizi wa maeneo pamoja na kuepusha uharibifu unaoweza kujitokeza kwa kutokuwepo kizuizi katika uingiaji wa maeneohayo.
- Maeneo ya koridoo ya kituo hicho yanaonekana kutuwama maji wakati wa mvua hali ambayo imesababishwa na hali halisi ya ujenzi wajengo.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Mkataba wa awali ulikuwa hauna kazi ya uwekaji wa uzio katika 'Hub' zilizotajwa, kwa kupokea ushauri wa Wakaguzi, Uongozi wa Wizara ikapanga kuweka uzio kwa mwaka unaofuata katika Hub zifuatazo na tayari zimeshawekwa uzio:-

**Pemba:-**

Makangale, Kiuyu Mbuyuni, Wingi ziwakijwe Fundo, Limbani na Kojani.

**Unguja:-**

Tumbatu, Mkwajuni, Kitope, Jangombe, Chuwini, Bwejuu na Uroa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na juhudi zilizozichukuliwa na Wizara kwa kujenga uzio katika Hub zilizotajwa na Mkaguzi na hatua ya kurekebisha koridoo inayoonekana kutuwama maji.

**MPANGO WA LISHE MASHULENI (HGSFP)**

Katika mwaka 2020/2021, kutokana na ugatuzi wa madaraka kwa elimu ya Awali na Msingi, Mpango wa utekelezaji wa programu ya kusambaza chakula mashuleni (Home Grown School Feeding Program - HGSFP) ulikuwa chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ambapo ilitoa tenda kwa vikundi vya wakulima kwa ajili ya kusambaza chakula katika shule zilizopo chini ya mradi na kufanya malipo kwa wakulima hao kuanzia Agosti, 2020 hadi Disemba, 2020. Mradi huu una muda wa miaka mitatu (3) kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 mpaka 2022/2023.

**Hoja nambari 3.5.3.1: Fedha iliyokosa maelezo ya matumizi dola za kimarekani USD 121,720.36**

Ukaguzi umebaini mradi wa HGSFP umetoa fedha kupeleka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa jumla ya dola za kimarekani USD 121,720.36 zilizolipwa kupitia hati ya malipo nambari 5/10 ya tarehe 26/10/2020 lakini hadi ukaguzi unakamilika maelezo ya matumizi ya fedha hizo hayakuweza kupatikana. Kufanya hivyo kunapelekea uwepo wa viashira vya ubadhirifu katika matumizi ya fedha na rasilimali za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mradi kuhakikisha inaweka udhibiti mzuri wa matumizi kwa shughuli za mradi pamoja na kutoa maelezo ya kina juu ya matumizi ya fedha zilizotumika kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi ili kuepusha tuhuma zinazoashiria kutokuwepo kwa matumizi sahihi ya fedha

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Vocha ya malipo nambari 5/10 ya tarehe 26/10/2020 ilikuwa ni fedha zilizohaulishwa kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwenda Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ajili ya malipo ya usambazaji wa chakula cha wanafunzi Unguja na Pemba. Kama ilivyo barua yenye kumbukumbu No. OR/TMSMIM/V.11/3VL.111/51 ya tarehe 21/10/2020 inahusika, na risiti ya malipo nambari 528704 ya tarehe 27/10/2020 ilitolewa kama uthibitisho wa kupokelewa fedha hizo na TAMISEMI (UGATUZI) Maelezo kamili ya malipo hayo yanapatikana TAMISEMI.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa kipindi cha ukaguzi Mkaguzi hakupatiwa vielelezo vya matumizi ya dola za kimarekani USD 121,720.36 na kuelezwa vipo TAMISEMI ambapo hadi vielelezo vinapatikana kwa ajili ya kupatiwa Mkaguzi muda ulikuwa ushamaliza wa ukaguzi ndio maana hoja ikajitokeza, wakati wa kamati ya PAC ipo katika uchunguzi wake ilihoji kuhusiana na vielelezo hivyo na kupapatiwa vielelezo hivyo ikiwemo mikataba ya Bimize Hamadi wa tarehe 4/9/2020, Hiari Ali Mussa wa tarehe 4/9/2020 na Hidaya Shauri Mkombe wa tarehe 6/9/2020.

Aidha, kamati ilipitia vocha ya tarehe 21/1/2020 kuhusu malipo ya usagaji wa nafaka katika skuli ya Kidagoni Mtoapwani shilingi 5,360,000. Kamati imeridhika na majibu ya hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri kuwa kuwe na mashirikiano mazuri baina ya baina Wizara na Mkaguzi wakati wa ukaguzi kwani wote wana lengo moja la kuimarisha Malengo na Mipango ya Serikali na kuepusha changamoto zisijitokeze.

**Hoja nambari 3.5.3.2: Malipo yasiyokuwa na vielelezo ya dola za kimarekani USD 6,535**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya USD 6,535 zimetumika kupitia hati namba 3/8 ya tarehe 30 Agosti, 2020 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ushirikiano wa kimataifa lakini vielelezo vya matumizi hayo havikupatikana kwa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo ya matumizihusika.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo matumizi yasiyoridhishaya fedha za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Kifungu Nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika yanawekewa vielelezo pamoja na kuwasilisha matumizi na vielelezo vyake kwa ajili ya ukaguzi

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Ni ukweli usiopingika malipo yaliyofanywa kwa hundi nambari 000438 yenye thamani USD 6,535.00 kwa ajili ya mafunzo kwa maofisa wa mradi wa HGSFP na TAMISEMI, marejesho ya malipo hayoyalifunganishwa na vocha husika lakini ripoti ya mafunzo hayo hadi ukaguzi unafanyika ilkuwa haijafunganishwa na vocha husika, kwa kawaida ripoti anakuwa nazo Mratibu wa mradi huo. Kwa sasa tayari amewasilisha na zipo tayari.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa malipo ya U$D. 6,536 vielelezo vyake vilikuwepo kama majibu yanavyojileza isipokuwa ilikosekana ripoti ya mafunzo kwa ajili ya maafisa wa Mradi HGSFP na TAMISEMI ambapo hadi ukaguzi unakamalika Mkaguzi hakuwapatiwa.

Hata hivyo, baada juhudi za Wizara ya Elimu kufuatilia ripoti ya mafunzo, kamati ilipatiwa na kuzikagua ikiwemo (report of proposal Officer Local Government Authrority School and Community State Holder HGSFD na Ripoti ya Kuwajengea Uwezo Watumishi) na kamati kuridhika na juhudi zilizochukuliwa

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwa makini katika kufuatilia ripoti za Mafuzo ya miradi husika.

**MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA SEKTA ZA FEDHA NA MIPANGO MIJI**

**MRADI WA MABORESHO YA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA**

**(PFMRP)**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, IMF, UNDP na DFID, kuanzia mwaka wa fedha 2002/2003 imefanya tafiti kadhaa ambazo zinalenga kubainisha maeneo yenye udhaifu kupitia Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma – (Public Finance Management Programme (PFMRP)).

Tafiti zilizofanyika ni pamoja na kufanya; tathmini ya Uwajibikaji wa Fedha Nchini (CFAA), Mapitio ya Matumizi ya Umma (PER), Mapitio ya Matumizi ya Umma na Mapitio ya Uwajibikaji wa Kifedha (PEFAR), Memoranda ya Uchumi wa Nchi, Sekta ya Karafuu Zanzibar, pamoja na Ripoti ya Tathmini ya Manunuzi ya Nchi (CPAR), na Tathmini ya Masuala ya Serikali za Mitaa. Tafiti hizi zilileta Mageuzi makubwa matatu, ambayo ni Mageuzi ya Usimamizi wa Uchumi na Fedha, Maboresho ya Taasisi na Rasilimali Watu na Maboresho ya Utawala Bora.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006 hadi 2010/2011 NORAD ilifanya utafiti kuhusu hali ya Usimamizi wa Fedha za Umma Zanzibar kwa madhumuni  ya kutathmini mipango inayoendelea ya kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Umma Zanzibar.

Katika utafiti uliyofanywa 2015 na DFID kuhusu tathmini ya vihatarishi ulibaini uboreshaji wa utekelezaji wa bajeti, usimamizi wa mapato na ukaguzi wa ndani, huku kukiwa na changamoto katika manunuzi, usimamizi wa kodi na mishahara pamoja na utawala wa rasilimali watu.

Awamu ya nne ya Mpango huo ilianza mwezi Julai, 2012 ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara yake ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar ilifanya mchakato wa kuleta mageuzi ya fedha zake za Umma chini ya mpango wa maboresho ya usimamizi wa fedha za umma (PFMRP) ambao unalenga kuboresha maeneo yafuatayo:

i. Usimamizi wamapato;
ii. Bajeti namipango;
iii. Utekelezaji wa Bajeti, uwazi nauwajibikaji
iv. Udhibiti na usimamizi wa bajeti katika taasisi mbalimbali zaSerikali.

#### 4.1.1.1 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 38,415,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 38,415,000 zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa PFMRP lakini vielelezo vya matumizi ya fedha hizo havikupatikana kwa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo ya matumizi husika.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo matumizi yasiyoridhishaya fedha za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Kifungu Nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba malipo yote yanawekewa vielelezo na kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 9: Malipo yasiyokuwa na vielelezo**

| **Tarehe** | **Utekelezaji wa shughuli ya mradi** | **Idara iliyohusika** | **Kiasi Cha fedha kilichotumika (Tshs)** |
|---|---|---|---|
| 09.03.21 | Mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo kwa PDEs (wafanyakazi wa PMUs) juu ya miongozo ya ununuzi | ZPPDA | 29,085,000 |
| 08.07.20 | Kusaidia uratibu wa programu Zanzibar ifikapo Juni, 2021 | PFMRP | 5,120,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 14.08.20 | Kusaidia uratibu wa programu Zanzibar ifikapo Juni, 2021 | PFMRP | 4,210,000 |
| **Jumla** | | | **38,415,000** |

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Vielelezo kwa ajili ya malipo hayo vipo na vimeambatanishwa na vocha husika. Aidha malipo halisi ni shilingi 38,000,000 badala ya shilingi 38,415,000 zilizoainishwa katika ripoti.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini Wizara ya fedha walichanganya mwaka wa kukaguliwa ambao Mkaguzi alikagua vielelezo vya mwaka 2021/2022 na sio 2020/2021 na kupelelkea kujitokeza kwa hoja hii. Hata hivyo, kamati imeelezwa kuwa malipo halisi ni shilling 38,000,000 na sio shilingi 38,415,000 ambayo Mkaguzi kaiainisha kwenye kitabu. Aidha, kamati imepata fursa ya kuvikagua vielelezo hivyo na kuridhika navyo.

**Hoja Nambari 4.1.1.2: Kutokutekelezwa kwa Mradi wa Uondoaji wa Maji katika Bwawa la Mwantenga shilingi 1,736,773,216.56**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 1,736,773,216.56 zilipaswa kutumika katika utekelzaji wa mradi wa uondoaji wa maji katika Bwawa la Mwantenga katika awamu ya kwanza, lakini utekelezaji wa mradi huo katika awamu iliyopangwa haukufanyika hali iliyopelekea kupangwa kufanyika katika awamu ya pili ambayo pia haukufanyika licha ya fedha za utekelzaji wa mradi huo kutolewa kwa wakati.

Kufanya hivyo kunaweza kukupelekea kuwepo kwa viashiria vya kufanyika kwa ubadhirifu wa fedha za Umma pamoja na uwezekano wa kuathithiri makaazi ya wananchi wa maeneo hayo katika nyakati za mvua kubwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Zanzibar (ZMC) kuhakikisha unafanya ufuatiliaji wa fedha za utekelezaji wa miradi inayopangwa ili miradi hiyo iweze kufanyika ili kuweza kupunguza athari ambazo zinaweza kujitokeza kutokana na kutokufanyika kwa miradi hiyo

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kazi ya mwanzo katika Mradi huu ilikamilika kwa mujibu wa mchoro (design) mwezi April 2020. Hata hivyo, baada ya kukamilika kwa mradi huu ikaonekana bado tatizo la kutuwama kwa maji linaendelea kuwepo na kusababisha mafuriko. Hivyo, hatua za dharura zilichukuliwa kwa kusaini

mkataba wa nyongeza (Addendum) ili kutatua changamoto hiyo. Hata hivyo, kazi hii haikuweza kukamilika kutokana kumalizika kwa muda wa Mradi wa ZUSP uliofungwa rasmi mwezi Disemba 2020. Hivyo, kazi hii imepangwa kutekelezwa katika Mradi wa BIG-Z ambao kwa sasa upo katika hatua ya kutafuta mshauri elekezi wa kufanya usanifu na kusimamia mkandarasi

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa jumla ya shilingi 1,736,773,216.56 zilipaswa kutumika katika utekelezaji wa mradi wa uondoaji wa maji katika Bwawa la Mwantenga lakini utekelezaji wake haukufanyika kwa sababu muda wa mradi wa ZUSP ulikuwa ushamaliza.

Halkadhalika, Kamati imebaini kuwa mradi wa Bwawa la Mwantenga haukufikia lengo kwa sababu bado maji yanafurika katika bwawa, hali hii imetokana na kutokufanyika vizuri kwa upenguzi yakinifu na kupelekea bwawa kushindwa kufanyakazi kama ilivyotarajiwa. Kamati haikuruidhika na majibu ya hoja hii.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inashauri Wizara ya Fedha na Mipango kutumia fedha za miradi kwa wakati uliopangwa ili kunusuru fedha zisirudishwe kwa wafadhili wa miradi.
2. Kamati ya PAC inashauri watendaji kuwa makini katika kufanya upenguzi yakinifu kabla mradi haujaanza na kuepusha kufeli kwa baadhi ya miradi.

**Hoja Nambari 4.2.2.3: Kutokufanyakazi kwa mfumo wa maji taka katika jaa la Kibele shilingi 1,246,124,300**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa jaa la Kibele ambalo limewekewa mfumo wa maji taka (PCW) wenye jumla ya shilingi 1,246,124,300 lakini hadi ukaguzi unakamilika imebainika kuziba kwa mabomba yanayopitisha maji hayo na kupelekea mfumo huo kutokufanya kazi. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Manispaa kuhakikisha unasimamia ipasavyo miradi inayotekelezwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuanzishwa kwa miradi hiyo.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kuziba kwa 'pipe' za mfumo wa maji taka inatokana na watumiaji (user department) kutofuata taratibu za matumizi kama yalivyoanishwa kwenye "Operational Manual ya Mradi". Aidha kutokuwepo na wataalamu wenye ujuzi wa kutosha kumechangia kuziba kwa paipu za mfumo wa maji taka. Hii inatokana na sababu kwamba wataalamu wa mwanzo waliopewa mafunzo ya utumiaji wa mfumo huo wamehamishwa katika jaa la kibele na kuletwa wafanyakazi wapya amba hawana ujuzi na utaalamu wa kutosha wa kuendesha jaa la Kibele. Hali hii inakwenda kinyume na "Operational and Maintance Manual" ya Mradi wa Jaa la Kibele.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imekubaliana na hoja ya Mkaguzi ya kutokufanya kazi kwa mfumo wa maji taka na kubaini kuwa wataalamu ambao wamesomea masuala ya mitaro wameondoshwa na kupelekea matatizo kijitokeza. Hadi kamati inamaliza uchunguzi wake imebaini kati ya wafanyakazi 25 kuna wafanyakzi 15 tu ambao wote hawana ujuzi isipokuwa mmoja tu ambae ndie Mratibu wa Mradi. Katika uchunguzi wake Kamati ya PAC haikuridhishwa na majibu ya hoja hii na ilibaini mambo yafuatayo:-

1. Gari aina ya Katapila linalotumika katika ukusanyaji wa taka kimehabika kwa takriban miezi sita bila ya kufanyiwa matengenezo.
2. Kuwepo kwa upungufu mkubwa wa fedha za uendeshaji wa Mradi huo, Kamati imebaini jumla ya shilingi 200 zinahitajika kila mwezi wakati hivi sasa jumla ya shilingi 50 ndio zinazopatikana kwa mwezi.
3. Baadhi ya miundombinu ya Jaa ikiwemo pipe za kuingizia taka laini yameharibika.
4. Baadhi ya Majaa yameota majani ambayo hayastahiki kuwemo ndani yake.
5. Kuwepo kwa taka zilizokuwa zimezagaa katika njia ya eneo la kukusanyia taka.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inashauri Serikali kupitia Manispaa ya Mjini kufanya utaratibu wa kuwarudisha watumishi ambao wana ujuzi na masuala ya mitaro ili waweze kusaidia uendeshaji wa Jaa hilo kwa utaalau.
2. Serikali ihakikishe vyombo vilikuwa vimeharibika vinafanyiwa matengenezo na kutoa huduma iliyokusudiwa.

3. Serikali ihakikishe vyombo vya uchakataji taka kuwa mbolea vinatumika na kufanya kazi ipasavyo.
4. Serikali ifanyie matengenezo miundoombinu ya maji taka iliyoharibika.

**Hoja nambari 4.2.2.4: Kutokutumika kwa vifaa vya usagaji wa taka vilivyonunuliwa USD 420,580**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Fedha na Mipango imetumia jumla ya USD 420,580 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kusagia taka, gharama za ufungaji pamoja na mafunzo ya kuvitumia vifaa hivyo katika jaa la Kibele lakini hadi ukaguzi huu unakamilika vifaa vilivyonunuliwa na kupokelewa miezi tisa iliyopita ambavyo ni trekta la kilimo, mashine ya kugeuza na trela ya tanki la maji bado havijaanza kutumika kama ilivyokusudiwa.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Umma ambapo pia ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Zanzibar kuhakikisha Sheria, Kanuni na miongozo ya ununuzi na utumiaji wa vifaa vilivyonunuliwa inafuatwa kikamilifu.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Baada ya kununuliwa kwa mitambo ya kuchakata taka, maafisa wanaohusika na utumiaji wa mtambo huo walipatiwa mafunzo kwa muda wa wiki mbili yanayohusiana na utumiaji na utunzanji wa mtambo huo. Watumiaji wa mtambo huo (user department) walithibisha na kuridhia kwamba mtambo huo uko sawa na umekidhi vigezo vyote vilivyotakiwa kwa mujibu wa mkataba.

Kutokufanya kazi kwa mtambo huu inatokana na sababu kwamba wataalamu wa mwanzo waliopewa mafunzo ya utumiaji wa mtambo huo wamehamishwa katika jaa la kibele na kuletwa wafanyakazi wapya ambao hawana ujuzi na utaalamu wa kutosha wa kuendesha mtambo huo. Katika kutatua changomoto hiyo, Serikali kupitia Mradi wa BIG-Z imepanga program maalumu ya mafunzo kwa wataalamu waliopo Kibele ili kuwapa ujuzi wa matumizi ya mtambo huo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imesikitishwa na matumizi ya jumla ya U$D 420,580 kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya kuchakata taka pamoja na ufungaji wake lakini la kusikitisha vifaa hivyo havifanyi kazi ipasavyo kama ilivyokusudiwa.

Kamati ya PAC ilihoji juu ya kutokufanyika kazi kwa vifaa hivyo na kubaini kuwa wataalamu ambao wanatoka Baraza la Manisapaa Mjini waliopewa

mafunzo yanayohusiana na uendeshaji wa mashine wameondolewa na kupelekwa watumishi wengine ambao hawana ujuzi wa uendeshaji mashine hizo na kupelekea mashine hizo kutofanya kazi.

Kamati ya PAC ilipata fursa ya kwenda kutemblea mshine hizo ikiwemo (screen mashine ya kuchakata mbolea, compast system) katika jaa la kibele na kubaini yafuatayo:-

- Jumla ya mashine tatu ambazo zimenunuliwa USD 420,580 hakuna hata mashine moja inayofanya kazi.
- Hakuna bajeti ya kutosha kwa mwezi zinahizotaji lita 50 za mafuta ili mashine hizo zifanye kazi, kwasasa fedha ambazo zinatoka Manispaa ya Mjini na uwezo hawana.
- Baadhi ya mashine zimeharibika na zinahitaji fedha kubwa za matengenezo ukilinganisha na gharama ya kununulia.

Kamati ya PAC haikuridhishwa na majibu ya hoja hii kwani mashine zimenunuliwa kwa fedha nyingi lakini mashine zote hadi kamati inamaliza uchunguzi wake hazifanyi kazi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inalishauri Baraza la Manispaa Mjini kuwarudisha wataalum wa mwanzo ambao walipewa mafunzo kuhusiana na uondeshaji wa mashine hizo.
2. Kamati ya PAC inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kufanya upembuzi yakinifu kabla hawajanunua mashine za miradi ili kuepusha miradi mingi kutofanya kazi.
3. Wizara ya Fedha na Mipango itafute njia mbadala itakayohakikisha upatikanaji wa fedha za matengenezo na uendeshaji wa Jaa la Taka la Kibele.

**Hoja nambari 4.2.2.4: Kutokutumika kwa mfumo wa Usimamizi wa fedha USD 6,276**

Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar imeingia makubaliano ya mkataba na M/S Core Soft Limited ya Zanzibar kwa thamani dola za Kimarekani 56,404 kwa ajili ya usambazaji wa toleo jipya la mfumo wa usimamizi wa fedha (NAV system) katika Mradi wa ZUSP ambapo malipo ya fedha hizo yalifanywa kupitia hati za malipo nambari PV/PBZ/F/20 ya tarehe 21/9/20 yenye thamni ya dola za Kimarekani 2,500 na hati nambari PV/PBZ/F/20 ya tarehe 21/8/30 yenye thamani ya dola za Kimarekani 3,776

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokufanyakazi kwa mfumo wa usimamizi wa fedha na kupelekea taarifa za uhasibu za Mradi huo kuandaliwa

kwa fomu ya excel. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za Umma ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Zanzibar kuhakikisha Sheria, Kanuni na miongozo mbali mbali inafuatwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na kusimamia makubaliano yaliyofikiwa katika matumizi ya mfumo wa usimamizi wa fedha wa NAV System ili kuepusha matumizi ya fedha yasiyokuwa na tija kwa Serikali na jamii kwa ujumla.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Mfumo huu wa usimamizi wa fedha uliwekwa kwenye Sarver ya IFMIS ambao umeimarishwa (system upgrading) na kwa sasa tayari unatumika kwenye Mradi wa BIG-Z ambapo matumizi yote yanayofanyika kwenye Mradi yanafanywa kwenye

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini mfumo ulikuwa haufanyika kazi na kamati kuelezwa kuwa kwasasa umeimarishwa na kamati imeridhika na hatua ya Wizara iliyochukua.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaitaka Wizara ya Fedha kuwa makini katika ununuzi wa Mifumo mbali mbali ya Serikali kwa lengo la kuiepusha Serikali kuingia hasara.

**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI**

**MRADI WA KUSAIDIA SEKTA YA UCHUKUZI (TSSP)**

Mradi wa kusaidia Sekta ya Uchukuzi (Transport Sector Support Project - TSSP) ni mradi unaotekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar ambao unahusika na Sekta ndogo za barabara na reli na anga Nchini ambapo utekelezaji wa mradi huu ulianza rasmi tarehe 27 Mei 2016. Mradi huu kupitia Katika sekta ndogo ya barabara umehusika kufanya kazi zifuatazo:-

a. Kazi za kiraia za ukarabati/uboreshaji wa baadhi ya kilomita 462 za barabara kwa kiwango cha lami Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar.
b. Huduma za ushauri kuhusiana na kazi za barabara na masomo ya barabara;
c. Kujenga uwezo.

d. Ulipaji wa Fidia na utoaji wa makazi mapya.
e. Kufanya utekelezaji wa miundombinu ya kijamii.

Miongoni mwa watekelezaji wa mradi huu ni Wakala wa barabara Tanzania (TANROADS) na Wizara ya Miundombinu, Mawasiliano na Uchukuzi (MOICT) zinazotekeleza majukumu yake Tanzania Bara na Zanzibar kwa pamoja.

**Hoja nambari 7.3.2.1 Kutotumika kwa fedha za mradi Dola za Kimarekani USD 166,469.25**

Katika ukaguzi uliyofanyika imebainika kuwa Wizara ya Miundombinu, Mawasiliano na Uchukuzi imepokea jumla ya dola za kimarekani 166,469.25 kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi mbali mbali wa Wizara lakini fedha hizo hazikutumika kama ilivyokusudiwa hali iliyopelekea kutokukamilika kwa vipengele vya utekelezaji wa mradi huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Miundombinu, Mawasiliano na Uchukuzikuhakikishakwambafedhazotezilizopangwakwaajiliyautekelezaji mradi zinatumika kulingana na bajeti iliyoidhinishwa ili kuepusha uwezekano wa kufanyika kwa matumizi kinyume nautaratibu

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara inakiri katika bajeti ya Mradi wa TSSP ya mwaka 2020/2021 ilitenga jumla ya dola za kimarekani 166,469.25 kwa ajili ya kuwajengea uwezo baadhi ya maofisa wake lakini mafunzo hayo yalishindwa kufanyika kutokana na mripuko wa janga la maradhi ya COVID 19 iliyoikumba Dunia, hali iliyopelekea vyuo na taasisi nyingi za mafunzo ndani na nje ya nchi kusitisha shughuli zake pamoja na kufunga mipaka yote, hivyo mipango hiyo ya kwenda mafunzo hayo ikashindikana kufanyika kama ilivopangwa hapo awali.

Hata hivyo Wizara imetekeleza mafunzo hayo katika mwaka wa fedha 2021/2022 baada ya kupungua maradhi ya COVID 19 na kufunguliwa vyuo na taasisi za mafunzo. Orodha ya waliohudhuriana mchanganuo wake vipo kwa uhakiki.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Wizara imekiri kutokutumika kwa fedha za mradi kwa sababu ya maradhi ya Uviko 19 na kupelekea kwa baadhi ya vipengele vya mradi kutotumika. Hata hivyo, kamati imeelezwa kuwa baada ya maradhi kumalizika fedha zilitumika kwa mwaka mwengine wa 2020/2021 wa fedha na watumishi kupata mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo kam ilivokusudiwa awali na kamati imepata fursa ya kuona vilelezo vya wanafunzo ambavyo

watumishi wamepata mafunzo wakiwemo :

- Nafisa Madai Ali wanzo yalifanyika wiki mbili tarehe 18/8/2021 kiwango cha fedha shilingi 10,620,000
- Salmin Khamis Salim wiki tatu tarehe 18/8/2021 kiwango cha fedha shilingi 10,626,000.
- Juma Hamid Juma wiki tatu tarehe 18/8/2021 kiwango cha fedha shilingi 10,626,000.

Kamati baada ya kukagua vielelezo imeridhika na majibu ya hoja ya mkaguzi.

**Hoja nambari 7.2.3.2: Kutokulipwa kwa fidia kwa wananchi walioathirika na utekelezaji wa mradi (PAP) shilingi 188,486,250**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 188,486,250 ni fedha mbazo zingepaswa kulipwa kwa ajili ya fidia kwa watu walioathirika na mradi (PAP) ambapo dosari iliobainika na ukaguzi ni kutokulipwa kwa fedha hizo kwa watu hao hali ambayo inaweza kupelekea kuwepo kwa migogoro miongoni mwa wananchi na Serikaliambapo kunaweza kukapelekea viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma

Ukaguzi unashauri Wizara ya Miundombinu, Mawasiliano na Uchukuzi (MOICT) kuhakikisha kwamba inafanya malipo ya fidia kwa mujibu wa ripoti ya Mtathmini Mkuu kwa wananchi walioathirika na mradi (PAPs) ili kuepusha atahari zinazoweza kujitokeza. Mchanganuo wa wananchi waliyoathirika kupitia mradi huo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 42: Orodha ya fidia za waliothirika na mradi (PAA)**

| PALE - KIONGELE (4.6 KM) ROAD | | | |
|---|---|---|---|
| Tathmini ya Mazao | | | |
| **Nam** | **Jina** | **Shehia** | **Kiasi cha fedha kilichostahiki Kulipwa (Tshs)** |
| 1. | Kombo Ubwa Juma | Pale | 1,125,000 |
| 2. | Hadia Foum Khamis | Pale | 2,130,000 |
| 3. | Salum Foum Khamis | Pale | 735,000 |
| 4. | Riziki Ali Amour | Pale | 625,500 |
| 5. | Amour Ali Amour | Pale | 3,475,000 |
| 6. | Ngwali Kona Kheir | Pale | 389,500 |
| 7. | Tatu Moh'd Makame | Pale | 2,165,000 |
| 8. | Patima Jamal Foum | Pale | 142,500 |
| 9. | Kombo Hakim Makame | Pale | 933,000 |
| 10. | Moh'd Juma Ussi | Pale | 2,265,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11. | Said Mossi Makame | Pale | 2,425,000 |
| 12. | Kassim Machano Jaml | Pale | 706,500 |
| 13. | Abudu Makame Abudu | Pale | 13,185,000 |
| 14. | Khamis Khamis Makame | Pale | 1,630,000 |
| 15. | Khamis Ali Khamis | Pale | 978,000 |
| 16. | Ali Hamdu Makame | Pale | 616,500 |
| 17. | Mwajuma Juma Ussi | Pale | 447,000 |
| 18. | Khamis Juma Ussi | Pale | 1,253,500 |
| 19. | Ali Ussi Nyange | Pale | 834,500 |
| 20. | Shaib Makame Mashaka | Pale | 427,500 |
| 21. | Machano Mkinai Khamis | Pale | 399,000 |
| 22. | Muhamadi Ali Hamdu | Pale | 565,500 |
| 23. | Mboja Ali Hamdu | Pale | 3,085,000 |
| 24. | Mboja Muhammed Makame | Pale | 624,000 |
| 25. | Patima Makame Mossi | Pale | 2,860,500 |
| 26. | Haji Saburi Mtwana | Pale | 900,000 |
| 27. | Haji Haji Chetu | Pale | 631,500 |
| 28. | Nyange Hassan Kombo | Pale | 978,000 |
| 29. | Mda Saleh Haji | Pale | 465,500 |
| 30. | Mgeni Vuai Kheir | Pale | 760,000 |
| 31. | Ussi Jamal Foum | Pale | 315,000 |
| 32. | Mashavu Mrisho Omar | Pale | 1,017,000 |
| 33. | Zubeir Juma Abushiri | Mkwajuni | 750,000 |
| 34. | Kombo Simai Juma | Mkwajuni | 322,500 |
| 35. | Suleiman Mtwana Khamis | Mkwajuni | 100,000 |
| 36. | Khamis Nuhu Muhamadi | Mkwajuni | 496,000 |
| 37. | Ali Vuai Kona | Mkwajuni | 589,000 |
| 38. | Silima Hassan Silima | Mkwajuni | 1,212,500 |
| 39. | Bakari Khamis Ali | Kivunge | 250,000 |
| 40. | Bakari Zamir Bakari | Mkokotoni | 113,000 |
| 41. | Zakia Ali Makame | Mkokotoni | 75,000 |
| 42. | Jabir Bakari Jabir | Mkokotoni | 75,000 |
| 43. | Kombo Hakim Makame | Mkokotoni | 266,500 |
| 44. | Khamis Bakari Ali | Mkokotoni | 225,000 |
| 45. | Bakari Ali Makame | Mkokotoni | 225,000 |
| 46. | Mariam Shaabani Mohd | Mbaleni | 1,046,000 |
| 47. | Mchuzeni Khamis Juma | Kwagube | 450,000 |
| 48. | Masoud Kombo | Kikombweni | 325,000 |
| 49. | Khamis Haji Khamis | Kikombweni | 2,875,000 |
| 50. | Kassim Ali | Kikombweni | 652,000 |
| 51. | Nasoro Khamis Said | Kikombweni | 1,375,000 |
| 52. | Ega Shaame Khamis | Pale | 114,000 |
| 53. | Juma Ayubu Juma | Pale | 95,000 |
| 54. | Mgeni Vuai Kheir | Pale | 142,500 |
| 55. | Bimkubwa Said Khamis | Pale | 326,500 |
| 56. | Mashaka Makame Mashaka | Pale | 125,000 |
| 57. | Moh'd Juma Ussi | Pale | 592,000 |

| Jumla | 61,907,500 |
| --- | --- |

| PALE - KIONGELE (4.6 KM) ROAD | | | |
| --- | --- | --- | --- |
| Tathmini ya Nyumba | | | |
| **Nam** | **Jina** | **Shehia** | **Kiasi alichostahikikulipwa (Tshs)** |
| 1 | Salum Fumu Khamis | Pale | 9,200,000 |
| 2 | Khamis Fumu Khamis | Pale | 9,200,000 |
| 3 | Hadiya Fumu Khamis | Pale | 9,600,000 |
| 4 | Bakari Kheri Haji | Pale | 7,300,000 |
| 5 | Ali Mgwali Kona | Pale | 3,000,000 |
| 6 | Machano Mkinai Khamis | Pale | 3,000,000 |
| 7 | Ngwali Kheri Haji | Pale | 300,000 |
| 8 | Amina Miraji Haji | Mfenesini | 11,000,000 |
| 9 | Balozi Maskani | Mfenesini | 8,000,000 |
| 10 | Makame Mosi Makame | Pale | 400,000 |
| 11 | Juma Haji Khamis | Pale | 70,000 |
| **Jumla** | | | **61,070,000** |
| **FUONI - KOMBENI (8.56 KM) ROAD** | | | |
| **TATHMINI YA NYUMBA NA VIPANDO** | | | |
| **Nam** | **Jina** | **Shehia** | **Kiasi cha Fedha (Tshs)** |
| 1. | Ahmed Mbarak Matar | Fuoni | 7,567,000 |
| 2. | Kassim Khamis Ali | Kombeni | 5,341,750 |
| 3. | Khamis Suleiman Mwalim | Kombeni | 52,600,000 |
| **Jumla** | | | **65,508,750** |

## Majibu ya uongozi wa Wizara

Wizara inakiri wananchi walioorodheshwa kwa madai ya fidia wa mradi PAP wakati wa ukaguzi wa mwaka 2020/2021 walikuwa bado hawajalipwa fidia yao. Hata hivyo Wizara kupitia Bajeti ya mwaka 2021/2022 tayari imeshalipa madai hayo kwa wananchi wote waliohusika isipokuwa watu watatu ambapo wawili (Ndugu Zakia Ali Makame, na Maryam Shabani Mohamed) kati yao hawakupatikana kwa kipindi hicho. Wizara imechukua hatua za kuwasiliana na Sheha wa Shehia husika na wakipatikana wahusika hao watalipwa kwa vile fedha zao zipo. Na mtu mmoja kwa jina la Balozi Maskani, linatofautiana na jina liliomo katika fomu ya taarifa za kibenki za muhusika huyo. Mtu huyo

ametakiwa afuate taratibu za kusahihisha majina yake ili na yeye apatiwe fedha zake. Vielelezo vipo kwa uhakiki

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Baada ya Wizara kukiri, kamati ilipata fursa ya kukagua vielelezo kwa baadhi ya wananchi ambao waliolipwa fidia wakiwemo Ahmed Matari alilipwa tarehe 21/06/2021 vocha namba 2/6 jumla ya fedha 7,567,000 na kassim khamis tarehe 28/04/2021 vocha namba 4/6 jumla ya fedha aliyolipwa 5,341,750.

Kamati imeridhika na hatua iliyochukuliwa na Wizara.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaishauri Wizara ya Miundombinu, Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha kwamba inachukua juhudi kwa wahusika watatu waliobaki ili kuepusha migogoro na wananchi.

**Hoja nambari: 7.2.3.3: Dosari zilizobainika katika utekelezaji wa miradi ya Barabara.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa shughuli za ujenzi wa barabara kupitia mradi wa kusaidia sekta ya Uchukuzi (TSSP) zimetekelezwa lakini dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuchakaa kwa alama za barabarani (Bububu-Mahonda - Mkokotoni na Bububu Polisi - Kwanyanya Junction) hali inayopelekea uwezekano wa kukosekana kwa ufanisi wa madereva wanaotumia barabara hiyo. Hali halisi ya utekelezaji wa mradi huo ni kama inavyoonekana katika picha za hapo chini

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Mradi wa kusaidia sekta ya Uchukuzi (TSSP) ulikamilika mwaka wa fedha 2019/2020. Mradi ambao muda wake wa maangalizo (Defect Notification Period) ulikuwa ni mwaka mmoja. Wakati ukaguzi wa 2020/2021 unafanyika tayari muda huo wa uangalizi wa mradi ulikuwa umeshamalizika. Aidha, ukarabati wa alama za barabarani (Bububu-Mahonda - Mkokotoni na Bububu Polisi - Kwanyanya Junction) tayari ulikuwa umeshaingizwa katika mpango wa Wizara wa kuzipitia, kuzisafisha na kuzirejeshea rangi alama zilizofifia kwa kuzingatia utaratibu wa kawaida wa Wizara kama ilivyojipanga kwa njia zote za Unguja na Pemba. Kutokana na mipango ya Wakala wa Barabara ya kuzifanyia matengenezo alama za Barabarani, Barabara za (Bububu - Mahonda-Mkokotoni na Bububu Polisi - Kwanyanya Junction) zilikuwa hazijafikia.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa kweli kulikuwa na dosari kwa baadhi ya barabara zikiwemo Bububu Police Kwanyanya ambapo mudi mfupi baada ya kumalizika kwa mradi alama za barabarani zimefutika. Hali hii inatokana na sababu mbali mbali zikiwemo barabara kupitwa magari ya mchanga na kumwagika kwa mchanga na kupelekea alama hizo kufutika mara moja. Kamati baada ya uchunguzi imeridhika na majibu ya hoja.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri Serikali za Mitaa ziandae utaratibu mzuri wa kuzisafisha barabara ili kuondoa michanga inayomwagika kiholela barabarani na kuepusha alama zisifutike mara moja na kupelekea kutia hasara Serikali.

**MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA SEKTA YA UCHUMI WA BULUU, KILIMO NA MAMBO YA KALE**

**MRADI WA MAMLAKA YA UVUVI WA BAHARI KUU ZANZIBAR (SWIOFish 1 - GEF GRANT)**

Mradi wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Zanzibar (South West Indian Ocean Fisheries - SWIOFish 1: GEF Grant) ni programu ya awamu 3 ya miaka 15 ambayo inasaidia ushirikiano wa kikanda wa usimamizi wa uvuvi. Mkataba wa ufadhili wa mradi ni kati ya Benki ya Maendeleo ya Kimataifa (Benki ya Dunia) na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ulitiwa saini tarehe 12 Machi 2015 na kutangazwa rasmi kuanza kutumika tarehe 22 Juni, 2015. Mradi huu ulitarajiwa kumalizika tarehe 30 Septemba, 2021 lakini muda wa Mradi uliongezwa hadi tarehe 30 Septemba, 2022. Kiasi cha fedha kilichopangwa kutumika katika utekalezaji wa mradi kwa kipindi hiki ni jumla ya dola za Kimarekani1,977,000.5

Katika mradi huu wanufaika wakubwa ni pamoja na jumuiya za wavuvi ufugaji wa mwambao ambapo ni wavuvi wa kujikimu, kaya ambazo uvuvi ni sehemu muhimu ya maisha ya vijijini, wavuvi wadogo wadogo pamoja na wakulima wamwani.

**Hoja nambari 5.1.3.1: Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 1,189,815,582**

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Umma nambari 11 ya 2016 mtu, kampuni au taasisi haitashiriki katika manunuzi ya umma isipokuwa mtu huyo, kampuni au taasisi imesajiliwa kama msambazaji chini ya Sheria, vinginevyo kampuni hiyo imekataliwa na haitazingatiwa na taasisi yaununuzi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Mradi ulifanya manunuzi kwa watoa huduma mbalimbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA).

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na kifungu cha 23 (1) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa unasimamia ipaswavyo manunuzi yanafanywa chini ya utekelezaji wa miradi kwa mujibu wa Sheria, kanuni na miongozo iliyopo ili kuepusha upatikanaji wa watoa huduma ambao hawafai katika usambazaji wa bidhaa na utoaji wa huduma zinazotakikana katika miradi yaSerikali.

Mchanganuo wa watoa huduma hao ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 20: Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa**

| Nam | Jina la Mtoa Huduma | Huduma Inayotolewa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | RASHID M. SHARIF | Malipo yaliyofanywa kuhusiana na usaidizi wa mfumo kwa mfumo wa taarifa za uvuvi | 13,923,833 |
| 2. | Institute of Marine Sciences | Malipo kuhusiana na huduma za ush-auri kuhusu kipengele cha Oceano - graphic kinachoathiri samaki aina ya Jodari | 220,356,794 |
| 3. | Dar es salaam Merchant Group ltd | Malipo ya huduma za Ushauri kuchukua wasifu wa Kiuchumi wa Jodari kama rasilimali za Uvuvi | 117,387,738 |
| 4. | FT Technology (T) Limited | Malipo yaliyofanywa kuhusiana na matengenezo na usakinishaji wa programu ya leseni | 3,990,000 |
| 5. | Tanzania Fisheries Research Institute | Malipo yanayotolewa kwa asilimia 20 ya huduma za ushauri kwa ajili ya utafiti wa Biolojia na Ikolojia | 295,771,374 |
| 6. | TanWings Aviation (T) Ltd | Malipo kwa ajili ya kuwezesha ujumbe wa Doria ya Anga katika Ukanda wa Pekee wa Kiuchumi wa Tanzania | 352,887,976 |
| 7. | Mzumbe University | Malipo ya Kuwezesha awamu ya kwanza ya ailimia 20 ya huduma zaushauri kwa ajili ya Maendeleo ya Mpango wa Biashara wa Mamlaka ya | 185,497,866.67 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | baharikuu. | |
| **Jumla** | | | **1,189,815,582** |

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Mamlaka imepokea na kuridhishwa na hoja iliotolewa na Mkaguzi, Aidha kutokana na makubaliano rasmi baina ya Mamlaka na Benki ya dunia hakukua na kipengele kilichosisitiza maelezo ya hoja hii. Pamoja na hayo, kwa sasa Mamlaka inahakikisha kua manunuzi yote yanayofanyika yatazingatia utaratibu wa Sheria za Manunuzi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (TANePS) kupitia mfumo wa Pamoja na Serikali ya mapinduzi Zanzibar ili kuzuia uwezekano wa kujitokea hoja kama hiyo kwa kipindi kinachofata.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Baada ya Kamati kupata maelezo yanayohusiana na hoja hii kamati imebaini kuwa hakuna kipengele cha mkataba kinachoeleza Muongozo maalum wa kuwa Watoa huduma lazima wawe wamesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi kama Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za za Umma ya mwaka 2016 inavyoelekeza, hata hivyo kamati haikuridhishwa na majibu ya hoja hii kwani Wizara ilipaswa kufuata Sheria ya Manunuzi hata kama Mradi haukueleza kuwa Watoa huduma wawe wamesajiliwa.

Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa Wizara imechukua juhudi za kuandika barua kwa Mamlaka yenye kumbukumbu nambari CA 22/222/01/08 ya tarehe 23/09/2022 kwa ajili ya kuingizwa kwenye mfumo wa Manunizi wa TANePS ili kuepusha hoja kama hizi kujitokeza kwa kipindi kinachofuata. Kamati imepata fursa ya kukiona kielelezo hicho na kuridhika nacho.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaishauri Wizara ya Uchumi wa Buluu kuhakikisha kwamba Sheria za Manunuzi zinafuata hata kwenye miradi ya maendeleo ili kuepusha viashiria vya upotevu wa mali za umma na kuitia Serikali hasara.

**Hoja nambari 5.1.3.2: Mafanikio mabaya ya matokeo ya haraka ya mradi**

Kwa mujibu wa matokeo ya mradi (Project Result’s Matrix), ifikapo mwaka wa 6 wa kipindi cha mradi (yaani mwaka wa fedha 2020/2021) mradi ulitarajiwa kuwa umepata matokeo kadhaa ya haraka yenye lengo la kuwa na matokeo chanya katika uvuvi wa kipaumbeleuliochaguliwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa matokeo ya mradi yaliyoainishwa kwa mwaka wa 2020/2021 kama ilivyopatikana kutoka kitengo cha usimamizi

na ufuatiliaji kuwepo kwa mapungufu kati ya matokeo yanayotarajiwa ya mradi na matokeo halisi ya mradi ambapo inaonesha takwimu halisi ya utekelezaji wa malengo ya mradi ya kipindi cha miaka sita ambayo si ya kuridhisha, hali hiyo inaweza kuathiri utimilifu wa manufaa yanayotarajiwa katika uvuvi wa kipaumbele uliochaguliwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika miradi zinatekelezwa kwa mujibu wa mipango iliyopo ili kuweza kupata matokeo mazuri ya mradi kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mchanganuo wa mafanikio ya matokeo ya haraka ya mradi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 21: Mafanikio mabaya ya matokeo ya haraka ya mradi**

| Na | Viashiria | Malengo yaliyopangwa kwa kipindi cha miaka sita (6) | Utekelezaji halisi wa malengo kwa kipindi cha miaka sita (6) |
|---|---|---|---|
| 1. | Idadi ya wanufaika wa moja kwa moja wa mradi ambao asilimia kubwa ni wanawake | 65,000 | 1,000 |
| 2. | Hatua za usimamizi bora za uvuvi zilizochukuliwa kama matokeo ya usaidizi wamradi | 5 | 2 |
| 3. | Usimamizi wa ujuzi wa uvuvi wa uendeshaji | 12 | 3 |

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kamati ya PAC haikupokea majibu kuhusiana na hoja hii ipokuwa Wizara imeeleza kwamba matokeo ya Mradi huwa yanapimwa kwa ujumla wake na sio kuangalia eneo moja hasa ukizingatia Mradi huo unatekelezwa Tanzania nzima. Kwa mtazamo huo, Wizara imeifahamisha Kamati kwamba kuna mafanikio makubwa yamepatikana.

**Uchunguzi wa kamati ya PAC**

Licha ya Wizara kukanusha hoja ya Mkaguzi, hata hivyo Kamati imebaini kwamba takwimu zilizokuainishwa katika ripoti ya Mkadhibiti zilihusu Wizara ya Uchumi wa Buluu pekee ambapo zinaonesha wazi mafanikio yaliyopatikana haujafikia hata nusu ya mpango uliokuwepo. Kwa mnasaba huo, Kamati inakubaliana na hoja ya Mkaguzi kwamba mradi haukuwa na mafanikio mazuri.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ihakikishe shughuli zilizopangwa katika miradi zinatekelezwa kwa mujibu wa mipango iliyopo ili kuweza kupata matokeo mazuri ya mradi kwa maslahi ya wananchi wetu.

**MRADI WA MAMLAKA YA UVUVI WA BAHARI KUU ZANZIBAR (SWIOFish 1 - IDA)**

Mradi wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Zanzibar (South West Indian Ocean Fisheries - SWIOFish 1: IDA) ni programu yenye awamu 3 ya miaka 15 ambayo inasaidia ushirikiano wa kikanda wa usimamizi wa uvuvi ambao Tanzania iko katika kundi la kwanza la Nchi kupokea fedha. Mkataba wa ufadhili wa mradi kati ya Benki ya Maendeleo ya Kimataifa (Benki ya Dunia) na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulitiwa saini tarehe 12 Machi, 2015 na kuanza kutumika tarehe 22 Juni 2015 ambapo muda wa kukamilisha utekelezaji mradi ni 30 Septemba, 2022.

**Hoja nambari 5.2.3.1: Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na mamlaka ya ununuzi na uondoaji wa mali za umma shilingi 235,846,775 na USD 6,000**

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Namba 11 ya 2016, mtu, kampuni au taasisi haitashiriki katika manunuzi ya umma isipokuwa mtu huyo, kampuni au taasisi imesajiliwa kama msambazaji chini ya Sheria, vinginevyo kampuni hiyo imekataliwa na haitazingatiwa na taasisi ya ununuzi. Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Mradi ulifanya manunuzi kwa kutumia watoa huduma mbali mbali ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA) hali inayopelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi pamoja na gharama za usajili.

Ukaguzi unashauri uongozi wa mradi uhakikishe kuwa manunuzi yote yanafanyika kwa wazabuni waliosajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa mali za Umma ili kuepusha kufanya biashara na watoa huduma ambao hawaisaidii Serikali katika upatikanaji wa mapato. Mchanganuo wa malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 23: Malipo kwa Watoa huduma ambao hawakusajiliwa**

| Na | Jina la mtoa huduma | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs/USD) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Ena's Lik Decoration | Shilingi 2,500,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuwezesha gharama za kukodisha |
| 2. | Terabyte Solutions Co.Ltd | Shilingi7,369,600 | Malipo ya fedha kwa ajili ya vifaa vya uhamasishaji |
| 3. | Zeccon Company Limited | Shilingi 208,750,942 | Malipo ya fedha kwa ajili ujenzi wa Slipway kwa |
| 4. | Mohammed Kombo Maalim | Shilingi12,860,625 | Malipo ya huduma za ushauri katika Mtaalamu wa Ulinzi wa Mazingira |
| 5. | Salvatory Faustine Lyakurwa | Shilingi 4,365,608 | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma za ushauri |
| 6. | Zanzibar Telecom plc | Dola za Kimarekani 6,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma za mtandao |

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Mamlaka imepokea na kuridhishwa na hoja iliotolewa na Mkaguzi, Aidha kutokana na makubaliano rasmi baina ya Mamlaka na Benki ya dunia hakukua na kipengele kilichosisitiza maelezo ya hoja hii. Pamoja na hayo, kwa sasa Mamlaka inahakikisha kua manunuzi yote yanayofanyika yatazingatia utaratibu wa Sheria za Manunuzi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (TANePS) kupitia mfumo wa  Pamoja na Serikali ya mapinduzi Zanzibar ili kuzuia uwezekano wa kujitokea hoja kama hiyo kwa kipindi kinachofata.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Wizara imekiri kutokufuata Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Umma Na. 11 ya 2016, kama hoja ya Mkaguzi ilivyoeleza. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa baada ya Mkaguzi kumaliza ukaguzi wake Wizara imechukua juhudi za kuandika barua kwa Mamlaka, barua yenye kumb, na. CA 22/222/01/08 ya tarehe 23/09/2022 kwa ajili ya kuingizwa kwenye mfumo wa manunuzi wa TANePS ili kuepusha aina ya hoja kama hizi kujitokeza kwa kipindi kinachofata na kamati imepata fursa ya kuvikagua vielelezo hivyo na kuridhika navyo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri Wizara ya Uchumi wa Bluu kuhakikisha kwamba Sheria za Manunuzi zinafuata hata kwenye miradi ya maendeleo ili kuepusha viashiria vya upotevu wa mali za ummma na kuitia Serikali hasara.

**Haja Nambari 5.2.3.2: Kutokutekelezwa kwa baadhi ya shughuli za mradi USD 20,217**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya dola za Kimarekani 20,217 ni fedha ambazo zingepaswa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali za mradi lakini hadi ukaguzi unakamilika baadhi ya shughuli hizo hazikuweza kutekelezwa hali inayoweza kupelekea uwezekano wa kuongezeka kwa gharama zinazotokana na ongezeko la bei zavitu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mradi wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Zanzibar uhakikishe shughuli za mradi zilizopangwa zinafanyika kwa wakati kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa ili kufikia lengo la mradililililokusudiwa.

Mchanganuo wa baadhi ya Shughuli za mradi ambazo hazikutekelezwa ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 24: Kutokutekelezwa kwa baadhi ya shughuli za mradi**

| Namba ya shughuli ya mradi | Shughuli ya mradi | Kiasi cha fedha zilizotengwa (USD) |
|---|---|---|
| 4.2.3.7 | Tathmini ya mwisho (Bara, Zanzibar, Mamlaka ya bahari kuu) | 15,000 |
| 4.2.3.8 | Warsha za mashauriano | 5,217.39 |
| **Jumla** | | **20,217** |

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Uongozi umekubaliana na hoja ya Mkaguzi Pamoja na kukiri kua Warsha wa mashauriano na tathmini ya mwisho havikufanyika kwa wakati uliopangwa. Hii ilitokana na kuongezwa muda wa mradi kwa mwaka mmoja na shughuli hizo zilifanyika baada ya nyongeza wa muda huo

**Uchunguzi wa kamati ya PAC**

Wizara ya Uchumi wa Buluu imekiri kutokutekelezwa kwa baadhi ya Miradi kama hoja ya Mkaguzi ilivyoeleza. Kamati imeelezwa kuwa mradi ulitekelezwa baada ya mwaka mmoja kumaliza kwa mradi na tathmini ya mradi ilifanyika na matokeo yalipatikana. Kamati imepata fursa ya kuona nyaraka hizo na

kuridhika nazo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaushauri Uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Bluu kuwa makini katika kufuatilia Miongozo na Sheria zilizopangwa katika utekelezaji wa Miradi ili kuepusha Miradi mingi kutofanyika au kutomalizika kwa wakati uliopangwa.

**5.4 MRADI WA UHIFADHI WA ENEO LA KIHISTORIA LA MKAMANDUME PEMBA**

Mradi wa ujenzi wa maeneo ya kihistoria Mkamandume umetekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100. Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale – Zanzibar iliingia mkataba na kampuni ya Shamjo Company Limited kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha utoaji wa huduma pamoja na ukarabati wa maeneo ya kihistoria ya Mkamandume kwa kiasi cha shilingi 1,407,718,711 ambapo mkataba wa awali wenye kumbukumbu namba SMZ/JOI/W/RS/18/2018-2019 uliosainiwa tarehe 26/2/2019 ukiwa na thamani ya shilingi 529,409,124 pamoja na VAT.

Aidha, mkataba wa pili wenye kumbukumbu namba MZ/JOI/W/RS/21/2019-2020 uliosainiwa tarehe 14/10/2019 ukiwa na thamani ya shilingi 878,309,587 pamoja na VAT ulihusisha utekelezaji wa mradi huu katika vipindi vya awamu mbili tofauti kama ifuatavyo:-

Awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa nyumba ya utoaji wa huduma katika eneo la kihistoria la Mkamandume (facility building constraction) kwa gharama ya shilingi 367,496,913 pamoja na VAT na awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huo ilihusisha ukarabati wa eneo halisi la kihistoria la Mkamandume (Rehabilation of Mkamandume historical site) kwa gharama ya shilingi 507,812,674 pamoja na VAT.

**Hoja ya nambari 5.4.1.1: Kukosekana kwa daftari la kuhifadhia kumbukumbu za mali za kudumu**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba inamiliki mali mbali mbali za kudumu yakiwemo maeneo ya kihistoria katika kisiwa cha Pemba lakini daftari la kuhifadhia kumbu kumbu za mali hizo limekosekana kwa ukaguzi hali ambayo inapelekea kushindwa kuthibitisha uwepo na uhifadhi wa maeneo ya kihistoria katika kisiwa cha Pemba.

Kutokuwepo kwa daftari la kuhifandhia kumbukumbu za mali za kudumu ni kwenda kinyume na kifungu namba 29(2) cha sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unaanzisha na kulitumia daftari la kuhifadhia kumbukumbu za mali za kudumu kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo mbali mbali iliyopo.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Daftari la kutunzia mali za Serikali (Assets Register) kwa sasa Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ipo katika mchakato wa kulianzisha kwa Wizara na Taasisi zote za Serikali. Hata hivyo, Eneo hili limerikodiwa katika orodha ya maeneo 86 ya Kihistoria katika mwaka 1943 na kutangazwa Rasmi katika Gazeti la Serikali. Orodha ya maeneo ya Kihistoria inapatikana Wizarani.

Eneo hili limeshapimwa, michoro ya eneo ipo tayari, kinachosubiriwa ni kulipwa fidia kwa vipando vya Wananchi ili Wizara iweze kuomba kutengenezewa Hatim iliki na Wizara husika.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba ni kweli alipopita Mkaguzi Wizara ya Utalii na mambo ya Kale - Pemba haikuwa na daftari la kuhifadhia mali za Serikali kama ilvyoelezwa katika hoja ya Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa hivi sasa daftari hilo lipo na limejazwa ipasavyo. Kwa mnasaba huo, hoja hiyo imetekelezwa ipasavyo na Kamati haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja ya nambari 5.4.1.2: Kukosekana kwa vielelezo vya ulipwaji wa kodi ya VAT kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRB) Shilingi 56,058,851.**

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba imeingia mkataba na Shamjo Company Ltd kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha utoaji wa huduma katika maeneo ya kihistoria Mkamandume kwa mkataba nambari SMZ/JOI/W/RS/21/2019-2020 wa tarehe 14/10/2019. Kwa mujibu ya makubaliano ya mkataba na Bill of Quantity (BOQ), malipo ya kodi ya 18% VAT kwa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) ni shilingi 56,058,851 kutoka shilingi 311,438,062 za gharama ya ujenzi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebanika kukosekana kwa vielelezo vyenye jumla ya shilingi 56,058,851 ambazo zimelipwa kwa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa ajili ya ulipaji wa kodi ya ongezeko la thamani VAT itokanayo na ujenzi wa kituo cha utoaji wa huduma katika eneo la kihistoria Mkamandume. Hali iliyopelekea kufanya maombi ya vielelezo hivyo kwa barua yenye kumbu kumbu namba AUD/PUMK.IV/VOL.2 ya tarehe 16/12/2021 kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Pemba hata hivyo vielelezo husika havikuweza kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika yanaambatanishwa na vielelezo vya malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Mchanganuo wa malipo yasiyokuwa na vielelezo ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 27: Malipo ya kodi ya VAT yasiokuwa na vielelezo**

| Na | Maelezo | Kiasi cha fedha Kilicholipwa (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1 | Substructure | 37,309,000.00 |
| 2 | Frames | 18,344,600.00 |
| 3 | Walls and Partitions | 26,130,000.00 |
| 4 | Roofs | 41,228,000.00 |
| 5 | Doors | 11,100,000.00 |
| 6 | Windows | 10,600,000.00 |
| 7 | Finishes | 27,448,500.00 |
| 8 | Painting and decoration | 8,752,000.00 |
| 9 | Plumbing and drainage installation | 51,130,000.00 |
| 10 | Electrical installation | 23,235,000.00 |
| | Jumla ndogo (A) | 255,771,100.00 |
| 11 | Preliminaries (2% of sub total a) | 5,105,542.00 |
| 12 | Allow for 10% of sub total a as consultancy fee | 25,527,710.00 |
| 13 | Allow for provision sums for works unforeseen that could occur during implementation of the construction works (10% of sub total a) | 25,527,710.00 |
| | **Jumla ndogo (B)** | **311,438,062.00** |
| 14 | **Kodi ya asilimia 18 ya jumla ndogo (B)** | **56,058,851.00** |

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Vielelezo vya malipo ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa ZRB yaliyolipwa, viliwasilishwa kwa Mkaguzi wakati anafanya ukaguzi wake mwaka husika wa Ukaguzi.

Hata huvyo, vilelezo hivyo vipo kwa kujiridhisha. Malipo ya Ongezeko la Thamani yanalipwa baada ya kuwasilishwa maombi ya Malipo na Mkandarasi kupitia IPC kwa mujibu wa kazi ilifofanywa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika ufuatiliaji wa hoja hii, Kamati imebaini kuwa wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake ya ukaguzi katika eneo hilo la kihistoria la Mkamandume, hakupatiwa vielelezo na kuelezwa kwamba vielelezo hivyo vipo Unguja wakati kiuhalisia shughuli hiyo imetekelezwa Pemba. Kamati ya PAC imegundua kuwa kuna uzembe umejitokeza uliosababishwa na baadhi ya watendaji wa kutompatia Mkaguzi vielelezo wakati kiuhalisia vilikuwepo. Hilo limeonesha wazi kwamba watendaji hawakumpatia Mkaguzi ushirikiano wa karibu katika utekelezaji wa majukumu yake. Hata hivyo, Kamati ilifuatilia Unguja vielelezo hivyo na kubahatika kuviona isipokuwa kodi iliyoelezwa ililipwa kwa ujumla jumla.

Kamati ilipitia risiti nambari 54515 ya tarehe 24/6/2020 ambapo jumla ya Tzs. 47,045,926 ilikatwa kodi wakati risiti nambari 40819 ya tarehe 31/5/2019 jumla ya shilingi 238,036,750 ilikatwa kodi. Katika uchunguzi wake, Kamati ilibaini risiti hizo hakuziona Mkaguzi wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ihakikishe vielelezo vya Miradi inayotekelezwa Pemba vinakuwepo Pemba ili vikihitajika viweze kupatikana kwa wakati.

2. Watendaji wa Wizara ya Utalii na Mambo ya kale - Pemba wahakikishe wanashirikiana ipasavyo na Mkaguzi na kumpatia vielelezo anavyohitaji ili kuepusha hoja zenye majibu kuingia katika kitabu.

3. Watedaji wa kitengo cha fedha wawe wanawakata kodi ya ongezeko watoa huduma wote wanaowatumia ili kodi ya Serikali isiweze kupotea.

**Hoja ya nambari 5.4.1.3: Kukosekana kwa Taarifa za Malipo ya Mshauri Elekezi shilingi 25,527,710**

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba imeingia mkataba na Shamjo Company Ltd kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha utoaji wa huduma katika eneo la kihistoria la Mkamandume kwa mkataba nambari SMZ/JOI/W/RS/21/2019-2020 wa tarehe 14/10/2019.

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba AUD/PUMK.IV./VOL.2 ya tarehe 16/12/2021 iliyoitaka Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuwasilisha taarifa za malipo yote yaliyotumika kwa mradi wa maeneo ya

kihistoria Mkamandume katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Pemba kwa ukaguzi lakini taarifa hizo hadi ukaguzi unakamika hazikuweza kuwasilishwa hivyo kutia shaka juu ya malipo ya shilingi 25,527,710 ya mshauri elekezi yaliyofanyika. Kukosekana kwa taarifa za malipo ya mshauri elekezi kwa ukaguzi ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuhakikisha kwamba taarifa zote zinazotokana na malipo yaliyofanyika zinaambatanishwa katika hati za malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara haikuwa na Mkataba baina yake na Mshauri Elekezi. Hivyo, Wizara haikumlipa Mshauri Elekezi kwa kazi hiyo. Malipo ya Mshauri Elekezi yalifanywa moja kwa moja na Mkandarasi. Hata hivyo, ushauri uliopendekezwa unazingatiwa kwa Miradi ijayo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba haikuwa na Mkataba wa moja kwa moja na Mshauri Elekezi isipokuwa walikuwa wakitumia wataalamu wao wa ndani kama ndio Washauri Elekezi jambo ambalo halikutakiwa kufanyika kwa utaratibu huo kwa vile fedha za Mradi huo zilikuwa nyingi na hatimae kusababisha usimamizi usioridhisha katika utekelezaji wa Mradi huo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ihakikishe inapotekeleza Miradi yenye fedha nyingi, inaingia Mkataba na Mshauri Elekezi aliyekuwepo nje ya Ofisi ili inapotokezea kasoro yoyote itakuwa rahisi kurekebisha au kumpeleka Mahakamani.

**Hoja ya nambari 5.4.1.4: Kukosekana kwa Taarifa za Uhifadhi wa fedha za mfuko wa Dharura (Unforeseen Event Fund) shilingi 25,527,710**

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba imeingia mkataba na Shamjo Company Ltd kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha utoaji wa huduma katika eneo la kihistoria la Mkamandume kwa mkataba nambari SMZ/JOI/W/RS/21/2019-2020 wa tarehe 14/10/2019.

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba AUD/PUMK.IV./VOL.2 ya tarehe 16/12/2021 iliyoitaka Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale - Pemba kuwasilisha taarifa za malipo yote yaliyotumika kwa mradi wa maeneo ya

kihistoria ya Mkamandume katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali - Pemba kwa ukaguzi lakini taarifa hizo hadi ukaguzi unakamilika hazikuweza kuwasilishwa, hivyo kutia shaka juu ya matumizi ya shilingi 25,527,710 pamoja na utaratibu uliotumika katika uhifadhi na utumiaji wa fedha za Mfuko wa dharura. Kukosekana kwa taarifa za malipo ya mshauri elekezi kwa ukaguzi ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuhakikisha kwamba taarifa zote zinazotokana na malipo yaliyofanyika zinaambatanishwa katika hati za malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Fedha hizo zimetumika katika kazi za "Variations" zikiwemo ujenzi wa barabara ya kifusi iendayo eneo la Mkamandume kutoka barabara kuu hadi "site" kwa kuitia kifusi ili iweze kupitika. Barabara hiyo haikuweka katika kazi za awali za mradi huo. 'Final Payment Certificate" inaainisha mchanganuo wa malipo hayo. Tafadhali angalia ukurasa namba 6 kipengele (a). Hata hivyo, ushauri wa Mkaguzi tumeupokea.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Wizara kutumia shilingi 25,527,710 kwa ajili ya ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha kifusi lakini Kamati imebaini kuwa watendaji wa Wizara hawakuwasilisha vielelezo vya taarifa ya matumizi ya fedha hizo jambo ambalo linatia shaka katika uhalali wa matumizi yako. Aidha, watendaji wa Wizara hawakufanya upembuzi yakinifu kutambua nini Mradi unahitaji kabla ya kuanza utekelezaji wa Mradi huo. Hili limetokana na Wizara kushindwa kupanga fedha katika hatua ya awali ya ujenzi wa barabara itakayotumika kufikia katika eneo hilo la kihistoria.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Watendaji wa Wizara wawe makini hususan wanapoandaa mahitaji yanayotakiwa kutekelezwa na Mradi kabla ya kuanza utekelezaji wa Mradi huo.
2. Watendaji wa Wizara wahakikishe wanaambatanisha vielelezo vya matumizi mara tu wanapomaliza kufanya matumizi hayo.

**Hoja ya nambari 5.4.1.5: Kutokulingana kwa bei ya ununuzi wa vifaa ukilinganisha na bei halisi ya sokoni shilingi 30,260,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba ilifanya malipo yenye jumla ya shilingi 30,260,000 kwa ajili ya

ununuzi ya vifaa mbali mbali vya ujenzi wa kituo cha kutolea huduma kilichojengwa katika eneo la Mkamandume lakini manunuzi ya vifaa hivyo hayakuzingatia thamani halisi kwa wakati huo ambapo imebainika kwamba vifaa hivyo vingeweza kununuliwa kwa jumla ya shilingi 15,160,000 na kupelekea kupunguwa kwa gharama za jumla kwa thamani ya shilingi 15,100,000 ambazo zingeweza kutumika kwa ajili ya kazi nyengine.

Kufanya hivyo inapelekea uwepo wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali yasiyozingatia hali ya uchumi, ufanisi na malengo halisi ya utekelezaji wa mradi ambapo ni kwenda kinyume na kifungu 5(1) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021. Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba ukishirikiana na kamati ya ufundi ya tathmini ya zabuni (technical evaluation committee) kuhakikisha kwamba upembuzi yakinifu unafanyika ili kuweza kupata taarifa sahihi za bei za vifaa vinavyohitajika katika utekelezaji wa mradi kwa lengo la kuepusha manunuzi ya vifaa kwa bei za juu ikilinganishwa na bei halisi zinazopatikana sokoni katika kipindi cha wakati husika. Mchanganuo wa ununuzi wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 28: Kutokulingana kwa bei ya ununuzi wa vifaa ukilinganisha na bei halisi ya sokoni**

| Na | Aina ya Kifaa | Idadi | Jumla ya fedha zilizolipwa (Tshs.) | Jumla ya fedha kwa bei ya soko (Tshs.) | Tofauti ya Jumla (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Main Switch | 1 | 480,000 | 100,000 | 380,000 |
| 2 | Mfenesi (5,000 ltrs) | 6 | 1,080,000 | 660,000 | 420,000 |
| 3 | Madirisha (1500 x 1700 mm) | 2 | 7,000,000 | 2,400,000 | 4,600,000 |
| 4 | Simtank (5,000 ltrs) | 4 | 4,800,000 | 2,400,000 | 2,400,000 |
| 5 | Madirisha (1500 x 700 mm) | 6 | 3,000,000 | 1,800,000 | 1,200,000 |
| 6 | Madirisha (800 x 700 mm) | 8 | 2,800,000 | 1,200,000 | 1,600,000 |
| 7 | Milango (1000 x 2600 mm) | 2 | 1,900,000 | 1,400,000 | 500,000 |
| 8 | Milango (900 x 2600 mm) | 4 | 3,600,000 | 2,000,000 | 1,600,000 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 9 | Milango (750 x 2600 mm) | 8 | 5,600,000 | 3,200,000 | 2,400,000 |
| **Jumla** | | | **30,260,000** | **15,160,000** | **15,100,000** |

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Mradi huu umetekelezwa kupitia mfumo wa zabuni na sio "Quotation". Kwenye zabuni vifaa husika vinazingatia mambo yafuatayo kwa mujibu wa Mkataba huu; CGG Clause 40.1 (Bill of Quantity) inazingatia kama hivi ambapo kununua "main swicth" lazima yafanyike yafuatayo; Construaction, istallation, testing, commissioning na ipo clause inayosema kutoka katika mkataba huu inayosema kuwa "employer has accepted the tender by the contractor for the execution and completion of such works and the remedying of any defects therein…"

Ambapo GCC Clause 38.1 (correction of defects) ya makataba husika, marekebisho yanatakiwa kufanyika hadi mwisho wa Defects Liability Period (DLP). Aidha, kazi hii imetekelezwa kwa kuzingatia "Terms and Conditons of Contract".

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika uchunguzi wa hoja, Kamati ya PAC ililazimika kupata usaidizi kutoka kwa Mhandisi wa Baraza la Wawakilishi na kueleza kwamba hata kama kutakuwa na utofauti wa bei lakini tofauti hiyo isizidi nusu ya asilimia ya ununuzi wa vifaa husika. Aidha, aliendelea kueleza kuwa hilo la bei kubwa zaidi kupita kiasi limetokana na Wizara kutomtumia Mshauri Elekezi wa wa Majengo ya Serikali (ZBA). Kwa mnasaba huo, kuna uzembe mkubwa uliofanywa na watendaji wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale - Pemba wa kutomtumia Wakala huyo na kusababisha makisio ya bei kupanda mara dufu.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ihakikishe inamtumia Wakala wa Majengo Zanzibar kama ni Mshauri Elekezi ili kuepusha matumizi ya bei za vifaa isiyokuwa na ulazimu.

**Hoja ya nambari 5.4.1.6: Kutokuonekana kwa vifaa vilivyonunuliwa shilingi 15,130,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba mkandarasi wa ujenzi alifanya manunuzi ya vifaa vyenye thamani ya shilingi 15,130,000 ambavyo vilikusudiwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kituo cha utoaji wa huduma katika eneo la kihistoria la Mkamandume lakini vifaa

hivyo havikuonekana kwa ajili ya ukaguzi. Kufanya hivyo kunapelekea uwezekano wa kuwepo kwa upotevu wa vifaa vilivyonunuliwa hali inayopelekea kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa mali pamoja na bidhaa zilizonunuliwa ambapo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuhakikisha kwamba vifaa vyote vinavyonunuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi vinakuwepo na kutumika kama ilivyoainishwa katika mkataba wa ujenzi kwa lengo la kufanya matumizi ya vifaa yanayoendana na hali ya uchumi, ufanisi na malengo halisi ya utekelezaji wa mradi. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 29: Vifaa vilivyonunuliwa ambavyo havikuonekana**

| Na | Aina ya Kifaa | Idadi ya vifaa vilivyonunuliwa | Idadi ya vifaa vilivyoonekana | Tofauti ya vifaa ambavyo havikuonekana | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Security Light | 10 | 0 | 10 | 430,000.00 |
| 2 | Milango ya Mbao | 14 | 9 | 5 | 5,150,000.00 |
| 3 | Madirisha | 18 | 11 | 7 | 2,550,000.00 |
| 4 | Simtank (5,000 ltrs) | 2 | 0 | 2 | 7,000,000.00 |
| **Jumla** | | | | | **15,130,000.00** |

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Vifaa hivyo vipo vikiwemo matangi mawili (2) ya Maji ambayo yamewekwa juu ya Jengo la kutolea huduma na kusambaza maji hayo ndani ya Jengo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba kutokana na kukosekana kwa ushirikiano wa watendaji na Mkaguzi, kumepelekea vifaa hivyo Mkaguzi kushindwa kuviona. Hata hivyo, Kamati imefanikiwa kuviona vifaa husika na vinaendelea kufanya kazi. Hivyo, Kamati imewasisitiza watendaji wa Wizara kushirikiana ipasavyo na Mkaguzi anapofika katika maeneo yao kutekeleza majukumu yake.

**Hoja ya nambari 5.4.1.7: Dosari iliyobainika katika uchimbaji wa msingi wa upitishaji wa maji chumvi pamoja na ujenzi wa ukuta shilingi 350,371,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 350,371,000 zimetumika kwa ajili ya uchimbaji wa msingi wa upitishaji wa maji chumvi pamoja na ujenzi wa kuta pembezoni mwa msingi huo katika eneo la kihistoria la Mkamandume kwa lengo la kuwezesha maji chumvi kuingia na kutoka katika msingi huo ili kuonyesha uhalisia wa kihistoria wa eneo la Mkamandume lakini dosari iliyobainika ni kwamba lengo lililokusudiwa halikufi kiwa kutokana na kutokuingia na kutoka kwa maji hayo kama ilivyokuwa katika muonekano wa asili wa eneo hilo pamoja na makubaliano katika mkataba wa ukarabati wa eneo la kihistoria la Mkamandume.

Katika kufanya ufuatiliaji wa uchimbaji wa msingi wa upitishaji wa maji chumvi pamoja na ujenzi wa kuta pembezoni mwa msingi huo imebainika kwamba gharama zilizotumika ni kubwa na hivyo kutokuendana na thamani halisi ya kazi iliyofanyika kwa kutokuzingatiwa kwa hali ya uchumi, ufanisi wa kazi iliyokusudiwa pamoja na malengo halisi yaliyopangwa katika utekelezaji wa mradi huo. Kufanya hivyo kunapelekea uwezekano wa kuwepo kwa upotevu wa fedha za Serikali hali inayopelekea kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha ambapo ni kwenda kinyume na kifungu 5(1) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuhakikisha kwamba malengo yaliyopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi yanasimamiwa na kutekelezwa kama ilivyoainishwa katika mkataba wa ujenzi kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar na Taifa kwa ujumla. Hali halisi ya utekelezaji wa mradi katika eneo lililokusudiwa kuingia na kutoka kwa maji chumvi ni kama inavyoonekana hapo chini:-

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Lengo la kujenga mtaro huu ni kuonesha hali halisi ilivyokuwa ikitumiwa na Mkamandume kutoka Baharini na kuja katika eneo lake. Kuruhusu maji hayo kuingia na kutoka kama ilivyokuwa hapo awali kunaweza kupelekea maafa kwa majirani wa eneo hili.

**Uchunguzi waKamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba Mradi wa ujenzi wa njia ya maji uliamuliwa kufanyika bila ya kufanya tathmini ya athari za kimazingira ambazo zingeweza kutambua kwa namna gani ujenzi wake utakuwa rafiki na mazingira. Kwa kuzingatia hilo, kamati ya PAC haikuridhishwa na majibu ya Wizara na kusisitiza kwamba bado hoja hiyo haijajibika.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Ili kupunguza uwezekano wa kujitokeza majanga mbali mbali yanayohusiana na mazingira, Kamati inaitaka Wizara kabla ya kutekeleza miradi mikubwa kama hio, ni lazima ifanye tathmini ya athari ya kimazingira itakayosaidia kujitokeza matokeo mabaya na kupelekea fedha za Serikali kupotea bila tija.

**Hoja ya nambari 5.4.1.8: Dosari iliyobainika katika malipo ya fedha za ukarabati wa kisima cha wivu shilingi 116,661,400**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 116,661,400 zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa kisima cha wivu katika eneo la kihistoria la Mkamandume ili kuboresha muonekana mzuri na halisi wa kisima hicho lakini dosari iliyobainika ni kwamba thamani halisi ya fedha zilizotumika katika ukarabati wa kisima hicho hailingani na hali halisi ya kisima kilichofanyiwa ukarabati. Katika kufanya ufuatiliaji wa ukarabati huo imebainika kwamba gharama zilizotumika ni kubwa na hivyo kutokuendana na thamani halisi ya ukarabati uliofanyika kwa kutokuzingatiwa kwa hali ya uchumi, ufanisi wa kazi iliyokusudiwa pamoja na malengo halisi yaliyopangwa katika utekelezaji wa mradi huo Kufanya hivyo kunapelekea uwezekano wa kuwepo kwa upotevu wa fedha za Serikali hali inayopelekea kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha ambapo ni kwenda kinyume na kifungu 5(1) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuhakikisha kwamba utekelezaji wa ukarabaiti wa eneo husika unafanyika kulingana na uhalisia kwa mujibu wa mipango na malengo yaliyokusudiwa kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar na Taifa kwa ujumla. Hali halisi ya utekelezaji wa mradi katika eneo lililokusudiwa la ukarabati wa kisima cha wivu ni kama inavyoonekana hapo chini:-

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Kama inavyoeleweka kwa matengenezo ya Maeneo ya Kihistoria ni gharama kubwa ukilinganisha na gharama za ujenzi mpya wa nyumba za kawaida, kwani kinachozingatiwa ni thamani ya kitu na si gharama ya kitu kwa mfano ukarabati wa Beit - el - ajab na Jengo la ZURA.

**Uchunguzi waKamati ya PAC**

Katika kufuatilia ukweli wa maelezo ya hoja hii, Kamati ilitaka kujua ni kitu gani ambacho kilifanya gharama za ujenzi kuongezeka maradufu na kuelezwa kwamba kazi iliyofanyika katika kisima hicho ilifanywa kwa takriban kwzmiezi miwili kwa kuchimba eneo hilo kwa kutumia kijiko cha kujengea ili uhalisia wa eneo usiweze kuathiriwa ababo jumla ya wafanyakazi 10 walitumika kutekeleza kazi hiyo. Aidha, Kamati pia ilitaka kujua kwanini mkaguzi

hakuridhika na majibu ya Wizara na kubaini kwamba Wizara haikuandaa kumbukumbu na mchanganuo wa utekelezaji wa kazi hiyo. Hivyo, Mkaguzi alishindwa kufahamu malipo hayo yalitolewa kwa uhalali gani.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

Wizara inapofanya matumizi hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ihakikishe inaandaa na kuhifadhi vizuri mchanganuo na vielelezo vya hazi husika.

**Hoja ya nambari 5.4.1.9: Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 80,757,324**

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale - Pemba imeingia mkataba na Shamjo Company Ltd kwa ajili ya uchimbaji wa msingi wa upitishaji wa maji chumvi pamoja na ujenzi wa kuta pembezoni mwa msingi huo katika eneo la kihistoria la Mkamandume kwa mkataba nambari SMZ/JOI/W/RS/18/2018/2019 wa tarehe 26/02/2019. Katika ukaguzi uliofanyika imebaika kukosekana kwa vielelezo vyenye jumla ya shilingi 80,757,324 ambazo zimelipwa kwa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa ajili ya ulipaji wa kodi ya ongezeko la thamani VAT itokanayo na uchimbaji wa msingi pamoja na ukarabati wa ukuta katika eneo la kihistoria Mkamandume.

Kutokana na hali hiyo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Pemba ilifanya juhudi maalumu katika kuhakikisha kwamba vielelezo vyote muhimu vinapatikana kwa kuandika barua rasmi yenye kumbu kumbu namba AUD/PUMK.IV/VOL.2 ya tarehe 16/12/2021 lakini pamoja na juhudi hizo vielelezo husika havikuweza kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika yanaambatanishwa na vielelezo vya malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Mchanganuo wa malipo yasiyokuwa na vielelezo ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Vielelezo vya malipo ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa ZRB yaliyolipwa, viliwasilishwa kwa Mkaguzi wakati anafanya ukaguzi wake mwaka husika wa Ukaguzi.

Malipo kwa Mkandarasi yanalipwa kwa mujibu wa maombi kutoka kwa Mkandarasi baada ya kumaliza kazi husika (IPC). Hata hivyo, vilelezo hivyo vipo kwa kujiridhisha.

**Jadweli Nambari 30: Malipo ya kodi ya VAT yasiokuwa na vielelezo**

| **Na** | **Maelezo** | **Kiasi cha fedha kiliocholipwa (Tshs.)** |
|---|---|---|
| 1 | Side walls old fort | 183,950,000 |
| 2 | Jelous well | 20,710,000 |
| 3 | Historical stair case | 8,472,000 |
| 4 | Artificial sea channel | 172,200,000 |
| 5 | Signposts | 4,800,000 |
| 6 | Jumla ndogo (A) | 390,132,000 |
| 7 | Allow for proviosonal sums for works unforeseen that coud occure during implementation of the renovation works. | 58,519,800 |
| | Jumla ndogo (B) | 448,651,800 |
| 8 | Kodi ya asilimia 18 ya jumla ndogo (B) | 80,757,324 |
| **Jumla Kuu** | | **529,409,124.00** |

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba uchunguzi na mapendekezo ya hoja hii yanafanana na hoja ya nambari 5.4.1.1. kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC haikuwa na maelezo zaidi.

**Hoja ya nambari 5.4.1.10: Udhibiti na utunzaji wa majengo usioridhisha**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika udhibiti na utunzaji wa majengo yaliyomo katika eneo la kihistoria la Mkamandume hauridhishi ambapo majengo hayo yameonekana kutokuwa katika hali nzuri na baadhi ya majengo hayo kuanguka hali ambayo imepoteza uhalisia na historia ya majengo halisi katika eneo la Mkamandume. Kutokuyatunza vizuri majengo hayo kunaweza kupelekea kukosekana kwa umadhubuti, kuanguka, kushuka thamani na hatimaye kukosekana kwa tija iliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na uingiaji wa watalii katika maeneo hayo kwa lengo la kuona na kujifunza historia ya Mkamandume.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Ukaguzi unashauri uongozi wa

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuhakikisha kwamba malengo yaliyopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi yanasimamiwa na kutekelezwa kama ilivyoainishwa katika mkataba wa ujenzi kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar na Taifa kwa ujumla. Aidha, ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba kuhakikisha unayatangaza maeneo ya utalii wa ndani pamoja na utalii wa nje ili kuhakikisha kunapatikanwa kwa mapato ambayo yatasaida kufanya ukarabati wa majengo kwa lengo la kuhakikisha historia ya utalii inabakia katika uhalisia wake kwa maslahi ya vizazi vijavyo. Hali halisi ya maeneo ya kihistoria yanavyoanguka na kupoteza taswira ya uwepo wake bila ya kufanyiwa ukarabati kwa muda mrefu ni kama inavyoonekana hapo chini:-

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara imepokea ushauri wa Hoja ya Mkaguzi, Aidha tutaifanyia kazi na kuona kuwa Majengo yapo katika hali nzuri sambamba na kulitangaza eneo hili. Aidha, Picha ya Jengo linaloonekana ni Jengo la Muda (temporary shade) lililotumiwa na Mkandarasi wakati wa ujenzi huo, hivyo halikuwa sehemu ya mradi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Kamati ilifanikiwa kufika katika eneo la kihistoria la mkandume na kufanikiwa kulitembelea eneo hilo na kujionea majengo hayo yakiwa katika hali nzuri na yanarisha. Hali hiyo ilitokana na Wizara kuchukua juhudi za kuyafanyika matengenezo majengo yaliopo katika eneo hilo. Hata hivyo, Kamati imesisitiza Wizara kupanga bajeti maalum kwa ajili ya kumudu kuyafanyia matengenezo majengo hayo na kuyaweka katika hali yake inayostahiki.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara iandae Mpango Maalum wa Bajeti yake itakayokuwa ikitumika kwa ajili ya matengenezo na uimarishaji wa majengo yaliyopo katika eneo hilo.

**Hoja ya nambari 5.4.1.11: Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 77,462,950**

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba imeingia mkataba na Shamjo Company Ltd kwa ajili ya ukarabati wa eneo la kihistoria la Mkamandume kwa Mkataba nambari SMZ/JOI/W/RS/21/2019-2020 wa tarehe 14/11/2019. Katika ukaguzi uliofanyika imebaika kukosekana kwa vielelezo vyenye jumla ya shilingi 77,462,950 ambazo zimelipwa kwa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa ajili ya ulipaji wa kodi ya ongezeko la thamani VAT itokanayo na ukarabati wa eneo la kihistoria la Mkamandume. Kutokana na hali hiyo Ofisi ya Mdhibiti

na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Pemba ilifanya juhudi maalumu katika kuhakikisha kwamba vielelezo vyote muhimu vinapatikana kwa kuandika barua rasmi yenye kumbukumbu namba AUD/PUMK.IV/VOL.2 ya tarehe 16/12/2021 lakini pamoja na juhudi hizo vielelezo husika havikuweza kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika yanaambatanishwa na vielelezo vya malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.Mchanganuo wa malipo ya kodi yasiyokuwa na vielelezo ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

| **Na** | **Maelezo** | **Kiasi cha fedha kiliocholipwa (Tshs.)** |
|---|---|---|
| | Jumla Ndogo (A) | 341,547,422 |
| 1 | Preliminaries (3% of subtotal) | 10,246,422 |
| 2 | Allow for 8% of subtotal 1 as consultancy fee | 27,323,792 |
| 3 | Prime cost and Provisional sums for works unforeseen that could occur during implementation of the renovation works sub total 1 | 51,232,110 |
| | Jumla Ndogo (B) | 172,200,000 |
| 5 | Asilimia 18 ya kodi ya VAT ya jumla ndogo (B) | 430,349,724 |
| | **Jumla Kuu** | **507,812,674** |

## Majibu ya Uongozi wa Wizara

Vielelezo vya malipo ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa ZRB yaliyolipwa, viliwasilishwa kwa Mkaguzi wakati anafanya ukaguzi wake mwaka husika wa Ukaguzi. Malipo kwa mkandarasi yanalipwa kwa mujibu wa maombi kutoka kwa Mkandarasi baada ya kumaliza kazi husika (IPC). Hata huvyo, vilelezo hivyo vipo kwa kujiridhisha.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Watendaji wa Wizara kukanusha kwa kueleza kwamba walimpatia vielelezo Mkaguzo vinavyoonesha ulipwaji wa kodi lakini Kamati ya PAC imebaini kuwa vielelezo hivyo havikuwa na alama yoyote iliyoonesha kwamba Mkaguzi ameviona vielelezo vilivyowasilishwa mbele ya Kamati. Hivyo kamati haikuridhika na majibu yaliyowasilishwa.

**Moani, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Wizara wanatakiwa kutoa mashirikiano kwa Mkaguzi ili hoja kama hii isiweze kujirudia.

**MRADI WA UJENZI WA JENGO LA MAMA NA MTOTO HOSPITALI YA CHAKE CHAKE - PEMBA**

**Hoja nambari 6.3.1.1: Kutokutayarisha na kuwasilisha taarifa za hesabu za Miradi**

Kwa mujibu wa kifungu Nambari 119(1) cha sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016 inawataka Wakuu wa Taasisi kutayarisha taarifa za mapato na matumizi na kuziwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kukamilika kwa matumizi.

Ukaguzi umebaini Wizara ya Afya imetekeleza Miradi wa Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto Hospitali ya Chake Chake ambapo kwa mujibu wa taratibu za kisheria Wizara ilitakiwa kutayarisha na Kuwasilisha Taarifa za matumizi zinazohusiana na utekelezaji wa mradi huo kwa lengo la kukaguliwa na kutolewa ushauri wa kitaalamu.

Hadi ukaguzi unakamilika taarifa hizo hazikuwasilishwa jambo ambalo limenyima fursa ya kuweza kufahamu fedha halisi iliyopatikana na kutumika katika shughuli za uendeshaji na utekelezaji wa mradi huo.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Taarifa za hesabu za Miradi, mapato na matumizi yameainishwa katika ripoti kuu ya Hesabu ya Wizara (Final Account) ambayo imewasilishwa kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar. Final Account ya Wizara ya Mwaka 2020/2021

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika uchunguzi wa hoja, Kamati ya PAC imebaini mmbo yafuatayo:-
ni kweli Hesabu ya mwisho wa wa mwaka iliwasilishwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali lakini haikuwa na taarifa ya mapato na matumizi ya Mradi huu wa Ujenzi wa Hospitali ya Mama na Mtoto wa Chake chake.

1. Watendaji wa Wizara hawakuwa wakitoa ushirikiano unaotakiwa kwa Wakaguzi kwani imebaini walipokuwa wakiuliza kuhusu taarifa za fedha za Mradi waliambiwa kwamba majibu yake yapo Unguja wakati wanaelewa kuwa wao ndio watekelezaji wa Mradi huo walitakiwa kuwa na vielelezo hivyo. Kwa mnasaba huo, Kamati imegundua kulikuwa na uzembe uliofanywa na watendaji wa Wizara kwa kutokufuatilia vielelezo vilivyohitajika na kuviwasilisha kwa Mkaguzi ndani ya wakati wa ukaguzi.
2. Kuwepo kwa utunzaji usioridhisha wa kumbukumbu za Ofisi. Hili limebainika baada ya Mkaguzi kufika katika eneo la ukaguzi na alipohitaji taarifa hizo hakuweza kupatiwa. Kwa vile Ofisi ya Afisa Mdhamini ya Wizara ya Afya ndio watekelezaji wa Mradi walitakiwa kuwa na taarifa hizo ambazo wamezihifadhi katika Ofisi zao. Hatimae, hadi ukaguzi unakamilika, Mkaguzi hakupatiwa taarifa hizo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Ofisi ya Afisa Mdhamini wa Wizara ya Afya inapotekeleza Mradi ihakikishe inaziingiza taarifa za mradi huo ndani ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ili taarifa zake ziweze kukaguliwa.
2. Wizara ihakikishe inaandaa mazingira mazuri yatakayoiwezesha Ofisi ya Afisa Mdhamini inahifadhi taarifa zake ipasavyo na zinaweza kupatikana zinapohitajika.

3. Watendaji wa Ofisi ya Afisa Mdhanimi wahakikishe wanatoa ushurikiano unaotakiwa kwa Mkaguzi ili aweze kutekeleza majukumu yake kwa urahisi.

**Hoja nambari 6.3.1.2: Kuwepo kwa ucheleweshwaji wa Malipo**

Katika dosari hiyo imebainika kujitokeza kwa kasoro ya ucheleweshwaji wa upatikanaji wa malipo kwa mujibu wa barua yenye R/MOH/CMCH/18 ya tarehe 28/5/2021 iliyotolewa na Mkandarasi kwenda kwa Wizara ilionesha madai ya kuomba kulipwa fedha hizo. kwa mujibu wa ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 632,752,504.06 zimelipwa kwa certificate tatu za awali.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Ni kweli kulikuwa na ucheweleshwaji wa malipo, hali hii ilitokana na ucheleweshwaji wa kuingiziwa fedha za Maendeleo kutoka Hazina. Barua kutoka Tume ya Mipango ya tarehe 4.10.2022 Kumb. Na. ES-PC/BC.195/199/28/19

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Watendaji wa Wizara kukiri kujitokeza kwa hoja hii lakini Kamati ya PAC imegundua kwamba Wizara imekiuka masharti ya Mkataba kwa kumpatia Mkandarasi malipo kwa certificate tatu za awali wakati hawakupaswa kufanya hivyo.

Kadhalika, Kamati ya PAC imepata wasiwasi juu ya uwezo halisi wa Mkandarasi kutekeleza Mradi kama huo kwani pamoja na kwamba hajapatiwa malipo yake lakini utekelezaji wa Mradi ulikuwa ukisuasua hivyo inaonesha

alikuwa akitegemea fedha atakazolipwa kutumia katika ujenzi huo wakati katika hatua ya tathmini inatakiwa Mkandarasi ajimudu kifedha na kiutendaji.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ihakikishe inatekeleza miradi yake kama walivyokubaliana na Mkandarasi ndani ya masharti ya Mkataba huo.

2. Kamati ya Tathmini ya Wizara iwe makini inapowafuatilia Wakandarasi kuwafanyia tathmini ya uwezo halisi katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ili kuepushindwa kushindwa au kusuasua katika utekelezaji wa Miradi husika.

**Hoja nambari 6.3.1.3: Kuongezeka kwa gharama za Ujenzi**

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa ongezeko la gharama za ujenzi zilizowasilishwa kwa Mkandarasi kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba R/MOH/NCHP/04 ya tarehe 21/11/2019 yenye thamani ya shilingi 982,397,200 na kupelekea jumla ya gharama ya ujenzi kufikia shilingi 2,432,365,860 ambapo sawa na aslimia 67.75. Aidha, ukaguzi umebaini kuwepo ongezeko jengine la gharama kwa kazi za ziada zilizowasilishwa kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba R/MOH/CMCH/16 ya tarehe 29/7/2021 kutoka kwa Mkandarasi kwenda kwa Mshauri Elekezi ambapo barua hiyo ilikuwa na ongezeko la shilingi 1,306,575,000 na kupelekea gharama kamili kufi kia shilingi 3,738,940,860 sawa na ongezeko la asilimia 53.72 na kupelekea kuwepo kwa ongezeko la jumla ya shilingi 2,288,972,200 sawa na ongezeko la asilimia 157.86 kutokana na gharama za awali za mkataba.

Kutokana na kuongezeka kwa gharama za ujenzi mambo yafuatayo yamebainika:-

- Kutokana na kuwepo kwa ongezeko hilo kumejitokeza ukiukwaji wa sheria ya Ununuzi ambapo kanuni ya 49(4) na (5) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba " iwapo malipo yatazidi bei ya mkataba zaidi ya 15% yawasilishwe kwa mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata uthibitisho au Baraza la Wawakilishi (Approval)." Jambo ambalo ukaguzi haukupatiwa uthibitisho huo.
- kwa mujibu wa kifungu cha 6(1)(c) cha Sheria ya Manunuzi namba 11 ya 2016, pindipo inapotokezea nyongeza ya mkataba wa awali kupewa Mzabuni wa mwanzo kuendelea na kazi hiyo haitatakiwa kuongezeka kwa asilimia 25 ya thamani ya zabuni ya awali jambo ambalo halikuzingatiwa katika utowaji wa zabuni hiyo.

Ukaguzi umebaini gharama za ujenzi huengezeka kutokana na kuwepo kwa mabadiliko ya ramani ya awali na kupelekea kuengezeka kwa baadhi ya vitu ambavyo havikuwemo kwenye mchoro wa awali na kupelekea ongezeko la shilingi 2,288,972,200 sawa na ongezeko la asilimia 157.86 jambo ambalo linapelekea kuchelewa kukamilika kwa mradi kulingana na wakati uliopangwa ambapo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kusimamia kwa karibu ujenzi huo ikiwemo kuzifanyia kazi kasoro zilizobainishwa ili kuhakikisha kwamba ujenzi huo unamaliza kwa wakati na kwa kiwango kinachotarajiwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Ni kweli gharama za Ujenzi ziliongezeka:

Wizara ilimuajiri Wakala wa Majengo (ZBA) kuwa Msimamizi wa Ujenzi wa Mradi huu na kungundua mapungufu mengi katika mchoro ambayo

yangesababisha kutoweza kutumika kwa Majengo hayo baada ya kukamilika kwake, Mfano wa mapungufu hayo ni kukosekana kwa Ramp, vipimo vya Jengo kwenye michoro havikuwa vimekaa vizuri, kukosekana mifumo ya Gesi, mifumo ya mawasiliano na umeme. Hivyo Jengo hilo lingelimalizika bila kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza, jengo lingeshindwa kutoa huduma iliyokusudiwa.

Mshauri Elekezi aliwasilisha mapendekezo ya Michoro kwa barua yenye kumbukumbu nambari WM/AMM/10/6/VOL.II/55 ya tarehe 25/01/2022. Hata hivyo, gharama hizo zilizoongezeka hazikukubaliwa na Mkandarasi alitakiwa amalizie kazi zake kwa gharama za Mkataba wa TZS. 1,449,968,660.

Hivyo, Jengo hilo lingelimalizika bila kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza, jengo lingeshindwa kutoa huduma iliyokusudiwa. Mshauri Elekezi aliwasilisha mapendekezo ya Michoro kwa barua yenye kumbukumbu nambari WM/AMM/10/6/VOL.II/55 ya tarehe 25/01/2022. Hata hivyo, gharama hizo zilizoongezeka hazikukubaliwa na Mkandarasi alitakiwa amalizie kazi zake kwa Gharama za Mkataba wa TZS. 1,449,968,660. Barua ya ongezeko la gharama za mradi kumbukumbu ya kikao cha kujadili gharama hizo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuchunguza hoja hii, Kamati haikufurahishwa na utendaji wa Wizara katika kulishughulikia suala hili kwani kunaonekana kuwepo kwa uzembe mkubwa uliosababishwa na watendaji na Washauri Elekezi wasiokuwa na taaluma ya mahitaji ya vitu vinavyotakiwa kuwemo katika ujenzi wa hospitali. Hali iliyopelekea kujitokeza kwa kasoro nyingi hususan katika mchoro wa ujenzi huo.

Lakushangaza zaidi, ujenzi huo ulianza kutekelezwa pasi na kuwa na Mshauri Elekezi ambae angekuwa na jukumu la kumsimamia Mkandarasi pamoja na kubaini mapema hatua kasoro zilizojitokeza na kuzipatia

ufumbuzi wake mapema iwezekanavyo. Wizara inafahamu kwamba ujenzi mkubwa kama huo hauwezi kutekelezwa kwa mafanikio pasi na kuwepo Mshauri Elekezi mwenye taaluma na uweledi wa hali ya juu katika masuala ya ujenzi wa majengo ya hospitali.

Lakusikitisha zaidi, kuna jumla ya shilingi 2,288,972,200 sawa na ongezeko la asilimia 157.86 jambo ambalo linapelekea kuchelewa kukamilika kwa mradi kulingana na wakati uliopangwa.

Vile vile, kitendo hicho kimepelekea kukiukwa mashrti ya Kanuni za 49(4) na (5) za Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kwamba iwapo gharama za ujenzi zitazidi kwa asilimia 15% zinatakiwa ziwasilishwe kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata uthibitisho au Baraza la Wawakilishi (Approval).” Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 6(1)(c) cha Sheria ya Manunuzi namba 11 ya 2016, pindipo inapotokezea nyongeza ya mkataba wa awali kupewa Mzabuni wa mwanzo kuendelea na kazi hiyo haitatakiwa kuongezeka kwa asilimia 25 ya thamani ya zabuni ya awali jambo ambalo halikuzingatiwa katika utoaji wa zabuni hiyo.

Sambamba na hayo, Kamati ilifanya matembezi katika ujenzi huo na kubaini kwamba limeshakamilisha kwa zaidi ya asilimia 80 lakini bado matengenezo madogo madogo yanahitajika kufanyika kama vile utiaji wa madirisha na miundombinu ya maji. Aidha, hadi Kamati inakamilisha ukaguzi wake Mkandarasi (Rans Company Limited) ilikuwa inaidai Wizara jumla ya shilingi 25,700,005,120 na Wakala wa Majengo Zanzibar inadai kwa Wizara USD 150,435,547.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ihakikishe Miradi mikubwa ya Serikali inakuwa inasimamiwa na Mshauri Elekezi ili kuweza kutambua changamoto zitakazobainika

mapema iwezekanavyo.

2. Wizara ihakikishe inatekeleza Miradi yake ya Maendeleo kwa mujibu wa sheria, mikataba na miongozo inayotolewa na Serikali.
3. Wizara ihakikishe jengo lililojengwa na Mradi linakamilishwa ndani ya muda husika.
4. Wizara ihakikishe inakamilisha kulipa madeni yote yanayodaiwa wa Mkandarasi na Mshauri Elekezi.

**Hoja nambari 6.3.1.4: Kutokuainishwa kwa baadhi ya kazi katika BOQ**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba baadhi ya kazi ambazo zimeainishwa katika ramani ya ujenzi kwa mujibu wa mkataba wa awali hazikuoneshwa uhalisia wake katika BOQ. Kutokuonekana kwa ongezeko la baadhi ya kazi katika BOQ iliyowasilishwa kumepelekea kujitokeza kwa ongezeko la gharama kwa kazi za ziada ambazo zilihitajika kutekelezwa kwa mujibu wa matakwa ya mradi huo.

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba R/MOH/CMCH/16 ya tarehe 26/7/2021 iliyonakili makubaliano ya ongezeko la kazi za ziada kwa mujibu wa kikao kilichofanyika tarehe 24/7/2021 kilibainisha jumla ya kazi kumi na nne zilizoongezeka zenye thamani ya shilingi 1,306,575,000. Dosari ya ukaguzi iliobainika ni kushindwa kufunga mkataba mpya kutokana na mkataba wa awali umekiuka taratibu za kisheria.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Ni kweli baadhi ya kazi hazikuainishwa katika kuandaa gharama za kazi (BOQ). Jambo hili lilitokana na mapungufu ya Mchoro uliotayarishwa, hivyo mapungufu hayo hayakuweza kuainishwa kwenye BOQ.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Wizara kukubaliana na hoja ya Mkaguzi akini Kamati ilitaka kujua ni maeneo gani ambayo yaliongezwa ambayo katika Mkataba wa awali hayakuwemo na kuelezwa kuna mambo ya msingi yakiwemo ujenzi wa Ramp, mifumo ya Gesi pamoja na mifumo ya mawasiliano na umeme hayakujumuishwa. Kamati ilishangazwa sana na baadhi ya vitu kukosekana kuainishwa katika Mkataba wa awali wakati miongoni ni vitu vya msingi ambavyo kila hospitali inatakiwa kuwa navyo.

Kwa mnasaba huo, kamati imebaini kuwa baadhi ya Watendaji hutekeleza majukumu pasi na kuwa na uzalendo na nchi yao jambo ambalo linaashiria ubadhirifu wa mali za umma.

Vile vile, Kamati imegundua kuwa madhaifu hayo mengi yametokana na kutokuwepo kwa Mshauri Elekezi katika hatua za awali kwani yeye aneweza kubaini mapungufu hayo katika hatua za awali na kufanyiwa kazi mapema, jambo ambalo lisingepekea ongezeko la shilingi 1,306,575,000. Hata hivyo, Kamati imebaini jengo lipo katika hatua za mwisho na kutokana na changamoto za ujenzi zilizojitokeza, jengo halitotumika tena kama hospitali badala yake litatumika kama jengo la kutolea huduma za kiutawala za hospitali na mpango wa Serikali ni kuyavunja majengo ya hospitali yaliopo eneo hilo na kujengwa upya majengo mapya ya hospitali za kisasa.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inavishauri vyombo ya uchunguzi hususan ZAECA kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha wanafuatilia kwa karibu suala hili ili kubaini wale wote waliohusika na upotevu wa fedha za Serikali kwa kutowajibika ipasavyo na kuweka mbele maslahi binafsi kwa manufaa yao.
2. Wizara iwashirikishe Washauri Elekezi katika maandalizi na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

3. Wizara ya Afya iwe makini inapotekeleza Miradi mikubwa ya Maendeleo hasa ukizingatia wananchi wetu huwa na matarajio makubwa kutokana na miradi hiyo.

**Hoja nambari 6.3.1.5: Kutokamilika Mradi kwa Wakati**

kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wa ujenzi wa awali baina ya Wizara ya Afya na Mkandarasi RANS CO. LTD kwa mujibu wa mkataba wenye kumbukumbu namba SMZ/HO1/W/NCB/W/2018/2019/13 mkandarasi alitakiwa kukamilisha mradi huo ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili kuanzia tarehe 01/06/2020 hadi 01/06/2021.

Hadi ukaguzi unakamilika, Mradi huo bado haujakamilika, kutokukamilika kwa mradi huo kwa wakati kunaweza kukapelekea kushindwa kutekelezeka kutokana na kuongezeka kwa thamani ya vifaa vya ujenzi siku hadi siku jambo ambalo litapeleka kukosekana kwa tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya ni vyema kubuni miradi michache ambayo watakuwa na uwezo wa kuitekeleza kwa wakati ili kunusuru upotevu wa fedha za umma unaotokana na ongezeko la thamani ya dola kwa shilingi.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Ni kweli Mradi umeshindwa kukamilika kwa Wakati:

Wakati wa utekelezaji wa Mradi huu kulijitokeza changamoto mbali mbali zilizosababisha Mradi kushindwa kumalizika kwa wakati, baadhi ya sababu hizo ni:

i) Mapungufu kwenye Michoro iliyosababisha Mkandarasi kusimama kazi kusubiria mapitio ya Michoro.

ii) Majadiliano baina ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi juu ya njia ya Ujenzi (Construction Methodology) iliyopaswa kutekelezwa katika mradi huu.

iii) Kusubiria maamuzi ya Serikali kukubali au kukataa gharama zilizoongezeka katika utekelezaji wa kazi husika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati imebaini sababu kubwa iliyosababisha kutokukamilika kwa Mradi ni kukosewa kwa mchoro wa ujenzi tangu hatua za awali kulikosababishwa na kutomshirikisha Mshauri Elekezi. Hivyo uchunguzi na mapendekezo a hoja hii kama yalivyoelezwa katika Hoja nambari 6.3.1.4.

**Hoja nambari 6.3.1.6: Kutokulipwa kwa Fedha za Mshauri Elekezi shilingi 25,705,120.00**

Kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba baina ya Wizara ya Afya na Mshauri elekezi ambaye ni msimamizi wa jengo la mama na mtoto la hospitali ya Chake Chake Pemba imebainika makubaliano ya gharama ya usimamizi wa ujenzi huo ni shilingi 36,721,000 ambazo zilitakiwa kulipwa kwa awamu mbalimbali kama mkataba unavyoonesha. Ukaguzi umebaini kutokulipwa kwa fedha za mshauri Elekezi kwa malipo ya awamu mbili (2) tofauti zenye thamani ya shilingi 25,705,120 na kumepelekea kujitokeza kwa usimamizi usioridhisha wa kazi ya ujenzi, jambo ambalo huenda likapelekea utekelezaji wa mradi huo kutotekelezwa kwa wakati au

chini ya kiwango cha makubaliano.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha hatua za haraka zinachukuliwa za kumlipa mshauri elekezi kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wao kwa lengo la kunusuru kujitokeza kutokufahamiana na kuzorotesha maendeleo ya mradi.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Ni kweli Mshauri Elekezi hajalipwa. Wizara ya Afya ilipokea barua kutoka kwa Mshauri Elekezi (ZBA) wa Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto ya tarehe 22 Februari, 2021 yenye kumbukumbu namba WM/AMM/10/6/VOL.II/69 inayodai malipo ya TZS. 25,705,120.00 ambazo ni asilimia 70. (70%) ya Mkataba huo.

Wizara ya Afya kwa upande wake ilitayarisha maombi ya Fedha hizo kupeleka kwa Katibu Mtendaji Tume ya Mipango kwa barua ya tarehe 01 Machi, 2021 yenye kumbukumbu namba AB.73/108/02. Kwa bahati mbaya Fedha hizo Wizara haijaidhishiwa kwa ajili ya kufanya malipo hayo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile watendaji wamekubaliana na hoja ya Mdhibiti, Kamati haikuwa na hoja zaidi isipokuwa Kamati ilitoa maoni yake

machache ili Wizara iyafanyie kazi na kunusurika na madeni yasiyo ya lazima.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ifuatilie Wizara ya fedha na Mipango ili iweze kujua ni kitu gani kilichokwamisha ambapo hadi Kamati inakamilisha uchunguzi wake malipo hayo bado yalikuwa hayajafanyika.

**UCHUNGUZI WA RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM KWA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 ULIOFANYIKA TAREHE 13/07/2021 - 27/07/2021.**

**HUDUDI REJEA NAMBA 1:**

**Hoja nambari 3.12.1.1: Kukosekana kwa muongozo wa ukusanyaji wa mapato ya Taasisi**.

Kifungu cha 8 (1) cha Sheria namba 8 ya mwaka 2020 ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kimeeleza kwamba kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ambayo moja ya kazi zake ni kutoa muongozo kuhusiana na majukumu ya Taasisi.

Ukaguzi ulifanya mahojiano na Uongozi wa Taasisi katika kikao cha ufunguzi pamoja na maafisa wanaokusanya mapato katika nyakati tofauti na kubaini kwamba hakuna muongozo wowote uliowekwa kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato ya utalii na mapato ya mazao na miche.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo katika kikao chake cha kawaida cha tarehe 7 Oktoba, 2021, imelifanyia kazi jambo hili kwa kupitisha mapendekezo ya rasimu ya kanuni ya ada na tozo ambayo iliwasilishwa katika ngazi ya Wizara kwa hatua za mwisho. Hata hivyo, kwa upande wa miche ilionekana kwamba kutakuwa na tofauti ya bei za miche inayouzwa na Idara nyengine za Wizara kama vile Idara ya Kilimo na Idara ya Misitu na ikapendekezwa kukaa pamoja kuweka sawa hali hiyo. Wawakilishi wa Taasisi tatu (ZARI, Idara ya Kilimo na Idara ya Misitu) walifanya mapitio ya kanuni

kwenye bei za miche ya miti ya matunda na viungo na kuwasilisha mapendekezo yao ngazi ya Wizara. Aidha, katika kipindi cha mpito, Bodi ya Wakurugenzi ya ZARI iliruhusu kuendelea na bei zilizokuwepo. (kumbu kumbu za maamuzi ya kikao cha tatu cha Bodi cha tarehe 7 Oktoba, 2021)).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba wakati Mkaguzi anafika katika Taasisi hii, kulikuwa hakuna muongozo mahsusi wa ukusanyaji mapato ya Taasisi. Hilo lilitokana na kuwepo kwa muongozo wa ukusanyaji wa mapato wa Wizara ya Fedha na Mipango ambao unatumika kwa Serikali nzima, jambo ambalo hupelekea kuwepo kwa malalamiko kwamba Taasisi hiyo inapangiwa makisio makubwa. Sambamba na hilo, Kamati pia ilitaka kujua hali halisi ya uwepo wa muongozo huo kwa kipindi hiki kwani ni muda mrefu umepita tangu Mkaguzi alipoainisha hoja hii na kuelezwa kwamba kuna Kanuni ya uwekaji viwango vya mapato ya miche inaandaliwa lakini ndio kwanza ipo Wizarani inasubiri kufanyiwa kikao cha Kamati ya Uongozi ya Wizara ili iweze kufuata hatua za ukamilishaji. Aidha, Kamati imeshangazwa kwamba hadi leo Wizara inaendelea na vikao vya ndani kati ya Wizara na Wizara ya Fedha na Mipango vya kuweka sawa sera za ukusanyaji wa mapato.

Kamati haikuridhishwa na utekelezaji mdogo wa hoja hiyo na kuitaka Ofisi ya Mkaguzi kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wake ili Kanuni hiyo iweze kukamilishwa kwa haraka na kutumika kwa maslahi ya Taasisi na Serikali kwa ujumla.

Hata hivyo, Kamati imefanikiwa kuona maamuzi yaliyotolewa na Bodi ya Taasisi hiyo na kuridhika nayo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kulifuatilia kwa karibu utekelezaji wa hoja hii ili iweze kutekelezwa kwa maslahi ya Taasisi na Taifa letu.

2. Wizara ihakikishe inafanya haraka kukamilisha mchakato unaoendelea wa kukamilisha Kanuni (muongozo) ya makusanyo ya Mapato ya Taasisi hii ili kuondosha malalamiko yaliyopo ya kupangiwa makisio makubwa yanayofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango.

3. Wizara ishirikiane na Wizara ya Fedha na Mipango kufikia maamuzi ya vikao vyao vya ndani ili suala la upatikanaji wa muongozo wa ukusanyaji mapato hususan yanayotokana na miche vinakamilishwa kwa ufanisi unaotakiwa.

**Hoja nambari 3.12.1.2: Kuwepo kwa Makadirio ya Mapato ya ndani yasiokuwa na uhalisia.**

Ukaguzi ulipitia taarifa ya uwiano wa makadirio ya makusanyo ya mapato pamoja na mapato halisi ya vyanzo vya ndani vya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015 - 2021 na kubaini dosari zifuatazo:

**a) Kutokuwepo kwa mfumo mzuri katika utayarishaji wa bajeti**

Ukaguzi umebaini kwamba Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar haina mfumo mzuri wa utayarishaji wa bajeti katika vyanzo vya mapato. Hali hii imetokana na kuwepo kwa mabadiliko ya kila mwaka ya makadirio ya mapato yanayotokana na uuzwaji wa Miche, Mazao pamoja na mapato ya ukodishwaji wa Mashamba ambayo hupanda na kushuka bila ya kuwepo sababu za msingi.

Hali halisi ya mwenendo wa Bajeti unavyobadilika dhidi ya makusanyo halisi kwa kipindi cha miaka mitano (5) ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 25: Makadirio na Mapato Halisi**

**(i) Makadirio na Mapato Halisi ya Mauzo ya Mazao na Miche**

| Mwaka wa Fedha | Makadirio ya Makusanyo (Shs) | Makusanyo Halisi (Shs) | Tofauti (Shs) | Asilimia ya Tofauti (%) |
|---|---|---|---|---|
| 2016 -2017 | 40,000,000 | 9,164,200 | 30,835,800 | 77 |
| 2017 -2018 | 20,000,000 | 28,933,200 | (8,933,200) | - 45 |
| 2018 -2019 | 70,000,000 | 15,308,500 | 54,691,500 | 78 |
| 2019 -2020 | 52,080,000 | 13,719,200 | 38,360,800 | 74 |
| 2020 -2021 | 15,000,000 | 14,596,500 | 403,500 | 3 |

## (ii) Makadirio na Mapato Halisi ya Mashamba

| Mwaka wa Fedha | Makadirio ya Makusanyo | Makusanyo Halisi (Shs) | Tofauti (Shs) | Asilimia ya Tofauti (%) |
|---|---|---|---|---|

| | (Shs) | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2016 -2017 | Taarifa za Fedha hazikupatika kwa ukaguzi | | | |
| 2017 -2018 | Taarifa za Fedha hazikupatika kwa ukaguzi | | | |
| 2018 -2019 | 20,000,000 | 260,000 | 19,740,000 | 99 |
| 2019 -2020 | 14,880,000 | 76,300,000 | (61,420,000) | -<br>413 |
| 2020 -2021 | 60,000,000 | 1,050,000 | 58,950,000 | 98 |

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Hali hii inatokana na kuwa makisio ya mapato yanayokadiriwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo kupitia Wizara ya Kilimo hayazingatiwi na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na badala yake Taasisi hupangiwa ukomo (*ceiling)* kwa utekelezaji tu kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango. Makadirio ambayo Taasisi inayapeleka huwa yanazingatia misimu na hali ya mavuno yaliyopita ya mazao mbalimbali na mwenendo wa uingiaji wa wageni katika shamba la viungo Kizimbani.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuichunguza hoja hii, Kamati ya PAC ilitaka kujua Taasisi ya utafiti wa Kilimo inategemea vyanzo vingapi vya mapato yake hadi kufikia kuwekewa makisio makubwa kwa muda mrefu na kuelezwa kwamba Taasisi inategemea mapato yake kupitia vyanzo vikuu vitatu; ada ya kuangalia mashamba, ukodishwaji wa Mashamba na miembe yao pamoja na uzalishaji wa miche mbali mbali.

Katika majadiliano ya hoja hii, Kamati imebani kwamba pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Taasisi lakini bado uzalishaji wa miche ya Minazi na Mikarafuu hautoshelezi au haukidhi mahitaji ya wananchi na kupelekea kukosekana kwa miche itakayotumika kupanda katika mashamba yao. Sambamba na hilo, Kamati ya PAC imebaini kuwa mapato yote yanayotokana na uzalishaji wa miche yote hupelekwa hazina bila ya kubakia asilimia yoyote itakayotumika katika uendelezwaji au uatikaji wa miche mipya.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Uongozi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo usimamie ipasavyo uzalishaji wa miche ya Minzi na Mikarafuu na kuiwasilishwa kwa wananchi.

2. Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe inaipangia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar ili makusanyo yaweze kutoa taswira halisi ya uwezo wa Taasisi hiyo kulingana na mabadiliko ya misimu ya uzalishaji.

**b) Kuwepo kwa tofauti kubwa baina ya Makadirio ya Makusanyo na Mapato Halisi**

Ukaguzi umebaini uwepo wa tofauti kubwa kati ya bajeti iliyoidhinishwa na makusanyo halisi kutoka kwenye mapato yatokanayo na Ada ya Utalii kwa kipindi cha miaka mitano. Mchanganuo wa makadirio na makusanyo halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 26: Tofauti ya Makadirio na Mapato halisi ya Ada ya Utalii**

| Mwaka wa Fedha | Makadirio ya Makusanyo (Shs) | Makusanyo Halisi (Shs) | Tofauti (Shs) | Asilimia ya Tofauti (%) |
|---|---|---|---|---|
| 2016 -2017 | 50,000,000 | 11,903,000 | 38,097,000 | 76 |
| 2017 -2018 | 50,000,000 | 11,860,000 | 38,140,000 | 76 |
| 2018 -2019 | 50,000,000 | 11,184,000 | 38,816,000 | 78 |
| 2019 -2020 | 37,200,000 | 10,654,000 | 26,546,000 | 71 |
| 2020 -2021 | 20,000,000 | 3,262,000 | 16,738,000 | 84 |

**Majibu ya uongozi wa Taasisi**

Kamati haikupokea majibu ya maandishi ya hoja hii, hata hivyo kamati ilielezwa kwamba majibu ya (a) yanahusika pia na majibu ya (b).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imegundua kwamba mapato ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya uingiaji wa wageni katika mashamba yao yaliathiriwa sana na mripuko wa maambukizi Uviko - 19 kwani ilikuwa Taasisi inafikia hadi kupata wageni 1,000 mpaka 15,000 katika msimu mkubwa wakati walipungua hadi kufikia wageni 400 mpaka 500 katika wakati huo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ihakikishe inakiimarisha chanzo cha mapato ya ada ya Utalii ili kiweze kuongeza mapato.

**Hoja nambari 3.12.1.3: Kutokuwiana kwa majukumu ya kimkataba na kazi wanazofanya baadhi ya watumishi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar.**

Ukaguzi umepitia taarifa binafsi za watumishi wenye dhamana ya kusimamia na kukusanya mapato katika shamba la viungo Kizimbani na kufanya mahojiano na watumishi hao kwa muda tofauti.

Ukaguzi umebaini kwamba watumishi ambao wana jukumu la kusimamia duka la viungo hawakuwa wakifanya kazi kwa mujibu wa majukumu yao yaliyoainishwa kwenye mikataba yao ya ajira, aidha ukaguzi haukupata barua za kubadilishwa nafasi zao za kazi na majukumu ya watumishi hao.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Pamoja na kwamba hoja ni kutokuwiana kwa majukumu, Bodi ya ZARI ilijadili kwa kina suala la biashara ya duka la viungo katika kikao chake cha tarehe 7 Oktoba, 2021 ikagundua kasoro na mapungufu ya ufanisi wa kiutendaji, ilifanya maamuzi ya kulifunga kabisa duka la viungo na kuamuru bidhaa zilizomo kuuzwa kwa mujibu wa taratibu za Serikali. Aidha, katika utaratibu wa kulifunga Bodi iliamuru Taasisi kutoa taarifa rasmi kwa Katibu Mkuu kuhusu maamuzi yake ili achukue hatua zinazoendelea. Taasisi ilitekeleza agizo hilo kwa barua yenye kumb. Na. TUK/KZ/7/2/3/VOL.II ya tarehe 12 Oktoba, 2021. Kwa upande wake Katibu Mkuu aliwasiliana na Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ambae alileta mtu wa kuzifanyia tathmini bidhaa zilizoorodheshwa (kumb. Barua ya Mthamini Mkuu: OMMS/2021/U.21/9/139 ya tarehe 27 Oktoba, 2021). Hatua iliyofuata ilikuwa ni kuzitangaza bidhaa hizo zilizothaminiwa kuwa na thamani ya shilingi 378,600/. Hata hivyo, bidhaa hizo zilizohifadhiwa ghalani kwa muda zilikosa mnunuzi hadi kufikia wakati wa kukosa vigezo vya kukubalika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Watendaji wa Wizara kukubaliana na hoja kwamba kulikuwepo wafanyakazi waliokuwa wanafanyakazi kinyume na majukumu yaliyoainishwa katika Mikataba yao na kueleza kwamba kasoro hiyo imesharekebishwa, hata hivyo Kamati ilibaini kuwa ushauri wa Mkaguzi ilikuwa sio kulifunga duka isipokuwa watumishi wanaotumika watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa mikataba waliyoingia. Hivyo ni busara kwa Taasisi kufanya utafiti ili waweze kubaini kipi kitakuwa na tija kwa Serikali ama kufungwa duka au kuendelea.

Sambamba na hilo, Kamati ya PAC ilitaka kujua jukumu la uuzwaji wa bidhaa za viungo katika shamba hilo utafanywa na nani na kuelezwa kwamba Shirika la Biashara la Taifa litashughulikia uuzwaji huo.

**Maoni, ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Wizara wahakikishe wanafanya utafiti utakaowawezesha kutambua kama kufungwa kwa duka ambalo ni chanzo kimoja cha mapato ya Taasisi kuna tija na Taasisi au walikuwa watekeleze ushauri uliotolewa na Mkaguzi wa kuwapanga wafanyakazi kwa mujibu wa majukumu yao

**Hoja nambari 3.12.1.4: Dosari katika Utaratibu wa Uuzaji wa Mazao.**

Ukaguzi ulifanya mazungumzo na mtumishi mwenye dhamana ya shamba la Kizimbani kwa lengo la kujua utaratibu uliopo katika ukodishaji wa miti ya mazao kwenye shamba hilo. Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali katika ukodishwaji wa mazao hayo kama ifuatavyo:

a) Kutokufanyika kwa tathmini ya awali ya kiwango cha mazao yanayopatikana kabla ya ukodishwaji wa miti ya mazao kwa lengo la makadirio ya mapato ya ukodishwaji.

Ukaguzi ulifanya mahojiano na Mkuu wa shamba hilo na kukiri kwamba hakuna taarifa ya tathmini ya awali inayofanywa na kuwasilishwa kwa uongozi ambayo inabainisha idadi ya miti iliyozaa na wingi wa mazao yaliyopatikana kwa kila mzao.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Wakati wa msimu wa mazao na kabla ya ukodishaji timu ya wafanyakazi wa Taasisi (ikijumuisha: Mkuu wa shamba, Msaidizi mkuu wa shamba, Mwangalizi wa Ofisi, Mratibu wa ulinzi na mali za Taasisi, na Mhasibu) huwa inapita katika shamba husika na kufanya tathmini ya mazao yanayotarajiwa kukodishwa kwa njia ya kuangalia (*observation*) utaratibu ambao kwa bahati mbaya haukuwa ukitoa ripoti za maandishi. Hata hivyo, kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 tathmini ya ukodishaji wa mazao unaratibiwa na OR-Rais Fedha na Mipango baada ya kupewa taarifa kwa maandishi juu ya uwepo wa zao fulani. (Mifano ya barua na kumb. zipo).

b) kwa mujibu wa vifungu 21(1) na 29(a) vya Sheria namba 11 ya mwaka 2016 ya ununuzi na uondoshwaji mali za umma inaitaka kitengo cha manunuzi katika Taasisi kuunganisha shughuli zote za ununuzi na uondoshaji mali za umma kwa kila Idara ili kuleta ufanisi wa rasilimali za umma. Ukaguzi

umebaini kuwa kitengo cha ununuzi na Bodi ya Zabuni hazishirikishwi katika shughuli za ukodishwaji wa mazao hayo na badala yake Mkuu wa shamba ndie anaetekeleza jukumu hilo kikamilifu.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Ni kweli kwamba katika ukodishaji wa baadhi ya mazao; Taasisi ikitumia maafisa wake wa ndani akiwemo Afisa Manunuzi, Mkuu wa mashamba na Mhasibu katika ukodishaji wa mazao hayo. Aidha, kwa mazao makubwa ikiwemo karafuu, Taasisi ilikuwa inashirikisha kitengo cha manunuzi cha Wizara ya Kilimo katika manunuzi kwa kuzingatia matakwa ya Sheria No. 11 ya 2016 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma. Kama ilivyoelezwa hapo juu, kwa sasa Ofisi ya Msajili wa Hazina (OR-Fedha na Mipango) ndio inaratibu na kumaliza hatua zote.

c) Ukaguzi umebaini kwamba Mkuu wa Shamba la Kizimbani amekuwa akiingia mikataba na wanunuzi wa mazao kwa niaba ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na kusaini mikataba bila ya idhini ya kimaandishi kutoka kwa Afisa Mhasibu.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Ni kweli utaratibu huo uliwahi kutumika zamani kupitia vikao vya pamoja vya uongozi wa Taasisi na kuidhinishwa Mkuu wa mashamba kuendelea na mchakato huo ikiwa ni pamoja na kuingia kwenye mikataba ya ukodishwaji kwa niaba ya Mkurugenzi. Kufuatia hoja za ukaguzi huu utaratibu wa kuzingatia idhini za kimaandishi, kutunza kumbukumbu na kushirikisha Bodi ya Zabuni ulianza. Kama ilivyotangulia kuelezwa kasoro hizi zote sasa hazipo baada ya kazi hizi kuanzwa kufanywa na Mamlaka nyengine.

d) Ukaguzi ulipitia mikataba iliyofungwa na Taasisi kwa ajili ya ukodishwaji wa miti ya mazao katika mashamba yanayomilikiwa na Taasisi na kubaini kuwa mikataba hiyo haikuwa na muhuri wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kama inavyoainishwa katika kifungu namba 4(3) cha Sheria namba 8 ya mwaka 2020.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Ni kweli Taasisi haikuwa ikiweka muhuri katika mikataba yake ya ukodishaji, lakini ilianza kutekeleza matakwa ya kifungu No. 4 (3) cha Sheria No. 8 ya mwaka 2020 kwa kuweka muhuri katika mikataba yote inayoingia. Vile vile, katika kuongeza umadhubuti wa mikataba hiyo, Taasisi ikazingatia kutumia mikataba yenye vigezo kwa kutumia karatasi maalum (Legal Papers) kama

ilivyoshauriwa. Hata hivyo, mikataba ya ukodishwaji mazao sasa inafanywa na OR-Fedha na Mipango na Taasisi hubaki kama shahidi tu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC iliyapitia majibu yote ya (a), (b), (c) na (d) na kubaini kwamba hoja zote nne (4) hizo alizobaini Mkaguzi zilikuwa zikifanyika lakini hivi sasa Taasisi imeshajirekebisha hasa ukizingatia Muhusika (Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ameshaondolewa). Hata hivyo, Kamati imesikitishwa na kitendo cha Mkurugenzi Mkuu wa zamani alikuwa akiingilia majukumu ya watendaji wengine na kuharibu kazi zilikuwa zimepangwa. Hilo limebainika kupitia maelezo ya hoja ya Mkaguzi kwamba mikataba haikuwa na mihuri ya Taasisi.

Katika kulifuatilia hilo, Kamati ya PAC ilitaka kujua kwamba kwa kipindi hicho kulikuwa hakuna Mwanasheria wa kutekeleza suala mikataba na kuelezwa kuwa watendaji waliokuwepo katika ukumbi wote wakikuwa wapya na hata kama angeuwepo wanapata mashaka juu ya ushirikishwaji katika utekelezaji wa majukumu hayo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Wizara wafanye kazi kwa uweledi na ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao.

**Hoja nambari 3.12.1.5: Kutokuidhinishwa kwa Ada na Tozo nyengine za huduma zinazotolewa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo.**

Ukaguzi ulifanya mahojiano na watumishi mbalimbali pamoja na kupitia mihutasari ya vikao vya Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ili kujua uhalali wa tozo na ada zinazotumika.

Ukaguzi umebaini kwamba ada na tozo zote zinazotumika hazikupata idhini ya Bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ambayo ndiyo inayoidhinisha ada na tozo za huduma zinazotolewa kwa mujibu wa sheria. Hali hiyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 9(e) cha sheria Namba 8 ya 2020 ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwepo kwa mapendekezo ya mpango wa uendeshaji wa shamba la viungo unaojumuisha mapendekezo ya ada na tozo mpya na kuwasilishwa katika Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi kupitia kikao cha 8 cha Baraza la Kwanza, ambao bado haujaanza kufanyiwa kazi.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Ni sawa na jibu la Hoja nambari 3.12.1.1 kuhusu "Kukosekana kwa muongozo wa ukusanyaji wa mapato ya Taasisi".

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini ni kweli jibu nambari 3.12.1.1 linafanana na hoja hii. Hilo linatokana na kwamba tozo na ada zote zinakusanywa na WIzara ya Fedha na Mipango na huingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina na hadi hivi sasa hakuna muongozo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ihakikishe inafutalia kwa karibu Wizara ya Fedha na Mipango ili waweze kutoa muongozo wa fedha zinazopatikana zitumike vili.

**HUDUDI REJEA NAMBARI 2**

**Hoja nambari 3.12.2.1: Kutokuainishwa kwa baadhi ya vyanzo vya Mapato.**

Ukaguzi ulifanya mahojiano na maafisa mbali mbali pamoja na wananchi wanaotegemea shamba la viungo katika harakati zao za kiuchumi na kubaini kwamba kuna baadhi ya vyanzo vya mapato havikubainishwa katika taarifa za mapato ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar. Vyanzo vya mapato hayo ni kama vifuatavyo: a) mapato yatokanayo na uuzaji wa bidhaa katika duka la Taasisi liliopo katika shamba la viungo Kizimbani; b) mapato yatokanayo na wafanyabiashara wadogo wadogo waliomo ndani ya shamba; c). Kutokuainishwa kwa vyanzo hivyo vya mapato katika taarifa ya mapato ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo kunaweza kupelekea Serikali kutokujua vyanzo halisi vya mapato, upotevu wa mapato kwa Taasisi na matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Katika ukusanyaji wa mapato ya ada ya uingizaji wageni; Taasisi imejumuisha ada inayolipwa mlangoni na *mtembeza wageni* kutokana na idadi ya wageni wanapotaka kuwaingiza, malipo wanayolipa vijana wanaotembeza wageni (maarufu kwa jina la NZI) ndani ya shamba, pamoja na vijana wanaouza bidhaa ndani ya shamba. Tozo na ada zote hizi zinazohusiana na shamba la viungo zinajumuishwa katika kifungu cha ada ya uingizaji wageni.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba Mkaguzi aliyefanya ukaguzi katika Taasisi hii hakupatiwa mashirikiano yanayotakiwa maana kuna hoja nyingi ambazo zimeibuliwa lakini lakushangaza Kamati imepatiwa majibu ya kutosha. Katika kujadili hoja hii, Kamati imegundua kwamba hesabu za mwisho wa mwaka za Taasisi hii haikuweka wazi mchanganuo wa vyanzo vya mapato ya ada ya uingiaji wageni iliyojumuisha ada inayolipwa mlangoni na mtembeza wageni.

Kimsingi, Kamati imebaini kwamba katika uandaaji wa Taarifa ya Hesabu ya mwisho mwaka, pamoja na kuwepo kwa vyanzo hivyo, Taasisi ililazimika taarifa hizo hizo za fedha zingelibainishwa katika "note" ili ziweze kutoa taswira kamii na halahi,

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ihakikishe inaandaa utaratibu mzuri kwa vijana ambao walikuwa wakijipatia kipato na kuendesha maisha yao kwa kutumia shughuli ya uingiaji wa wageni.
2. Wizara iwe makini na itumie Wataalamu wenye uweledi katika uandaaji wa Taarifa ya Fedha ya Mwisho wa mwaka.

**Hoja nambari 3.12.2.2: Ucheleweshwaji wa uwasilishaji wa fedha za mapato**

Ukaguzi umepitia nyaraka mbalimbali za Taasisi zikiwemo katika daftari za mapato na vitabu vya stakabadhi za mapato na kubaini kuwa kuna ucheleweshwaji mkubwa wa uwasilishwaji wa mapato kutoka kwa Makarani wasaidizi na kwenda kwa Karani mkuu wa mapato ambao umesababishwa na utaratibu usioridhisha wa ukusanyaji na uhifadhi wa mapato hayo.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Ucheleweshwaji wa kupelekwa fedha za makusanyo ulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo uchache wa makusanyo yenyewe na uhaba wa wageni wanaongia katika shamba kwa baadhi ya miongo. Hata hivyo, Taasisi imelizingatia hilo na kuanza marekebisho mara moja kwa lengo la kwenda sambamba na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika ufuatiliaji wa majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, hakufanikiwa kupatiwa daftari pamoja na vitabu vya stakabadhi za mapato. Hata hivyo, hivi sasa, kasoro hiyo kutokana na kuwepo kwa Mfumo wa Teknolojia ambao unatumia 'control nmber' ili uweze kufanya makusanyo ya ada.

Kwa mnasaba huo, kwa vile Taasisi imekubaliana na ushauri wa Mkaguzi, Kamati haikuwa na maelezo zaidi kwani iliridhika na majibu ya Taasisi.

**Hoja nambari 3.12.2.3: Kutokuwepo kwa Daftari la Wageni.**

Ukaguzi ulitembelea Shamba la viungo la Kizimbani ambapo shughuli za utalii zinafanyika kwa lengo la kufanya tathmini juu ya utaratibu mzima wa ukusanyaji na uhifadhi wa mapato yatokanayo na ada ya utalii. Ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa daftari la wageni pamoja na wasaidizi watembezaji wageni wanaoingia ndani ya shamba. Kutokuwepo kwa daftari hilo kunapelekea ukaguzi kushindwa kufanya tathmini ya mapato ya ada ya utalii ili kupata idadi halisi ya wageni waliotembelea shamba hilo.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Taasisi ilikua ikitumia madaftari mawili katika shamba la viungo; moja likitumika kuweka orodha ya vijana watembezaji wageni wanaotoa maelezo kwa wageni, na daftari jengine likitumika kuorodhesha majina ya wanaoleta wageni pamoja na idadi ya wageni walioletwa. Hata hivyo, Taasisi imechukuwa hatua ya kuwa na daftari la kuoredhesha majina ya wageni kama ilivyopendekezwa.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa wakati Mkaguzi anafanya kazi zake daftari la wageni lilikuwa halipo. Hata hivyo, Wizara imechua juhudi ya zifaazo na kuwezesha kupatikana kwa daftari hilo ambapo Kamati ya PAC imefanikiwa kuoneshwa na kuridhika nalo. Hivyo, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa hoja hii na haikuwa na maelezo ya ziada.

**Hoja nambari 3.12.2.4: Kutokuwepo kwa Daftari la Mali zisizohamishika za Shambani.**

Ukaguzi ulifanya mahojiano na Mkuu wa mashamba na mwangalizi wa Ofisi na kubaini kwamba Taasisi haina Daftari la mali zisizo hamishika za shambani ikiwemo miti ya mazao. Kutokuwepo kwa daftari hilo kunapelekea kutokupata tathmini sahihi ya miti ya mazao na kujua idadi ya miti iliyozaa na wingi wa mazao yaliyopatikana kwa kila mzao ili kuweza kupata makadirio ya mapato ya ukodishwaji yenye kuonyesha uhalisia.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Taasisi ina daftari linaloonesha mali zake zote ikiwa ni pamoja na ukubwa wa ardhi, hata hivyo halikuwa linaonesha idadi na aina ya miti ya mazao. Kutokana na kasoro hii, Taasisi tayari imechukuwa hatua za kufanya kazi ya kukusanya taarifa (daftari la idadi na aina lipo) ya miti yote katika eneo lake kama ilivyoelekezwa.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati kwa hoja hii yanafanana na uchunguzi na mapendekezo ya Kamati yaliyoelezwa katika hoja nambari 3.12.2.4.

**Hoja nambari 3.12.2.5: Kutokuwepo kwa kumbukumbu za Miche inayozalishwa na kuuzwa**.

Ukaguzi ulifanya mahojiano na Maafisa wanaoshughulikia mashamba ambao pia ndio wauzaji wa miche inayozalishwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na kubaini kwamba Taasisi haina utaratibu wa kuweka kumbukumbu za orodha za miche inayozalishwa, inayouzwa na iliyobaki ili kuweza kufanya tathmini ya ufanisi katika uzalishaji wa miche hiyo. Kutokuwepo kwa kumbukumbu za orodha hiyo kumepelekea ukaguzi kushindwa kupata tathmini sahihi ya miche iliyozalishwa, iliyouzwa na iliyobakia.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Lengo kuu la kuzalisha miche katika Taasisi ya utafti ni kuweza kuhudumia mashamba yake na ziada huuzwa kwa wananchi. Aidha, Taasisi inalo daftari la kumbukumbu za miche inayozalishwa, hata hivyo baadhi ya taarifa zilikosekana ikiwemo taarifa za miche iliyopandwa katika shamba la Taasisi, iliyokufa, iliyouzwa na iliyobaki. Kutokana na kasoro zilizobainika, Taasisi tayari imechukua hatua za kuliimarisha daftari hilo kwa kuingiza taarifa zote

muhimu ikiwa ni pamoja na kuzihifadhi kwenye komputa kwa mfumo wa kielektroniki.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati kwa hoja hii yanafanana na uchunguzi na mapendekezo ya Kamati yaliyoelezwa katika hoja mbili zilizopita yaan hoja nambari 3.12.2.4 na hoja nambari 3.12.2.5.

**Hoja nambari 3.12.3.1: Kuwepo kwa matumizi ya stakabadhi za kukusanyia mapato zisizokuwa rasmi katika shamba la viungo.**

Ukaguzi ulifanya mahojiano na vijana wanaohusika na utembezaji wageni katika shamba la viungo kupitia kikao cha tarehe 13/07/2021 na kubaini kuwepo na stakabadhi zisizo rasmi katika ukusanyaji wa mapato kwa upande wa wasaidizi wa watembezaji wageni katika shamba hilo. Aidha, ulifanya mahojiano na Karani Mkuu juu ya uwepo wa stakabadhi zinazotumika kwa ajili ya ada wanayotozwa vijana hao na kukiri kuwepo kutumika kwa stakabadhi zisizokuwa rasmi kwa ajili ya kukusanya mapato. Aidha, ukaguzi ulibaini kwamba Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar iliacha kutumia stakabadhi zisizokuwa rasmi na kutengeneza stakabadhi nyengine zenye nembo na anuani ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar ambazo kwa sasa hazitumiki tena.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Utaratibu wa zamani kwa makarani kukusanya malipo kwa kutumia stakabadhi zisizokuwa rasmi kwa ajili ya malipo wanayofanya vijana wanaotembeza wageni, ulitokana na matumizi ya vitabu vingi vya risiti rasmi kwa siku. Vijana hao walikuwa wanalipa shilingi elfu moja (1000.00) kila wanapoingia kwenye shamba na hatimae ikabadilishwa kwa agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar kulipa kima hicho kwa siku nzima. Wakati mapato hayo yakiwasilishwa kwa Karani Mkuu baada ya kufunga makusanyo ya siku, idadi ya risiti zisizo rasmi hurikodiwa na kuandikiwa risiti moja rasmi na hatimae fedha hizo kupelekwa benki. Aidha, Taasisi ilianza kutumia Stakabadhi rasmi zenye nembo ya Taasisi, TIN Namba na ZRB Namba na baadae kufuatiwa na mfumo mpya wa EFD wa kupokea na kutoa risiti za kielektroniki kama ilivyoagizwa na Serikali.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaungana na hoja ya Mkaguzi kwamba ni kweli wakati wa ukaguzi Taasisi hii ilikuwa ikitumia stakabadhi za kukusanyia mapato

zisizokuwa rasmi katika shamba la viungo. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba changamoto hiyo kwasasa imerekebishika kutokana na matumizi ya mashine za kielektroniki. Hivyo, Kamati ya PAC imeridhika na hatua zilizochukuliwa na Taasisi.

**Hoja nambari 3.12.4.1: Kutokusajiliwa kwa tafiti zilizokamilika**

Ukaguzi ulifanya mahojiano na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti wa Kilimo na kubaini kuwepo kwa tafiti mbalimbali zinazofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kwa lengo la kuboresha Mbegu, Mbolea na Udongo. Matokeo yanayotegemewa kupatikana baada ya tafiti hizo kukamilika ni upatikanaji wa mbegu mpya, teknolojia mpya na mbinu bora za kilimo. Ukaguzi umebaini kuwepo kwa tafiti zilizomalizika za mbegu mpya za mpunga aina ya Super BC na mbolea ya UDP ambazo hazijasajiliwa.

Uvumbuzi wa mbegu inayojulikana kwa jina la Super BC ambao umekamilika kufanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar na matokeo ya utafiti huo ni kwamba mbegu hiyo kuwa miongoni mwa mbegu bora za mpunga zinazofanya vizuri kwa sasa katika sekta ya kilimo cha mpunga Tanzania.

Ingawa mbegu hiyo kuwa bora na kutoa matokeo mazuri ya uzalishaji, ukaguzi umebaini kwamba Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar haikusajili matokeo ya utafiti huo ili iweze kuwa hakimiliki kama inavyoainishwa katika kifungu cha 31(1) cha sheria Namba 8 ya mwaka 2020. Aidha, Kaimu Mkurugenzi alieleza kwa ukaguzi kwamba mbegu hiyo imesajiliwa Tanzania Bara na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa jina la TARIS.

Ukaguzi umebaini kwamba utafiti wa mbolea ya UDP umekamilika na matokeo ya utafiti huo hayajasajiliwa hadi kumalizika kwa ukaguzi. Aidha, uzalishaji wa mbolea hiyo kwa kiwango cha biashara haujaanza kufanyika ingawa mtambo wa kuzalisha mbolea hiyo una uwezo wa kuzalisha tani mbili kwa siku.

Ukaguzi ulihoji sababu za kutosajiliwa kwa tafiti hizo na kubaini kuwa hakuna sheria wala chombo kinachohusika na masuala ya usajili wa tafiti za kilimo hapa nchini. Kutokusajiliwa kwa tafiti hizo na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kunapelekea kukosesha Taasisi mapato ya mirabaha inayotokana na matumizi ya matokeo ya tafiti hizo, vile vile kufanya hivyo kunaweza kuzorotesha ufanisi wa ufanyaji kazi za utafiti kwa wafanyakazi wa Taasisi.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Kwa mujibu wa utaratibu, mtafiti baada ya kugundua au kupata matokeo ya utafiti wake anatakiwa kupeleka kwenye Taasisi yenye mamlaka ya kuthibitisha uhalisia na ubora wa alichokigundua. Kwa bahati mbaya, hadi sasa hapa Zanzibar hakuna chombo hicho. Aidha, kuhusiana na mtambo wa kutengeneza mbolea ya UDP, hapo awali mtambo huo baada ya kununuliwa na mradi wa NAFAKA ulikabidhiwa taasisi binafsi inayojulikana kwa jina la ZAIDI kwa mujibu wa makubaliano kwa lengo la kuzalisha mbolea hiyo kibiashara na kuwapatia wakulima. Hata hivyo, Taasisi hiyo ilishindwa kuendeleza kazi hiyo kwa hoja ya kwamba mbolea hiyo isingeuzika kutokana na kuwa Serikali inatoa mbolea kwa mfumo wa ruzuku. Hatimae, Wizara ilikabidhi mtambo huo kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo kwa lengo la kuzalisha mbolea hiyo kwa kulingana na mahitaji ya wakulima.

Katika kutekeleza maelekezo ya Wizara kuhusina na uendeshaji wa mtambo huo, Taasisi iliandaa na kuwasilisha Wizara ya Kilimo mpango biashara (*Business Plan*) kama ulivyotakiwa kwa ajili ya kuendesha mtambo huo. Lakini hadi sasa mpango huo umeshindikana kutekelezwa kutokana na ufinyu wa bajeti.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia utekelezaji wa hoja hii, Kamati ya PAC ilitaka kujua kwamba Zanzibar haina sera inayoelekeza utaratibu wa utafiti na matokeo yake na kuelezwa kwamba Rasimu ya Sera hiyo ipo lakini utekelezaji wake hadi kufikia kuwepo kwa chombo cha kusajili matokeo ya tafiti hadi hivi sasa hakipo.

Aidha, Kamati ilitaka kujua Wizara inatekeleza vipi maelekezo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba Wananchi wajikite zaidi na kilimo hai na kuachana na kilimo cha matumizi ya mbolea zenye kemikali na kuelezwa kwamba Taasisi inahamasisha ufanyaji wa utafiti wa mbolea asilia zinazozalishwa na huwa wanatoa matokeo ya utafiti wao na kuwaelekeza wananchi kuzitumia mbolea zilizopendekezwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo. Pamoja na juhudi hizo lakini Kamati haikuridhishwa nazo kwani ilibahatika kutembelea mashine ya kuboreshea mbolea ya kemikali ambayo ilitoa taswira kwamba ni kweli mbolea hiyo haifai maana mashine inayotumiwa ilikuwa imefanya kutu (rust). Hata hivyo, uzalishaji wake umesita kwa muda kutokana na kukosekana kwa malighali ya kuzalisha mbolea hiyo iliyoboreshwa.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Taasisi ichukue juhudi za makusudi kujikita katika utafiti wa mbolea ya kilimo hai na kuachana na kilimo cha kutumia mbolea za kemikali kwani kwa kiasi kiubwa huua viumbe viliopo ardhini ambavyo vinamchango mkubwa katika kuhuisha ardhi yetu.
2. Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kizimbani ihakikisha inalikamilisha zoezi la uanzishwaji wa Taasisi maalum itakayokuwa na jukumu la kusajili matokeo ya tafiti zote zilizofanyika Zanzibar ili tuweze kutambulika kitaifa na Kimataifa.

**Hoja nambari 3.12.4.2: Kukosekana kwa usajili wa mashamba ya Pemba**.

Ukaguzi ulipitia taarifa mbali mbali ikiwemo mihutasari ya Bodi ya Wakurugenzi, ripoti ya ziara ya Wajumbe wa Baraza la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo iliyofanyika kisiwani Pemba tarehe 28/06/2019 na kufanya mahojiano na baadhi ya wafanyakazi wa Taasisi kwa lengo la kujua mali zinazomilikiwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar. Ukaguzi umebaini Taasisi ya Utafiti wa Kilimo inamiliki mashamba yaliyopo katika vituo vyake vitano vilivyopo kisiwani Pemba ambapo dosari mbali mbali zimebainika katika maeneo hayo kama ilivyoainishwa katika ripoti ya ziara ya Wajumbe Pemba.

Ukaguzi umebaini Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar haikusajili mashamba hayo yaliopo Pemba, hivyo Taasisi haina ramani wala hatimiliki za maeneo ya vituo vilivyopo kisiwani Pemba.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Taasisi (kwa jina la Wizara) ilishayapima maeneo yake mawili (Matangatuani na Weni) na eneo la Matangatuani lina hati tayari kwa jina la Wizara. Eneo la Weni limebaki kuwa na ramani tu bila hati. Kazi hii haijakamilika kwa maeneo mengine kutokana na uhaba wa fedha pamoja na kuwa Taasisi inaweka bajeti za kufanya shughuli hizi karibu kila mwaka kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 lakini fedha hizo hazipatikani. Hata hivyo, Taasisi itaendelea kuzingatia utekelezaji wa kazi hii kadiri ya upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuifuatilia hoja hii, Kamati imebaini kwamba ni kweli wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake, hakukuwa na hatimiliki iliyopo lakini kwasasa hatimiliki ya Matangatuani imepatikana. Hata hivyo, Kamati haikuridhihwa na kutopatikana hatimiliki ya eneo la Weni hasa ukizingatia kwamba Kamati

ilitaka kupatiwa barua zilizopelekwa Wizara ya Ardhi kuomba kupatiwa hati ya maeneno tofauti ya Taasisi hii lakini kwa bahati mbaya Kamati haikupatiwa.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi ihakikishe hatimiliki ya eneo la Weni inapatikana ili kuondosha migogoro inayoweza kutokezea baadae.

## UCHUNGUZI WA HOJA ZA MDHIBITI ZA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI MAALUM WA UHAKIKI WA MADENI YA WIZARA NA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI 2021

### 4.7.1 WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

**Hoja nambari 4.7.1.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 16,324,665,566 na USD 11,701.20**

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliwasilisha agizo la kupatiwa vielelezo halisi (Original Documents) vinavyohusiana na deni la shilingi 25,082,562,879 kwa barua yenye kumbu kumbu nambari AUD/W/BMV/U/VOL.I/8 ya tarehe 22 Novemba, 2021 pamoja na kuomba kupatiwa mchanganuo wa deni hilo kwa kila anaedai na kwa kiwango halisi cha fedha kinachodaiwa kutoka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.

Katika uhakiki wa madeni ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 16,324,665,566 na USD 11,701.20 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imeridhia jumla ya shilingi 6,324,665,566 na USD 11,701.20 kuweza kulipwa kwa Wazabuni.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imepokea ripoti ya madeni ya Wazabuni wake hadi kufikia Juni 2021 baada ya kuwasilishwa kwa madeni hayo na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa lengo la kulipwa madeni hayo. Wizara iliwasilisha madeni yenye jumla ya TZS. 25,082,562,879 yakijumuisha na Taasisi zake 3 ambazo ni ZSTC, BPRA na ZFTC.

Kwa upande wa Wizara deni lilikuwa ni TZS. 503,150,701 na lilianza kupunguzwa na Wizara yenyewe kidogokidogo hadi kufikia Tzs 60,588,511 wakati tukisubiri uhakiki wa madeni kukamilishwa ns kupelekea deni halisi

kwa wakati huo ni TZS. 442,562,190.00 hivyo baada ya uhakiki wa CAG deni lilikuwa halikuthibitishwa kwa deni hili kumesababishwa pia na kukosekana kwa baadhi ya vielelezo vya malipo kuzingatiwa na muda mrefu wa madeni hayo. Pia uhamaji wa Ofisi kila baada ya muda kulipelekea kutoonekana kwa baadhi ya vielelezo hivyo kiurahisi kwa wakati.

Hata hivyo, Wizara iliendelea na juhudi za kutafuta vielelezo vya deni hilo lililobakia na kuwasilishwa kwa CAG tena kwa ajili ya uhakiki na kufanikiwa kuthibitishwa tena kwa deni la TZS 27,118,480.00. Hadi kufikia tarehe ya barua hii Wizara ina deni la TZS. 180,856,150 ambalo kati ya deni hilo liliwasilishwa halikuweza kuthibitika ambapo ndani yake kuna deni la Consultant wa ujenzi wa ZBS lenye thamani ya TZS. 111,675,175. Aidha Wizara haina taarifa rasmi juu ya madeni yaliyowasilishwa na taasisi zake kwa vile uwasilishwaji wa madeni hayo ulifanywa na taasisi zenyewe.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba watendaji wa Wizara hawakuwa na utaratibu mzuri wa kuhifadhi kumbukumbu zake kwani kuhama kwa Ofisi sio sababu ya msingi kwamba vielelezo vikosekane wakati wa kuwasilisha uhakiki.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara iandae utaratibu mzuri wa kuhifadhi kumbukumbu zake ili zitakapohitajika ziweze kupatikana kwa wakati.
2. Wizara iwasilishe vielelezo kwa Mdhibiti kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ili deni lililobakia la TZS. 180,856,150 liweze kuhakikiwa.

**Hoja nambari 4.7.1.2: Deni ambalo limekosa vielelezo vya uthibitisho kutoka kwa Mdai shilingi 1,499,983,594**

Katika uhakiki uliofanyika wa deni la Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) lenye jumla ya shilingi 24,482,223,177 ambalo liliwasilishwa na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa ajili ya kuhakikiwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwa mujibu wa barua yenye kumbu kumbu nambari WBMV/M.130/C20/VOL.1/84 ya tarehe 10 Disemba 2021. Ukaguzi umebaini kati ya deni hilo jumla ya shilingi 1,499,983,594 ni deni la kodi (Corpotative Tax) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

ambalo anadai kwa Shirika la Maendeleo ya Viwanda.

Hadi ukaguzi unakamilika TRA imeshindwa kukamilisha vielelezo vya uthibitisho wa uwepo wa deni hilo la shilingi 1,499,983,594. Kwa hivyo ukaguzi haukuweza kuthibitisha kuwa deni hilo ni halali kutokana na kukosekana kwa vielelezo kutoka kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu nambari CBC.A3/170/11/20 ya tarehe 12 Oktoba 2021 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilipokea barua niliyoinakili hapo juu inayoonesha Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda iliiwasilishia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango jumla ya deni la Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali shilingi 25,082,562,879 na USD 14,982.

Katika uhakiki wa deni hilo imebainika jumla ya shilingi 16,324,665,566 na USD 11,701.20 ndio deni halali kwa mujibu wa vielelezo nilivyowasilishiwa na kuvihakiki kutoka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda na kupelekea tofauti ya shilingi 8,757,897,313 na USD. 3,280.80 ambazo uwepo wa uhalali wa deni hilo haukuweza kuthibitika kutokana na kukosekana kwa vielelezo halisi vya deni hilo.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2021/2022 Shirika lilikuwa likikabiliwa na madeni kutoka katika Taasisi mbalimbali pamoja na Watoa huduma wengine, madeni hayo yalishindwa kulipwa kwa wakati kutokana na uhaba wa fedha uliokuwa unalikabili Shirika. Baadhi ya taasisi hizo ni pamoja na PBZ (bilioni 8.0 bila ya riba) na ZSSF (bilioni 5.0 bila ya riba). Aidha, Shirika lilikuwa linadaiwa jumla ya tani 596.4 za karafuu kutoka kwa wanunuzi wa karafuu, tani hizo za karafuu zilikuwa zina thamani ya jumla ya TZS 6.7 bilioni.

Katika upande wa watoa huduma ni kwamba hadi mwaka unaanza Shirika lilikuwa linadaiwa na watoa huduma wawili ambao ni Kampuni ya ZECCON Construction amabae alijenga Jengo la Kitega Uchumi liliopo Malindi (huyu alikuwa anadai jumla ya TZS 708.0 Milioni) pamoja na Kampuni ya SALEM CONTRUCTION ambae anajenga Jengo la Madungu (huyu alikuwa anadai jumla ya TZS 923.0 milioni).

Madeni mengine ya Shirika ni pamoja na TZS 377.0 milioni kutoka Wizara ya Vijana kwa ajili ya mradi wa Pilipili, madeni ya viinua mgongo TZS 1.002 bilioni, na madeni kutoka kwa taasisi za kodi (TRA TZS 32,7863,981.32 na ZRB 66,696,000.00)

Napenda kuiarifu Kamati kwamba hadi kufikia tarehe ya leo, Shirika lilishamaliza kuyalipa madeni yote ambayo ni TZS 21.7 bilioni yaliyotajwa hapo juu ambapo TZS, 8.0 bilioni zililipwa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango na kilichobakia TZS 13.7 bilioni zililipwa na Shirika lenyewe kupitia vyanzo vyake vya ndani vya mapato. Aidha, hivi sasa Shirika linadaiwa fedha za riba (2.4 bilioni) kutoka Mfuko wa Hifadhio ya Jamii (ZSSF).

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile Shirika limeeleza kwamba tayari wameshakamilisha malipo kwa Watoa huduma na wamebakia na deni la riba pekee. Hivyo, Kamati imeielekeza Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufuatilia ulipwaji wa madeni hayo kama umefuata misingi ya sheria na ukaguzi.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamari ya PAC**

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ifuatilie ulipwaji wa madeni hayo kama umefuata misingi ya sheria na ukaguzi.

**Hoja nambari 4.7.1.3: Madeni yasiyokuwa na vielelezo shilingi 45,869,775**

Katika uhakiki uliofanyika imebainika uwepo wa deni la shilingi 45,869,775 lililowasilishwa kudaiwa na wazabuni mbali mbali ambao kutokana na huduma au bidhaa walizotoa ambalo hadi uhakiki unakamilika hatukupatiwa vielelezo halisi vinavyothibitisha uhalali wa uwepo wa deni hilo. Kukosekana kwa vielelezo hivyo kunapelekea kushindwa kuishauri Serikali kufanya malipo kwa Wazabuni hao.

**Jadweli Nambari 33: Madeni yasiyokuwa na vielelezo**

| Nambari | Mzabuni/Mdai | Kiasi cha Deni (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Zan Catering and Take Away Co. Ltd | 800,000 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Katibu Mkuu WBVM | 720,000 | Kukosekana kwa uthibitisho wa vielelezo halisi vya uwepowa madeni hayo. |
| 3. | Katibu Mkuu WBVM | 560,000 | |
| 4. | Smart Future Company | 603,000 | |
| 5. | Skotch Gen Supplies Co.Ltd | 855,000 | |
| 6. | Double Two Gen. Supply | 900,000 | |
| 7. | Katibu Mkuu WBMV | 230,000 | |
| 8. | Katibu Mkuu WBMV | 900,000 | |
| 9. | Vetah Hardware Tools | 4,624,659 | |
| 10. | Tahfif Auto Parts | 2,030,000 | |
| 11. | Katibu Mkuu WBMV | 560,000 | |
| 12. | Katibu Mkuu WBMV | 7,984,000 | |
| 13. | Decco | 1,568,600 | |
| 14. | Nasir Take Away | 731,000 | |
| 15. | Deni la marehemu Hemed Bakari Kondo | 4,955,000 | |
| 16. | Miembeni Lubricant | 743,617 | |
| 17. | Katibu Mkuu WBMV | 4,119,899 | |
| 18. | Katibu Mkuu WBMV | 1,710,000 | |
| 19. | Fay Shao | 11,275,000 | |
| **Jumla** | | **45,869,775** | |

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ilielezwa kwamba majibu ya hoja hii yamejibiwa kwa pamoja kama yanavyojionesha katika hoja nambari 4.7.1.1.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile majibu yalijibiwa kwa pamoja. Hivyo, uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ni kama yanavyoonekana katika Hoja nambari 4.7.1.1:

**Hoja nambari 4.7.1.4: Kutokuwiana kwa vielelezo halisi vya deni la shilingi 2,083,800 na USD. 4,778.92**

Katika uhakiki wa deni la shilingi 62,083,800 na USD 4,778.92 uliofanyika imebainika uwepo wa utofauti wa vielelezo vilivyofunganishwa na uhalisia wa deni linalodaiwa jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa tofauti ya deni la shilingi 18,902,000 na USD 2,770.79 ambalo halikuthibitika uhalali wa uwepo wake.

| Namba | Mzabuni/ Mdai | Kiasi cha deni kilichowasili shwakwa ukaguzi (Tshs) | Kiasi cha deni kilichothibiti shwakwa mujibu wa Vielelezo (Tshs) | Uwepo wa tofauti ya denilisilo vielelezo (Tshs) |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | TZ STD NEWSPAPER | 6,241,800 | 4,141,800 | 2,100,000 |
| 2. | Smart Future Company | 1,000,000 | 920,000 | 80,000 |
| 3. | Katibu Mkuu WBMV | 1,305,000 | 1,275,000 | 30,000 |
| 4. | Katibu Mkuu WBMV | 4,246,000 | 2,070,000 | 2,176,000 |
| 5. | Shirika la Magazeti | 34,229,000 | 26,614,000 | 7,615,000 |
| 6. | Katibu Mkuu WBMV | 7,062,000 | 5,161,000 | 1,901,000 |
| 7. | Katibu Mkuu WBMV | 8,000,000 | 3,000,000 | 5,000,000 |
| 8. | Knight Frank | USD 4,778.92 | USD 2,008.13 | USD 2,770.79 |
| 9. | Simba Spare Part | 2,000,000 | 4,854,000 | 2,854,000 |
| 10. | ZBC | 6,354,300 | 9,666,350 | 3,312,050 |
| **Jumla Tshs** | | **62,083,800** | **43,181,800** | **18,902,000** |
| **Jumla USD** | | **4,778.92** | **2,008.13** | **2,770.79** |

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ilielezwa kwamba majibu ya hoja hii yamejibiwa kwa pamoja kama yanavyojionesha katika hoja nambari 4.7.1.1.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile majibu yalijibiwa kwa pamoja. Hivyo, uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ni kama yanavyoonekana katika Hoja nambari 4.7.1.1:

**Hoja nambari 4.7.1.5: Madeni yenye vielelezo pungufu shilingi 42,669,000**

Katika uhakiki wa madeni uliofanyika imebainika uwepo wa deni la shilingi 42,669,000 ambazo zinadaiwa na watoa huduma mbali mbali wanaoidai Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ukaguzi umebaini uwepo wa tofauti ya shilingi 7,708,000 ambapo deni hilo halikuwa na vielelezo vinavyojitosheleza. Aidha, kutokana na hali hiyo ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 28,961,000 ndizo zilizokuwa na vielelezo vinavyojitosheleza kulipwa deni hilo.

| Namba | Mzabuni | Kiasi kilichowasilishwa kwa uhakiki (Tshs) | Kiasi kilichothibitishwa kwa mujibu wa vielelezo (Tshs) | Tofauti (Tshs) | Vielelezo vilivyokosekana |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Katibu Mkuu WBMV | 3,000,000 | 700,000 | 2,300,000 | Orodha ya wajumbena |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ankara za malipo |
| 2. | Zenj Holding Ltd | 37,541,000 | 33,541,000 Deni hililimelipwa kiasi cha shilingi 6,000,000 na kinachodaiwa ni shilingi 27,541,000 | 4,000,000 | Mkataba wa madai hayo umekosekana kwa uhakiki |
| 3. | Katibu Mkuu WBMV | 2,128,000 | 720,000 | 1,408,000 | Iliyowasilishwa ni dokezo la 720,000 la tiketi za kusafiria |
| **Jumla** | | **42,669,000** | **28,961,000** | **7,708,000** | |

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ilielezwa kwamba majibu ya hoja hii yamejibiwa kwa pamoja kama yanavyojionesha katika hoja nambari 4.7.1.1.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile majibu yalijibiwa kwa pamoja. Hivyo, uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ni kama yanavyoonekana katika Hoja nambari 4.7.1.1:

**Hoja nambari 4.7.1.6: Kutokuthibitika kwa uhalali wa deni la shilingi 135,494,855 na USD 510**

Katika uhakiki uliofanyika ukaguzi uliangalia vielelezo vilivyofunganishwa yakiwemo madokezo, barua za madai pamoja na ankara za malipo ili kupata na kuona uhalali wa madeni hayo. Ukaguzi umebaini uwepo wa utofauti wa kiasi kilichowasilishwa baina ya ankara na dokezo kwa baadhi ya madeni, pamoja na utofauti wa kiasi kilicholipwa na kiasi kinachodaiwa, hivyo kupelekea uhakiki kushindwa kupata uhakika wa deni hilo.

| Namba | Mzabuni/Mdai | Kiasi cha deni kilichowasilishwa kwauhakiki (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Al–Qassmy Trading Corporation | 14,900,200 | Vielelezo vilivyoambatanishwa ni tofauti, kwa mujibu wa vielelezohavifanani na deni. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Katibu Mkuu Kitengo cha Mawasiliano | 1,200,000 | Vielelezo vilivyoambatanishwadeni hili vinaonyesha tayari limeshalipwa. |
| 3. | Tantred TZ | 7,719,480 | Kwa mujibu wa vielelezo vilivyoambatanishwa mzabunihuyu hadai. |
| 4. | Onspace Consult Co. Ltd | 111,675,175 | Vielelezo vilivyoambatanishwahavihusiani na deni hili |
| **Jumla (Tshs)** | | **135,494,855** | |
| 5. | ZRB (USD) | 510 | Kwa mujibu wa vielelezo denihili limeshalipwa |

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ilielezwa kwamba majibu ya hoja hii yamejibiwa kwa pamoja kama yanavyojionesha katika hoja nambari 4.7.1.1.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile majibu yalijibiwa kwa pamoja. Hivyo, uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ni kama yanavyoonekana katika Hoja nambari 4.7.1.1:

## 4.7.2 IDARA YA MAKUMBUSHO NA MAMBO YA KALE

**Hoja nambari 4.7.2.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 91,890,525**

Katika uhakiki wa madeni ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 91,890,525 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo livyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha Ofisi yaMdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imeridhia jumla ya shilingi 91,890,525 kuweza kulipwa kwa Wazabuni na wadai.

**Majibu ya Uongozi wa Idara**

Ni kweli Idara iliwasilisha deni la TZS.109,720,985 Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya uhakiki, na baada ya uhakiki huo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakatuwasilishia deni la TZS. 91, 890, 520.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara imebaini kwamba bado kuna madeni mengine ambayo Idara inadaiwa na Wazabuni yaliyokuwa hayajalipwa wala kuwasilishwa katika Ofisi ya Mkaguzi. Hivyo, Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Utalii awasilishe vielelezo vyake Wizara ya fedha ili yawasilishwe Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar.

### 4.7.3 TAASISI YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA

**Hoja nambari 4.7.3.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 50,624,408**

Katika uhakiki wa madeni ya Taasisi ya Nyaraka na Kumbu kumbu za Taifa imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 50,624,408 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imeridhia jumla ya shilingi 50,624,408 kuweza kulipwa kwa Wazabuni.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa ilibaini mapungufu katika madai ya wafanyakazi yaliyowasilishwa kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Aidha, tofauti hiyo ilitokana na kuachwa kwa madai ya muda wa ziada kwa wafanyakazi kwa mwezi wa Aprili 2021 na kupelekea tofauti iliyojitokeza. Hivyo, vielelezo vya madai hayo vipo na ni kutokana na uharaka wa uwasilishaji ndio ulichangia kutokea kwa kasoro hiyo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Taasisi kukiri kuwepo kwa kasoro za kutowasilisha deni la malipo kwa wanafunzi wao. Kamati ya PAC imeungana na hoja ya Mkaguzi na kubaini kwamba baadhi ya watendaji waliopo katika Wizara za Serikali huwa hawayatilii maanani maombi ya Taasisi zao inazozisimamia. Hili limebainika baada ya watendaji wa Taasisi hii kuandika barua katika Wizara yao yenye kumbukumbu nambari NKT/07/04/VOL.X/18 ya tarehe 2/8/2021 kuhusu uwepo wa vielelezo vya madeni ya Wanafunzi yaliyoelezwa katika na Mkaguzi kwamba yamekosa vielelezo lakini hadi Kamati ya PAC inapokea majibu ya Taaisisi hii, bado barua hiyo haijajibiwa.

Kamati imegundua kuwa baadhi ya watendaji wa Serikali (Wizarani) huwa wanazembea katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kutoyashughulikia madeni hususan yenye haki za watu ndani bila ya kuwa na sababu za msingi.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ihakikishe inaiandkia Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu uwepo wa vielelezo husika ili nao waiombe Ofisi ya Mkaguzi kujiridhisha kutokana na vielelezo hivyo.
2. Watendaji wa Wizara watekeleze majukumu yao kwa uweledi ili maombi yanayowasishwa kwao yasichukue muda yaweze kujibiwa kwa wakati.

**KAMISHENI YA UTALII**

### 4.7.4.1 Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 196,220,576 na USD 1,604

Katika uhakiki wa madeni ya Kamisheni ya Utalii imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 196,220,576 na USD 1,604 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha Ofi si ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imeridhia jumla ya shilingi 196,220,576 na USD 1,604 kuweza kulipwa kwa wazabuni na Wadai.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Kamisheni ya Utalii ni miongoni mwa taasisi za Serikali zilizowasilisha madeni yake katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya uhakiki na kupelekwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili malipo kwa bahati mbaya kuna baadhi ya madeni hayakuwepo kwenye orodha ya madeni yaliyopelekwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili malipo.

Madeni hayo ni ya wafanyakazi pamoja na Shirika la Magazeti la Serikali. Tuliulizia kwa barua KUM.K/UT/2013/2/73/VOL.1/10 ya tarehe 07/06/2022 yenye mada ya uhakiki wa deni la Serikali madeni hayo kwanini hayamo katika orodha ya madeni yatakayolipwa lakini hatukupata majibu yoyote, ukizingatia vielelezo vya madeni hayo vipo. Kwa hiyo madeni ambayo tuliambiwa ni sahihi ni TZS. 196,220,576 na USD 1,604 na RMB 5,800 lakini tulizoingiziwa ni TZS. 196,220,576 tu kwa ajili ya malipo ya madeni hayo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba wakati Mkaguzi anafanya uhakiki wake na kutaka vielelezo viwasilishwe Ofisini kwake, Wizara haikumpatia kaguzi vielelezo hivyo kwa kufanyiwa uhakiki na malipo. Kwa mnasaba huo, Kamati

imegundua Wizara haikuwa na utaratibu mzuri wa uwekaji wa kumbukumbu zake.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamisheni iandae utaratibu mzuri wa kuhifadhi kumbukumbu zake ili zitakapohitajika ziweze kupatikana kwa wakati.
2. Kamisheni iwasilishe vielelezo kwa Mdhibiti kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ili deni lililobakia la TZS. USD 1,604 na RMB 5,800 liweze kuhakikiwa.

### 4.7.5 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

**Hoja nambari 4.7.5.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 4,489,639,946.06**

Katika uhakiki wa madeni ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 4,489,639,946.06 ambayo yamehakikiwa na kuthibitisha uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha, Ofisi ya Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imeridhia jumla ya TZS 4,489,639,946.06 kuweza kulipwa kwa Wazabuni kama inavyoonekana katika Jadweli Nambari 41.

**Majibu ya Uongozi wa Idara**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iliwasilisha barua ya madeni ya kumbukumbu namba WEMA/W/OR/F/M/004/VOL.XV1.21 ya tarehe 24/11/2021, inakiri kuwa ilikuwa na orodha ya madeni Jumla TZS. 4,806,415,996.86 hadi kufikia tarehe ya kukabidhi madeni hayo tulikuwa na jumla ya deni la TZS 4,670,514,197.06 kwa Unguja na Pemba kwani Wizara kabla ya kuzuia ilikuwa ikitumia fedha zake kwa kupunguza madeni hayo. Kwa hiyo, miongoni mwa tofauti iliyojitokeza ilikuwa tayari tushapunguza deni la TZS. 135,901,799.80.

Kufikia tarehe 30 Machi 2022 Ofisi ya Rais, fedha na Mipango ilichukuwa jitihada nzuri na kutuingizia jumla ya TZS. 4,834,000,388.06 kwa Wizara na Taasisi zake kwa ajili ya kulipia madeni hayo ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameyakubali na tayari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imelisimamia na kulipa fedha hizo kwa wadai stahiki.

Tofauti kwa mujibu wa kiambatanisho cha Wizara ni TZS. 180,874,251 kati ya hizo TZS. 88,949,625 kwa upande wa Unguja na TZS. 91,984,626 kwa upande wa Pemba na sio tofauti ya TZS. 314,112,297.64. Kwa upande mwengine kuna baadhi ya madeni Mkaguzi hakuweza kujiridhisha na kazi iliyofanywa na Mkandarasi SARASAA CONSTRUCTION LTD. ambaye aliingia mkataba na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, mkataba namba SMZ/K01/W/Q/2020 - 2021/28. Mkataba ulikuwa na jumla ya TZS. 41,682,900 akalipwa TZS. 10,420,7250 bakaa ya deni TZS. 31,262,175. Baadhi ya madeni yalikuwa ya mwaka wa fedha unofuata wakaguzi waliishia 30 Juni, 2021.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini jumla ya deni la shilingi milioni 80 limegunduliwa na Mkaguzi kwamba limewasilishwa na Wizara lakini halikuwa na vielelezo. Hatimae, halikuidhinishwa na Mkaguzi kulipwa. Aidha, Kamati imebaini kwamba Wizara iliwasilisha madeni mengi katika Ofisi ya Mdhibiti lakini adeni hayo yamekosa uhalali kwa vile hayakuwa katika muda wa ukaguzi maana yalikuwa ya mwaka 2021. Hata hivyo, Kamati imeelekeza kwamba madeni hayo yatakuja kulipwa baada ya uhakiki kufanyika.

Kamati inaungana na Mkaguzi kwamba deni lililokuwa halijahakiki milioni 17 kwa vile Mkaguzi alipofika katika Idara hii, hakupatiwa vielelezo pamoja na kuwa Kamati imeelezwa vielelezo vipo lakini Kamati haijavipokea vielelezo hivyo. Hali hii ilichangiwa zaidi na kutokuwepo mashirikiano baina ya Mkaguzi na Watendaji wa Idara.

Aidha, Kamati imeelezwa kwamba bado kuna vielelezo vya madeni ya Wazabuni ambao tayari wameshatoa huduma lakini hakuna vielelezo vya kupatiwa malipo kwa huduma waliyoitoa. Hii ni kwasababu kuna Wazabuni wawili baada ya kuhakikiwa madeni yao na Ofisi ya Mdhibiti walifuatilia haki ya malipo yao kwa kutafuta vielelezo na kuviwasilisha katika Idara ya Makumbusho ili waweze kulipwa malipo yao. Hata hivyo, Idara haikuyarudisha malipo hayo katika Ofisi ya Mdhibiti ili yaweze kuhakikiwa na kupatiwa mrejesho juu ya uhalali wa madeni hayo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Idara ihakikishe inakusanya vielelezo vya madeni ya Wazabuni wanaoidai Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuiandikia Wizara ya Fedha ili wawaandikie Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa uhakiki.

### 4.7.6 BARAZA LA MITIHANI ZANZIBAR

**Hoja nambari 4.7.6.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 245,945,000**

Katika uhakiki wa madeni ya Baraza la Mitihani Zanzibar imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 245,945,000 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha Ofi si ya Mdhibiti na MkaguziMkuu wa Hesabu imeridhia jumla ya shilingi 245,945,000 kuweza kulipwa kwa wazabuni.

**Majibu ya Uongozi wa Idara**

Fedha hizo zimeshalipwa na vielelezo vipo Madeni yenye jumla ya TZS 67,614,305 yalikusudiwa kulipwa kama ifuatavyo:

- TZS 16,208,000 ni fedha ambazo zililipwa hapo awali kupitia fedha za Matumizi mengineyo (OC) zilizoingiziwa Baraza hapo awali ambapo ufafanuzi wake ulishaelezewa katika barua yenye kumbu kumbu BMZ/MDH/M/MKUU/VOL.1 ya tarehe 23/11/2021 (Barua imeambatanishwa)
- TZS 24,953,400 ni sehemu ya fedha za Mkataba wenye jumla ya TZS. 213,380,000/= zilizotarajiwa kulipwa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa ajili ya ulishaji wa chakula katika kambi za Usahihishaji wa Mitihani ya Taifa ya mwaka 2020, ambap hapo awali jumla ya TZS 138,697,000/= zililipwa (kopi ya mkataba umeambatanishwa).
- TZS 1,525,905 ni sehemu ya fedha za Mkataba wenye jumla ya TZS. 46,320,300/= zilizotarajiwa kulipwa Taasisi ya utalii kwa ajili ya ulishaji wa chakula katika kambi za Usahihishaji wa Mitihani ya Taifa ya mwaka 2020, ambap hapo awali jumla ya TZS 30,108,195/= zililipwa (kopi ya mkataba umeambatanishwa).
- TZS 21,600,000 ni fedha zilizokusudiwa kulipwa watendaji wa Baraza walioshiriki kazi mbali mbali za Usimamizi, Usahihishaji, Utoaji wa matokeo pamoja na Uandaaji wa Ripoti ya Mitihani ya Taifa ya mwaka 2020 (kopi za vielelezo zimeambatanishwa).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba pamoja na madeni yaliyowasilishwa na Baraza katika Ofisi ya Mkaguzi, hata hivyo kuna deni la shilingi milioni 67 Baraza halijaliwasilisha kwa ukaguzi. Kamati imesisitiza deni litakalowasilishwa liwe ndani ya mwaka husika (2015 hadi Agosti, 2020).

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo**

Baraza liyatafute madeni pamoja na vielelezo vyake na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango ili yaweze kuhakikiwa na Ofisi ya Mkaguzi.

### 4.7.7 TAASISI YA ELIMU YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA KARUME

**Hoja nambari 4.7.7.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 93,860,892**

Katika uhakiki wa madeni ya Taasisi ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia Karume imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 93,860,892 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imeridhia jumla ya shilingi 93,860,892 kuweza kulipwa kwa Wazabuni.

**Majibu ya Uongozi wa Taasisi**

Ni kweli Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliwasilisha agizo la kupatiwa vieleleza halisi (original Supporting Documents) vinavyohusiana na deni la shilingi 111,192,892/= kwa barua yenye kumbukumbu namba AUD/WEMA/TKST/10/4/VOL.1/1 ya tarehe 22 Novemba 2021. Hata hivyo, baada ya uhakiki uliofanywa na Ofisi ya Mdhibiti wamebaini deni linalostahili kulipwa kutokana na vielelezo vyake kukamilika ni jumla ya shilingi 93,860,892, ambazo fedha zake ziliingizwa kwa ajili ya ulipaji wa wazabuni husika. Madeni ya Wazabuni yamefanywa kwa mujibu wa taratibu za fedha zinavyoelekeza ambapo vielelezo vya malipo hayo pamoja na risiti zake vimeambatanisha kwa ajili ukaguzi zaidi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Taasisi kukubaliana na hoja ya Mkaguzi, hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini watendaji wa Taasisi hii hawakutoa mashirikiano kwa Mkaguzi na ndio maana baada ya kupita Kamati vielelezo vinaonekana kuwepo lakini Kamati imeshindwa kuvikagua kutokana na kuwepo wasiwasi wa usahihi na uhalali wake.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya kamati ya PAC**

Kwa vile Taasisi imeeleza kwamba vielelezo vipo, ni vyema ikaviwasilisha Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ili viwasilishwa Ofisi ya Mkaguzi kwa uhakiki na ukaguzi juu ya uhalali wake.

## 4.7.8 WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

### Hoja nambari 4.7.8.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 574,784,657

Katika uhakiki wa madeni ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 574,784,657 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha Ofi si ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 574,784,657 kuweza kulipwa kwa Wazabuni.

(OR)KSUUB inapenda kukujuulisha kuwa ilipokea Jumla ya Tsh 162,411,846.00 kwa ajili ya malipo ya Madeni kwa mchanganuo ufuatao;

OR-KSUUB – UNGUJA – TZS. 54,691,019.002. Ofisi ya Mufti – 7,912,939.00 3. Chou cha Utawala wa Umma (IPA) – 6,757,050.00 4. Tume ya Utumishi Serikalini – TZS. 9,654,500 5. Tume ya maadili ya viongozi wa umma – TZS 73,396,338.00 Madeni haya yalilipwa kwa wahusika na madeni yaliyobakia Jumla ya Tsh. 412,372,811.00 waliingiziwa taasisi mbali mbali na kukamilisha malipo ya deni la Tsh. 574,784,657.00 taasisi hizo ni;-

a) Ofisi ya Rais KSUUB- Pemba.
b) Mahkama Kuu.
c) Tume ya Maadili ya Viongozi wa umma.
d) Tume ya Maadili ya Viongozi wa umma - Pemba.
e) DPP.

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kwa vile Wizara imeeleza kwamba tayari imeshakamilisha malipo ya deni lililokaguliwa na kuhakikiwa na Ofisi ya Mkaguzi, Kamati inaielekeza Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufuatilia ulipwaji wa fedha hizo ili kujua kama zimelipwa kwa mujibu wa taratibu ama vyenginevyo.

## 4.7.9 WAKALA WA SERIKALI MTANDAO (e-Government of Zanzibar)

Wakala wa Serikali Mtandao iliwasilisha madeni yenye jumla ya shilingi 136,942,806.44 kutoka kwa watoa huduma ICOMNET TECHNOLOGIES (shilingi 18,821,000) na DIMENTION DATA TANZANIA LTD (shilingi 118,121,806). Ukaguzi umepitia taarifa zilizo ambatanishwa pamoja na orodha ya madeni hayo, sambamba na kufanya mahojiano na maafisa wa Wakala wa Serikali Mtandao kuhusiana na uwepo wa madeni hayo na kubaini yafuatayo:

1. ICOMNET TECHNOLOGIES (Redundancy Web&Mail server Development, integration & Data Migration charges C-panel Annual licences fee for 100 domains) . Ukaguzi haukupata Mkataba halali wa makubaliano ya utoaji wa huduma baina ya Mtoa huduma (ICOMNET TECHNOLOGIES) na Wakala (e-Government of Zanzibar) na kwamba makubaliano ya utoaji wa huduma hiyo hayakuwa rasmi. Aidha huduma iliyotakiwa kutolewa na Mtoa huduma huyo haikukamilika. Hivyo ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa deni hilo.

**Majibu ya Uongozi wa Wakala**

Taarifa za madeni ya Wakala wa Serikali Mtandao zilizowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, zinahusika na madeni ya nyuma ambayo yamerithiwa na Wakala kutoka kwa iliyokuwa Idara ya Serikali Mtandao ya Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

Wakati wa uhakiki wa Deni hilo la Shilingi 18,821,000, Wakala wa Serikali Mtandao ilifanya jitihada za kuwasiliana kwa njia ya simu na Mtoa huduma ICOMNET TECHNOLOGIES ambae ofisi zake zipo Dar es Salaam bila mafanikio hivyo ikaona ni vyema kukubaliana na Ofisa Mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa uthibitisho wa Deni lililotajwa umeshindwa kupatikana.

2. DIMENTION DATA TANZANIA LTD (Microsoft 365 E3 renewal). Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Serikali Mtandao haijawahi kupokea huduma hiyo kutoka kwa Mtoa huduma huyo. Na kwamba, Deni la shilingi 118,821,000 lililoainishwa katika orodha ya madeni ni mapendekezo ya fees mpya (kama inavyoonekana katika “quotation” ya tarehe 14 Machi, 2021) ambayo Wakala alitakiwa kulipa katika makubaliano mapya ya upatikanaji wa huduma hiyo. Hata hivyo Wakala hakuingia tena katika makubaliano hayo. Hivyo, ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa deni la shilingi 136,942,806 kama lililowasilishwa na Wakala wa Serikali Mtandao.

**Majibu ya Uongozi wa Wakala**

Ni kweli kuwa Deni la Shilingi 118,821,000 la mtoa huduma DIMENTION DATA TANZANIA LTD liliorodheshwa kimakosa katika Orodha ya madeni ya taasisi za Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa kuwa makubaliano mapya ya kuendelea na huduma za mtoa huduma huyo hayakufikiwa.

Ni kweli kuwa Deni la Shillingi 118,821,000 la mtoa huduma DIMENTION DATA TANZANIA LTD liliorodheshwa kimakosa katika Orodha ya madeni ya taasisi za Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa kuwa

makubaliano mapya ya kuendelea na huduma za mtoa huduma huyo hayakufikiwa. Maktaba Zanzibar imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 4,554,550 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 4,554,550 kuweza kulipwa kwa Wazabuni kiasi cha fedha shilingi milioni nne laki tano hamsini nan ne elfu mia tano na hamsini tu (4,554,550.00) zimeingizwa kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na madeni yenye kiasi kilichoainishwa hapo juu yameshalipwa. Hata hivyo deni hili ni kwa upande wa Afisi ya Shirika la Huduma za Maktaba Pemba na fedha hizo zilihaulishwa kwenda kwenye akaunti namba 0404444000 Maktaba Kuu Pemba tarehe 10 Mei, 2022.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile Wakala umeeleza kwamba tayari wameshakamilisha malipo kwa Watoa huduma na wala hawana deni wanalodaiwa. Hivyo, Kamati inielekeza Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufuatilia ulipwaji wa madeni hayo kama umefuata misingi ya sheria na ukaguzi.

### 4.7.10 SHIRIKA LA HUDUMA ZA MAKTABA ZANZIBAR

**Hoja nambari 4.7.10.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 4,554,550**

Katika uhakiki wa madeni ya Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 4,554,550 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 4,554,550 kuweza kulipwa kwa Wazabuni.

**Majibu ya Uongozi wa Shirika**

Hoja hii imepokelewa, deni hili lilihakikiwa na kiasi cha fedha shilingi milioni Nne Laki Tano Hamsini na Nne Elfu Mia Tano na Hamsini tu (4,554,550.00) zimeingizwa kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na madeni yenye kiasi kilichoainishwa hapo juu yameshalipwa. Hata hivyo, deni hili ni kwa upande wa Afisi ya Shirika la Huduma za Maktaba Pemba na fedha hizo zilihaulishwa kwenda kwenye akaunti namba 404444000 Maktaba Kuu Pemba tarehe 10 Mei 2022.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile madeni ya Shirika yaliyohakikiwa na kuthibitishwa yameshalipwa, Kamati haikuwa na hoja zaidi isipokuwa imesisitiza kwamba Shirika liweke utaratibu mzuri wa kuyalipa madeni yake kwa wakati.

### 4.7.11 WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR

**Hoja nambari 4.7.11.1 Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 103,606,168**

Katika uhakiki wa madeni ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 103,606,168 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 103,606,168 kuweza kulipwa kwa Wazabuni.

**Majibu ya Uongozi wa Wakala**

a) ZCSRA iliwasilisha Tshs. 216,471,910 kama deni kwa kuwa ilikuwa ndio Fedha ambayo ilikuwa haijalipwa kwa ZIT katika mkataba wa vifaa vya Tshs. 336,000,000. ZCSRA haikuwa imeangalia kuwa wakati inawasilisha deni hilo bado ZIT ilikuwa haijakamilisha idadi ya vifaa vilivyotakiwa kufika ZCSRA.

b) Kabla Ofisi ya CAG kufanya uhakiki wa deni, ZCSRA ilipata Fedha kupitia OC ya mwezi Machi 2022, na kuelekezwa kuwa itumie Fedha hizo kupunguza madeni (hiyo ilikua kabla kutolewa toleo la kuzuia kulipa madeni kupitia Fedha za OC). Hivyo, wakati uhakiki unafanyika, ZCSRA ilikuwa tayari imeshalipunguza deni hilo kwa kulipa Tshs. 102,041,000 deni hilo kwa kulipa Tshs. 102,041,000.

Kwa sababu hizo mbili za hapo juu ni kwamba, idadi ya vifaa ilivyokuwa imepatiwa ZCSRA na ZIT sambamba na kupunguzwa kwa deni, ndio maana ilionekana kuwa deni halisi ni Tshs. 23,114,015. Tofauti inayoonekana katika uhakiki wa deni la ZAGPA inatokana na kwamba, kama ilivyoelezwa hapo juu, deni llilipunguzwa kwa kulipwa Tshs. 32,000,000 kabla ya Ofisi ya CAG kufanya uhakiki. Tofauti inayoonekana katika uhakiki wa deni la Super Refregeration inatokana na kwamba, kama ilivyoelezwa hapo juu, deni llilipunguzwa kwa kulipwa nusu ambayo ni sawa na Tshs. 1,770,000 kabla ya Ofisi ya CAG kufanya uhakiki. Tofauti inayoonekana katika uhakiki wa deni la Jawaja Auto Parts inatokana na kwamba, kama ilivyoelezwa hapo juu, deni llilipunguzwa kwa kulipwa Tshs 6,730,950 kabla ya Ofisi ya CAG kufanya uhakiki. Uhakiki wa CAG wa Deni hili umebaini kuwa, deni halisi ni Tshs 6,886,611. Tofauti iliyopo inatokana na sababu ambazo ni:

Mkaguzi kutokubaliana na baadhi ya vielelezo vilivyowasilishwa. Deni lilipunguzwa kwa kulipwa Tshs. 2,845,000 kabla ya Ofisi ya CAG kufanya uhakiki.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa Baadhi ya Taasisi zimefanya malipo ya madeni kabla ya kuhakikiwa na kuthibitishwa na Mkaguzi (CAG). Hata kama malipo hayo yatakuwa yamelipwa kwa wahusika lakini Kamati imegundua malipo ya namna hiyo hayajafuata utaratibu unaotakiwa kwani yalitakiwa yahakikiwe kwanza na ndipo malipo yafanyike kwa yale madeni yaliyohakikiwa pekee na sio vyenginevyo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ihakikishe inafanya Ukaguzi Maalum kwa fedha zote zilizolipwa na Wakala na zile zinazodaiwa ili kuweza kubaini kama zimelipwa au kudaiwa kwa mijubu wa sheria na baadae kuyainisha katika Ripoti ili kubaini fedha za Serikali zilizotumika na kupotea pasi na kuwepo kwa tija yoyote.

### 4.7.12 HOSPITALI YA MNAZIMMOJA

**Hoja nambari 4.7.12.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 147,245,100**

Katika uhakiki wa madeni ya Hospitali ya Mnazi Mmoja imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 147,245,100 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 147,245,100 kuweza kulipwa kwa Wazabuni.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, baada ya uhakiki kukamilika deni lote lililohakikiwa limekubalika kulipwa. Mnamo tarehe 22/03/2023 Hospitali ya Mnazi mmoja ilipokea barua ya ulipaji wa deni hilo yenye kumbukumbu namba CDB.121/199/01/4/07 ya tarehe 17/03/2023 yenye mada: Malipo ya deni lililohakikiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Na mnamo tarehe 22/03/2023 TZS. 147,245,100 na tayari malipo yameshafanyika.

**Majibu ya Uongozi wa Wakala**

Hospitali ya Mnazi mmoja inakiri kuhakikiwa kwa deni la TZS.147,245,100 kutoka kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar. Na baada ya uhakiki kukamilika deni lote lililohakikiwa limekubalika kulipwa. manamo tarehe 22/03/2023 Hospitali ya Mnazi mmoja ilipokea barua ya ulipaji wa deni hilo yenye kumbukumbu namba CDB.121/199/01/4/07 ya tarehe 17/03/2023 yenye mada: Malipo ya deni lililohakikiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Na mnamo tarehe 22/03/2023 TZS.147,245,100 na tayari malipo yameshafanyika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na kulipwa kwa deni lililohakikiwa na kuthibitishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati ilitaka kupatiwa kielelezo cha malipo ya fedha hizo na kuelezwa kwamba malipo yalifanyika. Aidha, Kamati pia imewaelekeza Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti kufuatilia kwa undani malipo yaliyofanywa ili kubaini kama yamefuata matakwa na taratibu zote za sheria.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ihakikishe inafanya uhakiki kwa fedha zote zilizolipwa na Hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuweza kubaini kama zimelipwa au kudaiwa kwa mujibu wa sheria na baadae kuwasilisha taarifa yake kwa Kamati ya PAC ili Kamati iweze kubaini fedha za Serikali zilizotumika na kupotea pasi na kuwepo kwa tija yoyote.

### 4.7.13 BARAZA LA MJI KASKAZINI “B”

**Hoja nambari 4.7.13.1 Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 89,194,001**

Katika uhakiki wa madeni ya Baraza la Mji Kaskazini “B” imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 89,194,001 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 89,194,001 kuweza kulipwa kwa Wazabuni.

**Majibu ya Uongozi wa Baraza**

Kupitia barua nambari AUD/WN/AR/TMMS/4/9/VOL.I/3 ya tarehe 22 Novemba, 2021 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

iliwasilisha agizo la kupatiwa vielelezo halisi “original documents” zinazohusiana na deni la Baraza la Mji ililowasilishwa kwa barua nambari BM/KASK.B/BA.1/VOL.I/15 ya tarehe 23 Agosti, 2021 yenye kiasi cha shilingi 308,738,351.68. Kupitia barua nambari BM/KASK.B/CON/MMH.2/VOL.I/10 ya tarehe 24 November, 2021. Baraza la Mji liliwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa uhakiki deni kwa kiasi cha shilingi 204,138,280.00 badala ya deni la awali la kiasi cha shilingi 308,738,351.68 katika barua hiyo, Baraza la Mji limetoa ufafanuzi wa sababu za deni kupungua kama ifuatavyo:-

Baadhi ya madeni yamelipwa na Baraza kwa kiasi cha shilingi 58,098,871.68 kwani malalamiko kutoka kwa watoa huduma yalikuwa ya kiwango cha juu kutokana na kukamilika kwa miradi ndani ya wakati:

Halkadhalika, kiasi cha shilingi 46,501,200.00 lilikuwa ni deni la malipo ya likizo na posho za nauli kwa Walimu na Watumishi wa Sekta ya Afya, sekta ambazo zilizogatuliwa (ugatuzi). Kupitia barua nambari OR/TMSMIM/U.11/VOL.II/04 ya tarehe 23 Agosti, 2021 iliagiza madeni yote ya sekta za ugatuzi kuwasilishwa katika Wizara husika. Baraza la Mji kwa barua nambari BM/KASK.B/BA.1/VOL.I/12 ya tarehe 27/08/2021 na BM/KASK.B/BA.1/VOL.I/11 ya tarehe 27/08/2021 iliwaasilisha madeni hayo katika Wizara husika.

Katika ukamilishaji wa Ilani ya CCM 2020, Baraza la Mji lilikuwa linaendeleza ujenzi wa barabara ya kifusi yenye urefu wa kilomita 3 kwa gharama za kiasi cha shilingi 218,347,200.00 katika Wadi ya Mkataleni na Wadi ya Vijibweni, hadi ujenzi unasitishwa Baraza lilikuwa limeshalipa kiasi cha shilingi 106,100,000.00 na bakaa ilikuwa ni kiasi cha shilingi 112,247,200.00.

Kufuatia ziara ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliyoifanya katika Mkoa wa Kaskazini mwanzoni mwa Julai, 2021, Mhe. Rais aliahidi kumalizia ujenzi huo wa barabara na Baraza la Mji liendelee na utekelezaji wa miradi mengine. Kupitia barua nambari M/KASK.B/CON/TM.1/VOL.V/105 ya tarehe 12 Julai, 2021 tulimuarifu Mjenzi kusita kwa kazi hiyo na kumuomba kuwasilisha bakaa halisi ya fedha anayodai (deni) kulingana na hatua ya ujenzi aliyofikia. Lakini kwa bahati mbaya, hakuijibu barua.

Hivyo, Baraza lilishindwa kuwasilisha kielelezo halisi cha deni analodai Mjenzi kwa uhakiki, na kila tukimfuatilia tunaarifiwa kuwa yupo nje ya nchi. Kutokana na sababu nilizozielezea hapo juu imepelekea kupungua kwa deni lililoainishwa awali jambo ambalo wakati wa ukaguzi ukifanyika katika Baraza kwa mwaka wa fedha 2020/2021, vielelezo vya malipo kwa kila chanzo cha deni na barua zinazohusika ziliwasilishwa kwa hatua za ukaguzi ili kukamilisha uhakiki wa deni hilo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kufuatia majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC iliridhika na majibu yaliyowasilishwa na kulitahadharisha Baraza kwamba kama kuna mtu ambae amekabidhiwa kazi hiyo wafanya utaratibu wa kumtafuta na kumlipa haki yake ili kuepusha Serikali kuja kupelekwa Mahakamani kudai haki zake.

## 4.7.14 BARAZA LA MJI MKOANI PEMBA

### Hoja nambari 4.7.14.1 Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 83,257,950

Katika uhakiki wa madeni ya Baraza la Mji Mkoani Pemba imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 83,257,950 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 83,257,950 kuweza kulipwa kwa Wazabuni.

**Majibu ya Uongozi wa Baraza**

Baraza la Mji Mkoani lilipokea agizo kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango la kuyawasilisha madeni yote inayodaiwa pamoja na vielelezo halisi vya madeni hayo. Baraza liliwasilisha deni pamoja na vielelezo vyake lenye thamani ya shilingi 117,876,350. Katika uhakiki uliofanyika ilibainika kuwa madeni halali yanayostahiki kulipwa ni shilingi 83,257,950 na tayari madeni hayo yameshalipwa kwa wahusika.

Kuwepo kwa deni lenye thamani ya shilingi 12,691,000 ambalo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imesema imekosa vielelezo, ni kwamba deni hilo lililipwa sehemu ya malipo na kubakia deni ambalo halijalipwa kwa baadhi ya Wazabuni waliotajwa katika Jadweli nambari 58 la hoja hii. Aidha, kuna madeni mengine ambapo Baraza la Mji Mkoani ilijiridhisha na uwepo wa vielelezo kamili na kuviwasilisha lakini kwa bahati mbaya Ofisi ya Mdhibiti haikukubaliana navyo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Baraza kukiri kuwepo kwa deni lililoibuliwa na Mkaguzi lililohakikiwa na kudhibitishwa na kuchukua hatua madhubuti ya kulilipa deni hilo. Hata hivyo, Kamati imetaka vielelezo vinavyithibitisha ulipwaji huo na kuelezwa kwamba malipo hayo yamefanyika. Aidha, kuhusu deni lililobakia, Baraza liwasilishe vielelezo vyake Ofisi ya Mdhibiti kupitia Wizara ya Fedha na Mipango.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Sambamba na hilo Kamati ya PAC imewasisitiza watendaji wanaopewa dhamana kutekeleza majukumu yao kwa uweledi na uzalendo wa hali ya juu ili kasoro za madeni hewa yasiweze kujitokeza.

2. Baraza lihakikishe linaweka kumbukumbu zao vizuri ili zinapohitajika ziweze kupatikana kwa urahisi zaidi.

## 4.7.15 OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

**Hoja nambari 4.7.15.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 85,655,750**

Katika uhakiki wa madeni ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 85,655,750 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 85,655,750 kuweza kulipwa kwa Wazabuni.

**Majibu ya Uongozi wa Ofisi**

Jumla shilingi 85,655,750 zilitumika kwa ajili ya kuwalipa watoa huduma wafuatao; Wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti, National Board of Accountants and Auditors (NBAA), TAC Associates na Zanzibar Insurance Corporation na tayari wameshalipwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile madeni hayo tayari yameshalipwa, Kamati ya PAC haikuwa na hoja zaidi isipokuwa ilitaka kupatiwa vielelezo vya malipo hayo. Vielelezo hivyo viliwasilishwa na Kamati kuridhika navyo.

## 4.7.16 WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

**Hoja nambari 4.7.16.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 9,222,283,378.17 na USD 669,550.35**

Katika uhakiki wa madeni ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 9,222,283,378.17 na USD. 669,550.35 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 9,222,283,378.17 na USD 669,550.35 kuweza kulipwa kwa wazabuni.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Katika fedha alizoridhia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Shilingi 9,222,283.378.17, fedha zilizoingizwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ni Shilingi 2,628,621,537.00, na Shilingi 6,593,662,840.11 zilikuwa za Shirika la Meli. Fedha za Wizara zilizotumika Shilingi 1,668,875,473.02, Fedha zilizorejeshwa Mfuko Mkuu wa Serikali Shilingi 418,004,103.55 Fedha zilizopo katika hesabu ya Deposit ya Serikali Shilingi 498,850,813.00 na Fedha zilizopo katika Hesabu za Wizara Shilingi 42,891,147.43 kwa mchanganuo ufuatao:

Shilingi 37,738,647.43 Vielelezo havijakamilika taratibu za kuwafuata wahusika zinaendelea zikikamilika watalipwa. Shilingi 2,386,500.00 Vielelezo vipo tayari Wizara ipo katika hatua ya kukamilisha malipo. Shilingi 2,766,000.00 Wizara ilifanya jitihada ya kumtafuta mtoa huduma kwa kumpigia simu na kumfuata eneo aliloainisha kwenye invoice yake hajapatikana ili kupata nambari yake ya hesabu kuweza kulipwa malipo yake, hata hivyo Wizara inaendelea na taratibu za kumtafuta. Kuhusu USD 669,550.35 Wizara iliwasilisha vielelezo vya USD 14,851 Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya malipo na USD 654,699.35 za Shirika la Meli Zanzibar.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kutokana na majibu yaliyowasilishwa, Kamati ya PAC imebaini kwamba kuna fedha tayari zimeshalipwa kwa Watoa huduma lakini baadhi ya fedha hazijalipwa. Kwa mnasaba huu, kuna haja ya kufuatiliwa zaidi fedha hizo ili kubaini kama zimelipwa kwa mujibu wa Sheria na miongozo halali iliyopo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuyafuatilia kwa karibu malipo yaliyofanywa na fedha zilizokuwa hazijalipwa ili kubaini ukweli wa majibu yaliyowasilishwa kwa Kamati na kupata nafasi ya kuishauri ipasavyo Serikali.

**Hoja nambari 4.7.16.2: Madeni ya muda mrefu ambayo hayakuhakikiwa shilingi 76,551,136**

Katika uhakiki wa madeni uliofanyika imebainika uwepo wa deni la shilingi 96,551,136 ambalo ni la muda mrefu la mwaka wa fedha 2014/2015 linalodaiwa na watoa huduma mbali mbali kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Kwa mujibu wa maelekezo tuliyoyapokea kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ni kwamba Serikali ina mpango wa kulipa madeni ya karibuni kuanzia mwaka 2016/2017 hadi mwaka 2020/2021. Kwa hivyo, madeni ambayo yaliyobainika kwa mwaka wa fedha 2016/2017, madeni hayo yatawekewa utaratibu maalum wa uhakiki pamoja na malipo yake ambao utaelezwa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango. Kutokana na hali hiyo ukaguzi haukuweza kulihakiki deni hilo kutokana na kuwa nje ya upeo wa kipindi cha muda wa madeni ambao umetakiwa kuhakikiwa na kulipwa na Serikali. Aidha ukaguzi umebaini uwepo wa deni la shilingi 20,000,000 linalodaiwa na ZECCON ambapo kwa mujibu wa vielelezo tulivyowasilishiwa na kuvihakiki ilibainika deni hilo tayari limeshalipwa kupitia hesabu ya Revolving Fund kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**
Ni kweli deni hili lipo hadi sasa, Wizara bado inadaiwa kama alivyoeleza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Wizara inasubiri utaratibu maalum wa uhakiki wa madeni haya kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ili kuweza kuyalipa. Aidha, Wizara bado inayo madeni mengine ya zamani kwa Watoa huduma mbali mbali ambayo yanahitaji kupata muongozo wa Serikali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa Wizara bado inaendelea kudaiwa madeni hayo. Hata hivyo, baadhi ya madeni yaliyowasilishwa kwa Mdhibiti yapo nje ya muda wa uhakiki, hivyo hayakuweza kufanyiwa kazi. Kwa mnasaba huu, Kamati imebaini kuna uzembe uliofanywa na watendaji wa Wizara ambapo barua ya Mkaguzi ilikuwa ikieleza wazi madeni yanayotakiwa lakini watendaji waliingiza hadi madeni ya miaka ya nyuma.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara iyatafute madeni yote ambayo yamo ndani ya muda wa uhakiki pamoja na vielelezo vyake ili kuyawasilisha Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kuandikiwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Hoja nambari 4.7.16.4: Deni ambalo limekosa vielelezo vya uthibitisho kutoka kwa Mdai shilingi 45,029,205**

Katika uhakiki uliofanyika wa deni la Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) lenye jumla ya shilingi 167,350,078.25 ambalo liliwasilishwa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa ajili ya kuhakikiwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu nambari MOICT/M80/3/VOL.VI/VOL.140 ya tarehe 7 Januari 2021. Ukaguzi umebaini kati ya deni hilo jumla ya shilingi 45,029,205 ni deni kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ambalo anadai kwa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar. Hadi ukaguzi unakamilika ZMA imeshindwa kukamilisha vielelezo vya uthibitisho wa uwepo wa deni hilo la shilingi 45,029,205. Kwa hivyo, ukaguzi haukuweza kuthibitisha kuwa deni hilo ni halali kutokana na kukosekana kwa vielelezo kutoka kwa ZMA.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Vielelezo vipo, Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar tayari imeshalipa deni hili kwa TCRA.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imegundua kuwa Wizara imelipa madeni inayodaiwa na TCRA bila ya kufuata utaratibu uliowekwa wa kufanyiwa uhakiki na kuthibitishwa madeni ndio hatua ya kufanyiwa malipo iweze kutekelezwa badala yake Wizara imeamua kuchukua maamuzi vyenginevyo. Hata hivyo, Kamati ilitaka kujua kwanini malipo hayo yamelipwa kinyume na utaratibu na kuelezwa kwamba kulikuwa na deni la jumla ya shilingi 45,029,205 ambalo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inaidai Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar ambapo TCRA walikuwa katika hatua ya kusitisha huduma za kutoa 'control number' za malipo ya upatikanaji wa mawasiliano. Kwa msingi huo, Kamati imepata mashaka kuhusu malipo yaliyofanyika na yanahitaji kuthibitishwa na Ofisi ya Mdhibiti.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Watendaji wa Wizara wahahkikishe wanafanya malipo kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyowekwa ili kuepusha fedha za umma kutumika vyenginevyo.

2. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ifuatilie kwa karibu malipo yaliyofanywa kama yamefanywa kama zinavyoelekeza Sheria za Ununuzi na Usimamizi wa Fedha za Umma.

**Hoja nambari 4.7.16.5: Madeni ambayo yamekosa vielelezo vya uthibitisho kutoka kwa Wadai shilingi 2,580,892,356.76 na USD 8,549.81**

Katika uhakiki uliofanyika wa deni la Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) lenye jumla ya shilingi 3,541,295,748.39 ambalo liliwasilishwa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa ajili ya kuhakikiwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu nambari MOICT/M80/3/VOL.VI/VOL.140 ya tarehe 7 Januari 2021. Ukaguzi umebaini kati ya deni hilo jumla ya shilingi 2,580,892,356.76 na USD 8,549.81 ni deni kutoka Wazabuni na Wadai mbali mbali ambao wameshindwa kuwasilisha taarifa za madeni yao za kuthibitisha uwepo wa deni hilo kwa ukaguzi. Kwa hivyo ukaguzi haukuweza kuthibitisha kuwa deni hilo ni halali kutokana na kukosekana kwa vielelezo kutoka kwa Wazabuni na Wadai.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Jadweli Nambari 73: Madeni ambayo yamekosa vielelezo vya uthibitisho kutoka kwa Wadai Shilingi 2,580,892,356.76 na USD 8,549.81. Vielelzo vyote vipo na tayari Shilingi 790,698,305.00 zimeshalipwa baada ya kupata ridhaa kutoka kwa Mdhibiti na Maguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa watoa huduma Wafuatao: COSMOSMAP Consultancy Coastal Dridge Zena Mola General trading Future Century Kuhusu USD 8,549.81 bado hazijalipwa lakini vielelezo vipo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba kuna uzembe umefnayika wa kutoshirikiana na Mkaguzi ili kumpatia vielelezo vinavyohitajika. Aidha, kuna madeni ambayo Wizara haijayawasilisha katika Ofisi ya Mdhibiti pamoja na vielelezo vyake ambayo yamefanyika katika kipindi ambacho Mkaguzi anakifanyia kazi (2015 hadi Agosti, 2020). Huu ni uzembe mkubwa na Kamati haikuridhishwa na hatua ambazo Wizara ilizichukua kushughulikia madeni ya Serikali yaliyopo katika WIzara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara iyawasilishe madeni inayodaiwa ndani ya muda wa uhakiki katika Ofisi ya Mdhibiti kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

## 4.7.17 AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

### Hoja nambari 4.7.17.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 117,288,982

Katika uhakiki wa madeni ya Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 117,288,982 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imeridhia jumla ya shilingi 117,288,982 kuweza kulipwa kwa Wazabuni.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Madeni yaliyohakikiwa ni Jumla ya Shilingi 140,661,336.10 yaliyostahiki kulipwa kwa Mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni Jumla ya Shilingi 117,288,982/-. Jumla ya Fedha tulizoingiziwa kutoka Afisi ya Rais, Fedha na Mipango ni Shilingi 117,288,982/-. Katika Fedha tulizoingiziwa kwa ajili ya kulipa madeni Shilingi 2,626,608 ni deni la TRA. Imeshindikana kulipwa Fedha hizi kwa kukosa kupatiwa Control namba na Taasisi husika (TRA). Barua yenye Kumbukumbu nambari AC.339/405/01/15 ya Tarehe 28/5/2023 inahusika na tumeiambatanisha.

Bakaa ya Fedha hizi shilingi 2,626,608/- tumezipeleka C. Miscellaneous Deposit Account. (Fedha zenye Commitment) Kwa barua nambari Cac.69/455/01/72 ya tarehe 12 Juni 2023 inahusika na imeambatanishwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa Ofisi ya Mkaguzi imenusuru kiasi cha shilingi milioni 23 kama fedha hizo zingelifanyiwa malipo bila ya kuyafanyia uhakiki na kuyathibitisha madeni yanayodaiwa na Watoaji hutuma. Hali hiyo ilitokana na Hilal Supply kushindwa kuwasilisha vielelezo vya huduma aliyotoa. Kwa mnasaba huo, fedha hizo zote zingetumika kinyume na utaratibu.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Mkaguzi afanye Ukaguzi Maalum kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ili kubaini kama fedha za Sekali zimetumika ipasavyo.

2. Wizara iandae utaratibu mzuri wa kuhifadhi kumbukumbu za vielelezo vyake na kuviwasilisha kwa Mkaguzi anapopita kutekeleza majukuu yake.

### 4.7.18 WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

**Hoja nambari 4.7.18.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 192,483,411**

Katika uhakiki wa madeni ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imebainika uwepo wa madeni ya shilingi 192,483,411 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 192,483,411 kuweza kulipwa kwa Wazabuni.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Ni kweli tulipokea jumla ya Tsh. 192,483,411 na Wizara imefanya malipo ya madeni hayo kwa wadai wote kwa mchanganuo kama ifuatavyo:-

1. Tsh. 187,819,961 zimelipwa kwa Wadai.
2. Tsh. 4,663,450 zimerudishwa hazina sababu ni Wadai hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi (ZPPDA).

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile fedha hizo zimelipwa kama alivyoelekeza Mkaguzi. Kamati ya PAC haikuwa na hoja zaidi isipokuwa inamtaka Mdhibiti ambae amekagua na kuibua hoja hii, akafanya uhakiki kuthibitisha maelezo yaliyoelezwa na kuipatia Kamati mrejesho kuhusiana na majibu hiyo.

### 4.7.19 OFISI YA MKOA WA MJINI MAGHARIBI

**Hoja nambari 4.7.19.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 53,577,520**

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliwasilisha agizo la kupatiwa vielelezo halisi (orginal documents) vinavyohusiana na deni la shilingi 106,491,517 kwa barua yenye kumbukumbu nambari AUD/WN/AR/TM/MS//4/11/VoL.1/35 ya tarehe 2/11/202I pamoja na kuomba kupatiwa mchanganuo wa deni hilo kwa kila anaedai na kwa kiwango halisi cha fedha kinachodaiwa kutoka Ofisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi kutokana na deni lilowasilishwa.

Hata hivyo, Ofisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi iliwasilisha deni la shilingi 60,831,924 na kupelekea kuwepo wa tofauti ya shilingi 45,659,593 na taarifa ya deni alililoliwasilisha Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango. Kutokana na deni

lilowasilishwa la shilingi 60,831,924 na Ofisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Katika uhakiki wa madeni ya Ofisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi imebainika uwepo wa madeni shilingi 53,577,520 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha, Ofi si ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesbu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 53,577,520 kuweza kulipwa kwa Wazabuni/Wadai.

**Majibu ya Uongozi wa Mkoa**

Ni kweli tarehe 30/08/2021, Afisi ya Mkoa iliwasilisha Afisi ya Rais, Fedha na Mipango orodha ya madeni jumla ya shilingi 106,491,517.00. Hata hivyo, kwa kipindi cha mwezi Septemba, Oktoba, Novemba, Disemba 2021 na Januari 2022 Afisi ya Mkoa ililipa fedha za matumizi ya kawaida kutoka Hazina. Hivyo ilifanya malipo ya baadhi ya madeni yenye jumla ya shilingi 30,762,277.00. Kwa kipindi cha mwezi Septemba 2021, Afisi ya Mkoa ilifanya uhakiki wa madeni wa ndani na kubaini baadhi ya madeni ya taasisi za Serikali yanadaiwa kwa kutumia barua tu na hakuna nakla halisi ya invoice uinayoonesha deni, deni la Shirika la Magazeti ya Serikali lilipungua 4,275,000.00 baada ya uhakiki.

Zoezi la uhakiki wa ndani wa madeni pia uliondosha baadhi ya madeni yenye jumla ya shilingi 14,897,316.00 kwa manunuzi ambayo haya kuwa yamekamilisha taratibu, ikiwemo kuhakikisha kila deni lazima liwe lile lililoingizwa kwenye ghala ya Mkoa. Baada ya Afisi ya Mkoa kufanya baadhi ya malipo ya madeni na kuyapitia upya madeni, orodha ilibadilika na kuwa ile yenye jumla ya shilingi 60,831,924.00.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuna uwezekano mkubwa wa kuwepo kwa ubabaishaji unaoleta wasiwasi kuhusu deni halali linalodaiwa na Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa mnasaba huo, Kamati ineielekeza Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya mambo yafuatayo:-

a) Kuhakiki upya madeni halisi ambayo Mkoa wa Mjini Magharibi inayodaiwa na Wazabuni tofauti.
b) Kuhakiki vielelezo vya malipo yaliyofanywa na Mkoa wa Mjini Magharibi ili kubaini kama yalilipwa kwa mujibu wa utaratibu au laa.

### 4.7.20 CHUO CHA MAFUNZO

**Hoja nambari 4.7.21: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 573,640,142**

Katika uhakiki wa madeni ya Chuo Cha Mafunzo imebainika uwepo wa madeni shilingi 573,640,142 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 573,640,142 kuweza kulipwa kwa Wazabuni/Wadai.

**Majibu ya Uongozi wa Chuo cha Mafunzo**

Ni kweli Chuo cha Mafunzo Zanzibar kilikua na madeni ambayo yalihakikiwa na kustahiki kulipwa yenye thamani ya Tsh. 573,640,142/-, jumla ya fedha hizo zote tulipokea kutoka Mfuko Mkuu wa Serekali na kuzilipa kwa Wazabuni husika kama ilivyotakiwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imegundua kuwa Chuo cha Mafunzo kiliwasilisha jumla ya shilingi 847,115,708/- katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na jumla ya shilingo 573,640,142/- zilithibitishwa kulipwa na shilingi 273,475,566/- hazikuthibitishwa kulipwa kutokana na kukosa vielelezo vya matumizi yake.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inasisitiza kwamba Watendaji wa Chuo cha Mafunzo hususan wa kitengo cha uhasibu kuwa makini wanapofanya malipo ya madeni ya Serikali ili kuepusha matumizi hewa ya fedha za Serikali.

### 4.7.22 KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

**Hoja nambari 4.7.22.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 47,624,115**

Katika uhakiki wa madeni ya Kamisheni ya Utumishi wa Umma imebainika uwepo wa madeni shilingi 47,624,115 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesbu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 47,624,115 kuweza kulipwa kwa Wazabuni/Wadai.

**Majibu ya Uongozi wa Kamisheni**

Kamisheni ya Utumishi Umma iliwasilisha kwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora jumla ya deni lake shilingi 54,552,440/- madeni haya yalihakikiwa na Ofisi ya Mdibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na kuridhiwa kwa hatua za malipo kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa kumbukumbu ya barua namba CAB.366/420.01.68 ambapo jumla ya madeni yaliyothibitishwa kwa malipo ni 47,624,115/-. Aidha, Kamisheni ya Utumishi wa Umma ilipokea fedha na kulipa madeni kwa mujibu wa mrejesho wa madeni yaliyorudi na kuthibitishwa kwa hatua za malipo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na kulipwa kwa deni hilo, Kamati ilitaka vielelzo vya malipo hayo ili kujiridhisha ulipwaji wake. Hata hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi isipokuwa ilisisitiza kama vielelezo vyengine vya milioni 7 iliyobakia wanavyo basi Kamisheni iwasilishe maombi ya kukaguliwa vielelezo hivyo Ofisi ya Mdhibiti kupitia Wizara ya Fedha na Mipango.

### 4.7.23 WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO.

**Hoja nambari 4.7.23.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 1,644,372,158**

Katika uhakiki wa madeni ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imebainika uwepo wa madeni shilingi 1,644,372,158 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 1,644,372,158 kuweza kulipwa kwa Wazabuni/Wadai.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Hoja Nambari 4.7.23.1 inahusiana na madeni yaliyowasilishwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango yenye jumla ya Tshs. 1,644,372,158.00 Baada ya kuwasilishwa deni hili Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Wizara ilipokea barua yenye Kumbukumbu Nam. AUD/W/KUMM/14/VOL.1/15 ya tarehe 21/02/2022 (kiambatanishi No.23/1) iliyoitaka Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kuwasilisha vielelezo halisi (Original) vilivyoambatana na uthibitisho wa deni la Tshs. 1,644,372,158.00. Aidha, Wizara iliwasilisha vielelezo hivyo kwa barua yenye Kumbukumbu Nam. WKUMM/29/4/28/VL.II ya tarehe 17/03/2022 (kiambatanishi No. 23/2) kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa uhakiki. Baada ya kufanyiwa uhakiki madeni hayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuthibitisha uhalali wa madeni aliahidi kuwasilisha deni Ofisi, Rais Fedha na Mipango kwa utekelezaji kwa Barua yenye Kumbukumbu AUD/W/KUMM/14/VOL.1/10 ya tarehe 28/04/2022 (kiambatanishi No. 23/3). Mnamo mwezi wa Juni, 2022 Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango iliingizia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo jumla ya Tshs. 290,379,544 kwa kuwalipa Wazabuni na jumla ya shilingi 264,675,223.48 zimeshalipwa.

Kuhusu Deni la Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ Ltd) 1,353,992,614.0 kwa Wakala wa Serikali na Huduma za Matrekta hazikuingizwa fedha zake kwa wakati huo kutokana na kuwa deni hili linalipwa kupitia fedha za OC kila mwezi inapoingizwa na kwa sasa deni hilo limebakia Tshs. 353,676,364.05 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2023. Aidha, Wakala itaendelea na utaratibu huo wa malipo hadi deni hilo litakapomalizika.

## 4.7.24 WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO.

### Hoja nambari 4.7.24.1: Madeni yaliyohakikiwa na yanayostahiki kulipwa shilingi 1,256,135,604

Katika uhakiki wa madeni ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni, na Michezo imebainika uwepo wa madeni shilingi 1,256,135,604 ambayo yamehakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa ukaguzi wa madeni hayo. Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesbu za Serikali imeridhia jumla ya shilingi 1,256,135,604 kuweza kulipwa kwa Wazabuni/Wada.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo iliwasilisha Ofisi ya Rais Fedha na Mipango deni la shilingi 1,265,076,604 kwa barua yenye

kumbukumbu nambari WHUVUM22/CONF.5/VOL.1/35 ya tarehe 2/03/2022 kwa ajili ya kufanyiwa malipo. Katika uhakiki wa madeni hayo uliofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilibainika uwepo wa madeni ya shilingi 1,256,135,604 ambayo yalihakikiwa na kuthibitishwa uhalali wa uwepo wake kwa mujibu wa vielelezo vilivyowasilishwa kwa Mkaguzi wa madeni hayo. Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliridhia jumla ya shilingi 1,256,135,604 kuweza kulipwa kwa wazabuni/wadai. Hata hivyo, uhakiki huo ulibainika utofauti wa shilingi 41,965,459 ambazo uwepo wa uhalali wa deni hilo haukuweza kuthibitika kutokana na kukosekana kwa vielelezo halali vya deni hilo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba jumla ya shilingi milioni 41 zimeokolewa kwa vile zimekosa vielelezo. Aidha, Kamati imepata mashaka juu ya utendaji wa baadhi ya Wafanyakazi wa Serikali ama watakuwa wanafanya kazi kwa uzembe mkubwa au watakuwa wanashiriki katika ubadhirifu wa mali za umma. Hali hii inatia wasiwasi kwamba kuna fedha nyingi za Serikali hulipwa bila ya kuleta tija kwa wafanyakazi wala Taifa letu, matokeo yake hutumika kwa maslahi binafsi.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara iwasimamie ipasavyo Watendaji wake hususan wanaohusika na ulipaji wa madeni hayo ili kuepusha kufanyika malipo hewa yasiyokuwa na tija yoyote.

**Maoni ya jumla**

1. Kwa vile Wizara zimeeleza kwamba kuna juhudi imechukuliwa ya kulipa au kupunguza madeni wanayadaiwa na watoa huduma mbali mbali, Kamati ya PAC inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufuatilia ulipwaji wa madeni hayo katika Wizara au Taasisi zote zilizokaguliwa na kubainika kuwa na madeni ili kujua kama kweli yamelipwa na ulipwaji wake ulifuata utaratibu na miongozo inayokubalika.

   Aidha, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hatimae aiwasilishe ripoti hiyo kwa Kamati ya PAC ili iweze kujua uhalisia wa utekelezwaji wa hoja za Mdhibiti na kuliarifu ipasavyo Baraza pamoja na kuishauri Serikali uhalisia uliopo wa madeni ya Wizara/Taasisi zake.

2. Muhasibu Mkuu wa Serikali akutane na Wahasibu wote wa Serikali kuwaelimisha kuhusiana na utoaji wa mashirikiano na Watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili hoja ziweze

kujibiwa mapema kabla hazijaingizwa katika kitabu cha ripoti za ukaguzi.

**UCHUNGUZI KUHUSU RIPOTI YA UKAGUZI WA FEDHA ZA MUUNGANO**

**Hoja nambari 8.1.1.1: Kutokufunguliwa kwa Akaunti ya Pamoja ya Fedha za Muungano.**

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inabainisha kazi za Serikali ambazo ni miongoni mwa mambo ya Muungano pamoja na kutoa utaratibu wa kuzifadhili. Ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatamka kuwa "Serikali ya Jamhuri ya Muungano itafungua akaunti maalum itakayojulikana kama Akaunti ya Pamoja ya Fedha (JFA), na ambayo itakuwa sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Jamhuri ya Muungano ambayo italipwa fedha zote zinazochangwa na Serikali mbili kwa uwiano utakaopangwa na Tume ya Pamoja ya Fedha".

Aidha, Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeanzisha Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC), ikielezea majukumu. Miongoni mwa majukumu yake ni kuchambua mapato na matumizi yanayohusu usimamizi wa mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusiana na mchango na mgawo wa kila upande wa Serikali. Ukaguzi umebaini tangu kuundwa kwa Muungano wa Serikali mbili na kutungwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977, Akaunti ya Pamoja ya Fedha (JFA) haijafunguliwa kama ilivyoelezwa kwenye Katiba ambapo Serikali zote mbili zingepaswa kuweka michango yao iliyopangwa awali ambayo inaweza kuwa fedha hizo zitatumika kugharamia mambo ya Muungano. Aidha ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa uwiano ulioainishwa awali ambao ungeweza kutumika kama kigezo cha uchangiaji wa fedha kwa ajili ya gharama za Muungano.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya kuanzisha Akaunti ya Pamoja ya Fedha iliyoandaliwa na Serikali ya Muungano wa Tanzania baada ya kuwashirikisha wadaumbalimbali na kuwasilishwa Ofi si ya Rais Fedha na Mipango (Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar) kwa barua yenye kumbu kumbu CJA.547/594/01 ya tarehe 6 Desemba, 2019 kwa maoni. Hadi ukaguzi unakamilika hakuna maoni yoyote ambayo yamewasilishwa kuweza kufanyiwa kazi na Serikali ya Muungano wa Tanzania. Kwa kukosekana kwa Akaunti ya Pamoja ya Fedha, ukaguzi haukuweza kubaini kiasi halisi cha fedha kilichotolewa na wadau pamoja na fedha zilizotumika kugharamia masuala ya Muungano.

**Majibu ya Uongozi ya Wizara**

Baada ya SMZ kupokea Waraka wa Baraza la Mawaziri kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kutoa maoni, SMZ ilichukua hatua za kujijengea uelewa kuhusu masuala ya Uhusiano wa Kifedha ili iweze kuwasilisha maoni yake kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua zaidi. Wadau mbalimbali wa SMZ wamejengewa uelewa kuhusu masuala ya Uhusiano wa Kifedha, ikiwemo usimamizi na uendeshaji wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja.

Baada ya SMZ kukamilisha hatua za kujenga uelewa kuhusu Akaunti ya Fedha ya Pamoja, itayawasilishamaoni yake kwa SJMT kwa hatua zaidi ili akaunti hiyo iweze kufunguliwa na kutumika.

Kwa kuwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja bado haijafunguliwa, utaratibu uliopo sasa wa Uhusiano wa Kifedha kati ya SJMT na SMZ ni kuwa: Mapato yanayotokana na utekelezaji wa Mambo ya Muungano yanayokusanywa Zanzibar yanawasilishwa Hazina ya SMZ na kutumikakatika uendeshaji wa shughuli za SMZ; na Mapato yanayokusanywa Tanzania Bara yanawasilishwa Hazina ya SJMT na kutumika kugharamia Mambo ya Muungano katika pande

zote mbili za Muungano na yasiyo ya Muungano kwa Tanzania Bara. Hivyo, mapato ya Muungano na Matumizi yanajulikana chini ya uataratibu unaotumika sasa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Wizara ya Fedha na Mipango imekiri kweli akaunti ya Muungano haijafunguliwa kama majibu yanavyojieleze. Hata hivyo, Kamati imeelezwa kuwa Wizara imechukua juhudi mbali mbali katika kuhakikisha makubaliano yanapatikana ikiwemo Serikali zote mbili kuendelea kufanya vikao vya pamoja.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakisha akaunti ya pamoja inafunguliwa kwa haraka ili kuondo changamoto hiyo.

**Hoja nambari 8.1.1.2: Kutokuambatanishwa kwa vielelezo vya Makato ya kodi ya Mishahara ya wafanyakazi (PAYE) na kupelekwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**

Kwa mujibu wa Jadweli la kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato ya 2019 Sura ya 332 inaweka mabano ya malipo ya kodi yatakayotozwa kutokana na mapato ya mfanyakazi binafsi. Chini ya utaratibu wa sasa wa fedha wa vyama vya wafanyakazi, watumishi wa Umma wanatozwa PAYE na kiasi kinachotozwa kinatumwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kiasi cha ujumla ambacho kinachotumwa kila mwezi. Kanuni ya 95 (4) yaKanuni za Fedha za Umma, 2001 inaeleza kuwa 'Hati ya malipo ambayo haijakamilika kwa sababu ya nyaraka zake za uthibitisho kukosekana, itachukuliwa kuwa ni hati iliyokosekana'.

Ukaguzi ulipitia hati za malipo ya fedha zilizotumwa Hazina (Fungu 21) kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia akaunti ya BOT namba 9928139904 ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa kipindi cha miaka sita kuanzia 2015/16 hadi 2020/21 na kubaini jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 126 zimetumwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama PAYE ambayo ni pamoja na kiasi cha shilingi bilioni 21 zinazohamishwa kila mwaka na shilingi bilioni 1.75 kwa kila mwezi. Ukaguzi ulibaini dosari zifuatazo:-

- Kiasi kilichotumwa kama PAYE hakikuambatanishwa na vielelezo husika kama vile Malipo ya Mishahara au makubaliano yoyote ya fedha baina ya Serikali jambo ambalo ni kinyume na Kanuni Na. 95 (4) ya Kanuni za Fedha zaUmma, 2001. Hivyo, hali ya makato ya watumishi haikujulikana.
- Shilingi 15,750,000,000 zilihamishwa kwa mkupuo mmoja kupitia hati ya Malipo Namba. 574543 ya tarehe 20/10/2020 kiasi cha PAYE kwa miezi tisa (9) kinyume na utumaji wa fedha hizo kila mwezi. Kukosekana kwa nyaraka husika na kutolingana kwa kiasi kilichohamishwa kama PAYE kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mahususi kwa mwaka 2020/21 inatia shaka juu ya uhalisia wa fedha zilizotumwa. Kutokana na kukosekana kwa nyaraka husika za PAYE zilizotumwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ukaguzi haukuweza kuthibitisha uhalisia wa fedha zilizotumwa.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Kiasi kilichotumwa kama PAYE hakikuambatanishwa na vielelezo kwa vile viambatanisho vinabaki Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano na haviwasilishwi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hivyo Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2021 hazihusiki na kiwango cha Shilingi **15,750,000,000** kiliwasilishwa kwa mkupuo baada ya maombi yaliyowasilishwa na Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar kutokana na hali ya mapato kutokua nzuri kipindi cha Kovid-19.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 fedha ya PAYE iliyoingizwa ni shilingi bilioni 21 ambayo sawa na asilimia 100 ya Bajeti.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli malipo yaliyokuwa yakifanyika hayakuwa na vielelezo kama ilivyoelezwa na Mkaguzi. Hali hiyo imetokana na kuwepo ufuatiliaji usiorodhisha wa malipo ya fedha hizo za PAYE.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango ya Zanzibar kuwa na mawasiliano ya karibu na Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili malipo yakifayika na risiti za kuhalalisha matumizi hayo iweze kuambatanishwa.

**Hoja nambari 8.1.1.3: Kukosekana kwa uhalisia wa gawio la fedha zilizolipwa na Benki Kuu ya Tanzania**

Kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaunda Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC)ikiainisha majukumu yake, mojawapo ni kuchambua mapato na matumizi yanayohusiana na usimamizi wa mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgao kwa kila Serikali moja katika Muungano huo. Mnamo Mwezi Julai, 2006 Tume ya pamoja ya Fedha ilifanya utafi ti wa mahusiano ya Kifedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo utafi ti huo ulifanywa na Kampuni ya Price waterhouse Coopers. Lengo kuu la utafi ti huo lilikuwa kuwezesha Tume ya Pamoja ya Fedha kushauri Serikali zote mbili juu ya utaratibu endelevu wa kugawana mapato na matumizi.

Kifungu cha 1.3 cha ripoti hiyo ya utafi ti uliofanywa kimeeleza utaratibu wa fedha baina ya Serikali na mambo mengine ikiwa ni sehemu ya asilimia 4.5 ya Gawio la Benki Kuu ya Tanzania ambalo linapaswa kuwasilishwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika mapitio ya fedha zilizotumwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015/2016 hadi 2019/2020, ukaguzi ulibaini jumla ya hisa iliyokokotolewa upya ya asilimia 4.5 ya gawio la BOT kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha ukaguzi ilikuwa ni shilingi bilioni 57.6 lakini fedha halisi zilizotumwa kutoka Serikali ya Muungano kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha ukaguzi zilikuwa ni shilingi bilioni 52.8.

Hali hii imepelekea uwepo wa upungufu ya shilingi bilioni 4.8 kwa fedha zilizopelekwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mgawanyo usio sawa wa gawio la Benki Kuu ya Tanzania kati ya Serikali mbili unaweza kuchelewesha mchakato wa kutatua changamoto za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Benki Kuu ya Tanzania ilifanya malipo ya gawio kwa kipindi cha miaka mitano ya fedha 2015/2016 hadi 2019/2020 kama inavyoonekana kwenye nyaraka za benki (bank statements). Fedha hizo zililipwa kupitia akaunti ya Msajili wa Hazina (9921141401-Treasury Registrar) iliyoko Benki Kuu ya Tanzania. Kiwango cha malipo ya gawio kwa SMZ yalifanyika baada ya kupata maelekezo kutoka kwa Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka yote mitano. Ukiondoa mwaka 2015/2016 malipo mengine yote ya gawio kwa SMZ yalifanyika sawa sawa kulingana na maelekezo ya Wizara ya Fedha ya Muungano.

Fedha hizo ziliingizwa kwenye akaunti namba 9928139904 ya SMZ iliyopo Benki Kuu ya Tanzania. Taarifa za kibenki kuhusu akaunti hiyo zinaonyesha kwamba mwaka 2015/2016 gawio lililolipwa kwa SMZ lilikuwa ni TZS

7,000,000,000.00 badala ya TZS 13,500,000,000.00 ikiwa ni asilimia 4.5 ya gawio kwa SMZ linalotokana na gawio lililolipwa kwa SMT la TZS 300,000,000,000,00 kulingana na ripoti ya kifedha za Benki Kuu kwa mwaka 2015/2016. Kwa vile Benki Kuu hufanya malipo haya baada ya kupata maelekezo kutoka Wizara ya Fedha ya SMT, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango inafanya mawasiliano na Wizara ya Fedha ya SMT kuhusiana na tofauti iliyolipwa SMZ kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba licha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulipa fedha za miaka mitano kwa pamoja lakini bado kuna bakaa ya shilingi bilioni nne ambazo hazikujumuishwa katika malipo yaliyofanyika. Hata hivyo, Kamati imeridhishwa na jitihada za Wizara za kulifuatilia kwa karibu suala hilo kwa kuwasiliana (kwa njia ya simu) na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha ya SMT ili kuhakikisha fedha hizo zinalipwa.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar ihakikishe inaiandikia barua WIzara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiambatanisha na vielelezo stahiki vya malipo yaliyofanywa ili kukumbushia malipo ya deni la bilioni 4 lililobakia.

**WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO**

**Hoja nambari 12.1.1.1: Kutokuwepo kwa miongozo inayopaswa kutumika katika usimamizi na uendeshaji wa Mashamba ya mikarafuu.**

Kutokuwepo kwa miongozo inayopaswa kutumika katika usimamizi na uendeshaji wa shamba za mikarafuu ambapo kunaweza kupelekea mashamba hayo kukosa matunzo na udhibiti mzuri na hatimae kutopatikana kwa tija inayokusudiwa.

Uongozi wa Wizara uhakikishe unaandaa miongozo ambayo itafuatwa katika usimamizi na uendelezaji wa shamba za mikarafuu ili kuepuka mizozo ambayo inaweza kutokezea kutokana na vitendo vya baadhi ya wananchi kurithishana maeneo ya Serikali bila ya kufuata taratibuy na miongozo ya kisheria.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara imepokea ushauri uliotolewa na itaongeza kasi ya kuhakikisha mashamba ya mikarafuu yanayosimamiwa na Wizara yanasimamiwa na kuendelezwa ipasavyo. Kwa sasa Wizara inaendelea kufanya marekebisho ya Sera ya Kilimo ya mwaka 2002 na pia inaandaa Mpango wa Mageuzi ya Kilimo nchini, hivyo, mashamba hayo yatapimwa na kuwekewa mipango ya matumizi ambapo makundi ya wanawake na vijana yatapewa kwa mikataba maalum ili kuyaendeleza. Upungufu mkubwa wa wafanyakazi katika mashamba hayo wakiwemo walinzi kumepelekea hali iliyopo sasa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Pemba haikuwa na muongozo wa usimamizi na uendeshaji wa Mashamba ya mikarafuu wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake alipofika katika eneo hilo. Hata hivyo, Kamati ya PAC haikuridhishwa na juhudi zilizochukuliwa na Wizara ya kutoikamilisha Rasimu ya Muogozo huo ulioandaliwa kupitia ufadhili wa Shirika la Chakula Duniani (FAO), kwa vile muda umekuwa mkubwa takriban miaka miwili iliyopita, bado Rasimu hiyo haijafikishwa na kujadiliwa na Kamati ya Uongozi wa Wizara. Kwa mnasaba huu, Kamati inaitaka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufuatilia utekelezaji halisi wa hoja hii ili iweze kuondolewa katika vitabu vya Ukaguzi.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ya Kilimo ihakikishe inakamilisha hatua iliyobakia ya uandaaji wa muongozo ili kutatua changamoto za usimamizi na uendeshaji wa Mashamba ya Karafuu zinazojitokeza hivi sasa ikiwemo mizozo na wananchi.

**Hoja nambari 12.1.1.2: Ukataji wa Mikarafuu kiholela**

Kuwepo kwa ukataji wa mikarafuu kiholela katika baadhi ya shamba za mikarafuu ya Serikali ambapo kunaweza kupelekea shamba hizo kupoteza muonekano wake wa asili na hatimae kushuka kwa kiwango cha uzalishaji wa karafuu katika shamba hizo.

Wizara kuhakikisha kwamba shamba za Serikali zinawekewa udhibiti wa kutosha ili kuepusha ukataji holela wa mikarafuu pamoja na uvamizi wa maeneo hayo. Aidha, Wizara kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara katika maeneo hayo kwa lengo la kujiridhisha hali halisi ya utunzwaji wa mashamba hayo.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara imepokea ushauri uliotolewa ambapo itaendelea kuomba ajira mpya za wahudumu wa mashamba ili kuongeza ulinzi katika mashamba hayo. Kwa sasa udhibiti unafanywa kwa kiasi kidogo kutokana na uchache wa wahudumu kwenye mashamba hayo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia ukweli wa hoja hii, Kamati ya PAC ilitaka kujua ni wafanyakazi wangapi wameoma waajiriwe ili kutatua changamoto iliyopo na kuelezwa kwamba kuna wafanyakazi 54 (Maofisa na Wasaidizi wao) wanaokusudiwa kuajiriwa ambapo kibali kimeshatoka. Kupitia maelezo hayo Kamati ilibaini kuwa wafanyakazi hao ni kidogo ukilinganisha na kazi pamoja na wingi wa Mashamba wanayomiliki Wizara. Vile vile, Kamati haikufurahishwa na ajira iliyopwa kufanyika kwani haikulenga kuondoa changamoto iliyopo kwa vile mashamba hayo yanahitaji wafanyakazi wa ngazi ya chini wakiwemo wahudumu wa kusafisha na kuyaendeleza mashamba hayo.

Kamati ya PAC ilitaka kujua Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha hatua za dharura zinachukuliwa katika kuyahudumia Mashamba yaliopo kwa kutaka kufahamu ni wafanyakazi wangapi walionao wanaotumikia mashamba yaliopo na kujibiwa kwamba wanao wafanyakazi 11 lakini wanahitaji wafanyakazi 110 ili waweze kuondosha changamoto iliyopo hususan ya kuwepo kwa misitu katika mashamba ya Mikarafuu na Minazi. Aidha, Wizara huwa inashirikiana na Wanajamii katika usafishaji wa Mashamba kwa kuwafidia asilimia fulani ya fedha lakini Kamati ilipouliza kuhusu utaratibu gani unaotumika katika ufanyaji kazi hizo, ilielezwa wanaingia nao mikataba. Hata hivyo, Kamtati haikupatiwa Mkataba wowote kuthibitisha maelezo hayo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara kwa kushirikiana na Wizara inayoshughulikia Utumishi wa Umma pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango zihakikishe zinaajiri au

‘kutransfer’ wafanyakazi wa ngazi ya chini (hususan Wahudumu) watakaoenda kushughulikia mashamba ya Mikarafuu pamoja na Minazi.

2. Wizara inapowatumia wanajamii katika usafishaji wa Mashamba yake, iwe inatiliana Mikataba nao ili kuepusha malalamiko baadae.

**Hoja nambari 12.1.1.3: Kufanyika kwa kilimo kisichokuwa rafiki katika shamba za mikarafuu.**

Kuwepo kwa kilimo cha mihogo na migomba ndani ya shamba za mikarafuu ambapo kutokana na maelezo ya bwana shamba mikarafuu inaathirika sana kwa kulima mazao mengine ndani ya shamba la mikarafuu, hali inayoweza kupelekea mikarafuu hiyo kudhoofika na hatimae kufa

Uongozi wa Wizara kuhakikisha unachukua jitihada za makusudi katika ufuatiliaji wa maeneo ya mashamba ya mikarafuu pamoja na kuweka misingi ya udhibiti mzuri kwa kutoruhusu wale wote waliokodishwa au waliopewa kuyatunza mashamba hayo kwa kutolima kilimo changine ndani ya shamba hizo ili kuweza kunusuru upotevu wa rutuba pamoja na unyonywaji wa maji maji yanayoka katika mashamba hayo ambayo hutumika kustawisha ubora wa shamba na ukuaji mzuri wa miche ya mikarafuu.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara imepokea ushauri uliotolewa na imefanya ufuatiliaji wa kina ili kuhakikisha kilimo chengine kikiwemo cha mihogo na migomba hakifanyiki ndani ya mashamba za mikarafuu baada ya mikarafuu kufikia kijitegemea (baada ya miaka 3 au 4).

Wizara imeshaanza kuufanyia kazi ushauri huu kwa kuwaita wananchi wanaolima katika maeneo ya shamba ambao wengi wao ni wafanyakazi wa WKUMM na kuwataka walime kilimo himilivu kinachoendana na mikarafuu, kama vile ulimaji wa mazao ya viungo hasa tangawizi, manjano na vanilla na kuachana na kilimo cha muhogo ambacho sio rafiki kwa karafuu. Aidha kilimo cha migomba kikifanyika vizuri kinalea miche ya mikarafuu kwa kusaidia kivuli na maji. Wafanyakazi wa WKUMM wamepewa maeneo haya ili kusaidia kufanya ulinzi kutokana na uhaba wa walinzi katika mashamba hasa la Makuwe.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa wakati Mkaguzi anakutana na watendaji wa Wizara ya Kilimo Pemba na kutembelea Mashamba ya Mikarafuu hususan la Kinyasini ni kweli changamoto ya kuwepo ukulima usifuata utaalamu ulikuwa ukifanyika. Changamoto hiyo imesababishwa zaidi na uhaba wa wafanyakazi wa Wizara kusimamia ipasavyo ukulima unaofanywa na Wakulima.

Hata hivyo, kupitia maelezo ya watalaamu, Kamati imebaini kuwa kilimo mchanganyiko huhitajika wakati Mkarafuu unapokuwa mdogo lakini hutakiwa kuondolewa kadiri mkarafuu unvyokuwa kwani mizizi ya mkarafuu huwa inatanuka na wakulima (wasiokuwa na ujuzi) huwa wanaikata wakati wa kupalilia.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ihakikishe inafuatilia kwa karibu ukulima wa kilimo cha Mikarafuu hususan katika ngazi ya jamii ili waweze kuwapatia utaalamu wa kilimo cha mikarafuu wakati inapokuwa midogo, utaratibu wa kupalilia na maumizi mazuri ya mazao mbadala ndani ya shaba la mikarafuu.

**Hoja nambari 12.1.1.4: Kutokuendelezwa kwa upandaji wa mikarafuu mipya ndani ya shamba za mikarafuu.**

Kuwepo kwa maeneo mengi yaliyo wazi ambayo hayajapandwa mikarafuu mipya baada ya kuondoka mikarafuu ya asili iliyokuwepo ambapo kunaweza kupelekea kutoa mwanya kwa wakulima kupanda mazao mengine katika maeneo yaliyoachwa wazi kufuatia kufa au kukatwa kwa mikarafuu iliyokuwepo ndani ya shamba za mikarafuu.

Uongozi wa Wizara kuhakikisha unaendeleza upandaji wa mikarafuu katika maeneo ya wazi yaliyomo ndani ya shamba za mikarafuu pamoja na kutokuruhusu kufanyika kwa kilimo chengine ndani ya shamba hizo kuweza kunusuru uharibifu umaoweza kutokezea ikiwemo kuharibika au kufa kwa mikarafuu hiyo

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara imepokea ushauri uliotolewa na itafanya ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha kilimo chengine hakifanyiki ndani ya mashamba za mikarafuu.

Hata hivyo, Wizara inaiomba Kamati ya PAC kupitia kwako Mwenyekiti utuombee ziada ya bajeti/fedha kwa kuwa ushughulikiaji wa mashamba haya ya Serikali zamani ulitegemea sana ajira za muda (daily paid) au ajira za kudumu za wahudumu wa shamba. Kwa sasa Serikali imeondosha ajira za muda. Hivyo, inakuwa vigumu kuwa na wafanyakazi wa kutosha wa kupanda na kusimamia mikarafuu mipya kutokana na ukubwa wa mashamba.

Aidha, Wizara imeupokea ushauri huu na imeshaanza kuufanyia kazi. Kwa mfano, mnamo mwaka 2021 jumla ya miche 200 ya mikarafuu ilipandwa katika shamba la Mikarafuu la Makuwe. Miche 50 mikarafuu ilipandwa katika shamba la Mikarafuu la Daya. Kwa mwaka 2023, miche 450 ya mikarafuu imepandwa katika shamba la Makuwe. Wizara itaendelea kupanda mikarafuu mipya kila mwaka katika mashamba yake. Hata hivyo, ukuwaji wa miche hii unahitaji huduma za usafi wa mashamba ambazo zinahitaji fedha ambazo upatikanji wake unakuwa sio wa uhakika. Tunaiomba Kamati yako iishauri Serikali Kuu iweze kuruhusu ajira za muda ili mashamba haya yawe katika hali ya usafi muda wote.

Kuhusu kunusuru uharibifu wa mikarafuu unaoweza kutokea kutokana na kulima mazao mengine ndani ya mashamba, Wizara imechukuwa hatua ya kuwaita wananchi wanaolima katika maeneo ya shamba na kuwataka walime kilimo himilivu kinachoendana na mikarafuu, kama vile ulimaji wa mazao ya viungo hasa tangawizi, manjano na vanilla badala ya kilimo cha mihogo na migomba.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba Wizara pekee bila kupata msaada unaohitajika haiwezi kuendeleza ipasavyo maeneo matupu yasiyokuwa na mikarafuu ndani ya mashamba ya Mikarafuu. Hili linatokana na ukweli kwamba Wizara inao wafanyakazi wachache mno wa kutekeleza kazi hiyo. Kwasasa, wafanyakazi wa Wizara huwa wanajikusanya na kwenda kupanda kwa pamoja mikarafuu katika maeneo matupu.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Ili kuweza kuyanusuru mashamba yetu ya mikarafuu, Serikali ifanye maamuzi magumu yafuatayo:

1. Kurudisha utaratibu uliokuwepo zamani wa kuruhusu ajira ya wafanyakazi wa muda (wahudumu) wa kupanda mikaafuu mipya katika maeneo au mashamba yaliyokuwa hayana mikarafuu.

2. Kuiongezea bajeti maalum Wizara ya Kilimo itakayohakikisha inatumika kwa kazi za usimamizi na uendelezwaji wa ukulia wa mikarafuu katika maeneo matupu.

3. Kuwepo na usimamizi wa karibu wa uhuishaji wa kilimo cha mikarafuu katika maeneo matupu kwa vile kilimo hicho kinahitaji utaalamu katika ukuaji wake.

**Hoja nambari 12.1.1.5: Kutokufanyiwa usafi kwa shamba za mikarafuu**

Uwepo wa baadhi ya shamba za mikarafuu zenye mapori ambazo hazijafanyiwa usafi na kuondolewa mapori hayo ili kuifanya mikarafuu iweze kupata nafasi ya kustawi na kukua na hatimae kuweza kutoa mazao makubwa. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea mikarafuu hiyo kukosa kukua kwa haraka kutokana na kuzidiwa na miti mingine iliyomo ndani ya shamba hizo.

- Uongozi wa Wizara kuhakikisha unafanya usafi wa mara kwa mara ndani ya shamba za mikarafuu ili kutoa nafasi kwa mikarafuu hiyo kuweza kustawi na kukua na hatimae kupatikana kwa mazao yaliyokusudiwa.
- Kuendeleza upandaji wa mikarafuu katika maeneo ya wazi yaliyomo ndani ya shamba za mikarafuu pamoja na kutokuruhusu kufanyika kwa kilimo chengine ndani ya shamba hizo ili kunusuru kupoteza haiba na taswira ya mashamba hayo.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara imepokea ushauri uliotolewa, hata hivyo, inaomba Kamati ya PAC kupitia kwako Mwenyekiti utuombee ziada ya bajeti/fedha kwa kuwa ushughulikiaji wa mashamba haya ya Serikali ulitegemea sana ajira za muda (daily paid) au ajira za kudumu za wahudumu wa shamba. Kwa sasa Serikali imeondosha ajira za muda, na pia imeweka mkazo wa kuajiri wataalamu.Hivyo, inakuwa vigumu kuwa na wafanyakazi wa kutosha wa kuyafanyia usafi mashamba kutokana na ukubwa wake.

Katika kuufanyia kazi ushauri huu WKUMM imeshachukua juhudi mbali mbali: Kwa mfano mnamo mwaka 2022, Ofisi Kuu Pemba ilipokea Tzs. 20,000,000.00 kwa ajili ya kulifanyia usafi shamba la Mikarafuu la Makuwe. Kazi hii ilifanywa kwa ushirikiano na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kikosi cha Mafunzo). Aidha, kupitia fedha za OC, Idara ya Kilimo ilifanya usafi wa Shamba la Mikarafu la Daya ambapo Tzs. 2,000,000.00 zilitumika. Wizara itaendelea kufanya usafi wa mashamba haya kadiri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu. Aidha; upandaji wa mikarafuu katika maeneo ya wazi ya Shamba la Dayana Makuwe unaendelea.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imegundua kuwa uwepo wa misitu katika mashamba ya mikarafuu unasababishwa zaidi na uwepo wa wafanyakazi wachache ukilinganisha na wingi wa Mashamba yaliopo pamoja na upungufu wa fedha za usafishaji wake. Hata hivyo, Kamati imeridhika na hatua zinazochukuliwa na Wizara Pemba za kuwatumia Wafungwa katika usafishaji wa baadhi ya mashamba hayo kwa kuwapatia fedha zinazotumika katika ununuzi wa vifaa vya usafishaji, mafuta ya gari na chakula. Kamati imelithibitisha hilo kwa kuona nyaraka zilizothibitisha matumizi yake ikiwemo hati ya malipo ya tarehe 1/3/2022 yenye nambari 0897.

Sambamba na hilo, Kamati ya PAC ilifanikiwa kulitembelea shamba la Kinyasini na kushuhudia kwamba limefanyiwa usafi wa kufyekwa lakini tayari msitu mwengine ulikuwa ushaanza kuota. Hata hivyo, mapendekezo ya hoja ili kuweza kuifanyia kazi ipasavyo, mapendekezo yake yanalingana na yale yaliyoainishwa katika hoja nambari 12.1.1.4.

**Hoja nambari 12.1.1.6: Kutokufikiwa kwa malengo ya uzalishaji na usambazaji wa miche ya mikarafu**

Kuwepo kwa vitalu vya miche ya mikarafuu katika maeneo mbali mbali ya Pemba vilivyoanzishwa na Wizara kwa ajili ya kuatika miche ya mikarafuu na kusambaza kwa wakulima mbali mbali nchini ili kuweza kunyanyua kilimo cha mikarafuu kwa kupanda mikarafuu mipya katika shamba za Serikali na shamba za wananchi binafsi.

Dosari iliyobainika ni kutokufikiwa kwa malengo yaliyowekwa ya uzalishaji na usambazaji wa miche ya mikarafuu katika vitalu hivyo ambapo ni kurejesha nyuma juhudi za Serikali za kunyanyua kilimo cha mikarafuu nchini.
Kukosekana kwa muongozo sahihi unaotumiwa na Wizara katika ugawaji wa miche kwa wananchi wanaomiliki maeneo yao ya uzalishaji ambapo Sera ya

Serikali ni kuwagaia wananchi hao miche bila ya kutozwa fedha yoyote kwa lengo la kutoa fursa kwa wakulima kuen deleza kilimo cha mikarafuu kwa lengo la kuiwezesha Serikali kukuza uchumi wake unaotegemea zao la karafuu.

- Uongozi wa Wizara kuhakikisha unazalisha na kusambaza miche kadri iwezekanavyo ili kuweza kukuza kilimo hicho nchini.
- Uongozi wa Wizara kuchukua jitihada za makusudi ikiwemo kuwaekea mazingira mazuri ya upatikanaji wa maji ya kumwagilia na udongo wenye rutba kwa wale wote wanaoshiriki katika upandaji wa miche ya mikarafuu ili kuhakikisha tija inayokusudiwa inapatikana ikiwemo pamoja na upatikanaji wa miche kwa wingi ambapo itakuza kilimo na Serikali kupata faida inayoitegemea kutokana na uvunaji wa mazao hayo.
- Wizara iweke miongozo na mipango imara ya upandaji wa miche ya mikarafuu katika maeneo ya ekari ili kuweza kukuza na kuongeza idadi ya miche ya mikarafuu kwa lengo la kisaidia Serikali kupanga shughuli zake za baadae zinazotegemea uvunaji wa zao la karafuu ili kukuza kipato cha Serikali katika kutoa huduma bora kwa wananchi

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara imepokea ushauri uliotolewa na kuufanyiakazi kwa kuomba mashirikiano zaidi na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ili kupatiwa fedha kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu ambao unapaswa kuwezesha upatikanaji wa mahitaji yote yanayotakiwa kwa ajili ya uzalishaji wa miche ya mikarafuu yakiwemo ya udongo na miundombinu ya umwagiliaji maji.

Aidha, Wizara ina mipango mizuri ya ugawaji wa miche ya mikarafuu isipokuwa tatizo lililopo ni kwamba miche hiyo haitoshi kutokana na uzalishaji mdogo. Tatizo jengine ni kwa wananchi wenyewe kutoisimamia vyema wakati wanapokabidhiwa.

Ni kweli Wizara haijaweza kufikia malengo ya uzalishaji na usambazaji wa miche ya mikarafuu kutokana na changamoto mbali mbali zinazoikabili ikiwa ni pamoja na upatikanaji mdogo wa fedha. Hata hivyo, WKUMM imeanza kuchukua juhudi ili kuhakkisha inaelekea kwenye uzalishaji mkubwa wa miche ya mikarafuu. Aidha, nichukue fursa hii kuithibitishia Kamati yako kwamba WKUMM imeendelea kutoa miche mizuri na yenye sifa kubwa.

Upatikaji wa maji ya kumwagilia miche umeimarishwa katika Shamba la Makuwe kwa uchimbaji wa kisima ambacho kimeshaanza kutumika. Tatizo la ukosefu wa maji ya kumwagilia limetatuliwa pia katika Vitalu vichache. Kupatiwa ufumbuzi kwa tatizo la maji kutasaidia uzalishaji wa miche katika maeneo haya.

Vile vile Wizara ya Kilimo Ofisi Kuu Pemba ilipeleka maombi (OR Fedha na Mipango) ya kutaka kuachiwaploti mbili kupata mbegu za karafuu au kukodisha ili fedha zitakazopatikana zitumike kuongeza uzalishaji wa miche lakini haikupata majibu.

Pia Wizara imepanga kuwasilisha maombi ya kupatiwa fedha kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu ili kufanikisha uzalishaji na usambazaji wa miche. Uzalishaji wa miche utakapoongezeka kupitia juhudi hizi, hata wamiliki mashamba ya eka tatu watapatiwa miche itakayopandwa katika eka hizo hatua kwa hatua.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inatambua kwamba kihistoria zoezi la uwezeshaji katika uzalishaji wa miche lilikuwa likitekelezwa na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) na Wizara hubakia kutoa utaalamu wa uzalishaji wa miche ya mikarafuu. Kamati imebaini kuwa zoezi hilo kwasasa limesita kwa kipindi ambapo ZSTC hawatoi fedha za kutosha zitumikazo katika uzalishaji wa miche. Lakushangaza ni kwamba karafuu zikiwa tayari kuvunwa ndio ZSTC hujitokeza kushughuliki masuala ya ununuzi na uuzwaji wa malighafi hiyo nje ya nchi.

Kamati pia imegundua kuwa utaratibu wa uatikaji miche uliokuwa ukitumika zamani wa kutumia matende ya karafuu hivi sasa umekuwa mgumu kutumika kwa vile karafuu huwa haziachiwi mpaka zikapea sana kufikia hatua ya kupatikana matende na hatimae kuoteshwa au kuatikwa miche. Aidha, baada ya karauu kupea, Wizara ya Kilimo huwa haiachiwi hata shamba moja kwa ajili ya kuziwacha zipee ili ziwe matende badala yake karafuu zote huchumwa, kuuzwa na kusafirishwa.

Kwa utaratibu huu, Kamati ya PAC imebaini kuwa kilio cha upatikanaji wa miche mizuri na ya kutosha itabakia kuwa ndoto kama hakuna juhudi za makusudi zitakazochukuliwa na Serikali katika utatuzi wa changamoto ya upatikanaji wa malighafi (matende) ya uzalishaji miche pamoja na kuwepo kwa watendaji wataalamu wa kutosha wa kufanya kazi hiyo.

Wizara hutumia wafanyakazi wake na baadhi ya wananchi kuokota matende na kuchimba miche ambayo huatikwa na kusimamiwa kwa leng la kuzalisha miche.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kutokana na uwepo wa changamoto ya kutopatikana miche, Serikali (ZSTC) ihakikishe inaipatia Wizara ya Kilimo japo shamba moja litakalotumika kwa ajili ya kuziwacha karafuu hadi kuwa matende na kuziatika kwa lengo la upatikanaji wa miche.

2. Wizara ipeleke taarifa rasmi katika Kamati Maalum ya Ukodishaji Mashamba ya Mikarafuu kwamba ishughulikie pia na changamoto ya upungufu wa Miche.

3. Serikali kwa kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango iandae utaratibu utakaowezesha Wizara ya Kilimo inapatiwa asilimia fulani kutoka katika mapato ya ukodishwaji na uuzaji wa karafuu kwa ajili kazi ya uatikaji miche ya mikarafuu.

4. Wizara iwatumie ipasavyo wafanyakazi walionao vizuri kwa kuwaelekeza washuke chini waipo wananchi ili waweze kuatika miche kitaalamu.

**Kilimo Hoja nambari 12.1.1.7: Malimbikizo ya madeni ya mapato shilingi 66,125,000**

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inawadai wananchi mbali mbali jumla ya shilingi 66,125,000 kutokana na ukodishwaji wa mashamba ya mikarafuu katika vipindi tofauti vya zao hilo ambapo kunaweza kupelekea kuwepo kwa upotevu wa mapato yatokanayo na ukodishwaji wa shamba hizo jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma yam waka 2016.

Uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba hatua za kulipwa madeni hayo zinachukuliwa ili wananchi waliokodishwa shamba hizo waweze kulipa madeni yao na hatimae kuongeza mapato ya Serikali. Aidha ni vyema Wizara kujipangia sera maalumu ya ukodishwaji wa mashamba ya mikarafuu ikiwemo kutoza asilimia 50 ya thamani ya shamba linalokodishwa na asilimia iliyobaki itapaswa kulipwa mara baada ya kuuza kwa mazao ya mikarafuu.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara inasikitika kueleza mbele ya Kamati yako kuwa deni la TZS 66,125,000.00 bado halijalipwa pamoja na juhudi mbali mbali ambazo zimechukuliwa. Kwanza; wahusika ambao wanadaiwa waliitwa na Kamati ya Ukodishaji wa Mashamba ambayo inajumuisha Taasisi mbali mbali za SMZ vikiwemo Vyombo vya Ulinzi na Usalama na kutakiwa kulipa deni lao. Hata hivyo wadaiwa hawakuweza kulilipa deni hili kama walivyokubaliana na Kamati. Baada ya hapo Wizara ya Kilimo, Ofisi Kuu Pemba ilitoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama ya Mkoa ili kusaidia ufuatiliaji wa kulipwa madeni hayo. Kamati ya Usalama ya Mkoa iliwaita wahusika wote wanaodaiwa na kuwataka kutimiza wajibu wao wa kulipa deni, vinginevyo taratibu za kisheria zifuatwe. Wadaiwa waliiahidi Kamati ya Usalama ya Mkoa kuwa italilipa deni hilo. Hata hivyo, mpaka sasa hizi watu hao bado hawajalipa.

Changamoto ya malimbikizo ya madeni tunategemea kutokuwepo tena siku za usoni. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imefanya marekebisho ya Mkataba wa Ukodishaji wa Mashamba ambapo kwa sasa Mwananchi yeyote atakaekodi Shamba la Mikarafuu, atalazimika kulipa fedha zote za kukodia kabla hajaanza kuchuma karafuu zilizomo shambani.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia ukweli wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba sababu kuu inayopelekea kutolipwa kwa malimbikizo ya madeni hayo ni muhali uliopo kwa Wizara unaopelekea kushindwa kuwachukulia hatua za kisheria Wadaiwa wakati fedha ya Serikali imeshatumiwa bila ya kuwepo tija yoyote, umefika wakati kwa Wizara ya Kilimo kuwafungulia mashitaka ya Madai Wadaiwa wote ili fedha hizo ziweze kurudishwa na kutekeleza mipango ya Serikali iliyokusudiwa.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ya Kilimo ishirikiane na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufungua mashauri ya Madai (Mahakamani) kwa Wadaiwa wote wa fedha za Mashamba ya Mikarafuu ili waweze kulazimishwa kulipa fedha zinazodaiwa.

**Hoja nambari 12.1.1.8: Kutokufanyiwa usafi kwa shamba za mikarafuu za Ekari Tatu Tatu**

Kuwepo kwa baadhi ya shamba za eka tatu tatu zenye mapori ambazo hazijafanyiwa usafi na kuondolewa mapori hayo ili kuifanya mikarafuu iweze

kupata nafasi ya kustawi na kukua na hatimae kuweza kutoa mazao makubwa. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea mikarafuu hiyo kukosa kukua kwa haraka kutokana na kuzidiwa na miti mingine iliyomo ndani ya shamba hizo.

- Uongozi wa Wizara kuhakikisha unafanya usafi wa mara kwa mara ndani ya shamba za mikarafuu ili kutoa nafasi kwa mikarafuu hiyo kuweza kustawi na kukua na hatimae kupatikana kwa mazao yaliyokusudiwa,
- Kuendeleza upandaji wa mikarafuu katika maeneo ya wazi yaliyomo ndani ya shamba za mikarafuu pamoja na kutokuruhusu kufanyika kwa kilimo chengine ndani ya shamba hizo.
- Serikali kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha inaandaa mazingira madhubuti ya kuandaa fungu la fedha linalotokana na ruzuku ya kuweza kuwapatia Wizara kwa lengo la kuisaidia Wizara kufanya usafi wa mashamba hayo mara kwa mara ili kuyapa nafasi nzuri ya kukua, kunawiri na hatimae kuzaa mazao bora.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara imepokea ushauri uliotolewa na itaufanyiakazi. Hali ya kutosafishwa mashamba ya ekari tatu iliyopo sasa imesababishwa na baadhi ya wananchi kusubiri mzao wa karafuu ili kupata faida bila kuyasafisha mashamba hayo. Wizara katika jitihada za kuhamasisha usafi wa mashamba ya ekari tatu tatu, wakati wa ukodishaji iliweka vigezo vifuatavyo:

- Shamba lililosafishwa ndani ya mwaka husika na kuendelezwa kwa kupandwa mikarafuu alilipwa kifuta jasho cha **asilimia 40** ya thamani ya kodi ya shamba.
- Shamba lililosafishwa ndani ya mwaka husika lakini halikupandwa mikarafuu alilipwa kifuta jasho cha **asilimia 30** ya thamani ya kodi ya shamba.
- Shamba ambalo limesafishwa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita alilipwa kifuta jasho cha **asilimia 20** ya thamani ya kodi ya shamba.
- Shamba lisilosafishwa kabisa na halijapandwa mikarafuu lakini anailinda miti iliyomo alilipwa kifuta jasho cha asilimia 10 ya thamani ya kodi ya shamba.

Kwa sasa, Wizara ikimkabidhi mwananchi shamba ya ekari tatu inampa masharti likiwemo la kulitunza na kupanda mikarafuu mipya au vinginevyo atanyang'anywa. Hivyo Wizara itafanya ufuatiliaji wa karibu na ikibidi itachukuwa hatua stahiki.

**Hoja nambari 12.1.1.9: Wananchi kuuza shamba za ekari tatu walizokabidhiwa na Serikali**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa shamba za ekari tatu tatu walizokabidhiwa wananchi mbali mbali na Serikali ili kuzishughulikia na kuruhusiwa kutumia shamba hizo kwa ajili ya shughuli mbali mbali za kujikwamua kimaisha. Dosari iliyobainika ni kuuzwa kwa shamba hizo kunakofanywa na wananchi waliokabidhiwa shamba na Serikali ambapo ni kinyume na matakwa ya waraka wa ugawaji wa ekari jambo ambalo linakwamisha na kurejesha nyuma juhudi na malengo ya Serikali ya ugawaji wa shamba hizo kwa wanachi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unasimamia mashamba ya ekari tatu ipasavyo ili kuepusha uwezekanao wa kuporwa mashamba hayo na wananchi kwa kisingizio cha ukali wa maisha.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara imepokea ushauri uliotolewa na itaufanyiakazi kwa umakini mkubwa. Tathmini ya Sera ya Ardhi inaonesha uwepo wa hali hiyo na kwamba shamba za ekari zinabadilishwa matumizi yake. Wizara katika mipango yake ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya Sera ya Kilimo ni kuendelea kushirikiana na Wizara ya Ardhi kuyapima mashamba hayo na kusimamia matumizi yake ili kufikia malengo ya kutolewa kwake.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Wizara imekiri kuwepo kwa kasoro hiyo, Kamati ya PAC, haikuwa na hoja zaidi isipokuwa imesisitiza kwamba juhudi za makusudi zinahitajika ili kutatua kasoro hiyo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ihakikishe inasimamia mashamba ya ekari tatu ipasavyo ili kuweza kubaini mashamba ambayo yameuzwa au kutumika kinyume na utaratibu.

**Hoja nambari 12.1.1.10: Madeni ya ukodishaji wa mashamba ya ekari tatu na vifutajasho kwa wasimamizi wa shamba hizo shilingi 848,944,000**

Kuwepo kwa shamba za ekari tatu tatu walizokabidhiwa wananchi mbali mbali na Serikali ili kuzishughulikia na kuruhusiwa kutumia shamba hizo kwa ajili ya shughuli mbali mbali za kujikwamua kimaisha.
Dosari iliyobainika ni kuuzwa kwa shamba hizo kunakofanywa na wananchi waliokabidhiwa shamba na Serikali ambapo ni kinyume na matakwa ya waraka wa ugawaji wa ekari jambo ambalo linakwamisha na kurejesha nyuma juhudi na malengo ya Serikali ya ugawaji wa shamba hizo kwa wananchi.

Uongozi wa Wizara kuhakikisha unasimamia mashamba ya ekari tatu ipasavyo ili kuepusha uwezekano wa kuporwa mashamba hayo na wananchi kwa kisingizio cha ukali wa maisha.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara inakiri kwamba madeni yaliyopo ni muda mrefu. Hata hivyo, Wizara inaamini kuwa kiasi kikubwa cha madeni hayo yameshalipwa na wananchi. Kinacholeta tabu ni namna ya kufanya uhakiki wa ulipaji wa madeni hayo na kuweza kuwafuta wadaiwa kwenye orodha. Baadhi ya sababu ambazo tulipata kuzieleza huko nyuma, ni kwamba:

(a) Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango) kutotupatia orodha ya wananchi waliolipa kupitia malipo ya vifuta jasho. Serikali ilitoa fedha nyingi kwa ajili ya ulipaji wa vifuta jasho katika awamu ya kwanza kupitia Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango) Pemba, na ilitoa maelekezo kuwa kila mwenye kudaiwa akatwe deni lake na apewe stakabadhi ya malipo ya deni lake. Hadi leo Wizara yetu haijapatiwa taarifa hizo.

(b) Zoezi la ukodishaji lilivyoanza Wizara ilitakiwa kuwa na Hesabu (Account) moja inayosomeka WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI PEMBA 041101000013 kwa ajili ya kukusanyia mapato yake ambayo ilikuwa inakusanya fedha za mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali. Baadae Wizara ikatakiwa kutumia Hesabu (Account) maalum ya kukusanyia mapato ya mashamba ya karafuu inayosomeka MAPATO YA MIKARAFUU 0735684001. Katika mabadiliko haya, wananchi walioanziwa zoezi la ukodishaji hawakurejewa kufanyiwa mabadiliko ya Hesabu hizi na hivyo waliendelea kulipa kwa kutumia Hesabu ya zamani ambayo mapato ya karafuu hayakuwa yanafuatiliwa kwenye Hesabu hiyo.

- Wizara ilifanya uhakiki mdogo kwa kuwaandikia barua za indhari ya kuwapeleka Mahakamani wananchi 60 wanaodaiwa (26 wadaiwa wa 2017 na 34 wadaiwa wa 2019) kutoka Wilaya zote Pemba – matokeo ni kwamba

wananchi wengi walikuja na stakabadhi ya malipo kutoka Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango) na wengine walikuja risiti za Benki ambazo walikaa nazo nyumbani. Baadhi ya wananchi walidai madeni yao kufutwa au kupunguzwa kutokana na ufuatiliaji wa Kamati Maalum ya BLM iliyoundwa kufuatilia malalamiko ya wananchi waliokodishwa.

- Kwa ujumla juhudi za kudai fedha hizi zinahitaji mashirikiano ya hali ya juu. Zoezi la ukodishaji liliwashirikisha taasisi tofauti zikiwemo Ofisi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Wizara ya Fedha, ZAECA, Ofisi ya Rais (Usalama), na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya zilizoongozwa na Wakuu wa Wilaya. Kwa kutambua hali hii, Serikali kupitia kikao cha Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza la Mapinduzi (BLM) kilichoongozwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kilichofanyika mwezi Septemba, 2018 katika kujadili taarifa ya zoezi la ukodishaji na madeni ya mashamba ya karafuu kwa mwaka 2017, pamoja na mambo mengine kiliagiza orodha ya wananchi wanaodaiwa kukabidhiwa kwa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ili hatua madhubuti ziweze kuchukuliwa katika kudai fedha za Serikali. Wizara, kupitia kwa Mhe. Waziri, ilichukua hatua za kukutana na Kamati ya kila Wilaya na kukabidhi orodha ya wadaiwa mwezi Oktoba, 2018.

Kuhusu, deni la vifuta jasho ambalo ni la awamu ya pili tayari Wizara imeshawasilisha Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango) orodha kamili ya majina ya wakulima wanaodai vifutajasho kwa ajili ya kufanyiwa malipo hayo. Utaratibu uliopo ni kwamba Wizara yetu inawasilisha Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango) orodha ya wanaodai na kufanyiwa malipo kupitia Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango) Pemba.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya juhudi ambazo Wizara inazichukua za kuwatumia wananchi waliopatiwa Mashamba ya ekari tatu kuyasafisha, bado ni jukumu la Wizara kuhakikisha inawasimamia wananchi hao ipasavyo. Hata hivyo, Kamati ya PAC imegundua kuwa kuwepo kwa bajeti isiyotosheleza mahitaji ya uendeshaji wa mashamba hayo ndio kumepelekea kutosafishwa kwake.

Sambamba na hilo, Kamati ya PAC imebaini kucheleweshwa kwa malipo ya kifutajasho kwa wahudumiaji wa mashamba hayo nako kunasababisha kuwepo kwa msitu (uchafu) katika mashamba hayo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ya Kilimo ihakikishe inasimamia kwa karibu zoezi la usafishaji wa mashamba ya ekari tatu ili yaweze kuwa masafi wakati wowote.
2. Wizara ya kilimo ifuatilie kwa karibu Wizara ya Fedha na Mipango ili fedha za kifutajasho zipatikane na kuwafikia walengwa.

**Hoja nambari 12.1.1.11: Dosari zilizobainika katika shamba za ekari tatu.**

Kuwepo kwa madeni ya mapato yenye jumla ya shilingi 848,944,000 yatokanayo na ukodishaji wa shamba za mikarafuu pamoja na jumla ya shilingi 83,166,000 kama ni vifuta jasho kwa wananchi wa Wilaya nne za Pemba kwa ajili ya ushughulikiaji wa shamba za mikarafuu za ekari tatu zilizokodishwa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 3 cha mkataba wa ukodishaji kinachomtaka mkodishwaji kulipa ada ya ukodishaji ndani ya wiki mbili tokea tarehe ya kukodishwa.

Uongozi wa Wizara kuhakikisha unaandaa idadi sahihi ya mashamba ya ekari 3 ikiwa ni pamoja na kuyafanyia uhakiki wa kina shamba hizo.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara imepokea ushauri uliotolewa na itaendelea kuufanyiakazi kwa umakini zaidi. Kwa sasa, Wizara ina taarifa za uwepo wa mashamba ya ekari tatu **9,982** yaliyopo Pemba ambayo yamekabidhiwa kutoka Wizara ya Ardhi pamoja na tathmini iliyofanyika kwa Masheha. Hadi mwaka 2018 mashamba 6,315 sawa na asilimia 63 yameshapatikana au kujulikana wapi yalipo.

Hali ya mashamba hayo zimetofautiana, mfano mashamba 5,822 yaliyotambuliwa mwaka 2015 na 2016 yameonesha kuwa mashamba 2,222 ni ya mikarafuu, mashamba 721 ni ya minazi na ardhi halia, na mashamba 1,884 ni ya mazao mchanganyiko. Vile vile, mashamba 395 yameachwa kwa muda mrefu hivyo yamekuwa misitu ya asili, na mashamba 600 yamegeuzwa kuwa makaazi. Aidha, kati ya mashamba 5,822 ni mashamba 1,200 tu ndiyo yaliyoonekana kuwa na mikataba inayotambuliwa, mashamba 3,197 hayana mikataba, na mashamba 1,425 hayana usimamizi. Baadhi ya changamoto zilizopo katika utafutaji wa mashamba hayo ni pamoja na:

- Utayari mdogo wa baadhi ya taasisi, viongozi, watendaji, na wananchi juu ya kuyahifadhi mashamba ya eka tatu hali inayopelekea mashamba hayo kujengwa, kuuzwa, kurejeshwa kwa wamiliki wa asili, nk.

- Uwepo wa mashamba ambayo hayakutolewa Mikataba hali inayopelekea mashamba hayo kufichwa na wanaoyajua.
- Uwepo wa mashamba ambayo hayana kitu (ardhil halia) hali inayopelekea viongozi wa eneo hilo kutozingatia masharti ya mashamba ya eka.
- Uwepo wa wananchi waliopewa mashamba ya eka kuwepo katika Shehia totafuti na yalipo mashamba hayo hali inayopelekea viongozi wa eneo lenye mashamba ya eka kutojuwa uwepo wa mashamba hayo.

Mashirikiano madogo kutoka kwa wananchi wanaoyajuwa mashamba ya eka kwa kuhofia kurogwa, kutengwa katika jamii, na kupata lawama kwa wanaoyashikilia.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Uchunguzi wa hoja hii kwa kiasi kikubwa unafanana na uchunguzi uliofanywa na Kamati ya PAC katika hoja nambari 12.1.1.10 (hoja iliyopita). Hata hivyo, Kamati imebaini bado kuna wananchi wengi wanayajua mashamba ekari tatu ambayo yanamilikiwa na wananchi kiyume na utaratibu.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara iyafanyie uhakiki wa kina Mashamba ya ekari tatu ili yaweze kubainika na kuwa na idadi sahihi ya mashamba hayo.
2. Wizara itafute mbinu mbadala ikiwemo ya kuwapa wananchi motisha ili waweze kutoa ushirikiano katika ufichuaji wa mahamba ya ekari tatu ambayo bado yanamilikiwa na kutumiwa na wananchi kwa maslahi yao binafsi.

**UCHUNGUZI WA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA YA BOHARI KUU YA DAWA KWA MWAKA 2020/2021**

**Hoja nambari 2.4.1.1: Kuwepo kwa Idadi ndogo ya watumiaji wa Mfumo wa mSupply**

Ukaguzi umebaini kupitia mfumo wa mSupply Bohari Kuu ya Dawa imeweka jumla ya watumiaji (system users) wanane (8) ambapo idadi hiyo ni ndogo ukilinganisha na mahitaji na kazi zinazofanyika ndani ya mfumo za kushughulikia taarifa za upokeaji wa mahitaji ya dawa na vifaa tiba , uhifadhi wa dawa unaojumuisha kuhesabu (physical counting), kushughulikia taarifa za maombi kutoka vituo zaidi ya 190, Hospitali za Mikoa na Wilaya, na

Hosptali za Rufaa na kuandaa taarifa za dawa na vifaa tiba kwa ajili ya usambazaji kwenye vituo vya afya na Hospitali zote Unguja na Pemba.

Aidha, ukaguzi umebaini kua uhaba huu wa watumiaji wa mfumo wa mSupply umechangiwa kutokana na kuwepo kwa uchache wa leseni za watumiaji wa mfumo (user licences) ambapo ukaguzi umebaini uwepo wa leseni nane zinazotumika kwenye mfumo wa mSupply kwa wakati mmoja kwa wafanyakazi wa Bohari Kuu ya Dawa waliopo Unguja na Pemba.

Hali hii inaweza kuondoa ufanisi wa kazi na kupelekea kutokea kwa ucheleweshaji wa kusambazwa dawa na vifaa tiba kwa wakati katika vituo vya afya na hospitali jambo linaloweza kusababisha uhaba katika mahitaji ya dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa na hatimae kutokea ongezeko la maradhi na vifo kwa wakati mmoja kwa wagonjwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuongeza leseni za watumiaji wa mfumo wa mSupply kwa kuwapa ruhusa ya kufanya kazi kwenye mfumo (user licenses and access) kwa kiwango kikubwa ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa ikiwemo kurahisisha upatikanaji wa huduma za usambazaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya na Hospitali zote kwa wakati mmoja.

**Majibu ya Bohari Kuu ya Dawa**

Serikali imeamua kuongeza leseni 8, jumla zitakuwa 16, utaratibu huu utaanza baada ya kuingia mkataba mpya baina ya Wizara ya Afya na "Sustainable Solution" ambao unategemea kuanza Oktoba 2023 na kuengeza idadi ya watumiaji wa mfumo wa mSupply.

Hatahivyo, Uongozi wa Bohari umeanza mazungumzo na "Sustainable Solution" ili kuangalia uwezekano wa kutumia mfumo wa Open mSupply ambao utapunguza gharama kwa vile hautokuwa na malipo ya leseni, malipo yatakuwa ni "maintanance cost."

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya majibu ya Bohari Kuu ya kupanga kuongeza leseni nyengine nane za mfumo wa mSupply endapo wakiingia mkataba mpya na kampuni ya "Susainable Solutions" ifikapo Oktoba 2023, Kamati haijaridhishwa na kasi ndogo ya Bohari katika kuongeza leseni hizo, ambapo tangu ukaguzi kufanyika mwaka 2021 mpaka sasa bado kuna leseni nane (8).

**Hoja nambari 2.4.1.2: Dosari katika Usimamizi na Mgawanyo wa majukumu ya kazi za mfumo wa mSupply (SoD).**

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari mbali mbali katika usimamizi na mgawanyo wa majukumu ya kazi zinazofanywa kwenye mfumo (separation of duties) ambapo mtumiaji mmoja wa mfumo anafanya kazi zaidi ya moja kama vile kupokea taarifa za dawa kutoka kwa wasambazaji, kuhesabu dawa (physical counting), kushughulikia mahitaji ya dawa ya vituo na hospitali zote na kuandaa shehena ya dawa zinazohitajika na kuzisambaza katika vituo mbali mbali vilivyowasilisha mahitaji yao. Uwepo wa dosari hiyo umepelekea kujitokeza kwa dosari mbali mbali katika udhibiti wa dawa na vifaa tiba ndani ya Bohari Kuu ya Dawa.

Ukaguzi unaishauri uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa kupitia Wizara ya Afya kuongeza idadi ya wafanyakazi wenye ujuzi wa kutumia na kusimamia mahitaji ya mfumo kwa lengo la kunusuru utokeaji wa hali ya kutokupatikana kwa dawa na vifaa tiba kwa wakati ambapo kutatokana na kutokuwepo kwa mgawanyo sahihi wa majukumu, udhibiti imara na usimamizi mzuri wa taarifa za mahitaji ya dawa katika vituo vya Afya na Hospitali.

**Majibu ya Bohari Kuu ya Dawa**

Uongozi wa Bohari Kuu tayari umeshatengeneza miongozo ya kazi (SOPs) kwa kila kitengo na inatarajia kutayarisha majukumo ya kazi (Job discription) kwa wafanyakazi wake wote. Kila mfanyakazi atapewa uwezo wa kuingia kwenye mfumo kulingana na majukumu yake.

Ushauri umepokea wafanyakazi wa ziada kwa ajili ya Bohari Kuu Pemba wameombwa kama inavyoonekana katika barua yenye kumbukumbu nambari CMS/023/2022 ya tarehe 15/09/2022.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na hoja hii ya CAG ambapo dosari hii inapunguza ufanisi katika kuhakikisha dawa na vifaa tiba vinasambazwa kwa wakati ili kuleta tija. Halkadhalika, Kamati imeridhika na juhudi za Idara katika kuhakikisha ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali unafanyiwa kazi.

**Hoja nambari 2.4.1.3: Kukosekana kwa uidhinishaji wa utoaji wa dawa na vifaa tiba kwa kila hatua kupitia mfumo**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa watumiaji wachache wa mfumo ambapo mtu mmoja hufanya jukumu zaidi ya moja ikiwemo kupokea taarifa za mahitaji ya dawa na vifaa tiba kutoka katika vituo vya afya na hospitali, kuyafanyia kazi mahitaji hayo, kuhesabu na kuandaa shehena za dawa zinazohitajika na kuzisambaza katika vituo vinavyohitajika bila ya kuwepo mtu mwengine ambae atathibitisha na kuidhinisha uhalisia wa kilichohitajika na kilichoandaliwa kupelekwa sehemu husika ambapo

kunaweza kupelekea kujitokeza kwa vitendo vya upotevu mkubwa wa dawa na vifaa tiba na hatimae kuingiza hasara Serikali.

**Majibu ya Bohari Kuu ya Dawa**

Uongozi wa Bohari imewapangia majukumu ya kazi kwa Costonian, Dispatch Officer, Huduma za mteja na Afisa msambazaji.

Custodian anapokea maombi na kuyafanyia kazi, Dispatch Officer anahakiki mzigo uliofanyiwa kazi na Custodian na kuitayarisha kwa usambazaji, Huduma kwa wateja wanahakiki na kutoa ankara "invoice" na mwisho Afisa msambazaji anakabidhi mzigo kituoni.

(*KIELELEZO: SOPs*)

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imejiridhisha na hoja ya CAG na kubaini kua hali hii ingeweza kupelekea kupotea kwa dawa, vifaa tiba na fedha za Serikali kwa ujumla.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Licha ya Idara kuwapangia majukumu watendaji na wataalamu wa mfumo huo, Kamati inaishauri Idara kuhakikisha ugawamyaji huo wa majukumu kusimamiwa ipasavyo ili kuleta ufanisi katika utumiaji wa mfumo huo.

**Hoja nambari 2.4.1.4: Kutopatikana ipasavyo kwa huduma ya Msaada wa kiufundi "Techincal Support" kutoka kwa Mtengenezaji wa Mifumo (Kampuni ya SUSOL)**

Ukaguzi umebaini kwamba Bohari Kuu ya Dawa imeingia mkataba wa miaka mitatu na Kampuni ya SUSOL iliyopo New Zealand kuanzia tarehe 1 Julai 2020 ambapo mkataba huo una jumla ya thamani ya USD 8,083.24 kila mwaka ikiwa ni malipo kwa ajili ya leseni ya matumizi na msaada wa kifundi kwa mifumo mitatu ambayo ni mfumo wa mSupply, mfumo wa eLMIS - CE na mfumo wa Money Works.

Hata hivyo ukaguzi umebaini Bohari Kuu haipati vizuri msaada wa kiufundi kutoka kwa kampuni husika (SUSOL) licha ya kwamba gharama hizo bado zinaendelea kulipwa kwa muda wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2020.

Kutokupata kwa huduma ya msaada wa kifundi ipasavyo kumepelekea mifumo hiyo kutofanya kazi vizuri *"under performance"* na kupitwa na wakati *"out of date".* Hali hii inapelekea kukosekana kwa usalama wa taarifa zinazohifadhiwa ndani yake, kutokua na ufanisi katika utendaji kazi kutokana

na kutokunufaika na maboresho ya mifumo yanayotolewa na watengeneza mifumo kupitia mitandao.

**Majibu ya Bohari Kuu ya Dawa**

Kwa sasa Bohari inawasiliana mara kwa mara na SUSOL kwa njia ya email na zoom meeting, ambapo changamoto hujadiliwa na kufanyiwa kazi. SUSOL kwa kutumia "Helpdesk" wanapata mawasiliano moja kwa moja na mfumo wa Bohari na kuweza kurekebisha changamoto zozote zinazojitokeza.

Huu mfumo unafanyiwa maboresho kama ifuatavyo:

- 21/9/2022 version 6.03
- 16/2/2023 toleo 7.01
- Hivi sasa, Bohari inatumia mfumo wa mSupply Version 7.05 (20/06/2023) ambayo inaendana na kasi ya uendeshaji.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kua nafasi ya mawasiliano baina ya SOSUL na idara kupitia njia ya "Helpdesk" ilikuwepo tangu awali, ila imeonekana watumiaji wa mfumo huo hawakua na utaalamu wa kutumia "helpdesk" hiyo ya mSupply na kushindwa kuwajuulisha SOSUL changamoto zao.

Hali hii inapelekea kukosekana kwa thamani halisi ya fedha (Value for money) kwa fedha ambazo serikali inailipa SOSUL ili kutoa msaada wa kiufundi kwa mfumo huo wa mSupply.

**Hoja nambari 2.4.1.5: Kupitwa na wakati kwa mfumo wa mSupply unaotumiwa na Bohari Kuu ya Dawa**

Ukaguzi umebaini pamoja na kutokupatikana kwa msaada wa kiufundi unaotegemewa kutolewa na kampuni ya SUSOL kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba yaliyofungwa tarehe 1 Julai 2020 imebainika mfumo wa *"mSupply Version 4.12.04 "* unaotumiwa na Bohari Kuu ya Dawa kwa sasa umepitwa na wakati *(out of date)* kuanzia tarehe 29-07-2020 na kupelekea kujitokeza kwa taarifa zilizomo ndani ya mfumo kutokuwa sahihi na kutokupatikana wakati zinapohitajika na hivyo kupelekea Serikali kuingia hasara kubwa kwa kupoteza kumbu kumbu za dawa na vifaa tiba nchini.

Aidha kwa mujibu wa toleo la tarehe 19-10-2021 lililotangazwa na Mtengenezaji wa Mifumo "Vendor" limebainisha kwa sasa mfumo huo umefanyiwa maboresho na kutolewa toleo jipya la " mSupply Version 5.05 " Kiambatisho Nambari 3 kinahusika ambapo licha ya Serikali kuingia gharama za kulipia toleo jipya kwa gharama za dola za kimarekani USD 3,557.62 sawa

na shilingi 8,193,198.86 bado Bohari Kuu ya dawa haijafaidika na toleo jipya lililototangazwa na “Vendor” na kupelekea kuibebesha Serikali hasara kwa kutumia toleo la zamani ambalo halina usalama wa kutosha wa kutunza taarifa za dawa na vifaa tiba.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa kupitia Wizara ya Afya kufuatilia kwa kina suala la uboreshwaji wa mfumo kuwa katika toleo jipya *“ mSupply Version 5.05 ”* pamoja na upatikanaji wa msaada wa kiufundi katika mifumo yake kwa kampuni ya SUSOL ili kuweza kuimarisha mifumo hiyo iweze kufanya kazi vizuri kwa mujibu wa thamani halisi ya fedha (VFM) zilizoekezwa na zinazoendelea kuekezwa na Serikali kila mwaka.

**Majibu ya Bohari Kuu ya Dawa**

- Kwa sasa Bohari inawasiliana mara kwa mara na SUSOL kwa njia ya email na zoom meeting, ambapo changamoto hujadiliwa na kufanyiwa kazi. SUSOL kwa kutumia “Helpdesk” wanapata mawasiliano moja kwa moja na mfumo wa Bohari na kuweza kurekebisha changamoto zozote zinazojitokeza.

Huu mfumo unafanyiwa maboresho kama ifuatavyo:
- 21/9/2022 version 6.03
- 16/2/2023 toleo 7.01
- Hivi sasa, Bohari inatumia mfumo wa mSupply Version 7.05 (20/06/2023) ambayo inaendana na kasi ya uendeshaji.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na majibu ya Idara. Aidha, Kamati inaishauri Idara kuhakikisha mfumo huo unaendana na matoleo yanayotolewa na mtengenezaji mfumo ili kuhakikisha usalama na usahihi wa taarifa mbalimbali za mfumo.

**Hoja nambari 2.4.1.6: Kubadilika kwa gharama za dawa na vifaa tiba zilizowekwa katika Mfumo wa mSupply.**

Moja kati ya hatua za uendeshaji zinazofanyika ndani ya mfumo wa mSupply ni kutengeneza ankara za malipo ya dawa na vifaa tiba “Invoices”. Ankara hizo hutengenezwa na watumiaji wa mfumo ndani ya Bohari Kuu ya Dawa kupitia mfumo wa mSupply na huonesha bei na thamani halisi ya dawa na vifaa tiba zilizopo sokoni “Market Price” ambapo kama dawa hizo zingekuwa zinauzwa katika vituo vya afya na hospitali zingelionesha bei halisi ya soko.

Aidha, dhumuni la kuweka gharama za bei ya dawa na vifaa tiba kwenye ankara za malipo ndani ya mfumo wa mSupply ni kuisaidia Bohari Kuu ya

Dawa katika kutengeneza makisio ya bajeti ya ununuzi ya dawa na vifaa tiba kwa mwaka unaofuata.

Hata hivyo ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa mSupply una tatizo la kuzibadilisha wenyewe bei halisi za dawa na vifaa tiba zilizoingizwa kwenye ankara za malipo ndani ya mfumo na kuonesha bei nyengine zisizo na uhalisia jambo ambalo linapelekea kujitofautisha kwa bei zilizooneshwa katika ankara za awali ndani ya mfumo " data integrity issue ". Kubadilika kwa bei za dawa na vifaa tiba zilizowekwa kunaweza kupelekea kupoteza uhalisia wa taarifa za fedha za dawa zinazoingizwa katika mfumo pamoja na kukosekana kwa makisio ya bajeti za manunuzi na matumizi ya dawa na vifaa tiba kwa Bohari Kuu ya Dawa kwa miaka inayofuata.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kupitia Bohari Kuu ya Dawa kufuatilia kwa kina suala la uboreshwaji wa mfumo kuwa katika toleo jipya liliopo sokoni pamoja na upatikanaji wa msaada wa kiufundi katika mifumo yake kwa kampuni ya SUSOL ili kuweza kuimarisha mifumo hiyo iweze kufanya kazi vizuri kwa mujibu wa thamani halisi ya fedha (value for money) zilizoekezwa na zinazoendelea kuekezwa na Serikali kila mwaka.

**Majibu ya Bohari Kuu ya Dawa**

Version ya 7.05 mSupply imepunguza changamoto nyingi za mfumo, ila mawasiliano ya ukaribu baina ya SUSOL na CMS yanaendelea kwenye kuboresha mfumo huo. Pamoja na mawasiliano ya Helpdesk (mfumo unaotumika kutoa majibu ya changamoto zinzojitokeza papo kwa papo).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na jitihada za Idara za kuhakikisha mfumo huo unaendana na wakati (updated). Kamati inaishauri Idara iweze kufuatilia mfumo huo ili uwepo hai na katika wakati (updated) kwa muda wote.

**Hoja nambari 2.4.1.7: Kukosekana kwa miundombinu imara ya Mawasiliano ya Mtandao baina ya Bohari Kuu ya Dawa ya Unguja na Pemba**

Bohari Kuu ya Dawa kwa upande wa Unguja ipo Maruhubi ambapo miundombinu pamoja na mfumo mkuu unaoshughulika na taarifa za upokeaji, uhifadhi na usambazaji wa dawa na vifaa tiba imewekwa hapo. Kwa upande wa Pemba Bohari Kuu ya Dawa ipo Vitongoji ambapo Bohari hiyo hutumika kusambaza dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya na hospitali zote za Pemba.

Ukaguzi umebaini Bohari ya Dawa iliyopo Vitongoji - Pemba haipati huduma nzuri ya matumizi ya mfumo wa mSupply kutoka Maruhubi Unguja. Hali hii

imetokana na kukosekana kwa miundombinu imara ya mawasiliano ya mtandao baina ya Bohari Kuu ya Dawa Unguja na Bohari ya Pemba (VPN Connection).

Aidha ukaguzi umebaini kuwepo kwa upungufu wa taaluma katika matumizi ya mifumo hiyo kwa wafanyakazi wa Bohari ya dawa Pemba.

Kutopatikana kwa huduma bora ya mawasiliano ya mtandao pamoja na kukosekana kwa taaluma ya matumizi ya mfumo ya dawa kunaweza kupelekea kutokea kwa ucheleweshwaji wa upatikanaji wa dawa zinazohitajika katika vituo vya afya na Hospitali zilizopo Pemba.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa kupitia Wizara ya Afya kuimarisha miundombinu ya mawasiliano ya Mtandao baina ya Ofisi zake mbili za Unguja na Pemba pamoja na kuongeza taaluma ya matumizi ya mfumo kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi wanaotumia mifumo ya dawa na vifaa tiba ili kuweza kutumika ipasavyo katika Bohari zote mbili za dawa.

**Majibu ya uongozi wa Bohari Kuu**

Tatizo hili tayari limesharekebishwa, Wizara ya Afya imenunua kifaa cha SOPHOS ambacho kimewezesha mfumo kutumika katika Bohari ya Unguja na Pemba.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati haijaridhishwa na majibu ya Wizara kutokana na ukweli kua SOPHOS ni software ambayo inatumika kuepusha kifaa kuvamiwa na virusi (Anti-virus) na sio kifaa ambacho kitasaidia kutatua changamoto ya mawasiliano baina ya Ofisi ya Bohari Kuu ya Dawa Unguja na Pemba. Aidha, Idara iliieleza Kamati kua tayari Idara ya Bohari Kuu ya Dawa imeshajiunga na mkonga wa Taifa ikiwa ni njia ya kuanza kutatua changamoto hii ya mawasiliano.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaishauri Idara kuhakikisha ushauri wa Mkaguzi unafanyiwa kazi ili kutatua suala la kutokuwepo mawasiliano mazuri baina ya sehemu izo mbili za Unguja na Pemba Pamoja na kuwapa mafunzo watendaji wa Idara kwa upande wa Pemba.

**Hoja nambari 2.4.1.8: Kutotumika Ipasavyo kwa Mfumo wa mSupply ndani ya Bohari Kuu ya Dawa "Under Utilization of mSupply System"**

Ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa mSupply umegawika katika moduli tofauti *"modules and sub modules"* **Kiambatisho Nambari 4 kinahusika** ambapo baadhi yake ni kama ifuatavyo:-

*Customer, Supplier, Item, Reports, Special, Admin, Issuing goods, Incoming Goods, Purchase Orders, Tender Management, Safety Measures, Dispensing, na Patient Medical Records n.k.*

Baada ya kufanyika ukaguzi wa matumizi ya moduli hizo, ukaguzi umebaini kwamba Bohari Kuu ya Dawa inatumia moduli kidogo ukilinganisha na uhalisia wa moduli zilizomo katika mfumo huo licha ya kwamba Bohari imelipia matumizi ya moduli zote.

Kufanya hivyo kunasababisha Bohari Kuu ya Dawa kuingia hasara kutokana na kulipa gharama kubwa ya fedha kwa ajili ya matumizi ya mfumo kinyume na mahitaji.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kupitia Bohari Kuu ya Dawa na kufanya malipo kulingana na mahitaji ya moduli zinazohitajika ili kuepusha kuingiza hasara Serikali kwa kufanya malipo yasiyohitajika jambo ambalo lingelipelekea kuokoa gharama kubwa ya fedha za umma.

**Majibu ya uongozi wa Bohari Kuu**

Kwanza Bohari kuu ya Dawa imeondoa malipo ya mfumo wa MoneyWork ambao ulikuwa unalipiwa bila ya matumizi. Vile vile, mfumo wa mSupply umegawanywa kwenye module, gharama za malipo ya leseni yaliendana na module zinazotumika ambapo malipo hayo hulipwa mara moja. Kinacholipwa kila mwaka ni "Maintance Cost and Updating of Version", Mainatance and updating ya Server ya mfumo huo.

Kwa vitu nyengine kama "Dispensing, na Patient Medical Records, nk". Bohari Kuu haitumi huduma hizi. Endapo Bohari itahitaji huduma za ziada, makubaliano ya gharama nyengine yatafanyika. Mkataba unapatikana kwa kuthibitisha

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini wakati wa ukaguzi kweli Bohari Kuu ya Dawa ilikua ikulipia "full package" ya moduli zinazotolewa na mfumo wa mSupply licha ya kua Bohari inatumia moduli chache. Hii inapelekea kupotea kwa fedha za Serikali ambazo zingeweza kutumika katika masuala mengine tofauti muhimu.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Bohari kuhakikisha wanalipia huduma ambazo wanazitumia ili thamani halisi ya fedha ipatikane (Value for money).

**Hoja nambari 2.4.1.9: Kufanyika kwa manunuzi ya dawa na vifaa tiba nje ya Mfumo**

Ukaguzi umebaini kwamba miongoni mwa wasambazaji wengi wanaouza dawa na vifaa tiba kwa Serikali kupitia Bohari Kuu wanatumia mifumo kwa ajili ya kuuza dawa na vifaa tiba, lakini msambazaji pekee anaejulikana kwa jina la Medical Store Department (MSD) ndiye ambae aliyemuunganisha Bohari Kuu ya Dawa kupitia mfumo wake uitwao ILS ambapo Bohari Kuu hufanya maombi ya dawa na vifaa tiba moja kwa moja kupitia kwenye mfumo huo hali inayopelekea taarifa za maombi ya madawa, taarifa za upokeaji, taarifa za madeni ya dawa na kumbukumbu za malipo yanayofanyika hutunzwa vizuri, kwa usahihi na kupatikana kwa wakati kupitia kwenye mfumo huo wa ILS uliopo kwa msambazaji MSD.

Aidha ukaguzi umebaini sehemu kubwa ya dawa na vifaa tiba vinavyonunuliwa na Bohari Kuu ya Dawa zinatoka kwa wasambazaji binafsi ambapo taratibu za manunuzi hufanyika kwa njia ya kawaida “manually” nje ya mfumo licha ya kuwa wasambazaji hao wanatumia mifumo ya manunuzi na usambazaji wa dawa na vifaa tiba.

Hali hii inapelekea upotevu mkubwa wa kumbukumbu za dawa zinazoagizwa na kupokelewa, zinazolipwa pamoja na kukosekana kumbu kumbu za madeni halisi yanayodaiwa na yaliyobaki.

Kwa upande wa Bohari Kuu ya Dawa ukaguzi umebaini mifumo ya Bohari ina uwezo mkubwa wa kufanya taratibu zote za manunuzi ya dawa na vifaa tiba kutoka kwa wasambazaji kuanzia hatua ya awali ya kutangaza na kusimamia zabuni, kuchagua wasambazaji wenye vigezo, kufanya manunuzi ya dawa kwa msambazaji alieshinda Zabuni hadi kukamilika kwa malipo ya dawa na vifaa tiba, lakini Bohari Kuu ya Dawa hutumia taratibu hizo kwa njia ya kawaida “manually” nje ya mfumo.

Kufanyika kwa utaratibu wa manunuzi ya dawa na vifaa tiba bila ya kutumia mfumo kunapelekea kupotea au kuchanganyika kwa kumbukumbu za taarifa za dawa na vifaa tiba zilizoagizwa, zilizoletwa na zilizobakia na hatimae kusababisha kupokea idadi pungufu ya dawa.

Aidha kutokutumia mfumo ipasavyo kunapelekea kujitokeza kwa upotevu mkubwa wa dawa na vifaa tiba na hatimae kuingiza hasara Serikali kutokana na kununua bidhaa za madawa pasipo na mahitaji (duplicates), ukizingatia kwamba wasambazaji hawana kawaida ya kuwasilisha mahitaji kamili kwa mujibu wa mikataba yao.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kupitia Bohari Kuu ya Dawa kufanya utaratibu wa manunuzi ya dawa na vifaa tiba kupitia mifumo yake ili kuweza kudhibiti taarifa za manunuzi, mapokezi na usambazaji wa dawa na

vifaa tiba na kuweza kuongeza ufanisi na weledi katika utaratibu wa manunuzi ya dawa na vifaa tiba.

Orodha ya Wasambazaji wa dawa na vifaa tiba “Medical Suppliers” waliobainika na ukaguzi kufanya manunuzi ya dawa na vifaa tiba kwa Bohari Kuu ya Dawa bila ya kutumia mfumo ni kama inavyoonekena katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 1: Wasambazaji ambao hufanya manunuzi na Bohari Kuu ya Dawa bila ya kutumia Mfumo**

| Namba | Jina la Msambazaji Dawa/Vifaa Tiba | Huduma anayoitoa |
|---|---|---|
| **WASAMBAZAJI WALIOPO NCHINI (LOCAL SUPPLIERS)** | | |
| 1 | Salama Pharmaceuticals | Dawa na Vifaa Tiba |
| 2 | KAT Med Group (T) LTD | Vitendanishi “Reagents” za Maabara na Huduma za za Damu Salama |
| 3 | KAS Medics | Vitendanishi “Reagents” za Maabara |
| 4 | Abbott Diagnosis | Vitendanishi “Reagents” za Mashine ya PCR (UVIKO - 19) |
| 5 | Nebula Health Care LTD | Vifaa vya Mfupa na Vipimo vya UVIKO - 19 |
| 6 | LAB Equip LTD | Vifaa Tiba |
| 7 | Bahari Pharmacy | Mikoba ya Vifaa vya Uzazi |
| 8 | Indepth Scientific | Vitendanishi “Reagents” za Maabara |
| 9 | Anudha LTD | Vitendanishi “Reagents” za Maabara |
| 10 | M&D Chemicals | Consumables za Maabara |
| 11 | IDA Foundation – Nertherland | Dawa Muhimu |
| 12 | DAWA Arus | Dawa na vifaa tiba |
| 13 | Life Care | Dawa na vifaa tiba |
| **WASHIRIKA WA MAENDELEO (DONORS)** | | |
| 14 | UNICEF | Virutubisho vya Watoto na Vifaa vya Kipindupindu |
| 15 | Global Fund | Dawa za Mradi wa UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria |
| 16 | WHO | Vifaa vya UVIKO – 19 |
| 17 | UNFPA | Dawa na Vifaa vya Uzazi |
| 18 | GLOBAL LIFE SHARING – SOUL, KOREA | Dawa na Vifaa Tiba |
| 19 | CHINA GOVERNMENT | Dawa za Kichina |
| 20 | USAID | Vifaa vya UVIKO – 19 |
| 21 | HILL LIFECARE – INDIA | Dawa Muhimu |
| 22 | UNDP | Vifaa Tiba |
| 23 | ENGEDER HEALTH | Vifaa Tiba |
| 24 | SD BIOSENSOR - KOREA | Test kit za Kupima UVIKO – 19 |

**Majibu ya uongozi wa Bohari Kuu**

Wizara ya Afya ina makubaliano ya kimkataba na MSD na hivyo mfumo na Bohari umeunganishwa na mfumo wa MSD unaowezesha kufanya manunuzi moja kwa moja kupitia mfumo.

Kwasasa Bohari Kuu haina mamlaka ya ununuzi wa dawa, hivyo basi Sheria ya kuipa hadhi ya Wakala ikipitishwa Bohari itaanza kuunganisha mfumo wake wa manunuzi na mifumo ya wasambazaji.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kua Idara inakosa wataalamu (Developers) wa kuweza kuunganisha mifumo ya wasambazaji wa dawa na mfumo wao unaotumika Idarani. Kamati ilitegemea kukuta kua Bohari Kuu ya Dawa inafanya manunuzi ya dawa na vifaa tiba kupitia mifumo ya wasambazaji ili kupata usahihi wa taarifa mbali mbali zinazohusiana na dawa na vifaa tiba. Aidha Kamati imebaini kua Idara ingeweza kukodi utaalamu wa nje na kuja kufanya kazi ile ya kuiunganisha mifumo ya Idara pamoja na ya wasambazaji wa dawa na vifaa tiba.

**Hoja nambari 2.4.1.10: Kutofanya kazi ipasavyo kwa Moduli ya Ripoti katika Mfumo wa mSupply**

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa mSupply una moduli mbali mbali ikiwemo moduli ya Ripoti ambayo hutumika kwa ajili ya kutoa ripoti za dawa na Vifaa tiba Bohari Kuu ya Dawa, aidha imebainika moduli hiyo haitoi taarifa sahihi za dawa zilizoisha muda au zinazotarajiwa kuisha muda wa matumizi kwa binadamu (expiries).

Hali hii inapelekea kuharibika kwa dawa nyingi kutokana na kubakia katika ghala kwa kutopata taarifa sahihi za dawa zinazoisha muda.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa kupitia Wizara ya Afya kuchukuwa jitihada za makusudi katika kutatua dosari hizo ili kuweza kupatikana ripoti zitakazoonesha taarifa sahihi za dawa zinazokaribia kuisha au zilizoisha muda wa matumizi kwa binadamu jambo ambalo litapelekea kuinusuru Serikali kuingia gharama kubwa za manunuzi ya dawa kutokana na kutokupatikana kwa taarifa sahihi na kwa wakati kwa dawa zinazokaribia kuisha muda wa matumizi.

**Majibu ya Bohari Kuu ya Dawa**

Version ya 7.05 mSupply imepunguza changamoto nyingi za mfumo, ikiwemo kutoa ripoti tofauti kulingana na mahitaji kama taarifa ya Dawa, kiwango kilichopo cha dawa na muda wa kumalizia kutumika (expiry)

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na hatua zilizochukuliwa kuhakikisha mfumo unakua hai muda wote (updated) ili changamoto kama hizi zinazotokana na mfumo kua "outdated" kuondoka. Aidha, Kamati inaitaka Idara kuhakikisha mfumo huo unakua "updated" kila ambapo kutakua na toleo jipya "version" ya mfumo.

**Hoja nambari 2.4.1.11: Dosari zilizobainika baina ya Kitengo cha Ununuzi na Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba**

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali za kiutendaji baina ya kitengo cha Manunuzi cha Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto na Bohari Kuu ya Dawa. Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo: -

- Kutoshiriki kikamilifu kwa Kitengo cha Ununuzi (PMU) kwenye mchakato wa upokeaji wa dawa na vifaa tiba wakati zinapowasilishwa Bohari Kuu kutoka kwa Wasambazaji ikiwa kitengo hicho ni wahusika wakuu wa uagizaji dawa na ndio wenye taarifa sahihi za dawa zilizoagizwa.
- Kukosekana kwa miongozo na sera imara zilizoandikwa (Documented Standard Operating Procedures) zitakazotumika baina ya Bohari na Kitengo cha Manunuzi/ Wizara ya Afya kuanzia hatua ya mchakato wa manunuzi ya dawa na vifaa tiba, upokeaji wa dawa hadi kukamilika kwa uhifadhi na usambazaji wa dawa na vifaa tiba.
- Kuwepo kwa dosari katika mgawanyo wa majukumu na mgawanyo wa kazi kwa wafanyakazi wa vitengo mbali mbali ndani ya Bohari Kuu ya Dawa.

**Majibu ya Bohari Kuu ya Dawa**

Uongozi wa Bohari umetayarisha miongozo ya kazi (SOP), moja katika miongozo hiyo ni "Muungozo wa Upokeaji wa dawa." Kuna timu inayojumuisha Afisa Mapokezi, Msambazaji wa Dawa, Afisa Manunuzi na mtumiaji (kwa bidhaa maalumu).

Hata hivyo, Wizara iko kwenye mchakato wa kuifanya Bohari kuwa Wakala ili shughuli zote za dawa zikiwemo ununuzi zitafanywa na Bohari.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya juhudi za Wizara katika kutaka kuifanya Bohari kua Wakala ili ifanye shughuli zake ikiwemo ununuzi wa dawa na vifaa tiba, Kamati imebaini kua bado kuna changamoto ya watu wa kitengo cha manunuzi cha Wizara ya Afya kutoshirikin kikamilivu wakati wa kupokea dawa ambapo kitengo hicho cha manunuzi ndo kinachojua idadi halisi ya dawa na vifaa tiba zilizonunuliwa na kutokuwepo kwa watu wa kitengo hichi kunaweza kupelekea Bohari Kuu ya Dawa kupokea dawa na vifaa tiba pungufu kutoka kwa msambazaji jambo ambalo linapelekea kupotea kwa mali ya Serikali na upotevu wa fedha za walipa kodi kiujumla.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara ya Afya kuhakikisha watendaji wa kitengo cha manunuzi (PMU) wanashiriki kikamilifu katika upokeaji wa dawa na vifaa tiba kutoka kwa wasambazaji ili idadi kamili ya dawa na vifaa tiba vilivonunuliwa vipatikane vikiwa ni idadi sahihi na katika ubora unaotakiwa, katika kipindi hichi ambapo Bohari Kuu ya Dawa bado haijapewa Uwakala.

**Hoja nambari 2.4.1.12: Dosari katika Usambazaji wa dawa na vifaa tiba kutoka kwa Kampuni binafsi.**

Ukaguzi umebaini kujitokeza kwa dosari mbali mbali kutoka kwa kampuni binafsi za kusambaza dawa na vifaa tiba, baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo: -

- Kutokuwekwa alama za utambulisho “Code/Nembo” kwa dawa na vifaa tiba vinavyosambazwa na kampuni binafsi. Hali hii inapelekea kutojulikana kwa idadi kamili ya dawa na vifaa tiba vinavyosambazwa na kampuni binafsi jambo ambalo ni tofauti na MSD ambae bidhaa zake za dawa na vifaa tiba zimewekwa alama za utambulisho.

Kutokuwepo kwa alama za utambulisho wa dawa zinazoagizwa na kununuliwa kunaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu mkubwa wa dawa na vifaa tiba zilizonunuliwa na Serikali kuweza kutumika katika maduka binafsi.

- Kujitokeza kwa uwepo wa ankara zenye tarehe tofauti zinazothibitisha kufanyika kwa malipo ya shilingi 976,275,934 kwa kampuni binafsi mbali mbali za usambazaji wa dawa na vifaa tiba ambazo ankara hizo zimerikodiwa nambari ya aina moja ya kumbukumbu ya uthibitisho wa upokezi wa dawa na vifaa tiba zilizopo Bohari Kuu ya dawa jambo ambalo limetia shaka juu ya uwepo wa uhalali wa bidhaa na fedha zilizolipwa. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo: -

**Jadweli Nambari 2: Ankara zenye namba za utambulisho uliofanana**

| Namba | Nambari ya hati ya Uagizishaji | Tarehe ya Ankara | Nambari ya Ankara | Thamani (Tshs) | Tarehe ya kupokea Bohari | SMZ Ref No. |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 4119050 | 15/08/2019 | 4128128 | 5,540,955 | 19/08/2019 | SMZ/RV 01/19/20 |
| 2 | 4131278 | 3/7/2020 | 4140149 | 115,290,000 | 4/7/2020 | SMZ/RV 01/19/20 |
| 3 | 4119143 | 17/08/2019 | 4128220 | 5,200,000 | 9/8/2019 | SMZ/RV 19/19/20 |
| 4 | 4122109 | 5/11/2019 | 4131149 | 244,285,789 | 7/11/2019 | SMZ/RV 19/19/20 |
| 5 | 4122210 | 7/11/2019 | 4131249 | 131,518,816 | 9/11/2019 | SMZ/RV 22/19/20 |
| 6 | 4122539 | 14/11/2019 | 4131576 | 11,929,434 | 16/11/2019 | SMZ/RV 22/19/20 |
| 7 | 4109261 | 9/11/2018 | 4118439 | 8,879,418 | 14/11/2018 | SMZ/RV 23/18/19 |
| 8 | 4108957 | 2/11/2018 | 4118143 | 71,826,563 | 3/11/2018 | SMZ/RV 23/18/19 |
| 9 | 4122323 | 11/11/2019 | 4131360 | 3,450,000 | 11/11/2019 | SMZ/RV 23/19/20 |
| 10 | 4122536 | 14/11/2019 | 4131571 | 68,187,762 | 16/11/2019 | SMZ/RV 23/19/20 |
| 11 | 4113074 | 28/02/2019 | 4122212 | 30,049,698 | 2/3/2019 | SMZ/RV 42/18/19 |
| 12 | 4113234 | 6/3/2019 | 4122372 | 19,785,000 | 7/3/2019 | SMZ/RV 42/18/19 |
| 13 | 4114091 | 27/03/2019 | 4123210 | 103,840 | 30/03/2019 | SMZ/RV 48/18/19 |
| 14 | 4114434 | 5/4/2019 | 4123551 | 79,279,200 | 8/4/2019 | SMZ/RV 48/18/19 |
| 15 | 4125616 | 31/01/2020 | 4134601 | 64,667,450 | 1/2/2020 | SMZ/RV 48/19/20 |
| 16 | 4125618 | 31/01/2020 | 4134603 | 30,621,770 | 6/2/2020 | SMZ/RV 48/19/20 |
| 17 | 4125551 | 30/01/2020 | 4134538 | 1,380,000 | 30/01/2020 | SMZ/RV 52/19/20 |
| 18 | 4126755 | 27/02/2020 | 4135721 | 201,691 | 28/02/2020 | SMZ/RV 52/19/20 |
| 19 | 4127661 | 18/03/2020 | 4136611 | 43,600,000 | 19/03/2020 | SMZ/RV 59/19/20 |
| 20 | 4127785 | 20/03/2020 | 4136727 | 40,478,548 | 24/03/2020 | SMZ/RV |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | 59/19/20 |
| **Jumla** | | | | **976,275,934** | | |

**Majibu ya uongozi wa Bohari Kuu**

Kuweka nembo inawezekana ikiwa Wizara itanunua dawa kutoka kiwandani kama vile ilivyo kwa MSD. Bohari inakusudia kuweka Nembo yake pale itapokuwa Wakala na hivyo kununua dawa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji dawa.

Kweli hilo tatizo limeonekana la kuwa na ankara za wazabunbi tofauti kuwa na nambari ya mapokezi inayofanana. Ila hili halina mahusiano na taratibu za malipo kwavile malipo hufajika kwa uthibitisho unaotokana na nambari za ankara halisi kutoka kwa mzabuni. Hoja hii itatatuliwa kwa kutumia register maalumu ya mapokezi ambayo litafuata mtiririko wa nambari maalumu kwa kila msambazaji.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na hoja hii ya CAG ambapo kufanana kwa namba ya ankara mbil tofauti zenye malipo ya aina mbili tofauti ni ukiukwaji wa taratibu za kifedha. Aidha, kutowekwa kwa nembo kwa wasambazaji binafsi tofauti na MSD kunapelekea kupatikana kwa mianya ambayo inaweza kutumiwa na watu wasiokua waaminifu kwa Serikali ambapo Dawa hizo zinaweza zikatolewa na kuuzwa katika maduka ya watu binafsi. Hii inaweza kupelekea kupotea kwa Dawa na kupunguza ufanisi wa huduma kwa wananchi.

**Hoja nambari 2.4.1.13 Uwepo wa Ankara za madeni ambazo hazikuthibitishwa na wasambazaji wa dawa na vifaa tiba.**

Katika ukaguzi wa madeni imebainika uwepo wa ankara za madeni yenye thamani ya shilingi 1,284,795,591.11 pamoja na USD 750,144.69 kutoka Bohari Kuu ya Dawa ambazo taarifa zake hazikuonekana katika orodha ya ankara zilizowasilishwa na wasambazaji wa dawa na vifaa tiba katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi. Aidha ankara hizo hazikuweza kubainika katika kumbukumbu za hati za malipo.

**Jadweli Nambari 3: Ankara za madeni ambazo taarifa zake hazikuthibitishwa na wasambazaji**

| Nam. | Tarehe | Namba ya ankara | Hati ya mapokezi | Kumbukumbu Namba ya Mapokezi Bohari | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | **HARSH** | | |
| **1.** | **22**/10/2018 | INV/2018/590 | DEL/2018/907 | SMZ/RV07/18/19 | 59,385,000 |
| **2.** | 10/04/2018 | INV/2018/552 | DEL/2018/849 | SMZ/RV06/18/19 | 39,590,000 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Jumla Ndogo | | | | | 98,975,000 |
| **LIFE CARE** | | | | | |
| **3.** | 14/7/2021 | 154 | - | **-** | 3,645,000 |
| **4.** | 23/7/2021 | 156 | - | SMZ/RV03/21/22 | 1,685,000 |
| Jumla Ndogo | | | | | 5,330,000 |
| **SALAMA PHARMACEUTICAL LTD** | | | | | |
| **5.** | 06/03/2019 | 4122378 | - | SMZ/RV42/18/19 | 19,785,000 |
| **KAT Med** | | | | | |
| **6.** | 22/09/2021 | 0242 | 0265 | SMZ/RV28/21/22 | 1,584,000 |
| **7.** | 03/09/2021 | 0240 | 0263 | SMZ/RV26/21/22 | 8,560,500 |
| **8.** | 06/09/2021 | 0241 | 0264 | SMZ/RV25/21/22 | 1,600,000 |
| Jumla Ndogo | | | | | 11,744,500 |
| **ABBOTT** | | | | | |
| **9.** | 25/2/2021 | 13-03459317 | - | SMZ/RV01/20/21 | USD 743,664.69 |
| **10.** | 25/2/2021 | 13-03469585 | - | SMZ/RV02/20/21 | USD 6,480 |
| Jumla ndogo | | | | | **USD 750,144.69** |
| **INDEPTH SCIENTIFIC** | | | | | |
| **11.** | 20/7/2018 | 12 | - | - | 5,200,000 |
| **12.** | 11/1/2019 | 87 | - | - | 2,954,318 |
| **13.** | 11/01/2019 | 88 | - | - | 13,274,353 |
| **14.** | 16/12/2019 | 99 | - | - | 25,199,353 |
| **15.** | 17/2/2020 | 100 | - | - | 5,400,000 |
| **16.** | 16/12/2019 | 90 | - | - | 8,000,000 |
| **17.** | 17/6/2020 | 1 | - | SMZ/RV06/19/20 | 9,215,000 |
| Jumla ndogo | | | | | **69,243,024** |
| **LAB EQUIP** | | | | | |
| **18.** | 24/6/2020 | 7668 | 18411 | SMZ/ RV01/2020/21 | 59,000,000 |
| **19.** | 05/07/2021 | 8218 | 24483 | SMZ/ RV13/2021/22 | 1,955,200 |
| **20.** | 26/8/2020 | 6992 | 18337 | SMZ/RV04/20/21 | 86,222,000 |
| **21.** | 09/01/2020 | 7002 | 18347 | SMZ/RV05/20/21 | 8,778,000 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **22.** | 07/03/2020 | 6855 | 18444 | SMZ/RV02/2021 | 38,000,000 |
| **23.** | 29/3/2021 | 7850 | 12499 | SMZ/RV10/2021 | 19,781,500 |
| **24.** | 24/6/2021 | 8308 | 24624 | SMZ/RV12/21/22 | 882,000 |
| Jumla ndogo | | | | | **214,618,700** |
| **NEBULLA** | | | | | |
| **25.** | 15/1/2021 | NEB/INV.407 | - | - | 256,000,000 |
| **26.** | 22/6/2021 | NEB/INV.0114 | - | - | 647,500 |
| Jumla ndogo | | | | | **256,647,500** |
| **MEDICAL STORE DEPATMENT** | | | | | |
| **27.** | 28/8/2019 | 6497935 | - | - | 122,059,095.6 |
| **28.** | 31/10/2019 | 6510176 | - | - | 90,148,000 |
| **29.** | 16/10/2019 | 6505239 | - | - | 6,767,020 |
| **30.** | 29/11/2019 | 6520876 | - | - | 2,546,000 |
| **31.** | 19/9/2018 | 623778 | - | - | 144,000,000 |
| **32.** | 11/03/2018 | 6347141 | - | - | 2,588,352 |
| **33.** | 10/10/2018 | 630642 | - | - | 2,113,800 |
| **34.** | 24/10/2018 | 636043 | - | - | 25,989,600 |
| **35.** | 09/11/2019 | 6494186 | - | - | 32,861,904 |
| **36.** | 31/7/2019 | 6477160 | - | - | 3,998,862.40 |
| **37.** | 18/3/2020 | 6558922 | - | - | 44,509,400 |
| **38.** | 18/2/2020 | 65546243 | - | - | 7,354,000 |
| **39.** | 17/9/2021 | 289915 | - | - | 56,615,842.14 |
| **40.** | 16/9/2021 | 2889116 | - | - | 86,684,990.97 |
| **Jumla ndogo** | | | | | **628,236,867.11** |
| Jumla kuu (Tshs) | | | | | **1,284,795,591.11** |
| Jumla kuu (USD) | | | | | **USD 750,144.69** |

**Majibu ya uongozi wa Bohari Kuu**

**HARSH**

INV/2018/590 with 59,385,000; pamoja INV/2018/552 with 39,590,000 imeshathibitishwa.

**LIFE CARE**

Ankara 0154 ina 3,645,000 na ankara 0156 ina 1,685,000 hakuna ankara halisi (original) hivyo haijawezekana kudhibitishwa. Manunuzi ya LPO.

**SALAMA PHARMACEUTICAL LTD**

4122378 Ankara ina 19,785,000 imeshathibitishwa.

**KAT Med**

Ankara 0242 na 1,584,000, ankara 0240 na 8,560,000, ankara 0241 na 1,600,000 imeshathibitishwa**.**

**ABBOTT**

Ankara 13-03459317 na USD 743,664.69, ankara 13-03469585 na USD 6,480

**INDEPTH SCIENTIFIC**

Ankara 12 ina 5,200,000, anakara 87 ina 2,954,318, ankara 88 ina 13,274,353, ankara 99 ina 25,199,353, ankara 100 ina 5,400,000, ankara 90 ina 8,000,000 zimethibitishwa

**LAB EQUIP**

i. Ankara 7668 ina 59,000,000 imethibitishwa.
ii. Ankara 6992 ina 86,222,000 na Ankara 6992 ina 8,778,000 imethibitishwa.
iii. Ankara 6855 ina 38,000,000 imethibitishwa.
iv. Ankara 7850 ina 19,781,500 imethibitishwa.
v. Ankara 8218 ina 1,955,200 haijathibitishwa, ankara halisi zipo Bohari.
vi. Ankara 8308 ina 882,000 haijathibitishwa, ankara halisi hazipo Bohari, LPO.

**NEBULLA**

Ankara NEB/INV.407 ina 256,000,000, ankara NEB/INV.0114 ina 647,500 imeshathibitishwa.

**MEDICAL STORE DEPATMENT**

i. Ankara 6497935 ina 122,059,095.6, ankara 6510176 ina 90,148,000 zimethibitishwa.
ii. Ankara 6505239 ina 6,767,020 haijapokelewa.
iii. Ankara 6477160 ina 3,998,862.40 Haijapokelewa.
iv. Ankara 6558922 ina 44,509,400 imethibitishwa.
v. Ankara 289915 ina 56,615,842.14 na 2889116 ina 86,684,990.97 zimethibitishwa.
vi. Ankara 623778 ina 144,000,000 imethibitishwa.
vii. Ankara hii 636043 imewekwa kwenye ripoti inatakiwa iwe 636047 ina 25,989,600 ishathibitishwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Wizara kuchukua juhudi za kuzithibitisha ankara ambazo wakati wa ukaguzi hazikuweza kuthibitishwa. Hata hivyo, Kamati ya PAC imepata wasiwasi juu ya uhalali wa ankara hizo hasa ukizingatia Mkaguzi hakuweza kuzithibitisha. Kwa mnasaba huo, Kamati haikuweza kuzithibitisha.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Bohari ihakikishe inaweka ankara zake na kuzihifadhi vizuri mara tu baada ya kufanya malipo ili kuepusha kutopatikana wakati wa ukaguzi.

**Hoja nambari 2.4.1.14: Kutokuwepo kwa usalama na udhibiti mzuri wa taarifa zilizomo ndani ya mifumo ya Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba**

Ukaguzi umebaini kwamba Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba ipo katika hatari ya kupoteza taarifa zake za dawa na vifaa tiba zinazohifadhiwa ndani ya mifumo yake kutokana na kutotumia njia salama za udhibiti wa taarifa zilizomo ndani ya mifumo hiyo. Hali hii imesababishwa kutokana na kujitokeza kwa mambo yafuatayo: -

- Kutofanyika ipasavyo kwa mchakato wa uwekaji wa nakala za taarifa zilizomo ndani ya mfumo (Daily backup process is not conducted).

- Endapo Janga lolote likitokea katika Taasisi ya Bohari, hakuna mpango imara wa kuokoa taarifa zilizomo ndani ya mifumo yake na kuendeleza utoaji wa huduma zake (No Business Continuity Plan and Disaster Recovery Plan).
- Mifumo ya Bohari kuwa nje ya muda "Systems Out of Date".
- Kutoingizwa programu za kuweka usalama "Antivirus" ndani ya kompyuta za mifumo "Servers".

Ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kupitia uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba kuwajengea uwezo wasimamizi wa mifumo hiyo ikiwemo kuwapatia mafunzo ya udhibiti na usalama wa mifumo ya Bohari ili kuweza kusimamia vizuri na kuimarisha usalama wa taarifa zilizomo.

**Majibu ya Bohari Kuu ya Dawa**

Baada ya kufanya update ya version 7.05 Mfumo unapeleka "backup data" wenyewe kwenye Dropbox kila siku, vile vile Bohari inafanya "Backup" kila siku kwa kutumia njia ya External Hardisk.

Wizara inaandaa kuweka recovery site Pemba, Anti virus kwenye server, kweli haipo na Uongozi wa Bohari unachukua mapendekezo na kuyafanyia kazi na Wizara inachukua ushauri na kuufanyia kazi wa kuwaengezea uwezo wasimamizi wa mifumo ndani ya Bohari.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na majibu ya Bohari kuu ya Dawa. Aidha, Kamati imesikitishwa na uhalisia kua tangu ukaguzi kufanyika Mwaka 2021, "Servers" zinazotumika kuhifadhi taarifa za mifumo inayotumiwa na Bohari Kuu ya Dawa mpaka sasa bado hazijawekwa "antivirus", hali ambayo inaweza kupelekea uvamizi wa mfumo huo kwa wepesi na kupoteza taarifa muhimu za Serikali.

**Hoja nambari 2.4.1.15: Dosari zilizobainika katika Mifumo ya Dawa na Vifaa Tiba inayotumika katika Vituo vya Afya na Hospitali za Unguja na Pemba**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa vituo mbali mbali vya Afya na Hospitali za Wilaya na Mkoa kwa upande wa Unguja na Pemba ambapo ukaguzi huo ulijumuisha ukaguzi wa mifumo ya dawa na vifaa tiba inayotumika katika vituo na hospitali hizo na kukagua sehemu mbali mbali zinazohifadhiwa dawa na vifaa tiba (Stores) kwa lengo la kuangalia udhibiti na usalama wa huduma

za dawa na vifaa tiba katika vituo hivyo. Vituo vya afya na Hospitali zilizopitiwa ni kama zinavyoonekana katika jadweli lifuatalo: -

**Jadweli Nambari 4: Mifumo inayotumika katika Vituo vya Afya na Hospitali zilizofanyiwa Ukaguzi.**

| Namba | Jina la Kituo/Hospitali | Mfumo inayotumika |
|---|---|---|
| **UNGUJA** | | |
| 1. | Hospitali ya Mnazi Mmoja | • eLMIS – CE<br>• eHMS |
| 2. | Hospitali ya Wilaya ya Makunduchi | • eLMIS – FE<br>• eLMIS – CE |
| 3. | Hospitali ya Wilaya ya Kivunge | • eLMIS – FE<br>• eLMIS – CE<br>• Aspire – HER |
| 4. | Hospitali ya Mpendae | • eLMIS – FE<br>• eLMIS – CE |
| 5. | Kituo cha Afya Shauri Moyo | • eLMIS – FE<br>• eLMIS – CE |
| 6. | Bohari Kuu ya Dawa na Vifaaa tiba Maruhubi | • mSupply<br>• eLMIS – FE<br>• eLMIS – CE |
| **PEMBA** | | |
| 7. | Hopitali ya Wilaya ya Wete | • eLMIS – FE<br>• eLMIS – CE |
| 8. | Hospitali ya Abdallah Mzee Mkoani | • HMIS<br>• eLMIS - CE |
| 9. | Hospitali ya Wilaya ya Chake Chake | • eLMIS – CE |
| 10. | Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa tiba Vitongoji Pemba | • eLMIS – CE |

Aidha, baada ya kupitia vituo na hospitali hizo ukaguzi umebaini uwepo wa dosari mbali mbali kama zinavyoonekana hapo chini:-

**a) Wafanyakazi kukwepa kutumia Mifumo iliyopo katika uwekaji wa kumbukumbu za usambazaji wa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa.**

Ukaguzi umebaini wafanyakazi wengi waliopo katika vituo vya afya na hospitali wanaohusika na upokeaji dawa kutoka katika stoo za hospitali pamoja na

usambazaji dawa na vifaa tiba kwa wagongwa wanakwepa kutumia mifumo iliyopo katika kuweka kumbukumbu za taarifa hizo.

Aidha taarifa za maombi ya dawa zinazotoka katika vitengo vya dawa (pharmacies) na kupelekwa Stoo kwa ajili ya kuomba dawa hurikodiwa kwa njia ya kawaida "manually" ambapo taarifa nyingi zinakuwa haziko sahihi ukilinganisha na idadi kamili ya dawa na vifaa tiba zilizopo au zilizotolewa. Vile vile baadhi ya hospitali kutokuweka kabisa rikodi za dawa zinazotolewa kwa wagonjwa na kupelekea kutojulikana kwa idadi halisi ya dawa zilizotolewa kwa wagonjwa.

Hali hii imebainika katika vituo vya afya na hospitali tofauti kama vile Hospitali ya Wilaya ya Chake Chake, Hospitali ya Abdallah Mzee wilaya ya Mkoani, Hospitali ya Wilaya ya Wete, Hospitali ya Wilaya ya Makunduchi na Hospitali ya Wilaya ya Kivunge pamoja na vituo vyote vya afya.

Kutotumia mifumo katika vituo vya afya na hospitali kwa ajili ya mchakato wa kuweka kumbukumbu za upokeaji na usambazaji wa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa kunapelekea kutokea kwa upotevu mkubwa wa dawa na vifaa tiba kwa kutopatikana kumbukumbu sahihi za dawa na vifaa tiba zinazotolewa na kusambazwa.

**b) Kukosekana kwa vifaa vya kuongeza usalama "CCTV Cameras" pamoja na "Door Security Machines" katika Vyumba vya kuhifadhia dawa ndani ya Vituo vya Afya na Hospitali.**

Moja kati ya njia bora za kudhibiti na kuongeza usalama wa uhifadhi wa dawa na vifaa tiba ndani ya vituo vya afya na hospitali ni kuweka vifaa maalum vya ulinzi na usalama ambavyo vitasaidia kuonesha kumbukumu za matukio yote yanayofanyika katika vyumba vya kuhifadhia dawa na vifaa tiba pamoja na muda wa matukio. Mfano wa vifaa hivyo ni "CCTV Cameras" pamoja na mashine maalum za milango zinazozidhibiti uingiaji wa watu wasiohusika "Door Security Machines".

Ukaguzi umebaini kwamba hospitali ya Mnazi Mmoja na Hospitali ya Abdallah Mzee ndio vituo pekee vilivyokuwa na kamera katika sehemu za kuhifadhia dawa (store).

Hata hivyo Hospitali ya Abdallah Mzee ina kamera moja tu katika sehemu ya kuhifadhia dawa na vifaa tiba (store) ambayo haitoshi kwa mujibu wa uhalisia wa dawa zinavyowekwa.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuongeza ulinzi kwa kuweka kamera na vifaa vya ulinzi kwenye milango ya sehemu za kuhifadhia dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya vyote pamoja na Hospitali kwa Unguja na Pemba.

**c) Kukosekana kwa Mafunzo Endelevu ya watumiaji wa Mifumo ya Dawa na Vifaa Tiba.**

Ukaguzi umebaini kwamba wafanyakazi wanaotumia mifumo iliyopo katika Vituo vya Afya na Hospitali hawana uwelewa mzuri wa utumiaji wa mifumo hiyo, hali hii imepelekea wafanyakazi hao kupata changamoto kubwa za kiutendaji katika matumizi ya mifumo hiyo ambapo baadhi yao kuona usumbufu na kutotumia kabisa mifumo iliyopo kwa utendaji kazi na kuandika kumbukumbu za matumizi ya dawa katika madaftari (manually).

Aidha wafanyakazi wa vituo vyengine kuamua kutumia programu ya “Microsoft Excel” katika kurikodi taarifa za dawa kutokana na kutoelewa vizuri namna ya kutumia mifumo ya dawa iliyopo.

Hali hii inapelekea kutopatikana kwa ufanisi na tija katika uhifadhi wa dawa na vifaa tiba kwa vituo vya afya na hatimae kupelekea kuongezeka kwa upotevu wa dawa na vifaa tiba kwa kisingizio cha kutokuwa na uelewa wa matumizi ya mifumo.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kutilia mkazo suala la kujenga uwezo kwa watumiaji wa mifumo ya dawa na vifaa tiba waliopo katika hospitali na vituo vya afya ili kuweza kuimarisha ufanisi na kupatikana kwa tija katika uhifadhi wa dawa na vifaa tiba.

**Majibu ya uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa**

a. Wizara inakiri kwamba kuna mapungufu kwa watendaji kutumia mifumo iliyopo ya kutunzia kumbukumbu za usambazaji wa dawa na vifaa tiba. Sababu ya kutokutumia mifumo hiyo ni pamoja na usimamizi mdogo, uelewa mdogo, miundombinu na vifaa kama computers na mtandao.
   - Wizara itaendelea kutoa mafunzo kuwasimamia kwa karibu ili waweze kutumia mifumo
   - Wizara imejipanga kuviunganisha vituo vyote vya afya na mkonga wa Taifa ili kuhakikisha upatikaji wa mtandao
   - Wizara inakua inaongeza idadi ya vifaa kila wakati hali ya fedha inaporuhusu

b. Wizara ya Afya imepokea ushauri wa kuweka kamera za ulinzi CCTV cameras kwenye hospitali zote mpya zilizojengwa kuanzia mwaka 2022, na vifaa hivyo vitaendelea kuwekwa kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu
c. Wizara ya Afya bado inaendelea kutoa mafunzo kwa watendaji kadri ya fedha zinapotikana ili kutoa mafunzo kuanzia ngazi ya Vituo vya Afya na Hospitali. Wizara inajitahidi kutafuta fedha kwa wafadhili ili kuweza kupatiwa mafunzo mara kwa mara kwa watendaji

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati haijaridhishwa na uhalisia uliopo katika udhibiti wa vyumba vya kuhifadhia dawa. Udhibiti huu usioridhisha unaweza kupelekea kupotea kwa dawa ukizingatia dawa nyingi hazina mihuri ya kuthibitisha ni dawa za Serikali.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Bohari Kuu ya Dawa kuhakikisha wanaweka udhibiti wa usalama katika vyumba vinavyohifadhiwa dawa ili kutotoa mianya kwa watu wasiowaaminifu. Halkadhalika, Kamati inaishauri Bohari kuandaa mpango kazi unaoonesha mipango yake kuwafanyia mafunzo wafanyakazi ili waweze kutumia mifumo kwa ufanisi na weledi.

**Hoja nambari 2.4.1.16: Kutofuatwa kwa Taratibu na Miongozo ya Uhifadhi wa Dawa na Vifaa Tiba.**

Kwa mujibu wa Muongozo mpya wa utendaji kazi uliotolewa mwaka 2019 na Wizara ya Afya ambao hadi sasa ndio unaotumika *“ Logistics Systems Standard Operating Procedure Manual ”* unaeleza taratibu zote za utendaji kazi katika vituo vya afya na hospitali ikiwemo miongozo na taratibu mbali mbali zinazopaswa kutumika katika vyumba vya kuhifadhi dawa na vifaa tiba (Stores).

Aidha ukurasa wa 13 wa Muongozo huo umeainisha taratibu 13 zinazotakiwa kufuatwa katika sehemu za kuhifadhia dawa na vifaa tiba (Storage Guidelines).

Hata hivyo ukaguzi umebaini vituo vya afya na hospitali zote kwa Unguja na Pemba hazifuati ipasavyo taratibu 13 za kuhifadhi dawa zilizoainishwa katika Muongozo huo.

Baadhi ya dosari zilizoonekana kujitokeza kutokana na kutokufuatwa kwa miongozo na taratibu za utunzaji dawa na vifaa tiba katika Stoo za hospitali na vituo vya afya ni kama zifuatazo: -

- Kuwepo na hali isiyoridhisha katika mafriji na mafriza ya kuhifadhia dawa ambapo hali hii imebainika katika Hospitali ya Wilaya ya Kivunge. Kiambatisho Nambari 5 kinahusika.
- Kuwepo na joto kali katika Stoo ya kuhifadhia dawa ambapo hali hii imebainika katika Hospitali ya Wilaya ya Chake Chake Pemba na imetokana na ubovu wa muda mrefu wa kiyoyozi kilichopo (Air

Condition) ambapo imepelekea kuharibika kwa baadhi ya dawa kutokana na kukosekana kwa "room temperature" iliyo bora.

- Kukosekana kwa vifaa vya kuzimia moto "Fire Extinguisher" ambapo hali hii imebainika katika hospitali ya Wilaya ya Makunduchi kwa vile hospitali nzima haina "fire extinguisher" hata moja.
- Kuwepo kwa "Fire Extinguisher" ambazo zimeshaisha muda wa kufanya kazi (Expired) ambapo dosari hii imebainika katika vituo vingi vya afya na hospitali.
- Kutotumika kwa utaratibu bora wa kupanga dawa katika makabati ya dawa (Shelves) yaliyomo Stoo katika vituo na hospitali zote ambapo utaratibu bora unaohitajika kufuatwa kwenye muongozo wa kupanga dawa ni (First Expire First Out – FEFO).
- Kuwepo kwa nafasi ndogo za maeneo ya kuhifadhia dawa na vifaa tiba ukilinganisha na ujazo wa shehena halisi za dawa na vifaa tiba inaotakiwa kuhifadhiwa, hali hii imebainika katika vituo na hospitali zote za Unguja na Pemba.

Kutokufuata taratibu na miongozo iliyowekwa kwa ajili ya kuhifadhi dawa kunaweza kupelekea upotevu, uharibikaji (expiries) wa dawa, na vile vile kutokea kwa miripuko ya kemikali za dawa zilizopo.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhamasisha wafanyakazi wanaohusika na utunzaji dawa kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa na Wizara katika uhifadhi wa dawa na vifaa tiba.

Aidha Wizara ya Afya kusambaza nakala za miongozo hiyo (SOP) kwa Vituo na Hospitali zote za Unguja na Pemba ili kuweza kutumika ipasavyo pamoja na kuchukuwa jitihada za makusudi za kuimarisha maeneo ya kuhifadhia dawa na vifaa tiba ikiwemo kuongeza nafasi na kuweka viyoyozi, kudumisha hali ya usafi n.k.

**Majibu ya uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa**

Wizara inakubali uwepo wa dosari zilizoonekana. Hivyo Wizara imetayarisha mpango wa maboresho na kujenga upya vituo ambavyo vimeonekana vina hitilafu kubwa vikiwemo hivi vilivyookana kwenye taarifa ya ukaguzi. Ramani ya majengo mapya na yatakayofanyiwa ukarabati yatakua na sehemu ya kutosha ya kuhifadhi na kugawa dawa na sehemu hizi zitakua kwenye hali joto inayokubalika. Wizara itaendelea na mkakati wa kuisambaza miongozo na kuwafundisha watendaji katika Vituo vya Afya na Hospitali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na hoja hii ya CAG. Aidha, Kamati pia imeridhika na majibu ya Wizara na juhudi zao za kutaka kuitatua hoja hii.

**Hoja nambari 2.4.1.17: Dosari zilizobainika katika Mfumo wa eLMIS - Facility Edition**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya gharama zilizotumika kwa ajili ya utengenezaji na uendeshaji wa Mfumo wa eLMIS Facility Edition ni USD 87,442. Gharama hizo zimepatikana kupitia mkataba wa manunuzi ya mfumo huo uliosainiwa tarehe 09-07-2018 baina ya Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto na Mshauri elekezi Kampuni ya John Snow Inc (JSI) wenye thamani ya USD 57,921 na mkataba wa ziada wa msaada wa kiufundi wa mfumo huo uliosainiwa tarehe 12-11-2020 baina ya wahusika hao ambao una thamani ya USD 29,521. Taarifa kamili za mikataba hiyo zimebainishwa katika Kiambatisho Nambari 2(A) na 2(B).

Aidha mfumo huo ulikuwa na lengo la kuongeza huduma za kusimamia uwekaji wa kumbukumbu za dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya na hospitali ambapo mfumo ungepaswa kuendesha vitengo vyote vinavyohitajika kusambazwa dawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya.

Vitengo vyenyewe ni kama vifuatavyo: -

*Medical Store, Pharmacy, Wards, Theatres, Maternity, Outpatient department, Inpatient department, Laboratory, Dental department, Emergency, CTC/ARV n.k.*

Aidha, ukaguzi ulibaini dosari mbali mbali za kiutendaji katika mfumo huo wa eLMIS Facitiliy Edition ambapo baadhi ya dosari ni kama zifuatazo:-

- Mfumo kukosa uadilifu wa taarifa (Lack of Data Integrity) kutokana na kujibadilisha wenyewe taarifa za kimahesabu za dawa na vifaa tiba (mathematical Errors) ambazo zimeingizwa na watumiaji wa mfumo hasa wakati wa kuomba dawa katika bohari Kuu.
- Kutopatikana kwa huduma ya mfumo kwa baadhi ya hospitali kutokana na matatizo ya mtandao na kutofanya kazi kwa mashine za UPS zilizounganishwa na kompyuta zenye kutumia mifumo ya dawa na vifaa tiba ambazo vifaa hivyo husaidia kuhifadhi umeme wa kompyuta kwa muda endapo umeme mkuu ukikatika.
- Mfumo kutumika katika vitengo viwili tu ambavyo ni kitengo cha Store za Dawa na kitengo cha Pharmacy katika vituo vyote vya afya na

hospitali ambapo kiuhalisia mfumo huo una uwezo wa kutumika katika vitengo vyote kama ilivyoainishwa hapo juu.

- Mfumo kutoweza kutoa ripoti kamili ya orodha ya dawa zinazoisha muda (expiries), hivyo kusababisha changamoto kubwa kutaka kujua orodha ya dawa zinazokaribia kuisha muda (expire) katika Store ya Dawa ili zitumike mapema.
- Kutopatikana kwa msaada wa kiufundi wakati mfumo unapoleta changamoto za kiutendaji.

**Majibu ya uongozi wa Bohari Kuu**

- Mkataba uliokutikana wakati wa ukaguzi ulikua ni wa matumizi ya majaribio (Pilot) katika maeneo mawili ya sehemu ya kutolea Dawa na sehemu ya kuhifadhia Dawa
- Wizara imeandaa mfumo mwingine ambao utatumika kwenye maeneo yote ya kutolea huduma (kusajili wangojwa, kumuona daktari, kufanya vipimo, na kutolea dawa). Wizara imeanza kuutumia mfumo huo tangu mwaka 2022/23 na tayari umanza kutumika kwenye hospitali za Mnazi Mmoja, Kivunge, Makunduchi, Kitogani na Rahaleo kwa Unguja na Abdaala Mzee, Chake chake, Vitongoji, Micheweni na Wete kwa Pemba. Wizara itaendelea matumizi ya mfumo huo kwenye hospital izote za Mkoa, Wilaya pamoja na vituo vya Afya vyote vya ngazi ya msingi kuanzia na mwaka wa fedha 2023/24.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imearifiwa kua mfumo wa eLMIS – FE umeghairishwa na umeundwa mfumo mwengine, hali inayopelekea upotevu wa fedha zisizopungua Dola 87,442. Imeonekana na Kamati kua Bohari haikufanya “feasibility study” ya kutosha ili kujihakikishia ubora wa mfumo huo.

**Hoja nambari 2.4.1.18: Dosari zilizobainika katika Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba kwa Unguja na Pemba**

**a) Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba - Pemba**

Ukaguzi ulitembelea Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba iliyopo Vitongoji Pemba ambapo Bohari hiyo hupokea shehena za dawa na vifaa tiba kutoka katika Bohari Kuu ya Unguja na kuhifadhi katika bohari yake ya Vitongoji, baadae kusambaza dawa na vifaa tiba kwa vituo vya afya na hospitali zote za Pemba kwa mujibu wa maagizo yaliyotolewa na uongozi wa Bohari Kuu ya Unguja. Hata hivyo ukaguzi ulibaini dosari mbali mbali katika Bohari hiyo ya Pemba ambapo baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo: -

- Kutofanya kazi wa mfumo wa CCTV Camera zilizopo ndani ya Bohari kutokana na kutokuwepo kwa msimamizi wa matokeo kwenye CCTV Camera.
- Kutofanya kazi kwa Jenereta ambalo limewekwa kwa ajili ya kurejesha umeme katika Bohari ya Dawa na Vifaa Tiba endapo umeme wa ZECO ukikakatika.

  Kuwepo kwa uhaba wa mashine za kunyanyulia na kupanga mizigo ya dawa na vifaa tiba (Focal Lift) ndani ya Bohari ambapo kwa sasa ipo mashine moja na jumla ya mashine zinazohitajika ni mbili. Aidha mashine ya kunyanyulia shehena ya dawa iliyopo sasa ni kubwa ukilinganisha na nafasi inayotakiwa mashine hiyo kufanya kazi ambapo inapelekea kutokea kwa usumbufu mkubwa wakati wa kugeuka mashine hiyo kwenye njia zake inazotakiwa kupita na vile vile kutoweza kupanga mizigo ya dawa kwa baadhi ya maeneo. Hali halisi ya Bohari Kuu ya Dawa Pemba ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho Nambari 6.

**Majibu ya uongozi wa Bohati Kuu - Pemba**:

Wizara ya Afya ipo kwenye mchakato wa kuajiri Afisa TEHAMA kwa Bohari Kuu ya Dawa, Pemba. Vile vile kwa sasa, uongozi wa Bohari umepanga kumpangia utaratibu Afisa TEHAMA aliyepo Maruhubi Unguja kwenda kikazi kila robo mwaka. Sasa hivi Jenereta linafanya kazi. Forklift iliyoonekana wakati wa ukaguzi ilirudishwa kwa mzabuni na Serikali imenunua forklift mbili mpya zinazokidhi mahitaji.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na juhudi zilizochukuliwa na Bohari Kuu ya Dawa katika kuhakikisha dosari zilizoonekana kwenye hoja hii wakati wa ukaguzi zinatatuliwa na kupatiwa ufumbuzi.

**b) Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba - Unguja**

Kwa upande wa Unguja ukaguzi ulitembelea Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba iliyopo Maruhubi na kubaini dosari mbali mbali ambapo baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kuwepo kwa nafasi ndogo ya kuwekea shehena za dawa na vifaa tiba ndani ya ghala la Maruhubi ambapo hali hii imetokezea kutokana na kubanwa kwa ghala ili kuweza kujengwa Ofisi ya Bohari kupitia nafasi hiyo iliyopo. Kwa upande wa Pemba Ghala ni kubwa na nafasi nzuri kwa

vile Ghala lake limetenganishwa na Ofisi ya Bohari ili kuweka mazingira vizuri.

- Kuwepo kwa nafasi ndogo katika chumba cha kompyuta za mifumo "Server Room" ukilinganisha na vifaa vilivyomo.
- Kutokuwepo na vifaa vya kuzimia moto katika chumba cha Kompyuta za Mifumo "Server Room".
- Kuwepo kwa uhaba wa vifaa vya kuzimia moto katika Ghala la Maruhubi.

Hali halisi ya Bohari Kuu ya Dawa Unguja ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho Nambari 6.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Bohari za Unguja na Pemba kuchukuwa jitihada za makusudi ili kuweza kurekebisha dosari zilizobainishwa.

**Majibu ya uongozi wa Bohari Kuu**

Wizara ya Afya ipo kwenye hatua za kutafuta mshauri elekezi kwa ajili ya ujenzi wa Bohari Kubwa la kisasa lenye uwezo wa kuifadhi mzigo Zaidi ya mara tatu kulinganisha na Bohari iliyopo sasa. Tayari Wizara imeshapata kiwanja huko Dunga Zuze, wilaya ya Kati, Unguja.

Nafasi sasa hivi hakuna, hatahivyo tunataraji "Server Room" itahamia Dunga Zuze kwenye Bohari mpya, Server room haina nafasi, hatahivyo kifaa cha kuzimia moto kimewekwa karibu na mlango wa Server Room, Idara ya Zimamoto na uokozi inaendelea kutoa elimu kwa wafanyakazi wa Bohari kuhusiana na kinga ya majanga ya moto

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati kwa ujumla kwenye hoja hizi kwa upande wa Pemba na Unguja imeridhika na juhudi zilizochukuliwa na Bohari Kuu ya Dawa katika kuhakikisha dosari zilizoonekana kwenye hoja hii wakati wa ukaguzi zinatatuliwa na kupatiwa ufumbuzi.

**Hoja nambari 2.4.1.19**: **Kutofanyika kwa Ukaguzi wa Ndani wa Dawa na Vifaa Tiba katika Hospitali.**

Ukaguzi umebaini kwamba Kamati za Ukaguzi wa Ndani wa dawa na Vifaa Tiba *(Hospital Medicines and Therapeutic Committees)* zilizopo katika Hospitali na vituo vya afya hazifanyi zoezi la ukaguzi wa dawa na Vifaa tiba. Hali hii

imepelekea Hospitali na vituo vingi vya Afya kutokuwa na kumbukumbu nzuri za upokeaji na usambazaji wa dawa.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhamasisha Kamati za Ukaguzi wa ndani wa Dawa na Vifaa Tiba ili kuweza kufanya majukumu yao ipasavyo ikiwemo kufanya ukaguzi wa dawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya.

**Majibu ya uongozi wa Bohari Kuu**

Wizara imepokea ushauri na tayari imeshaanza kuchukuwa hatua tofauti zikiwepo kupitia na kuboresha muongozo wa utendaji kazi wa Kamati ya Dawa na Tiba za Hospitali na Wilaya mwaka 2021. Aidha Wizara imeanzisha Kikosi kazi(IMPACT Team) kwa kila Hospitali na Wilaya ambayo inasidiana na Kamati ya Dawa na Tiba.

**(VIELELEZO; *Muongozo wa Kamati ya Dawa na Tiba, Ripoti za IMPACT Team za Hospitali na Wilaya*)**

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya juhudi za Wizara katika majibu yao, Kamati imebaini kua Kamati hizi za Ukaguzi wa ndani wa dawa na vifaa tiba zina miongozo yake. Changamoto kubwa ipo katika usimamizi wa ukaguzi ambapo inapelekea kutofanyika kikamilifu kaguzi hizo au kutofanyika kabisa.

**Hoja nambari 2.4.1.20: Kukosekana kwa Sera ya TEHAMA (ICT Policy)**

Moja ya Taratibu zilizo bora za kusimamia Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi ni kuwepo na Sera za TEHAMA ambazo zitaeleza utaratibu mzima wa kutumia mifumo na vifaa vya TEHAMA katika Taasisi ili kuweza kuimarisha usalama wa vifaa na taarifa zilizopo.

Ukaguzi umebaini Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba haina sera za TEHAMA ambazo zingesaidia kuimarisha na kurahisisha matumizi ya mifumo iliyopo ndani yake.

Kutokuwa na sera za TEHAMA kunapelekea kuwepo kwa matumizi mabaya ya mifumo na kukosekana kwa usalama wa taarifa na vifaa vya TEHAMA vilivyopo.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa kuandaa na kuimarisha sera za TEHAMA ili kuweza kupatikana kwa matumizi bora ya mifumo na kuongezeka kwa usalama wa taarifa zilizomo.

**Majibu ya uongozi wa Bohari Kuu**

Wizara ya Afya imeandaa Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Digitali za Afya Zanzibar (Five Years Digital Health strategy 2020/2025) ambapo moja ya vipaumbele vyake ni kuandaa miongozo inayotumika katika kutekeleza kazi za TEHAMA ndani ya Sekta ya Afya. Kupitia kipaumbele hicho mwezi wa Juni Wizara ilikamilisha kuandaa miongozo mitatu ambayo ni muongozo wa Sera ya TEHAMA, Muongozo wa kutekeleza mifumo ya digitali na Muongozo wa kutumia, kugawiana na kulinda taarifa za afya. Lengo la kutengeneza miongozo hiyo ni kuhakikisha kwamba Wizara inakua na utaratibu na viwango maalumu vinavyokubalika vinatumika katika kutekeleza kazi za TEHAMA. Miongozo hii yote inatumika katika Idara na Taasisi zote ndani ya Wizara ya Afya.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhishwa na juhudi za Wizara katika kuhakikisha ushauri wa ukaguzi unafanyiwa kazi ili kuleta tija na ufanisi katika matumizi ya mifumo yo Bohari Kuu ya Dawa na Wizara kiujumla.

**UCHUNGUZI WA UKAGUZI WA RIPOTI YA MFUMO WA MISHAHARA YA SERIKALI (GOVERNMENT PAYROLL SYSTEM) KWA MWAKA 2020/2021**

Katika ukaguzi wa Mfumo wa Malipo ya Mishahara ya Serikali, dosari mbali mbali zimebainika kama zifuatazo:-

**Hoja nambari 6.1.1.1: Kutokuwepo kwa nyaraka muhimu za mfumo wa ‘‘Payroll’’.**

Ukaguzi umebaini Mfumo huo hauna nyaraka zozote zinazohusiana na mfumo ikiwemo nyaraka muhimu katika matumizi endelevu ya mfumo inayoelezea namna mfumo unavyofanya kazi (system operations manual), mfumo ulivyosanifiwa (system architecture document), mfumo ulivyosanidiwa (system configurations manual), na nyaraka nyingine kama vile za mahitaji ya mfumo (system requirements document).

Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa mfumo huu wenye uwezo wa kufanya kazi za kuchakata taarifa za mabilioni ya fedha za mishahara ya watumishi wa umma kwa kila mwezi ukaguzi umebaini mfumo huu utengenezaji wake haukuzingatia miongozo na viwango bora vinavyokubalika (best practice) kuanzia hatua ya awali ya utengenezwaji wake mpaka hatua ya mwisho

(System Development Life Cycle - SDLC) ambayo inaelekeza kwamba mfumo unatakiwa kutengenezwa kwa kufuata hatua kwa hatua ambapo kila hatua inachangia katika kuhakikisha kwamba mfumo unaotengenezwa unakidhi mahitaji ya watumiaji kwa wakati uliopo na wakati ujao huku ukizingatia mikakati ya taasisi, udhibiti na usalama na kwamba unaongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi husika.

Kwa mfano, kuandaa mpango kazi wa kutengeneza mfumo (system planning) ni hatua ya kwanza katika "SDCL" ambapo pamoja na mambo mengine yanayofanyika ni kuandaa mpango kazi wa muda mrefu (long term plan), sera za kuchagua miradi ya TEHAMA, bajeti ya muda mfupi na muda mrefu ya TEHAMA, kufanya upembuzi yakinifu wa awali na kupata idhini ya uongozi wa taasisi ya kuendelea na mradi, andiko la pamoja na ratiba ya mradi (project schedule).

Hatua ya pili ni kufanya tathmini ya mfumo (systems analysis) ambapo wataalamu wa TEHAMA wanakusanya taarifa za mahitaji ya watumiaji wa mfumo (system users' requirements) na kuyachakata kisha huandaa nyaraka ya mahitaji (system requirements document), hatua nyingine ni pamoja na tatu mpaka nane katika mfuatano.

Kutokuwepo kwa nyaraka zote zinazohitajika katika utaratibu wa kutengeneza mifumo kunaweza kupelekea athari nyingi ikiwamo zifuatazo:-

Mfumo kuwa mali ya mtu/ watu wachache badala ya taasisi, hii inatokana na ukweli kwamba aliyeutengeneza na wanaoutumia mfumo kwa sasa ndio wanafahamu kilichomo kwenye mfumo na namna kinavyofanya kazi kwa sababu hakijaandikwa kwenye nyaraka yoyote, mtu huyu au kikundi cha watu hawa ikitokea hawapo ofisini basi mfumo huu hautaweza kutumika katika namna ambayo ni endelevu na kuikosesha taasisi haki ya kunufaika na uwekezaji uliofanywa na taasisi husika.

Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia mahitaji yote ya watumiaji ya sasa na ya wakati ujao katika usalama, udhibiti, ufikiaji, matumizi, urahisi wa kuutumia n.k kwani uandishi wa nyaraka mbalimbali za mfumo unawapa nafasi watu na

wadau wengine wa mfumo kuchangia mawazo yao katika namna ambayo ni rasmi ikiwa ni pamoja na kutathmini na kuidhinisha nyaraka husika ili kuendelea na hatua nyingine jambo linalopelekea kuboresha mfumo utakaotengenezwa.

Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia hali halisi ya mabadiliko ya teknolojia na kusababisha mfumo husika kuwa kama kisiwa kwa kushindwa kuwasiliana na mifumo mingine kwa sababu ya utofauti wa teknolojia jambo linarudisha nyuma urahisishaji wa kazi kwa kutumia TEHAMA.

Tasisi kushindwa kufahamu uwekezaji halisi kwenye mfumo ikiwa ni pamoja na gharama, muda, juhudi na jitihada zilizotumika mpaka kuupata mfumo uliokamili, hili hutokea pale ambapo hakuna bajeti ya muda mfupi na mrefu kwa ajili ya kutengeneza mfumo wote.

Taasisi kushindwa kudhibiti matumizi, muda na ubora wa mfumo husika kwa sababu hakuna mpango wala bajeti iliyoandikwa na kuidhinishwa na uongozi wa taasisi. Taasisi kushindwa kufanya maboresho au mabadiliko kulingana na mahitaji kwenye mfumo kwa kuwa haifahamiki au haikumbukwi namna mfumo ulivyo sanifiwa na kutengenezwa.

Kuendeleza utegemezi kwa mtoa huduma (system supplier) ikiwa mfumo umetengenezwa na mtoa huduma wa nje kwasababu taasisi inakuwa haina kumbukumbu muhimu ambazo ingeliweza kuzitumia kujenga uwezo wa ndani na kupunguza utegemezi kwa mtoa huduma jambo ambalo linaokoa gharama na kuipunguzia mzigo Serikali.

Ukaguzi unashauri kuzingatiwa kwa miongozo na viwango bora vinavyokubalika katika utengenezaji wa mifumo kama hii ambapo nyaraka zote za mifumo ikiwa ni pamoja na bajeti, ratiba, usanifu wa mfumo, tija, utendaji kazi wa mfumo, usanidi wa mfumo, mipango kazi, mahitaji ya mfumo na uidhinishwaji wa nyaraka hizo vizingatiwe kabla ya kutengeneza au kununua mfumo wowote.

Aidha, kwa kuwa mfumo huu wa ulipaji mishahara Serikalini bado unatumika ni vyema wataalamu wa TEHAMA kwa kushirikiana na watumiaji wa mfumo

ndani ya Wizara waandae nyaraka zote muhimu za mfumo na zipatikane kwa matumizi husika mapema iwezekanavyo ili kuondoa au kupunguza hatari iliyopo ya kupata athari kama zilivyoelezwa hapo juu.

Athari na ushauri huu pia utumike kwenye mifumo yote ya Wizara bila kujali Idara inayohusika na utenegnezaji au ununuzi wa mifumo husika ambayo haina nyaraka zote muhimu kama zilivyoelezewa hapo juu iwe inayotengenezwa na wataalamu wa TEHAMA wa ndani au nje ya Wizara au kununuliwa ama kukodishwa.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Ni kweli kwamba mfumo wa usimamizi wa Mishahara (Payroll) kwasasa hauna nyaraka muhimu za mfumo, jambo hili limetokana na kuwa wakati mfumo unatengenezwa hakukuwa na matakwa ya nyaraka za mfumo, ulitengenezwa kizalendo na mfanyakazi wa Wizara. Hata hivyo, mfumo mpya wa utumishi na mishahara umezingatia matakwa haya yaliyobainika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imesikitishwa baada ya kubaini kuwa mfumo huo haukuwa na nyaraka zozote, lakini pia haukufuata miongozo ya viwango bora vinavyokubalika, ukizingatia mfumo huo unachakata mabilioni ya fedha. Aidha, Kamati imearifiwa kuwepo kwa mfumo mpya wa utumishi na mishahara, na kusisitiza mfumo huo mpya uwe na nyaraka zote, ufuate miogozo ya viwango bora (Best practices) na miongozo inayotolewa na Wakala wa Serikali Mtandao (eGaz).

**Hoja nambari 6.1.1.2: Kutokuwepo kwa mpango wa kupona maafa (Disaster Recovery Plan) - Rejea Hoja Namba 5.5.1.11**

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Ofisi ya Rais, fedha na Mipango ipo na mpango wa kupona maafa kwa mifumo ya bajeti na mifumo ya matumizi (IFIMIS), kwa upande wa mfumo wa Udhibiti wa Mishahara changamoto hii imeonekana na Ofisi imeona ni busara kusubiria kuunganisha mfumo mpya wa rasilimali watu na mishahara baada ya kukamilika katika mpango wa kupona maafa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na hoja ya CAG. Aidha, Kamati imeelezwa kuwa kumeanzishwa mfumo mpya wa BAMAS ambao hoja kama hii itazingatiwa sana ili kuhifadhi taarifa za mfumo katika hali ya usalama.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha Mpango wa kupona maafa (Disaster Recovery Plan) unapatikana mapema iwezekanavyo pindi tu mfumo huo mpya utakapoanza.

**Hoja nambari 6.1.1.3: Kukosekana kwa mipango ya kuendeleza biashara (Business Continuity Plan) - Rejea Hoja Nambari 5.5.1.5**

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia kitengo cha Udhibiti wa Mishahara imeiona changamoto hii ila kwa kuwa Ofisi inatarajia kupata mfumo mpya wa mishahara, matarajio ni kwamba mpango wa kuendeleza biashara utakuwepo katika mfumo mpya wa rasilimali watu na mishahara utakapoanza kufanya kazi rasmi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na hoja hii ya CAG. Sambamba na hoja namba 6.1.1.2, Wizara imeiarifu Kamati kua kwa sasa kuna mfumo mpya ambao unatarajiwa kutumika hivi katibuni na changamoto kama hii katika mfumo huo mpya itaondoka.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha Mpango wa kuendeleza biashara (Business Continuity Plan) unapatikana mapema iwezekanavyo pindi mfumo huo mpya utakapoanza.

**Hoja nambari 6.1.1.4: Kutofanyika kwa majaribio ya nakala za taarifa za mfumo (Backup testing) - Rejea Hoja Nambari 5.5.1.6**

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kamati ya PAC imebaimi kwamba changamoto hii imeshafanyiwa kazi kwani hivi sasa taarifa zote muhimu zinapatikana zinapohitajika.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na majibu ya Wizara.

### 6.1.1.5 Kutokuwa na eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery site/offsite) – Rejea Hoja Nambari 5.5.1.4

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Majibu ya hoja hii yanafanana na majibu ya hoja nambari 6.1.1.2.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC ni sawa na yale yanayopatikana katika hoja nambari 6.1.1.2 inayohusu kutokuwepo kwa mpango wa kupona maafa (Disaster Recovery Plan).

### Hoja nmbari 6.1.1.6: Mfumo kuwa na taarifa pungufu bila kujali umuhimu wake

Ukaguzi umebaini kuwa katika Mfumo wa mishahara wa Serikali kuna baadhi ya taarifa ambazo hazijakamilika kwa mfano kuna waajiriwa wengi hawana namba za pensheni (pension numbers) lakini pia mfumo umewezeshwa kuwekwa picha za watu ili kurahisisha utambuzi lakini taarifa hizo za picha hazijawahi kuingizwa kwenye mfumo. Kutokamilika kwa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo kunaweza kupelekea usumbufu wakati wa kuhitaji taarifa hizo za wafanyakazi hususani wakati wa kuhakiki wafanya kazi, lakini pia jambo hili linapunguza utegemezi (reliability) wa taarifa zilizomo kwenye mfumo kinyume na malengo ya jumla ya kutekeleza mifumo kama hii ambapo ni kufanya upatikanaji wa taarifa kamili na sahihi kwa wakati ili kurahisisha ufanya maamuzi katika matumizi yake.

Ukaguzi unashauri kuwa, ni vyema taarifa zote za wafanyakazi katika mfumo huo kuingizwa kwa ukamilifu ili kukamilisha malengo yalioyokusudiwa ya kutakiwa kuingizwa taarifa hizo yanatimia na kuepusha athari zinazoweza kutokea kama hatua stahiki hazitachukuliwa kama ilivyoelezewa hapo juu.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango imeiona changamoto hii na inategemewa kufanyiwa kazi katika mfumo mpya unaotarajiwa kufanyakazi hivi karibuni.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imekubaliana na hoja hii ya CAG na kwa vile itaifanyia kazi katia mfumo mpya unaoandaliwa, Kamati ya PAC haikuwa na hoja zaidi.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inafuata miongozo inayotolewa na eGaz ili kuhakikisha changamoto kama hizi hazijitokezi katika mfumo mpya.

**Hoja nambari 6.1.1.7: Mfumo kuwa na taarifa zenye makosa**

Usahihi wa taarifa zinazoingizwa ndani ya mfumo ni jambo la muhimu kwa kuwa taarifa hizo hutumiwa kwa matumizi mbali mbali na Serikali ikiwemo kuwalipa watu mishahara na stahiki zao nyengine. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa kuna taarifa zilizomo kwenye mfumo ambazo zinamakosa, mfano wa taarifa hizo ni tarehe za kuzaliwa wafanyakazi hazikuwa sahihi kiasi ambacho ni ngumu kuzitumia kuamua muda wa kustaafu kupitia mfumo huo. Uwepo wa taarifa zenye makosa unapelekea athari zifuatazo:-

Kuchelewesha waajiriwa kustaafu kwa mujibu wa sheria za nchi kwa wale walioingiziwa tarehe za mbele jambo ambalo litapelekea Serikali kuwa na waajiriwa wengi ambao hawana uwezo wa kuzalisha kama inavyotarajiwa na kuisababishia Serikali hasara kwa kuwalipa watu mishahara wakati hawazalishi au hawatoi huduma kwa viwango vilivyowekwa. Pia, hali hii inaweza kuwazuia vijana kuingia kwenye ajira kwa sababu wazee hawaondoki na Serikali inaweza kuajiri sehemu ndongo tu ya wananchi.

Kuwahisha waajiriwa kustaafu kabla ya umri stahiki kwa wale ambao wameingiziwa tarehe za nyuma tofauti na uhalisia, hali hii inaweza kupelekea Serikali kupoteza nguvu kazi ambayo bado ina uwezo wa kuzalisha kwa tija na ufanisi kwa kuzingatia ujuzi wao na kusabisha kuchelewesha maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Taarifa zilizomo kwenye mfumo kutoaminika na kushindwa kutumika kwa matumizi yaliyokusudiwa, jambo hili linaashiria kwa kuikwamisha Serikali kupata matunda ya uwekezaji wake kwenye mfumo huu na TEHAMA kwa ujumla.

Ukaguzi unashauri mambo yafuatayo:

- Wizara izipitie kwa umakini taarifa zote za waajiriwa ili kuweza kubaini zile ambazo haziko sahihi na kuzichukulia hatua.
- Wizara iandae mpango kazi wa kuhakiki waajiriwa wote wa Serikali na kukusanya taarifa sahihi ikiwa ni pamoja na tarehe za kuzaliwa, mwaka wa ajira, taasisi wanazofanyia kazi, vyeo, stahiki zao, ustaafu wao, n.k. kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyopo.

- Kuutekeleza mpango kazi husika kwa kuzingatia weledi, tija na ufanisi ndani ya muda muafaka ili kuepusha madhara kama yalivyoelezwa hapo juu kwenye athari.
- Uingizaji wa taarifa kwenye mfumo ufanywe na mtu mmoja na pawepo na mtu mwengine anayethibitisha au kuidhinisha usahihi na uhalisia wa taarifa zinazoingizwa kabla ya kwenda kwenye hatua ya kutengenezewa mishahara na kulipwa.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Taarifa zote zilizokuwemo katika mfumo zinapokelewa moja kwa moja kutoka Taasisi husika, ikitokea kuna makosa, barua zimekuja na makosa na kubainika na Watendaji wa Payroll taarifa huwasilishwa kwa Taasisi husika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na majibu ya Wizara. Aidha, Kamati inaisisitiza Wizara kuendelea kuufanyia kazi ushauri wa CAG ili kuepusha mfumo kuwa na taarifa zisizo sahihi.

**Hoja nambari 6.1.1.8: Mfumo kushindwa kubaini hali ya ustaafu kwa watumishi wenyewe (automatically).**

Moja ya malengo ya kuanzishwa mfumo ni kurahisisha kazi, kuongeza tija na ufanisi na utendaji bora wa kazi hizo. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa mfumo huu hauna uwezo wa kubaini hali ya ustaafu ya waajiriwa hali ambayo inaweza kusabisha kuwepo kwa waajiriwa hewa wanatokana na mwajiriwa kustaafu utumishi lakini kwa sababu mfumo hauwezi kutambua hali hii na kwa sababu pia watumiaji wa mfumo wameshindwa kuchua hatua stahiki za kumsitishia mishara mstaafu husika, basi anaendelea kupokea mshahara kama kwamba bado yuko katika utumishi kwa muda usiojulikana.

Aidha, udhaifu huu wa mfumo unaweza kusababishia Serikali kupata hasara kwa kuwalipa watumishi hewa na kuchelewesha kufanya maendeleo katika huduma nyingine za jamii kama vile ujenzi wa hospitali, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Pia, hali hii inaweza kuweka ugumu katika mipango ya Serikali kwa kutofahamu gharama sahihi za mishahara ya kila mwezi na mwaka mzima.

Ukaguzi unaishauri kuwa, ni vyema kuuboresha mfumo na kuhakikisha kuwa unauwezo wa kubaini muda wa kustaafu na kuzuia malipo ya mshahara wenyewe (automatic detection and block) hususani pale mtumishi anapofikia

umri wa lazima wa kustaafu na ikiwezekana mfumo utume ujumbe (message alert) kwa njia ya simu ya mkononi au barua pepe kwa msimamizi wa mfumo (system administrator), Mkurugenzi rasirimali watu wa taasisi ya mtumishi, ili kuwakumbusha kuchukua hatua kwa upande mwingine.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Utaratibu wa kuzuia mishahara kwa watumishi waliostaafu kisheria unaratibiwa na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Ofisi ya Rais Fedha na Mipango hupokea barua za watumishi waliostaafu na kuzifanyia kazi mara tu baada ya kuwasilishwa na kuhakikisha kwamba hakuna mtumishi anaelipwa mshahara wake baada ya kustaafu na kupokelewa barua yake.

Aidha, katika mfumo uliopo wa udhibiti wa mishahara hakuna kipengele kinachobaini watumishi wanastaafu automatically hii inatokana na mahitaji ya mfumo yalivyopendekezwa wakati wa utengenezaji, ila suala hili limezingatiwa katika mfumo mpya wa udhibiti wa mishahara unaotarajiwa kuanza kufanyakazi hivi karibuni.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na majibu ya Wizara na kuitaka Wizara kuhakikisha kuwa katika mfumo huo mpya kuwe na udhibiti wa kutambua watu ambao wamestaafu (automatically) ili kuepusha fedha za Serikali kupotea.

**Hoja nambari 6.1.1.9: Ulipaji wa mishahara kwa watumishi waliostaafu.**

Ukaguzi umebaini mfumo wa ulipaji wa mishahara Serikalini umeruhusu ulipaji wa mishahara kwa watumishi waliostaafu, katika sampuli iliyofanyika ya uchunguzi ukaguzi umebaini uwepo wa mtumishi aliyestaafu mwezi wa Februari, 2021 lakini aliendelea kulipwa mishahara mpaka mwezi wa Julai, 2021 ambayo ni zaidi ya shilingi 3,129,000.

Aidha, hali hii inaashiria kuwepo kwa udhaifu kwenye taasisi inayosimamia watumishi wa umma kwa kushindwa kubaini watumishi wanaotarajia kustaafu ndani ya miezi walau mitatu kutoka kila taasisi ya umma na kuchukua hatua stahiki za kuhakikisha kua wanaandaliwa mazingira ya kustaafu salama ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwa Ofisi ya Fedha kuhusu kuwasitishia mishahara watumishi husika.

Hivyo basi, ukaguzi unashauri kufanyika uhakiki wa watumishi wote ili kubaini watumishi ambao tayari walisha staafu lakini bado wameendelea kulipwa mshahara kana kwamba bado wako kwenye utumishi na kisha kuchukua hatua za kuwasitishia mishahara hiyo na kuwaondoa wote kwenye mfumo wa ulipaji wa mishahara Serikalini.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kamati haikupokea majibu ya maandishi ya hoja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango licha ya juhudi ya kuyafuatilia kufanyika.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Licha ya kutopatiwa majibu, Kamati ya PAC imeelezwa na kubaini kwamba ni kweli mkaguzi aligundua kuwepo kwa kasoro hiyo lakini Wizara imeihakikishia Kamati kwamba changamoto hiyo haitokuwemo katika Mfumo mpya.

**Hoja nambari 6.1.1.10: Mfumo kutokuwa na usalama wa uhakika (Security)**

Moja kati ya vitu muhimu vinavyotakiwa kuzingatiwa sana katika utenegenezaji na utumiaji wa mfumo ni usalama wa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo ili taarifa hizo ziendelee kuwepo, ziendelee kuwa kamili na sahihi, na ziwe siri kwa kadri inavyohitajika.

Aidha ukaguzi umebaini kuwa hakuna usalama wa mfumo na taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo huo kutokana na mfumo kutengenezwa kwa teknologia ya zamani ya Visual Basic 6.0 ambayo kwa sasa kampuni ya Microsoft iliyotengeneza teknologia hiyo imeacha kuiboresha na kuimarishaji kiusalama wa baadhi ya sehemu za programu hiyo tangu tarehe 8 Aprili, 2008. Hali hii inapelekea kuhatarisha usalama wa mfumo na taarifa zinazoingizwa ndani ya mfumo husika kuwa uko katika hatari kubwa ya kuathiriwa kirahisi na virusi au udukuzi na kusababisha taarifa hizo kupotea, kubadilishwa au kuvuja na kuingia mikononi mwa watu wasio na nia njema.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuchukua hatua za makusudi mapema iwezekanavyo ili kupata mfumo mwingine kwa ajili ya malipo ya mishahara kwani mfumo uliopo kwa sasa unahatari kubwa kama ilivyoelezwa hapo juu.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kamati haikupokea majibu ya maandishi ya hoja hii kutoka Wizara ya Fedha na Mipango licha ya juhudi ya kuyafuatilia kufanyika.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Licha ya kutopatiwa majibu, Kamati ya PAC imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake ya ukaguzi katika mfumo huo kulikuwepo kasoro hiyo lakini Wizara imeihakikishia Kamati kwamba changamoto hiyo haitokuwemo katika Mfumo mpya.

#### 6.1.1.11 Udhaifu kwenye udhibiti wa utumiaji wa mfumo – Rejea Hoja Nambari 5.5.1.7

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kamati haikupokea majibu ya maandishi ya hoja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango licha ya juhudi ya kuyafuatilia kufanyika.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Licha ya kutopatiwa majibu, Kamati ya PAC imeelezwa na kubaini kwamba ni kweli mkaguzi aligundua kuwepo kwa kasoro hiyo lakini Wizara imeihakikishia Kamati kwamba changamoto hiyo haitokuwemo katika Mfumo mpya.

## 6.2 MATOKEO YA UKAGUZI KWENYE UDHIBITI WA TEHAMA KWA UJUMLA

Katika ukaguzi wa Mfumo wa Usajili wa mali za Serikali Mambo mbali mbali yamebainika ikiwemo dosari zifuatazo: -

### 6.2.1 Kutokuwa na Sera ya TEHAMA

Ukaguzi umebaini kwamba kitengo cha TEHAMA cha Wizara hakina sera za TEHAMA zilizowekwa kwa kusimamia taratibu na shughuli zote zinazohusiana na TEHAMA, badala yake shughuli za TEHAMA zinafanywa na kusimamiwa kama inavyoombwa na watumiaji wa mwisho, bila kufuata taratibu na miongozo rasmi inayotakiwa na iliyotengenezwa kulingana na mikakati na mipango ya Wizara na matumizi ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na miundombinu yake.

Kutokuwepo kwa sera madhubuti za TEHAMA kunaweza kupelekea udhaifu katika usalama, udhibiti, uratibu, usimamizi wa shughuli zote za TEMAHA

ikiwa ni pamoja na matumizi ya rasilimali za TEHAMA, mawasiliano kwa barua pepe, na uwekezaje kwenye Wizara.

Ukaguzi unaishauri Wizara kupitia cha TEHAMA kuandaa sera za TEHAMA kwa kuzingatia miongozo na sera za Wakala Serikali mtandao na miongozo ya kimataifa kama vile COBIT 2019, AFROSAI-E ambazo zitaidhinishwa na menejimenti ya Wizara. Aidha, Wizara inashauriwa kuzitumia sera hizo ili kupata matokeo bora ya udhibiti na usimamizi wa TEHAMA ndani ya Wizara.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Pamoja na kwamba Kamati haikupokea majibu ya maandishi kuhusiana na majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC imebaini ni kweli Sera ya TEHAMA haipo na haitumiwi na watendaji wa TEHAMA.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Ni vyema Wizara kupitia cha kitengo cha TEHAMA iandae sera za TEHAMA kwa kuzingatia miongozo na sera za Wakala Serikali Mtandao na miongozo ya kimataifa kama vile COBIT 2019, AFROSAI-E.

### 6.2.2 Kutumika kwa barua pepe (e-mails) zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kielektroniki ya kiofisi.

Sera za Wakala wa Serikali mtandao kifungu nambari 4.10.1.2(a) inazitaka taasisi zote za Serikali na watumishi wake kutumia barua pepe rasmi za Serikali kwenye mawasiliano yote ya kiofisi ya kielektroniki ili kuhakikisha usalama wa taarifa zote za Serikali. Hii inamaanisha kwamba mawasiliano yoyote ya kazi za Serikali yanapaswa kufanywa kwa kutumia barua pepe rasmi za Serikali kwa sababu za kiusalama kwenye taarifa hizo zinasafirishwa toka kwa mtu au taasisi moja kwenda kwa mpokeaji ambaye ni mtumishi au taasisi ya Serikali. Matumizi ya “Gmails”, “Yahoo mails”, “Hotmails” n.k hayaruhusiwi kwa watumishi wa Serikali.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini sehemu kubwa ya watumishi wa Wizara wanatumia barua pepe zisizo rasmi kwenye mawasiliano ya kikazi kama vile gmail, yahoo na hotmail. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sera za Serikali mtandao lakini pia ni kuhatarisha usalama wa taarifa za Serikali.

Ukaguzi unaishauri Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kipitia kitengo cha TEHAMA mambo yafuatayo:-

- Kufanya utafiti mdogo wa matumizi ya barua pepe kwenye mawasiliano ya kikazi ili kuelewa ni kwa nini watumishi wengi hawatumii barua pepe za Serikali na kuwasilisha ripoti ya utafiti huo kwenye menejimenti ya Wizara kwa ajili ya kuchukua hatua sitahiki kulingana na yatakayokuwa yamebainika, ikiwa ni pamoja na kuwatengenezea barua pepe rasmi watumishi wote wasio kuwanazo.

- Kuwapatia mafunzo endelevu ya namna ya kuzitumia parua pepe hizo ipasavyo na kuleta tija.

- Kusimamia na kuratibu miundombinu ya TEHAMA ya Wizara wakati wote kuhakikisha kwamba haikwamishi matumizi ya barua pepe hizo, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma ya barua pepe, mtandao (internet), uwezo wa kutuma na kupokea mafaili ili kuchechemua matumizi ya barua pepe hizo Wizarani.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Watumishi wote wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ishawapatiwa emails za Serikali na kila mmoja anatumia kwa kutuma nyaraka za Serikali

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na majibu ya Wizara. Aidha, Kamati inaisisitiza Wizara kuhakikisha kuwa watumishi wote wanazitumia barua pepe izo kwa kazi za Serikali na kuepuka kabisa matumizi ya barua pepe zisizo rasmi.

**UCHUNGUZI WA UKAGUZI WA RIPOTI YA MFUMO WA UVIKO 19 (WIZARA YA AFYA) KWA MWAKA 2020/2021**

**8.7.1 Dosari zilizobainika kwa upande wa Wizara ya Afya**

Kwa upande wa Wizara ya Afya ukaguzi ulibaini dosari kama zifuatazo: -

**Hoja nambari 8.7.1.1: Kitengo cha TEHAMA cha Wizara kutokushiriki kikamilifu kwenye utengenezaji na utekelezaji wa mfumo wa UVIKO 19.**

Ukaguzi umebaini kwamba mchakato wa utengenezaji wa mfumo wa UVIKO 19 ikiwa ni pamoja na Moduli ya Chanjo haukuwashirikisha kitengo cha TEHAMA ipasavyo katika hatua mbalimbali za utengenezaji wa mfumo huo.

Hali hii ilijidhihirisha wakati ukaguzi ulipokuwa unaendelea ambapo ilibainika kupitia majadiliano na wakaguliwa kwamba kwa nyakati tofauti ushauri na mapendekezo ya kitengo cha TEHAMA kwenye hatua za awali za kuutengeneza

mfumo huu hayakuwa yakizingatiwa na Menejimenti ya Wizara ya Afya. Ukaguzi ulibaini kwamba kitengo cha TEHAMA cha Wizara ya Afya hakikuwa na ufikiaji wa mfumo huu (access) mpaka wakati wa kukamilika kwa ukaguzi hali inayoashiria kwamba kitengo cha TEHAMA hakikuwa na uelewa wa namna mfumo huu unavyofanya kazi pamoja na changamoto za mfumo wote kwa ujumla wake tangu mwezi Machi 2021 ulipoanza kutumika.

Aidha, ukaguzi uliabaini kwamba kitengo cha TEHAMA hakikupewa mafunzo ya namna mfumo unavyofanya kazi na namna ya kuusimamia na kuuendeleza kinyume na matakwa ya mkataba baina na Wizara ya Afya na Rahisi Solution Company kwa mujibu wa kifungu 7.0 (ix na x) pamoja na kifungu 18.0 ambacho kinachomtaka Mtoa huduma kutoa mafunzo kwa watumiaji mbalimbali wa mfumo.

Kimsingi, kitengo cha TEHAMA ndicho kina jukumu la kuusimamia mfumo huu sawa na mifumo mengine iliyopo Wizarani hivyo, kukosa ufahamu wa kutosha wa vitu vya msingi vya mfumo ambavyo ni pamoja na nyaraka muhimu za mfumo kama vile nyaraka ya mahitaji (user requirements document), nyaraka za usanifu na usanidi, “source codes”, na teknolojia iliyotumika kwenye mfumo kunaiweka Wizara ya Afya na Serikali kwa ujumla wake kuwa kwenye hatari kubwa ya utegemezi wa Mtoa huduma kwa muda usiojulikana na kuongeza gharama za kuusimamia na kuuendesha mfumo huu katika namna endelevu ili kupatikana tija na ufanisi uliotarajiwa.

Kwa kuzingatia makubaliano ya kimkataba baina ya pande mbili sehemu 4.0 kwamba Wizara ya Afya itaumiliki mfumo kwa 100% kutoka tarehe ya mfumo kuanza kufanya kazi ilitarajiwa kuwepo na mpango mkakati wa Wizara unaoainisha namna ambavyo Wizara itaweza kulichukua jukumu hilo na kuisaidia Serikali katika kuokoa fedha ambazo vinginevyo zitatumika kumlipa mtoa huduma ili aendelee kuusimamia mfumo kwa muda mrefu zaidi badala ya kupeleka fedha hizo kwenye kutatua changamoto za Wananchi na kuleta maendeleo katika jamii. .

Kwa ujumla, hali hii inaweza kuleta athari za kiuchumi na kijamii kama zilivyoainishwa hapa chini;

- Kuongeza gharama Serikalini kwa kumtegemea mtoa huduma kwenye kuusimamia na kuuendeleza mfumo na kutoa msaada wa kiufundi kwa muda usiojulikana.
- Kudhoofisha jitihada za kujenga uwezo na kuibua vipaji vya wataalamu wa ndani kwa kutowapa nafasi na kutowahamasisha kufanya kazi zilizo ndani ya uwezo wao.

- Kushusha hamasa kwa watumishi wa Serikali kwenye eneo la TEHAMA hususani wale wenye vigezo vyote vya kufanya kazi na
- Kukatisha tamaa wanafunzi walioko vyuoni kusomea fani za TEHAMA.

Ukaguzi unashauri mambo yafuatayo kuzingatiwa:-

- Menejimenti ya Wizara ya Afya kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi Solution Company kuandaa mpando wa mafunzo na kuutekeleza ambao utahakikisha kua kitengo cha TEHAMA cha Wizara kinajengewa uwezo wa kuusimamia mfumo huu kikamilifu kabla ya kuhitimishwa kwa mkataba baina ya pande mbili.
- Kwa kua mfumo huu unatakiwa ufanye kazi masaa 24 siku 7 za wiki, ni vyema Wizara ya Afya ikajipanga kwa kuandaa watumishi wa kitengo cha TEHAMA wa kutosha watakao fanya kazi kwa "shift" mbili au tatu ndani ya masaa 24/7 ili kutoathiri ratiba na safari za wasafiri ambazo hupangwa muda wowote ndani ya siku.
- Kwa kuzingatia mazingira haya ya kazi kwenye kuhudumia wageni katika upimaji, uchanjaji na matibabu ya UVIKO 19 kwa kutumia mfumo huu kuna haja kwa Wizara kuangalia namna ya kutoa hamasa (motivation) kwa watumishi wanaohusika na shughuli za UVIKO 19 kwa lengo la kuweza kufanya kazi kwa muda wa saa 24 bila ya vikwazo vyovyote na kupelekea upatikanaji wa huduma bora tofauti na ilivyo sasa ambapo kazi hizo hufanywa na kampuni ya Rahisi Solution Company.
- Wizara izingatie mapendekezo na ushauri wa wataalamu wake wa TEHAMA kwenye masuala ya mifumo hususani ushauri unaolenga kulinda maslahi mapana ya Serikali na nchi kwa ujumla.
- Wizara kupitia kitengo cha TEHAMA ifuatilie kwa karibu nyaraka zote zinazohusu usanifu, ujaribu, usanidi, mpangilio, utekelezaji, uhifadhi, utumiaji, uunganishwaji, mafunzo n.k ya mfumo huu kabla ya kumalizika kwa mkataba uliopo baina ya Wizara ya Afya na kampuni ya Rahisi Solution Company.
- Kwa kuzingatia matakwa ya Mkataba na muda wa kumalizika kwa Mkataba huo jitihada za makusudi zichukuliwe na Wizara ya Afya kuhakikisha watendaji wa kitengo cha TEHAMA wanajengewa uwezo na kufahamishwa namna bora ya usimamizi na uendeshaji wa mfumo na kampuni ya Rahisi Solution Company kwa lengo la kuhakikisha tija iliyokusudiwa inaendelea kupatikana baada ya kumalizika kwa Mkataba huo.
- Wizara kupitia kitengo cha TEHAMA kuupitia vyema mfumo na mkataba kuhakikisha kwamba unafanya kazi kama ilivyotarajiwa kabla ya kuupokea na kuanza kuusimamia pindi mkataba utakapoisha baina ya Wizara na kampuni ya Rahisi.
- Wizara kupitia kitengo cha TEHAMA kua mstari wa mbele katika hatua zote tangu mwanzo na kupewa nafasi ya kusikilizwa kwenye masuala

yote yanayohusu mifumo ya Wizara ikiwa ni pamoja na huu wa UVIKO 19.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Ni kweli kulikuwa na ushiriki mdogo wa Kitengo cha TEHAMA kutoka hatua za awali za utengenezaji wa mfumo wa UVIKO-19 na hata wakati wa usimamizi wake. Hili lilisababishwa na hali ya dharura na uharaka wa kutengenezwa kwa mfumo husika.

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Kampuni ya Rahisi kupitia watendaji na watumiaji wa mfumo huo na wataalau wa TEHAMA wa Wizara imekuwa ikishiriki mara kwa mara katika kutoa mapendekezo ya mahitaji mapya ili kuuimarisha mfumo huo.

Wizara ya Afya iliteua timu ya Wataalamu wa ICT (4) ikiongozwa na Bw. Bwamadi ambayo ilikuwa timu iliyoshauri na kusimamia masuala ya mfumo wa UVIKO 19. Wataalamu haw ani;

- Bw. Bwamadi
- Mohd Habib
- Bi. Asma J Mwita
- Haji Ibrahim Masoud
- Sabra Issa Juma
- Maryam Haji

Wataalamu hawa waliombewa kupata access ya mfumo pamoja na mafunzo ya awali, ikijumuisha Watumishi (4) kutoka FM, Maabara ya Taifa Binguni (5) na Watumishi wengine (15) kutoka vituo vya Afya. Aidha, kwa sasa Wizara ya Afya haifanyi kazi kwa shift though inaendelea kujipanga pamoja na kuongeza idadi ya Watumishi ambapo tayari Serikali imeipatia jumla ya Developer 8.

Wizara ya Afya imekuwa ikitoa malipo ya ziada kwa Watumishi wote ambao walikuwa wakihusika na utoaji wa huduma za UVIKO 19 katika maeneo mbali mbali ya huduma ikiwemo baadhi ya Watumishi ngazi ya Taifa. Aidha, Watumishi wa ICT ni miongoni mwa eneo ambalo Wizara imelipa kipaumbele katika kuwajumuisha na kuwapatia malipo haya ya ziada ili kuongeza ari ya utendaji wa kazi.

Wizara ya Afya imepokea pendekezo hili na imeweza kuunda timu maalumu wa ICT ili kushauri na kusimamia mawasiliano yote baina ya Wizara na Rahisi. Wizara tayari imeunda timu ya Wataalamu wa ICT na tayari wamefanikiwa kupata nyaraka zifuatazo;

- Modules distription
- Report manual
- User manual
- System permission
- Saver, hosting and System Configurations Manual

Wizara tayari imeteua timu ya Wataalamu wa ICT kama ilivyoainishwa na kupatiwa mafunzo ya awali. Kupitia timu ya Wataalamu wa ICT walioteuliwa, wameshauri na kufanyika kwa mabadiliko ambayo yamelenga kuumiliki pamoja na kuusimamia mfumo wa UVIKO 19 kwa asilimia 100 %. Rejea mkataba namba mbili kwa maboresho. Kama ilivyoainishwa hapo juu kwani Wataalamu wa ICT, ndio washauri wa Wizara ya Afya kwenye masuala ya TEHAMA.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa mpaka sasa bado mfumo huo unasimamiwa na mtoa huduma ambae ni Rahisi Solution Company jambo ambalo linaiengezea gharama Serikali kwa vile mtoa huduma huyo ataendelea kulipwa kwa muda ambao atakuwa anausimamia mfumo huo. Aidha, Kamati haijaridhishwa na ushiriki mdogo wa wataalamu wa TEHAMA wa Wizara ambapo imeonekana kuna mtu ambae hana taaluma ya TEHAMA ndie aliepewa nafasi kubwa ya kushiriki katika kuutengeneza mfumo huo jambo ambalo linapingana na miongozo na "best practice" za kuandaa mifumo hiyo.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ihakikishe inawajengea uwezo wataalamu wa kitengo cha TEHAMA ili mifumo ya Wizara iweze kusimamiwa na kitengo hicho na kunusuru uwezekano wa taarifa za Serikali kuvuja kirahisi na pia kuipunguzia Serikali gharama inazolipa kwa Rahisi Solution Company za kuusimamia mfumo huo.
2. Kamati inaisisitiza Wizara kuhakikisha kuwa wataalamu wa kitengo cha TEHAMA wanashirikishwa kikamilifu katika matayarisho yoyote yanayohusiana na utengenezaji au upokeaji wa mifumo ya Wizara.

**Hoja nambari 8.7.1.2: Kutokuwepo kwa muongozo wa namna ya kuwahudumia wasafiri waliopimwa Rapid PCR Molecular Test Uwanja wa Ndege na kubainika kuwa na maambukizi**

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara haijaweka mwongozo wala mazingira rafiki ya namna ya kuwahudumia wasafiri wanopimwa Rapid PCR Molecular uwanja wa ndege na kubainika kuwa na maambukizi ya UVIKO 19 (Positive).

Ukaguzi umebaini wasafiri wanaopimwa Rapid PCR uwanja wa ndege na kusubiria majibu wanakaa pamoja, na hata baada ya kupokea majibu waliokutwa na maambuzi na wasiokuwa na maambukizi huendelea kukaa pamoja bila ya kujali hatari iliyopo ya kuendelea kuambukizana maradhi.

Uwepo wa hali hiyo inaweza kuwa chanzo cha kusambaa kwa maambukizi miongoni mwa wasafiri hususani kwa wale waliopimwa mwanzo na kubainika kuwa hawana maambukizi (negative) jambo ambalo linasababisha wanaposafiri kwenda nje ya nchi na kukutwa na maambukizi wakati vyeti vya vipimo vyao wakiwa Zanzibar vinaonesha walikuwa “negative” na kusababisha kutiliwa shaka vipimo na ubora wa Maabara za Zanzibar.

Ukaguzi unaishauri Wizira ya Afya kutengeneza mwongozo na kuhakikisha unatekelezwa utakaohakikisha kwamba wasafiri wote waopimwa UVIKO 19 uwanja wa ndege wanakaa kwa hali ya tahadhari na kwa wale wanaobainika kuwa na maambukizi (positive) wanatengewa eneo lao maalum, sehemu inayoruhusu hewa ya kutosha mbali na watu wengine walio “negative” ili kupunguza hatari ya kusambaa kwa maambukizi ndani ya uwanja wa ndege.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara ya Afya imefanikiwa kuandaa miongozo mbalimbali ambayo imekuwa sehemu ya maelekezo Watumiaji pamoja na watoa huduma katika AAKIA. Hii imejumuisha pia Wasafiri. Ifuatayo ni baadhi ya SOP & miongozo iliyotumika kipindi chote ambacho nchi ilikabiliana na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO 19

- TA - Travel Advisory zilizokuwa zikitolewa na Wizara ya Afya mara kwa mara kuwaelekeza Wasafiri na Watoa huduma AAKIA ikiwemo wapimaji wa UVIKO 19.
- Kupatikana kwa muongozo wa namna ya kumtambua msafiri au mtumiaji ambaye atashukiwa kuwa na ugonjwa wa UVIKO - 19 akiwa AAKIA ambapo utaratibu wa kumpatia huduma hadi kufika kituoa maalum cha matibabu umewekwa.
- Kutengwa na kupatikana kwa vyumba maalum pale AAKIA ambavyo vinatumika kwa ajili ya kumtenga mshukiwa au ambaye amethibitishwa kuwa na ugonjwa wa UVIKO 19.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhishwa na majibu ya Wizara kwamba miongozo yote inayohusiana na Uviko -19 ilikuwa ikitolewa na Taasisi za Kimataifa na kila nchi ilitakiwa iridhie miongozo hiyo kama utaratibu bora katika kuhakikisha usalama wa abiria katika maeneo yote ya kusafiri au kuingilia nchini (entry points). Aidha, Kamati imegundua kuwa ni kweli kulikuwa na makosa ya kuwachanganya abiria ambao wanasubiri majibu ya vipimo vya Uviko -19 na wale ambao hawakukutwa na maambukizi ya Uviko -19 jambo ambalo lingeweza kusababisha kusambaa kwa maambukizi hayo kwa kasi zaidi.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ihakikishe yanapotokezea maambukizi yanayosababishwa na virus, waathiriwa wa maambukizi hayo hawawekwi pamoja ili kunusuru kuenea kwa maambukizi hayo.

**Hoja nambari 8.7.1.3 Kutofanyiwa usuluhishi wa kibenki kwa hesabu zote za benki zinazopokea miamala ya UVIKO 19.**

Wizara ya Afya ikiwa na jukumu la kuratibu, kusimamia na kuongoza katika utoaji wa huduma za afya nchini, kudhibiti mripuko wa UVIKO 19 ni moja ya majukumu yake kisheria, hii inajumuisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na UVIKO 19 kulingana na Sera za nchi. Ukaguzi umebaini uwepo wa Hesabu za Benki zisizopungua 4 zinazotumika kupokea fedha za vipimo na chanjo za UVIKO 19 ambapo hesabu 2 zinazotumika moja ni ya TZS na ya pili ya USD ziko chini ya Wizara ya Afya wakati hesabu 2 zilizosalia TZS na USD zikiwa chini ya Ofisi ya Raisi Fedha na Mipango. Kwa nyakati tofauti hesabu hizi zote hupokea fedha za vipimo na zile za vyeti vya chanjo za UVIKO 19 kutoka kwa wananchi na wageni mbalimbali wanaohitaji huduma za UVIKO 19.

Aidha, katika hali isiyokuwa ya kawaida ukaguzi umebaini kwamba hesabu zote hizi hazikuwahi kufanyiwa usuluhishi wa kibenki tangu zilipoanza kupokea fedha za UVIKO 19 kinyume na kifungu nambari 105 (1) cha kanuni ya usimamizi wa fedha ya mwaka 2021.

Hata hivyo, ukaguzi haukuweza kupatiwa taarifa za kumbukumbu za Vitabu vya Fedha Taslimu (Cash Books) kwa ajili ya mapato hayo ya UVIKO 19 kwenye hesabu zote 4. Haya yote yalibainika kupitia vikao vilivyoitishwa na ukaguzi kujadili sababu na changamoto zilizowasilishwa kwa wakaguzi na Wizara ya Afya kwa upande mmoja na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa upande mwingine.

Aidha, ukaguzi umebaini Kukosekana kwa usimamizi mzuri wa hesabu za benki za UVIKO 19 na kupelekea kila Taasisi kuona haina jukumu la msingi la

kufanya usuluhisho wa kibenki na kupelekea Kukosekana kwa taarifa sahihi za mapato yanayokusanywa kupitia mfumo huo kwa pande zote mbili (Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha).

Kwa vile Mapato ya UVIKO 19 yako chini ya Wizara ya Afya na yanatakiwa kuwa kwenye bajeti yake ya mapato ya kipindi husika lakini kwa sababu ambazo ukaguzi haukuzielewa mapato hayo yaliamuliwa kukusanywa kupitia hesabu za benki za Ofisi ya Rais Fedha na Mipango (ORFM) ukiachilia mbali ukweli kwamba ORFM haikuwa na bajeti ya mapato hayo na wala sio chanzo chake cha mapato, hata hivyo ilitarajiwa Wizara ya Afya kuwa ndio msimamizi mkuu wa mapato yote yatokanayo na uchangiaji wa huduma za vipimo vya UVIKO 19 na baadae kuyahaulisha mapato hayo kuingia katika hesabu za UVIKO 19 zilizopo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa lengo la kuhifadhi kumbukumbu zote zinazohusiana na upokeaji wa mapato hayo jambo ambalo ukaguzi haukupatiwa usuluhishi wa kibenki uliofanyika.

Kwa upande wa Wizara ya Afya hakukuwa na sababu za msingi zilizopelekea kushindwa kutekeleza jukumu lake la kufanya usuluhishi wa kibenki kwa kipindi chote ambacho fedha za UVIKO 19 zilikuwa zinaingia kwenye Hesabu zake za Benki kabla ya kuhamishiwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, hata hivyo jukumu hili halikutekelezwa kwa mujibu wa miongozo na kanuni za fedha za mwaka 2021.

**Athari za kutofanyika kwa usuluhishi wa kibenki zinajumuisha zifuatazo: -**

- Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kutofahamu kwa uhakika mapato halisi yanayotokana na UVIKO 19 zaidi ya kutumia taarifa za “Bank Statement” pekee ambazo zinaweza kuwa na mapungufu makubwa.
- Serikali kupata hasara ikiwa kuna fedha ambazo hazikuingizwa kwenye hesabu za benki kwa sababu yoyote ile kama vile muamala kutokukamilika kwa sababu ya matatizo ya mtandao au sababu za kiufundi, kughushi stakabadhi za malipo, makato ya kibenki yasiyotambulika, n.k vitu ambavyo hubainika kupitia usuluhishi wa kibenki pekee.
- Kutumika kama mwanya wa kufanya ubadhirifu, wizi au matumizi mabaya ya fedha za Serikali kwa sababu ya udhaifu uliopo kwenye usimamizi wa mapato husika.
- Kwa kutokuwa na Cash Books za Mapato ya UVIKO 19 Serikali inakosa rejea (reference) ya kufanyia ulinganifu wa mapato yaliyokusanywa benki na kupelekea ugumu katika kazi za ukaguzi na kuinyima Serikali fursa ya kushauriwa ili kuboresha kazi zake.

Kwa kuzingatia athari na hatari zilizopo kupitia udhaifu huu uliobainika ukaguzi unashauri mambo yafuatayo: -

- Kwa kuwa bajeti ya mapato ya UVIKO 19 iko Wizara ya Afya na kwamba makusanyo yake yanatakiwa kuonekana sambamba na bajeti hii ni vyema mapato yote yatokanayo ya ulipiaji/ uchangiaji wa gharama za vipimo na chanjo za UVIKO 19 yakasimamiwa na Wizara ya Afya kwa 100% ikiwa in pamoja na hesabu za benki zinazotumika kupokea mapato husika ziwekwe chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya.
- Hesabu 2 za UVIKO 19 ambazo kwa sasa ziko chini ya ORFM ni vyema zikawekwa chini ya usimamizi na uangalizi wa Wizara ya Afya ili kurahisisha uendeshaji wa uwajibikaji kwenye hesabu hizi ikiwa ni pamoja na kuzifanyia usuluhishi wa kibenki.
- ORFM iendelee kubakia na jukumu la kusimamia rasilimali fedha za Serikali kwa ujumla wake kupitia njia mbalimbali kama vile kuomba ripoti za mara kwa mara za mapato, usuluhishi wa kibenki na utekelezaji kutoka Wizara ya Afya kwenye hesabu zote zilizopo chini ya Wizara ya Afya ili kuondoa mkanganyiko wa Wizara gani inafanya nini kwenye hesabu hizi.
- Wizara ya Afya na ORFM kila mmoja atengeneze "Cash Books" na kuingiza kumbukumbu zote za mapato halisi yaliyoingia kwenye hesabu husika za Wizara husika kulingana huduma za vipimo na chanjo za UVIKO 19 zilizotolewa na Serikali kupitia Zanz Medicals kwenye upimaji na Rahisi kwenye taarifa za chanjo za UVIKO 19 kuanzia mwezi Julai, 2021 mpaka sasa. Izingatiwe kwamba, "Cash Books" zinatakiwa kuandaliwa kutokana na stakabadhi za malipo ya huduma na sio kwa kutumia "Bank Statements", hivyo basi Wizara zinatakiwa zifanye mawasiliano na Benki ya PBZ ili kupata nakala zote za stakabadhi za malipo ya huduma za upimaji na chanjo za UVIKO 19 kwa kuwa Wizara ya Afya haina kumbukumbu kamili za stakabadhi hizo, kwa upande mwingine ziwasiliane na Kampuni ya Rahisi ili kupata taarifa za malipo ya huduma yaliyofanywa kwa kutumia Tigo Pesa na Visa/ Master Card ili kupata miamala yote iliyolipiwa kwa kipindi husika na kuiingiza kwenye Cash Book husika pia kabla ya kuanza usuluhishi wa Kibenki.
- Wizara ORFM ifanye usuluhishi wa kibenki kwenye hesabu zake za benki ili kubaini uhalisia wa mapato ya Serikali kwa kipindi cha Julai, 2021 mpaka sasa na kuendelea kwa mujibu ya Miongozo iliyopo.
- Wizara ya Afya ifanye usuluhishi wa kibenki kwenye sehabu zake za benki kuanzia mwezi wa Januari mpaka sasa na kuendelea kwa mujibu ya Miongozo iliyopo.
- Kwa kuwa mfumo wa UVIKO 19 unatumika pia kutunza kumbukumbu za mapato kwa kadri wateja wanavyolipia huduma, na kwa kuwa taarifa hizi huingizwa kwenye mfumo huu kwa kila muamala mmoja kwa mtu mmoja na huduma moja, lakini kwa kuwa fedha zinazohaulishwa kutoka Tigo Pesa na CRDB Bank kuingia kwenye Hesabu za Serikali zinaingizwa kwa mafungu (lumpsum) ya makusanyo ya kipindi fulani kama vile wiki nzima jambo ambalo linasababisha ugumu kwenye kufanya usuluhishi kwa kulinganisha taarifa za mapato zilizomo kwenye mfumo wa UVIKO 19 na zile zilizomo kwenye "Benki Statemnets" ukaguzi unaishauri

Wizara ya Afya kufanya uhaulishwaji wa fedha kutoka Tigo Pesa na CRDB Benki kwenda kwenye Hesabu za Benki za Serikali kwa kuzingatia mualamala mmoja mmoja kama ulivyopokelewa ili kuondoa tatizo hili linaloongeza ugumu kwenye usuluhishi wa kibenki.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Ni kweli Akaunti ya UVIKO -19 hazikufanyiwa usuluhisho kutokana na hesabu zote za miamala ya kibenki zinazopokea miamala ya UVIKO-19 kuwa chini ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

Wizara ilipokea barua yenye kumbukumbu namba AD.184/414/01/02/62 ya tarehe 31/12/2020 kutoka kwa Katibu Mkuu ORFM ya kuwajuilisha kuanzia tarehe 02/01/2021 kutakuwa na mabadiliko ya uingizwaji wa fedha zinazotokana na tozo ya upimaji wa UVIKO 19 na kuingizwa moja kwa moja ORFM kwenye hesabu namba "07489460001 yenye jina COVID-19 RESCUE FUND – TZS na hesabu namba 0748946002 yenye jina COVID-19 RESCUE FUND-USD". Kutokana na barua hiyo Wizara ilipelekea kupoteza uwezo wa usimamizi wa mapato ya UVIKO 19 kwa 100%, kama ilivyoshauriwa na CAG. Hata hivyo, Wizara ya Afya imewasilana na ORFM kwa barua ya tarehe 01/08/2023 yenye kumbukumbu namba CCA.127/107/01/ ili kupatiwa haki ya usimamizi kamili wa hesabu za mapato ya UVIKO 19.

Aidha baada ya mkutano uliofanyika (Julai 2022) baina ya Muhasibu mkuu wa Serikali na Mhasibu anaesimamia mapato ya UVIKO 19 wa Wizara ya Afya, kuanzia mwezi wa Julai 2022 Wizara ya Afya inafanya kazi kwa pamoja na ORFM katika kufanya usuluhishi (Reconsiliation 2022- 2023 na inaendelea) wa hesabu za mapato yanayotokana na UVIKO 19 kwa akaunti zote (TZS na USD).

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Taasisi ya mawasiliano ya Tigo na Benki ya CRDB imefanikiwa kupata vielelezo (benki statement na miamala ya Tigo pesa) vya kufanya usuluhishi kuanzia mwezi wa Julai 2022 na inaendela upata taarifa hizo hadi sasa. Wizara itaendelea na usuluhisho wa nyuma mara baada ya kupokea stakabadhi kutoka PBZ Benki.

Hivyo, Wizara ya Afya imezingatia ushauri wa CAG kwa kutengeneza "Cash Books" kwa huduma za Chanjo na kuingiza kumbukumbu zote za mapato halisi yaliyoingia kwenye hesabu kwa Wizara ya Afya. Aidha, kwa upande wa Zanz Medicals kwenye upimaji na Kampuni ya Rahisi zimetakiwa kutoa taarifa za malipo ya huduma yaliyofanywa kwa kutumia Tigo Pesa na Visa/ Master Card kwa kuwaandikia barua ya 01/08/2023 yenye kumbukumbu namba CCA.127/107/01/ ili kutupatia taarifa zote za mapato zinazotokana na huduma za vipimo vya UVIKO 19. Hii ni pamoja na kupewa uwezo kwa maofisa wa Wizara kuweza kuzifikia taarifa hizo kupitia mfumo. Jambo hilo

litakuwa ni sehemu ya mkataba namba 3 ili kuongeza ufanisi. Hata hivyo, Wizara ya Afya imefanya mawasiliano na Benki ya PBZ kwa kuwaandikia barua ya 01/08/2023 yenye kumbukumbu namba CCA.127/107/01/ ili kupata nakala zote za stakabadhi za malipo ya huduma za upimaji na chanjo za UVIKO 19 na kuweka kumbukumbu kamili za stakabadhi hizo.

Hili ni jukumu ambalo ORFM wamejulishwa kupitia barua ya kuwataka kukabidhi usimamiazi wa miamala yote ya UVIKO 19 kubaki chini ya dhamana ya Wizara ya Afya kama ilivyoshauria na CAG. Pia wamejulishwa umuhimu wa kufanya usuluhishi.

Katika kulitafutia ufumbuzi suala la uhaulishwaji wa fedha kwa mafungu (lumpsum) linalofanywa na Tigo pesa na Benki ya CRDB kwenda kwenye hesabu za benki za Serikali kila wiki. Wizara ya Afya imezitaka Taasisi hizi za fedha kuwasilisha taarifa za muamala mmjo mmoja kama zinavyopokelewa kwa 01/08/2023 yenye kumbukumbu namba CCA.127/107/01/ ili kuondoa tatizo hili linaloongeza ugumu kwenye usuluhishi wa kibenki.

VIELELEZO; (*Barua kutoka ORFM yenye kumbukumbu namba AD.184/414/01/02/62 ya tarehe 31/12/2020,* CCA.127/107/01/ CCA.127/107/01/*,* CCA.127/107/01/.*,* CCA.127/107/01/.)

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Wizara kudai kwamba hivi sasa usuluhishi wa kibenki unafanywa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango tangu tarehe 02/01/2021. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi ni kweli kwamba hakukuwa na usuluhishi wa kibenki uliokuwa ukifanywa na Wizara.

**Hoja nambari 8.7.1.4: Kutopatikana kwa nakala za stakabadhi za benki za malipo ya upimaji wa UVIKO 19**

Ukaguzi umebaini udhaifu mkubwa wa utunzaji wa kumbukumbu za stakabadhi za benki za malipo ndani ya Wizara ya Afya kiasi cha kutopatikana kwa stakabadhi zote za malipo ya huduma za UVIKO - 19 kuanzia Januari, 2021 mpaka Disemba 2021 kwa ajili ya ukaguzi. Hizi ni stakabadhi zinazoletwa na wateja kama ushahidi wa kuwa wamelipia huduma ili kupatiwa huduma husika, Wizara inatarajiwa kutunza nyaraka hizi kwenye mazingira safi na salama kwa kwa kipindi kisichozidi miaka 30 kwa mujibu wa sheria nambari 3 ya mwaka 2008.

Kukosekana kwa nyaraka hizo muhimu katika usimamizi wa fedha za umma kunaweza kuashiria uwepo wa rushwa, uvujifu wa mapato na matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kufanya tathmini ili kubaini chanzo halisi na ukubwa wa tatizo kulingana na udhaifu huu uliobainika katika utunzaji wa kumbukumbu hizo muhimu na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria. Pia, Wizara inashauriwa kuweka mikakati mahususi katika kuhakikisha kwamba udhaifu huu unadhibitiwa na kwamba haujirudii tena.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wakati upimaji wa UVIKO -19 ulipoanza shughuli za utoaji wa risiti zilikuwa zinatolewa na wafanyakazi ambao hawakuwa na taaluma za fedha na kukosa uelewa wa kuhifadhi nyaraka hizo kwenye mazingira safi na salama. Wizara itafanya jitihada za kufuatilia nakla za stakadhi hizi katika Benki husika na kuzihifadhi vizuri.

Wizara ya Afya imepokea shauri la kufanya tathmini kama ilivyoshauriwa na CAG na imeweka utekekelezaji wa kazi hii katika mpango wa bajeti 2023/24.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuchunguza majibu yaliyowasilishwa na Wizara, Kamati ya PAC ilitaka kujua kwanini mapato yaliyokuwa yakikusanywa yakahamishiwa Wizara ya Fedha na Mipango na kuelezwa kwamba awali mapato hayo yalikuwa kidogo lakini kutokana na kuongezeka kwake, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango iliamua mapato ya chanzo hicho kuingia katika hesabu yake kupitia barua nambari AD.184/414/01/02/62 ya tarehe 31/12/2020

Aidha, kupitia barua kumbukumbu na. CCA.127/107/01/ ya tarehe 01/08/2023 Wizara ya afya iliomba Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupatiwa haki ya kusimamia hesabu za mapato ya uviko -19 kama ilivyoshauriwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na barua hiyo kujibiwa tarehe 17/08/2023 na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwamba haina pingamizi na ombi hilo.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati**

Wizara iandae utaratibu mzuri utakaosaidia nyaraka za malipo zinahifadhiwa ipasavyo na zikihitajika ziweze kupatikana kwa wakati.

**Hoja nambari 8.7.1.5: Kutokuwepo kwa mkataba kati ya Wizara ya Afya na Kampuni ya Rahisi Solution Company kwa ajili ya utengenezaji wa Moduli ya Chanjo.**

Katika kuupitia mchakato wa utengenezaji wa nyogeza ya mfumo wa UVIKO 19 kwa ajili ya chanjo (Vaccination Module) ilibainika kuwa hakuna makubaliano rasmi baina ya Wizara ya Afya na mtoa huduma (M/S RAHISI SOLUTION COMPANY) katika utengenezaji na utumiaji wa moduli ya chanjo ya UVIKO 19. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016.

Kukosekana kwa makubaliano ya Mkataba kunaweza kukapelekea kutokuwekwa wazi kwa haki na wajibu wa kila upande, kutojua gharama zote za moduli hiyo zinazojumuisha utengenezaji na utekelezaji wake, kutofahamika utaratibu wa kufuatwa katika upatikanaji wa msaada wa kiufundi (technical support) hususani wakati ambapo moduli hiyo itakapokabidhiwa Serikalini, wataalamu wa TEHAMA wa Wizara ya Afya na watumiaji wengine kutokupewa mafunzo toshelevu na endelevu ya namna ya kuitumia na kuisimamia moduli hii kiufanisi ni sehemu ya athari za kukosekana kwa mkataba.

Kwa kuzingatia mapungufu hayo yaliyobainika ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya ikishirikiana na mtoa huduma kuweka makubaliano ya maandishi kwa mujibu wa sheria na taratibu za manunuzi na kuhakikisha kwamba kuna uzingatiaji wa masilahi mapana ya Serikali kwenye matumizi endelevu ya Moduli ya chanjo ili kuleta tija, ufanisi na kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati na zinazokidhi mahitaji ya Wizara na wadau wengine muhimu kwenye sekta ya Afya.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Nikweli mkataba wa kwanza baina ya Wizara ya Afya na kampuni ya Rahisi Salution haukuwa na moduli ya chajo ya UVIKO -19. Hata hivyo, mkataba huo ulifanyiwa marekebisho tarehe 02/08/2021 na kuongezwa moduli ya chanjo ya UVIKO - 19 kama ilivyoainishwa katika kielelezo hapo chini.

*Kielelezo:* “Addendum No. 1 Contract for Provision of System for Covid - 19 Booking for all Covid - 19 Test Center in Zanzibar.”

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Wizara imekiri kuwepo kwa changamoto hiyo na tayari imeshachukua juhudi ya kurekebisha kasoro zilizojitokeza, Kamati imeridhika na majibu ya Wizara na haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 8.7.1.6: Kutokuwepo kwa mkataba baina ya Wizara ya Afya na Hospitali ya Alrahmah katika kutoa huduma za UVIKO - 19**

Ukaguzi umebaini kuwa hakuna makubaliano yoyote yalipo kati ya Wizara ya Afya na Hospital ya Alrahmah katika utoaji wa huduma za UVIKO 19. Hali hii inapelekea kutofahamika kwa mipaka, wajibu na haki za Alrahmah dhidi ya Serikali kwa kuzingatia uwepo wa Zanz Medicals ambaye ameingia mkataba na Serikali na mipaka yake kufahamika ikiwa ni pamoja na wajibu na haki zake.

Kutokuwepo kwa makubaliano rasmi baina ya Serikali ya hospitali ya Alrahmah kunaweza kupelekea Serikali kupoteza mapato yanayotokana na upimaji wa UVIKO - 19 tofauti na Maabara binafsi nyengine zinazofanya kazi kama hiyo ambazo zinafahamika gharama na mgawanyo wa mapato ya Serikali pamoja na kupelekea wananchi kutozwa fedha nyingi ili kupata huduma hii kupitia Alrahmah kwani Wizara haifahamu hata gharama zinazotozwa.

Hivyo, ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuweka utaratibu mzuri katika kuratibu na kusimamia jambo hili ili lifanyike kwa kuzingatia maslahi mapana ya Serikali.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kwa mujibu wa uelewa wa Wizara ya Afya, Alrahama Hospitali sio sehemu ya ukusanyaji sampuli za UVIKO -19 kwa wasafiri, na hivyo kupelekea Wizara ya Afya kutokuwa na makubaliano yoyote na Hospitali hii juu ya uchukuaji wa sampuli za wasafiri kwa ajili ya upimaji wa UVIKO -19, japokuwa Wizara ya Afya inatambua kwamba Hospitali ya Alrahma inaendelea kutoa huduma za matibabu kwa washukiwa wa ugonjwa wa UVIKO 19 ikiwa ni pamoja na kuchukuwa sampuli za washukiwa hao kama sehemu ya matibabu. Hata hivyo kwa kutambua umuhimu wa hoja hii, Wizara ilifanya ufuatiliaji na kushindwa kuthibitisha bila shaka yoyote na hivyo kuwashirikisha kwa kuwaomba ZAECA kwa barua ya tarehe 11/04/2022 yenye kumbukumbu namba CAB.201/365/01 ili kufanya uchunguzi wa kiinteligensia ili Wizara iweze kuchukuwa hatua stahiki.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Wizara kukataa kufanyika kwa shughuli za ukusanyaji sampuli katika hospitali ya Alrahma. Hata hivyo, Kamati ya PAC umebaini kuwa hospitali ya Alrahmah inapima wasafiri vipimo vya Ukivo -19 na kujipatia kipato nje ya utaratibu na Wizara. Sambamba na hilo, Kamati imepata wasiwasi kwamba kuna uwezekano wa kuwepo kwa upendeleo hasa ukizingatia kuwa ruhusa ya kufanya kazi kama hiyo imetolewa kwa hospitali ya Global. Kufanya hivyo, kunatoa taswira mbaya na upotevu wa mapato ya Serikali.

Kadhalika, Kamati ya PAC haikuridhishwa na hatua iliyochukuliwa na Wizara ya kutofuatilia kwa karibu kadhia ya utoaji wa huduma za UVIKO - 19 uliokuwa ukifanywa kinyume na utaratibu na hospitali ya Alrahma.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inashauri Wizara ifanye juhudi za ziada za kufuatilia ZAECA suala la utoaji wa huduma za UVIKO - 19 uliokuwa ukifanywa kinyume na utaratibu na hospitali ya Alrahma.

**Hoja nambari 8.7.1.7: Kutokuwepo kwa mkataba baina ya Wizara ya Afya na ya Tasakhta Global Hospital katika kuchukua sampuli za wapimwaji**

Ukaguzi umebaini kuwa Wizara ya Afya haina makubaliano na Tasakhta Global Hospital katika ufanyaji kazi za UVIKO - 19 hali inayopelekea Serikali kushindwa kufahamu mazingira ya kazi, miongozo anayotumia, mipaka na wajibu wa Hospital ya Tasakhta Global Hospital katika utowaji wa huduma za UVIKO - 19 nchini. Udhaifu huu unaweza kusababisha Serikali kupoteza mapato kwa kushindwa kuelewa kiasi cha fedha inachotoza Hospital ya Global kwa watu wanaokwenda kupata huduma mbalimbali za UVIKO - 19, pia taarifa sahihi za UVIKO - 19 ambazo zinahitajika kwa Serikali kwa lengo la kuweka mikakati na mipango madhubuti zinaweza kupotea kutokana na kutoeleweka Hospital ya Global inavyokusanya na kutunza taarifa za UVIKO -19 kutoka kwenye jamii.

Hivyo, ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuchukuwa hatua za haraka za kuweka makubaliano (mkataba) kwa mujibu wa Sheria za nchi na Hospital ya Global katika kujihusisha na utoaji wa huduma za UVIKO - 19 na kwamba katika makubaliano hayo Wizara ihakikishe maslahi mapana ya Serikali yanazingatiwa muda wote.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara inakubaliana na hoja ya kutokuwepo kwa mkataba rasmi baina ya Wizara ya Afya na Hospitali Global juu ya ukusanyaji wa sampuli za UVIKO-19 kwa wasafiri. Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa hoja hii Wizara ilikutana na Uongozi wa Hospitali ya Global siku ya tarehe 10/06/2022 na kukubaliana kama ilivyoainishwa katika muhtasari wa kikao hicho.

Kutokana na kuzidiwa na wingi wa wasafiri wanaohitaji huduma hii, Wizara iliridhia ushiriki wa hospitali ya Global katika uchukuaji wa sampuli kwa wasafiri na kulikuwa na makubaliano ya uchukuaji wa sampuli kuzipeleka Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa uchunguzi ambayo majibu yake yalikuwa yanarudishwa Hospitali ya Global na kukabidhiwa kwa waliokuwa wamepima.

Kielelezo; (*Barua ya Wito wa kukutana na uongozi wa Hospitali ya Global yenye Kumb. Namba CCA.111/134/05 ya tarehe 07/06/2022 na Muhtasari wa kikao*).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Wizara na kubaini kwamba pamoja na kutokuwepo kwa Mkataba rasmi katika hatua za awali lakini Wizara ilikuwa na makubaliano ya uchukuaji sampuli za vipimo na hatimae kuziwasilisha sampuli hospitali ya Mnazi Mmoja kwa hatua za uchunguzi.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara iwe na utaratibu mzuri wa kuwa na makubaliano rasmi kuhusiana na shughuli za utoaji wa huduma za upimaji wa vipimo kwani kufanya hivyo kutapelekea kuiingizia mapato Serikali.

**Hoja nambari 8.7.1.8: Uwepo wa Vyeti vya UVIKO - 19 vya kughushi (Fake Certificates)**

Ukaguzi umebaini kuwa kuna vyeti vya kughushi ambavyo baadhi ya wananchi huvitumia ili kusafiri ikiwa ni kinyume na utaratibu. Vyeti hivi vimepatikana katika maeneo ya uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume kwa baadhi ya wasafiri wanapokwenda kwa ajili ya safari zao, hali hii imeanza kuwekwa bayana mara baada ya kuanza kutumia "Barcode/ QR Codes" kwenye vyeti vya UVIKO 19 kuanzia mwishoni mwa mwaka 2021, vyeti hivi vinavyotengenezwa kwenye mfumo wa UVIKO 19 ambapo wakati wa kusafiri vyeti vyote humulikwa (scaning) ili kuhakiki taarifa zake na ndipo baadhi hukutwa kwamba taarifa zinazosomeka kwenye cheti hazifanani na taarifa zinazoonekana kwenye "Bar Code/QR Codes". Kiambatisho Nambari 21 Kinahusika.

Jadweli lifuatalo linaonesha takribani vyeti 12 vyenye thamani isiyopungua shilingi 2,208,000 ndani ya muda wa chini ya mwezi mmoja, hali hii inatoa picha ya ukubwa wa tatizo ambalo linahitaji ufuatiliaji wa karibu na vyombo vya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na wadau wengine.

**Jadweli Nambari 36 : Baadhi ya taarifa za vyeti vya kughushi vilivyobainka na ukaguzi**

| Na. | Jina | Uraia | Nambari ya Cheti | Namba ya Kitambulisho cha Maabara | Tarehe ya Kupima | Tarehe ya Kupata Cheti | Kiwango cha fedha Kilichopotea (Tzs) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Abigall Isabella Craven | Afrika Kusini | ZCC20211231160275 | 12300836 | 30 Disemba | 31 Disemba | 184,000 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2021 | 2021 | |
| 2. | Akintomiwale Boluwatife Awodumila | Nigeria | ZCC202201059449 | 0401MGG0789 | 4 Januari 2022 | 5 Januari 2022 | 184,000 |
| 3. | Matt Feiertag | Afrika Kusini | ZCC2022011232424 | 1001MG0600 | 11 Januari 2022 | 11 Januari 2022 | 184,000 |
| 4. | Seiran Seropian | Urusi | ZCC2022011222425 | 0601MGG0070 | 11 Januari 2022 | 12 Januari 2022 | 184,000 |
| 5. | James Feiertag | Afrika Kusini | ZCC2022011232425 | 1001MGG0601 | 11 Januari 2022 | 11 Januari 2022 | 184,000 |
| 6. | Jenna Nicole Feiertag | Afrika Kusini | ZCC2022111232423 | 1001MGG0599 | 11 Januari 2022 | 11 Januari 2022 | 184,000 |
| 7. | Ekaterina Linnik | Urusi | ZCC20220112224260 | 0601MGG0070 | 11 Januari 2022 | 12 Januari 2022 | 184,000 |
| 8. | Kastytis Naslenas | Lithuania | ZCC202201116533 | ZM/F-4973 | 11 Januari 2022 | 12 Januari 2022 | 184,000 |
| 9. | Breedt Herman Van derberg | Afrika Kusini | ZCC202126126814 | 11100223 | 12 Januari 2022 | 12 Januari 2022 | 184,000 |
| 10 | Katarzyna Paulina Karczewska | Poland | ZCC202201021243 | Nil | 15 Januari 2022 | 15 Januari 2022 | 184,000 |
| 11 | Kacper Maksymilian Warchol | Poland | ZCC202201021243 | Nil | 15 Januari 2022 | 15 Januari 2022 | 184,000 |
| 12 | M.Sosnin Alexander | Nil | Nil | Nil | Nil | Nil | 184,000 |
| **Jumla ya fedha ambazo hazikukusanywa** | | | | | | | **2, 208,000** |

Kuwepo kwa vyeti vya kughushi kunaharibu sifa za nchi katika udhibiti wa upimaji na usimamizi wa UVIKO - 19 katika uwanja wa kimataifa na kupelekea kufifisha jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na janga la UVIKO - 19 Zanzibar. Pia inashiria udhaifu kwenye vyombo mbalimbali vya Serikali vyenye jukumu la kuzuia hali hii. Serikali kukosa mapato kwa kuwa uwepo wa vyeti feki unamaanisha kwamba wasafiri

hawa hawakufuata njia rasmi za kupima UVIKO 19 ambazo zingehakikisha kwamba wamelipia kihalali Serikalini na kupatiwa vyeti halisi. Kwa ujumala hali hii inaweza kusababisha madhara mbalimbali kiuchumi na kijamii katika ngazi ya Taifa.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama kufanya uchunguzi ili kuwabaini wote wanaohusika na utengezaji wa vyeti feki na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa Sheria.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara ya Afya ilitambua juu ya uwepo wa vyeti bandia (Fake Certificates) vya UVIKO - 19 katika Uwanjwa ndege wa AAKIA. Katika kukabiliana na tatizo hili Wizara ya Afya ilichukua hatua zifuatazo ikishirikiana na Taasisi za uchunguzi;

- Kuwaandikia ZAECA kuthibitisha kuwepo kwa jumla ya watu zaidi ya 200 kuwa na vyeti bandia ili wao waweze kuendelea na mchakato kupatikana kwa haki jinai. Mawasiliano hayo yalifanyika kwa barua ya tarehe 01/08/2023 yenye kumbukumbu namba CCA.127/107/01/
- Aidha, Wizara pia imechukua hatua ya kuwajulisha wadau (ALPHA CARE na Zanz Medicals) ambao ndio watekelezaji wa huduma hii katika eneo husika. Wizara ya Afya iliwataka kufanya ukaguzi pamoja na kuchukuwa hatua stahiki kama ilivyoainishwa kwa barua ya tarehe 01/04/2022 yenye kumbukumbu namba CCA.111/134/04.
- Kupeleka barua kwa Naibu Mkurugenzi wa upelelezi wa makosa ya jinai ya tarehe kumbukumbu namba CCA.111/134/04/84 ya tarehe 19/04/2022.
- Pia imeongeza mashirikiano na vyombo vya ulinzi na usalama ikiwemo jeshi la Polisi na kutoa taarifa kama inavyoonekana katika barua iliyotolewa na Wizara ya Afya.
- Uanzishwaji wa barcode ulikuwa ni jitihada za Wizara ya Afya kutatua tatizo la kughushi vyeti vya UVIKO-19 kwa wasafiri.

Vielelezo:

i. Barua iliyokwenda kwa DPP yenye kumbukumbu namba CCA.111/134/04/84 ya tarehe 19/04/2022 inayohusu utambuzi wa nyaraka.
ii. Barua ya kuwataka wadau wa usafiri kukagua kwa makini vyeti vya UVIKO-19. Zenye kumbukumbu namba CCA.111/134/04 ya tarehe 01/04/2022, zilizokwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji wa ALPHA CARE NA ZANZ MEDICS
iii. Barua kutoka ZAECA kuitaka Wizara ithibitishe majina ya wenye vyeti.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhishwa na jitihada ambazo Wizara imeanza kuzichukua katika ufuatiliaji wa kadhia hii. Hata hivyo, bado juhudi za ziada zinahitajika ili hatua za kisheria ziweze kutekelezeka kwa wale wote waliohusika.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaitaka Wizara kufuatilia ZAECA ili kupata mrejesho wa hatua zilizochukuliwa kwa watu wote wanaotuhumiwa kushiriki katika kutengeneza vyeti feki vya Uviko - 19.

**Hoja nambari 8.7.1.9: Wizara kushindwa kusimamia mfumo wa UVIKO - 19**

Kwa mujibu wa mkataba baina ya Wizara ya Afya na Kampuni ya Rahisi kifungu 4.0 kinachoelezea kuwa "mfumo ni mali ya Wizara kuanzia tarehe mfumo unapoanza kazi", lakini hadi sasa Wizara imeshindwa kuwa msimamizi mkuu wa mfumo katika matumizi yake na usimamizi wa ujumla ikiwa ni pamoja na kufanya maboresho na kutatua changamoto za mfumo huo kwa kadri unavyotumika na badala yake kazi hizi zinafanywa na kampuni ya Rahisi ambayo ni mtoa huduma.

**Athari zinazoweza kutokea kufuatia Wizara ya Afya kushindwa kuusimamia mfumo wa wa UVIKO 19 ipasavyo kama zifuatazo: -**

- Mabadiliko yoyote ya mfumo lazima aambiwe mtoa huduma kwa sababu maarifa yote ya mfumo anayo yeye pekee na kusababisha Serikali kumtegemea yeye kwa 100% kufanya mabadiliko yanayoweza kuhitajika muda wowote.
- Ukosefu wa nyaraka muhimu za usimamizi wa mfumo kwa kuwa Wizara haikushirikishwa kikamilifu katika kila hatua ya utengenezaji wa mfumo huu. Nyaraka ya madhumuni na faida za mradi (business case), nyaraka ya mahitaji ya mfumo, nyaraka ya vipengele vya mfumo vinavyotakiwa kujaribiwa (test cases), na ripoti ya majaribio ya utendaji kazi wa mfumo.
- Kukosekana kwa mpango wa matumizi endelevu ya mfumo hususani baada ya kumalizika kwa mkataba baina ya Wizara na kampuni ya Rahisi kwa sababu Wizara bado inaona haina jukumu la kuhakikisha mfumo unafanya kazi kwa miaka mingi ijayo kwa kuwa haijaumiliki na kuusimamia.
- Udhaifu katika utoaji wa ruhusa za kuufikia mfumo na usimamizi wa watumiaji wa mfumo.

Ukaguzi unaishauri uongozi wa Wizara kwa kushirikiana na mtoa huduma kuandaa mpango wa kuchukuwa umiliki na usimamizi wa mfumo mzima kama ilivyoelekezwa kwenye Mkataba ili kuhakikisha kwamba maslahi mapana ya Serikali yanalindwa muda wote na kwamba matumizi endelevu ya mfumo yanazingatiwa na unatumika katika namna inayohakikisha usalama na usiri wa taarifa zake zote zilizomo.

## Majibu ya uongozi wa Wizara

- Ni kweli Wizara inakiri uwepo wa mapungufu katika usimamizi wa mfumo wa UVIKO - 19 kutokana na upungufu wa miundombinu Rafiki ya TEHAMA ambayo inawezesha uwezo wa uwekaji wa mifumo hiyo hapa Wizarani, miundombinu yenyewe ni saver na umeme wa uhakika.

- Ili kuimarisha na kuboresha utendaji Wizara imeshawasilisha mapendekezo kwa Wakala wa miundombinu ya TEHAMA (ZICTIA) pamoja na wakala wa Serikali Mtandao (e-GAZ) ili kuweza kupata nafasi ya uwekwaji wa mfumo huo na kuwezesha kutoa huduma kwa wakati kama inavyotakiwa.
- Aidha Wizara ya Afya imefanikiwa kupata wataalamu wa TEHAMA (Developer) 12 ambao wataweza kusimamia mfumo huo baada ya kupata maelekezo kutoka kwa Kampuni ya Rahisi Solution.
- Wizara ya Afya imepokea saver 1 iliyopo ZICTIA ambayo inatumika kuhifadhia taarifa za magonjwa mbalimbali ikiwemo UVIKO 19.
- Mfumo wa UVIKO - 19 ni mfumo unaotumiwa na wateja wengi ndani na nje ya nchi na kwamba umakini mkubwa unatakiwa katika kuhakikisha kwamba unakuepo hewani kwa muda wa masaa 24. Kusimamia mfumo wa Uviko 19 kunahitaji kuwa na nyenzo na taaluma ya kuweza kutatua changamoto mbali mbali za wateja na kuhakikisha taarifa za wateja zinakua salama. Kutokana na kutopatikana fursa ya kuwajengea uwezo watendaji wa Wizara imekua ni vigumu kwa kuusimamia mfumo huo. Hata hivyo, Wizara tayari imeshafanya makubaliano na Rahisi Soulution ili kuwajengea uwezo watendaji wa Wizara ili wawe na uwezo stahiki wa kuusimamia mfumo huo (Mkataba no. 2 wa Rahisi Solution)

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Wizara kukubaliana na uwepo wa hoja ya Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kulikuwa na uzembe uliojitokeza kutokana na kutoyatekeleza matakwa ya Mkataba kuhusu kusimamiwa Mfumo huo na Wizara mara tu utakapoanza kufanya kazi. Sambamba na hilo, Kamati imeridhishwa na jitihada ambazo Wizara imezichukua katika kuifanyia kazi hoja hii.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara kwa kushirikiana na mtoa huduma ihakikishe inaandaa mpango wa kuchukuwa umiliki na usimamizi wa mfumo mzima kama ilivyoelekezwa kwenye Mkataba.

**Hoja nambari 8.7.1.10: Kutokuzingatiwa kwa ushauri wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu nambari L.D 615 VOL.XXV/31 ya tarehe 13 Mei, 2021 iliyotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali juu ya ushauri wa kisheria wa Rasimu ya Mkataba wa uwekaji wa mfumo UVIKO 19 Zanzibar ambapo alishauri mambo mbalimbali hata hivyo ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Afya haikuzingatia sehemu kubwa ya ushauri huo kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kiambatisho Nambari 22 Kinahusika.

Miongoni mwa athari zinazoweza kujitokeza kwa kutozingatizwa kwa ushauri wa kisheria kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kama zifuatazo: -

- Kutozingatiwa kwa maslahi mapana ya Serikali kwenye mkataba ulioandaliwa na Wizara kwa kukosa ushauri wa Kisheria kutoka chombo huru kilichobobea kwenye masuala ya Sheria ili kulinda maslahi mapana ya Serikali na kuhakikisha haki inatendeka kwa pande zote za Mkataba.
- Kukosekana kwa thamani ya fedha (Value for Money) kwenye mkataba kwa kutozwa fedha nyingi tofauti za bei za soko kwenye huduma/ bidhaa kama hii.
- Uwepo wa vipengele vya taarifa zenye utata kwenye Mkataba vinavyoweza kuisabibishia Serikali kupata hasara hususani panapotokea kutoelewana baina ya pande mbili za Mkataba na kulazimika kwenda Mahakamani kupata tafsiri sahihi.
- Kutozingatiwa kwa Sheria, Sera na Miongozo mbalimbali kwenye Manunuzi ya umma na kusababisha matatizo ya Kisheria katika utekelezaji wa mkataba husika.
- Kushindwa kudhibiti (control) na kuumiliki mfumo kwa kuwepo kwa kipengele cha "Software As Service – SAAS" ambacho kinaiondolea Wizara ya Afya haki ya kuumiliki.
- Uwezekano wa kubadilishiwa taarifa zilizomo ndani ya mfumo na mtu anayesimamia mfumo akiwa na ajenda zake binafsi na kusababisha uwepo wa taarifa zisizoakisi uhalisia wa hali ya mambo.

Hivyo ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuzingatia na kutekeleza yafuatayo:-

- Kwa kuzingatia manufaa ya ushauri wa Kisheria kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuwa Wizara haikuzingatia ushauri uliotolewa na Mwanasheri Mkuu ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kufanya mapitio ya Mkataba huu ili kubaini maeneo yanayoweza kufanyiwa marakebisho na kufanya marekebisho hayo kulingana na ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuleta tija na ufanisi kwenye mkataba huu.
- Wizara ifanye tathmini ya hasara iliyopata kwa kushindwa kuzingatia ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchukuwa hatua kwa mujibu wa Sheria kwa wote waliohusika katika kusababisha hasara hiyo.
- Wizara kufanya majadiliano mapya na mtoa huduma (re-negotiate) katika bei za Mfumo huu na umiliki wake ili kulinda maslahi mapana ya Serikali.

## Majibu ya uongozi wa Wizara

Wizara ya Afya imepokea ushauri uliotolewa na Ofisi yako na kwa kuzingatia hilo imefanya yafuatayo:

- Wizara imefanya majadiliano mapya na mtoa huduma ambayo yamepelekea kufanyika mapitio ya mkataba wa awali ambao ulionekana kuwa na mapungufu kama ilivyoainishwa na CAG. Mkataba huu mpya ulikamilika na kuanza kutumika tarehe 24/02/2022 ambao umepunguza malipo ya huduma za mfumo yanayoendana na gharama halisi ya utoaji wa huduma yenyewe ambapo mtoa huduma amelipwa USD 2.5 kutoka USD 4 kwa kila kipimo.

- Wizara ya Afya kwa sasa amekuwa mmiliki halali wa mfumo wa UVIKO - 19 kwa asilimia 100 kama matakwa ya mkataba wa awali ulivyobainisha.

Kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Ofisi ya CAG, Wizara ya Afya imeunda timu ya Wataalamu kwa ajili ya kufanya tathmini ya hasara iliyopata.

*Vielelezo;*

i. *Contract for the provision of system for COVID - 19 booking for all COVID - 19 test centers in Zanzibar wa tarehe 21/05/2021,*
ii. Addendum No. 1 of service contract for *provision of system for COVID - 19 booking for all COVID - 19 test centers in Zanzibar ya tarehe 02/08/202.*
iii. *Barua za uteuzi wa Wajumbe wa Timu ya Tathmini.*

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba ni kweli Wizara haikufuata ushauri kuotka wOfisi ya Mwanasheria Mkuu. Hata hivi, Kamati ya PAC imeridhika na hoja ya Mdhibiti na kuisisitiza Wizara kuwa na utaratibu wa kuufanyia kazi ushauri unaotolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sambamba na hilo Kamati ya PAC ilitaka ipatiwe ripoti ya Tathmini ya Wajumbe walioteuliwa ili kujua hasara ambazo zimetokea lakini haikupatiwa.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ya Afya ihakikishe inaipatia Kamati Ripoti ya Tathmini iliyotokana na timu ya Tathmini iliyoundwa.

**Hoja nambari 8.7.1.11: Uingizwaji wa taarifa zisizo sahihi kwenye mfumo wa UVIKO 19.**

Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya taarifa zinazoingizwa katika mfumo hazina uhalisia. Hii inatokea pale ambapo mtu wa kwanza anayechukuwa taarifa za wateja (Daktari au Muuguzi) anaandika kwenye fomu maalum ambayo imendaliwa kwa kazi hiyo, lakini mtu huyu kuamua kujaza baadhi tu ya taarifa na kuacha wazi sehemu za taarifa nyengine ambazo ni za muhimu. Inapokuja kwa mtu anayeingiza taarifa hizi kwenye mfumo ambao unalazimisha taarifa zote za muhimu kuingizwa kwenye mfumo hata taarifa ambazo hazikujazwa kwenye fomu muingiza taarifa huyu hujaza kwa kukisia tu anachokiona yeye kinafaa.

Miongoni mwa taarifa zinazojazwa kwa kukisia ni pamoja na Dalili za mgojwa kwa wale ambao ni washukiwa (suspects), Umri, Makazi n.k, muingiza taarifa hufanya hivyo ili aweze kuendelea na hatua inayofuata katika mfumo. Vile vile ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya fomu zilizojazwa zimeandikwa katika namna ambayo inawapa ugumu waingiza taarifa kwenye mfumo kuelewa kilichoandikwa na kupelekea kuandika kwa kubahatisha tu ili aweze kumaliza kazi yake.

Aidha, ukaguzi umebaini kukosekana kwa umakini kwa wanaoingiza taarifa za wanaopimwa UVIKO 19 kupitia vituo mbali mbali kwenye mfumo kuwa miongoni mwa chanzo cha taarifa ambazo sio sahihi zilizomo kwenye mfumo. Kukosekana kwa umakini na kutozingatia athari zinazoweza kujitokeza katika hili kumepelekea kutotegemewa kwa taarifa za jinsia, umri, majina, picha, nambari ya nyumba n.k. Mfano, mtu mwanye jinsia 'ke', hujikuta amapewa majina ya jinsia 'me' na kinyume chake, picha ya jinsia 'me' hupewa majina ya jinsia 'ke', nambari za nyumba huingizwa sizo kwa mfano 1234, nambari ya hati ya kusafiria na mwaka wa kuzaliwa pia huandikwa ili kujaza nafasi iliyowazi. Mchanganuo wa dosari hizo ni kama zinavyoonekana katika Kielelezo A, B, C na D.

Hali hiyo inaweza kupelekea athari zifuatazo: -

- Kutoa vyeti vya chanjo vyenye taarifa zisizo sahihi jambo ambalo litapelekea kutumia gharama mara mbili ili kurekebisha taarifa na kutengeneza vyeti vyengine vyenye taarifa sahihi.
- Vile vile itapelekea kutojua namba za kundi "batch number" gani iliyosababisha madhara ikiwa kati ya waliyochanjwa wamepata athari zitokanazo na chanjo (side effects) kama taarifa za kundi zilizoingizwa sio sahihi.
- Kuipotosha Serikali na wadau wengine kitaifa na kimataifa kuhusiana na takwimu za uchanjwaji kwa kuangalia jinsia, umri, maeneo n.k (demographic data).
- Kudhoofisha utegemezi wa mfumo katika kupata taarifa mbali mbali zilizo sahihi na kwa wakati ili kurahisisha ufanyaji wa maamuzi yenye kuleta tija, mfano kutengeneza sera za kuhamasisha uchanjaji, kujua ni maeneo yapi yako nyuma katika uchanjaji, kujua makundi ya umri au jinsia na mwitikio wao katika uchanjaji.
- Kurudisha nyuma jitihada za Serikali za uwekezaji na kupata manufaa ya uwekezaji uliofanywa kwenye mifumo ya TEHAMA.

Aidha, ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia, na Watoto kuzingatia mambo yafuatayo:-

- Kuandaa mafunzo kwa kushirikiana na mtoa huduma wa mfumo na kuwafundisha waingizaji wa taarifa kwenye mfumo (data entries) yatakayowajengea uwezo wa kujua umuhimu wa taarifa wanazoziingiza na athari zake ikiwa taarifa hizo hazitaingizwa kwa usahihi katika mfumo.
- Kuelimisha na kuhamasisha umma kufahamu umuhimu wa kutoa taarifa sahihi kwa ajili ya chanjo ya UVIKO -19 kwa kutumia njia zitakazowafikia makundi mbali mbali.
- Kuweka udhibiti wa utumiaji wa mfumo (application control) utakaohakikisha usahihi wa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo, mfano taarifa ziingizwe na mtu mmoja (data entry) na zikaguliwe na mtu mwengine (reviewer) ili kuhakikisha ubora na ukamilifu wa taarifa hizo kulingana na matakwa yaliyopo kabla ya kukamilika kwa zoezi hilo.
- Kuweka utaratibu utakaowezesha watu kufanya usajili binafsi na kuweka nafasi (self- registration and booking) kielekitroniki kabla ya kwenda kwenye

kituo kuchanja jambo hili litasaidia kuingiza taarifa sahihi na kwa wakati na kupunguza muda unaotukima kuingiza taarifa wakati mtu amekwisha chanjwa ambao pia unaongeza muda wa kusubiria vyeti n.k.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara ya Afya inakiri kuwepo kwa mapungufu ya ubora wa taarifa zinazokusanywa kwa wateja wa UVIKO 19 ambao ulichangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo kutopata mafunzo kwa watumiaji wa mfumo wa UVIKO 19, Vitendea kazi pamoja na uelewa mdogo wa umuhimu wa taarifa bora. Hata hivyo, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wadau imeweza kufundisha Watumishi 25 ngazi ya Taifa (Wizara). Watumishi 32 ngazi ya Vituo Unguja na Pemba ambapo Wizara ya Afya ilishirikiana na CHAI. Aidha, Wizara imefanya pia maboresho katika mfumo wa UVIKO 19 kwa kuongeza "Variable" ili kuakisi mahitaji katika kudhibiti mlipuko wa Ugonjwa wa UVIKO 19 Nchini.Hii ni pamoja na kutengeza "Regesters" ambazo zilisambazwa katika vituo ili kuboresha ubora wa taarifa zinazokusanywa.

Wizara ikishirikiana na wadau wa kitaifa na kimataifa iliweza kutoa elimu kwa kutumia njia mbali mbali ikiwemo ; kufanya vipindi vya redio na TV ambapo jumla ya programu 176 zimefanyika Unguja na Pemba. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na viongozi wa Dini na wale wa kijamii iliweza kuwafikia jumla ya Wanufaika 457 (Masheha, Viongozi wa Dini, Wawakilishi na Wabunge) ambao walipatiwa mafunzo ili kuilewesha jamii juu ya UVIKO 19 na namna ya utoaji taarifa.

Kutokana na kutambua umuhimu wa taarifa bora zinazokusanywa, pia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Rahisi waliweza kuweka "Quality Check" ambazo zilisaidia sana kupunguza makossa katika ujazaji wa taarifa za mteja katika mfumo. Aidha, Wizara kwa kutumia wataalamu wake waliopo ngazi ya Taifa walipitia taarifa zilizomo katika mfumo na pale linapobainika kosa, waliwasiliana na muhusika ngazi ya kutuo kwa ajili ya kufanya marekebisho

Kuweka udhibiti wa utumiaji wa mfumo (application control) utakaohakikisha usahihi wa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo, mfano taarifa ziingizwe na mtu mmoja (data entry) na zikaguliwe na mtu mwengine (reviewer) ili kuhakikisha ubora na ukamilifu wa taarifa hizo kulingana na matakwa yaliyopo kabla ya kukamilika kwa zoezi hilo.

Kwa upande wa kufanya usajili binafsi na kuweka nafasi (self- registration and booking) kielekitroniki kabla ya kwenda kwenye kituo kuchanja, jambo hili Wizara ililifanyia kazi na kwa sasa limetatuliwa na kwamba mteja anaweza kujisajili yeye mwenyewe au pale patakapobainika changamoto anasaidiwa na Watoa huduma linganifu na hali ilivyo.

Vielelezo; Ripoti ya mafunzo, Register Book.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Wizara kukubaliana na uwepo wa hoja ya Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kuwepo kwa uzembe na kutowajibika ipasavyo kwa baadhi ya wafanyakazi waliopewa dhamana ya usimamizi wa Mfumo wa Uviko 19 na kupelekea kuwepo kwa taarifa (takwimu) za udanganyifu katika mfumo huo wa Serikali yetu.

Hali hiyo inaweza kuisababishia Serikali kupanga mipango yake mbali mbali isiyoakisi uhalisia kupitia takwimu ambazo hazipo sahihi na jambo hili linaweza likapelekea kujikita katika maeneo ambayo kiuhalisia sio maeneo ambayo yanahitaji kutiliwa nguvu na badala yake kupunguza nguvu katika maeneo yanayohitaji kuwekewa nguvu katika masuala ya uwekezaji wa Serikali ili kuwatatulia wananchi changamoto zinazowakabili. Aidha, Kamati imeridhika na jitihada za Wizara katika kulitatua suala la taarifa zisizo sahihi kama ilivyoshauriwa na Mkaguzi.

**Hoja nambari 8.7.1.12: Ucheleweshwaji wa malipo kwa Kampuni ya RAHISI kinyume na makubaliano.**

Kwa mujibu wa Mkataba kifungu 3.0 (iii) kinachotaka malipo yalipwe kila mwezi na kwamba mtoa huduma atapeleka ankara siku ya 1 ya mwezi na Wizara italipa ankara ndani ya siku 14 baada ya kupokea Ankara. Hivyo, ukaguzi umebaini kuwa Wizara imeilipa kampuni ya Rahisi mwezi mmoja tu tangu mfumo uanze kufanya kazi mnamo tarehe 21 Mei, 2021 hadi ukaguzi unamalizika mwezi wa Disemba, 2021.

Hali hii inaweza kusababisha athari mbalimbali zikiwemo:-

- Kuzorotesha utoaji wa huduma unaofanywa na watoa huduma binafsi kwa kukosa nguvu za kifedha kutekeleza majukumu yao.
- Pia, mara kadhaa Serikali hushtakiwa na hata kupigwa faini vitu ambavyo vinaweza kuepukika ikiwa watumishi wa Serikali wenye jukumu la kuhakiki madai ya mtoa huduma na kuyaombea malipo watafanya kazi zao kwa uadilifu na uwajibikaji.
- Inaweza kuchochea rushwa inayopelekea huduma mbovu na kurudisha nyuma juhudi za Serikal katika kuleta maendeleo.
- Mtoa huduma kuongeza gharama za huduma (Mkataba) kwenye “tendering process” ili kufidia “time value for money” anayopoteza kwa kusubiria sana malipo yake na kupelekea thamani ya fedha zake kuwa ndogo kulinganisha na muda zilipokusudiwa kupokelewa.
- Kusitishiwa huduma ndani ya muda wa Mkataba kwa kuwa mtoa huduma hajalipwa na kupelekea usumbufu kwa jamii inayotumia huduma hizo.
- Serikali kukosa mapato.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kujipanga vyema na kuhakikisha kwamba madai ya watoa huduma wake yanafanyiwa kazi kwa wakati na kulipwa kwa mujibu wa makubaliano ya Mkataba, Sheria na Sera za nchi na kwamba maslahi ya Serikali ni muhimu yazingatiwe wakati wote.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara inatambua juu ya uwepo wa uchelewashaji wa malipo kwa kampuni ya RAHISI kinyume na makubaliano ya Mkataba. Hali hii ilichangiwa na ucheleweshwaji wa mapitio ya mkataba mpya baada ya kufikiwa kiwango cha mwisho cha makubaliano ya malipo katika mkataba wa awali. Aidha, kwa sasa tatizo hili tayari limeshatatuliwa.

Hata hivyo mdai aliwasilisha madai yenye makosa (error) ambapo ilichukua muda kuhakiki taarifa na pale Wizara ilivyojiridhisha iliiandikia Wizara ya Fedha kwa malipo. Katika kutatua changamoto hii Wizara imeshaweka Ofisa maalumu ambaye anasimamia na kuhakiki madai ya malipo ya Rahisi Solution na idadi halisi ya vipimo (Test) zinazostahiki kulipwa. Kwa sasa tatizo hili halitojitokeza tena.

Vielelezo; Barua kwenda Wizara ya Fedha.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Kamati ya PAC kubaini kuwepo kwa kasoro iliyobainishwa na Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati ya PAC imeridhika na majibu yaliyotolewa na Wizara hasa ukizingatia kwamba hatua ya kurekebisha kasoro hiyo imeshachukuliwa. Aidha, Kamati inaisisitiza Wizara kuhakikisha malipo yote yanafanywa ndani ya wakati na kwa usahihi wake kwa mujibu wa mkataba.

**Hoja nambari 8.7.1.13: Kutokuunganishwa kwa "Mobile App" ya "KoBoCollect" na Mfumo wa UVIKO 19.**

Mwa mujibu wa miongozo ya viwango bora vinavyokubalika (best practice guidelines) "system interoperability" ni miongoni mwa vigezo muhimu vya kuzingatia katika utengenezaji wa mfumo wowote, hii inamaanisha kwamba mfumo unaweza kuonana/kuunganishwa na mifumo mengine ili kurahisisha kubadilishana taarifa hali inayopunguza ulazima wa kuwa na mifumo mingi kwa wakati mmoja na kurahisisha upatikanaji wa taarifa zinazojitosheleza sehemu moja jambo linalofanya wepesi katika kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati.

Ukaguzi umebaini kuwa Wizara ya Afya (EOC) ilianza kutumia App ya Simu Janja (Mobile App) ijulikanayo kama KoBoCollect mnamo mwezi wa Disemba, 2021 katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya kuingiza taarifa za washukiwa (Suspects) wa UVIKO 19, pia kuna fomu ambayo hutumika kwa ajili ya kuingiza taarifa za wagonjwa wa uviko-19 aidha, imebainika App hii

haijaunganishwa na Mfumo mkuu wa UVIKO 19 ambao ndio wenye taarifa nyingi zaidi za hali ya UVIKO 19.

Hali hii inaashiria kwamba mpaka sasa taarifa za UVIKO 19 zimetawanyika ambapo baadhi ziko kwenye mfumo wa UVIKO 19, baadhi bado ziko kwenye makaratasi (fomu) maalumu za kuchukulia taarifa hizo na baadhi ziko kwenye hii App ya Simu Janja tofauti na matarajio ya Serikali na wadau wengine wa kitaifa na kimataifa kwamba taarifa zote za UVIKO 19 zinapatikana kwenye mfumo wa UVIKO 19.

Aidha, hali hii inaongeza ugumu wa kufanya maamuzi sahihi kwa wakati yanayohusu masuala mbalimbali ya UVIKO 19 ikiwa ni pamoja kutunga Sheria, Sera na miongozo ya usimamizi na uratibu wa UVIKO 19 pamoja na kutoa elimu kwa umma wa Wazanzibari kwa kukosa taarifa kamili sehemu moja na kwa wakati.

Hivyo Ukaguzi unashauri kuwa App ya KoBoCollect iunganishwe na mfumo wa UVIKO 19 taarifa zake kwa kuzingatia “format” ziende kwenye mfumo huu na zote zipatikane sehemu moja ili kurahisisha ufanyaji wa maamuzi kwa Serikali kama ilivyoelezewa hapo juu.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara inatambua kuwepo kwa mfumo wa App ya Kobo ambayo imekuwa ikitumika kukusanyia taarifa za jamii katika eneo la mama na mtoto. kwa kuwa App ya KoboCollect ina uwezo wa kukusanya taarifa “Offline”. Hivyo Wizara ya Afya iliamua kutumia Application hii pale ambapo kampuni ya RAHISI ilipoamua kusitisha huduma ya Internet. App hii ilitumika kwa muda wa mwezi mmoja mpaka pale huduma za internent ziliporejeshwa na Kampuni ya Rahisi. Aidha, Wizara iliweka utaratibu wa kuchukuwa taarifa hizo ambazo zilihamishiwa katika mfumo wa UVIKO 19 pale issue zilipotatuliwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli mifumo hiyo ilikuwa haijaunganishwa. Hata hivyo, Kamati imeridhishwa na juhudi ambazo Wizara imechukua hasa ukizingatia kwamba changamoto iliyobainishwa imeshatatuliwa lakini Kamati inaisisitiza Wizara kuhakikisha baadhi ya changamoto wazitatue wao wenyewe na ndani ya wakati ili kuleta ufanisi katika kazi.

### Hoja nambari 8.7.1.14: Uhaba wa matenki ya kuhifadhia maji safi na salama kwenye kituo cha kuchukulia sampuli cha Lumumba

Ukaguzi umebaini kuwa kituo cha kukusanya sampuli cha Lumumba hakina tenki la kuhifadhia maji safi yanayo hitajika sana kwa ajili ya kunawa mikono kama njia moja wapo ya kujikinga na maambukizi ya UVIKO 19, lakini pia

kutumika katika vyoo kwa ajili ya usafi. Hali hii inasababisha usumbufu mkubwa na kuhatarisha usalama wa kiafya kwa wahudumu wa Afya na wapimwaji hususani kipindi inapotokea hakuna maji ya mfereji jambo ambalo linaweza kutokea wakati wowote.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kununua matenki ya kuhifadhi maji safi na salama yenye ujazo mkubwa yasiyopungua mahitaji ya wiki nzima ya kituo na kuhakikisha maji haya yanafika maeneo yanapohitajika kwa ajili ya kunawa mikono (maji tiririka), na usafi wa vyoo.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Tatizo hili limeshatatuliwa, mnamo mwezi wa Novemba 2022 kazi ya kuweka matangi mawili ya maji pamoja na mashine ya kupadishia maji iliwekwa na tatizo la uwepo wa maji safi na salama kwenye kituo cha kuchukulia chanjo Lumumba limetatuliwa.

Kielelezo; *Ripoti ya kiufundi inayoonyesha kazi iliyofanyika na kukamilika kwake iliyotiwa saini baina ya mfadhili na wajenzi ya novemba 2022*

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imeridhika na jitihada zilizochukuliwa na Wizara kwa vile tayari matenki hayo yameshawekwa na yanafanya kazi ipasavyo. Hivyo Kamati haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 8.7.1.15: Maabara ya Mnazi Mmoja kutokuzingatia udhibiti wa ufikiaji (access control) kwenye komputa zinazotumika kuingiza taarifa za UVIKO 19 kwenye mfumo.**

Kwa mujibu wa Mwongozo Wa Kusimamia na Kuendesha Tovuti Za Serikali za eGovernment ya Tanzania katika kifungu 3.2 (ii) kinachowataka Maofisa wenye dhamana ya kusimamia Tovuti au kuweka taarifa kwanye Tovuti wawe na nywila (password) ambazo zinapaswa kubadilishwa angalau mara moja kwa kila mwezi".

Ukaguzi umebaini kuwa komputa zenye mifumo zinatumika bila ya kuwa na nywila (password) jambo ambalo linaweza kuhatarisha usalama wa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo. Hususani kama ikitokea mtu mwenye nia ovu akiingia kwenye komputa hizi na kukuta mfumo uko wazi anaweza kubadilisha, kufuta na kungiza taarifa zisizo sahihi kwenye mfumo.

Hivyo ukaguzi unashauri kuwa komputa zote ziwe na nywila (password) jambo ambalo litakalo weka usalama wa mfumo.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Nikweli hapo awali kompyuta zilikua hazina nywila kutokana na uhaba wa komputa na kusababisha watumiaji wengi kutumia komputa hizo kwa taarifa nyengine za maabara. Ongezeko la komputa na kutumika komputa maalum za UVIKO-19 kumewezesha kuwekwa nywila kwenye komputa hizo.

Vilevile wafanyakazi wote wa maabara ambao wamechaguliwa kupata ufikiaji wa taarifa katika mfumo (access control) wanatumia nywila (password) na haiwezekani kutumia nywila moja kwa watu wote. Aidha kutokana na kuhakikisha usalama wa taarifa, mfumo hauruhusu kutumika bila kuweka nywila kwa muhusika kwa kila wakati unapohitaji kutumia tena mfumo huo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Wizara. Aidha, Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha hoja kama hii ya kutobadilisha "password" haitokei tena kwani hili jambo linaweza likaonekana dogo ila athari yake inaweza kuigharimu Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kudukuliwa taarifa zake. Kwa mnasaba huo, Kamati haikuwa na maelezo zaidi.

**Hoja nambari 8.7.1.16: Kutokuwepo kwa mfumo wa 'Barcord' kwenye "Viral Transport Media (VTM)".**

Ukaguzi umebaini kuwa Maabara ya Taifa haina mfumo 'barcord' ambao ungetumika kwenye vibebeo vya sampuli vinavyojulikana kwa lugha ya kigeni kama 'Viral Transport Media (VTM)' kwa ajili ya kurahisisha zoezi la kuingiza taarifa za sampuli kwenye mashine ya kupima UVIKO 19 ambapo mtaalamu wa Maabara angepata taarifa zote kwa kumurika (scan) ile barcord iliyopo kwenye sampuli na kuingia kwenye kumbukumbu za mashine tayari kwa ajili ya kuanza upimaji, kinyume chake ni kwamba, mtaalamu wa Maabara huingiza taarifa sampuli kwa mikono (manually) moja baada ya nyingine, jambo hili linapelekea kuchukua muda mrefu zaidi na kuongeza hatari (risk) ya kufanya makosa ya kibinadamu (human errors) ambayo ni pamoja na kuingiza taarifa za sampuli zisizo sahihi.

Hivyo ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kupitia Maabara ya Taifa kuwa na mfumo 'barcord' ambao ungetumika kwenye vibebeo vya sampuli ili kurahisisha zoezi la kuingiza taarifa za sampuli kwenye mashine ya kupima UVIKO 19.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara imepokea ushauri uliotolewa katika ripoti hii ambao una lengo la kukuza ufanisi katika huduma za upimaji wa UVIKO - 19. Hata hivyo, utaratibu wa uwekaji wa Barcode katika VTM hufanyika katika hatua ya mwisho ya upimaji wa sampuli hizo na kwasasa huduma hii inafanywa na Mzabuni (ZANZ MEDICAL pamoja na ALPHA CARE) ambapo utaratibu huo wa kutumia barcode unafanyika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imeridhishwa na majibu ya Wizara kwa vile Wizara imefanikiwa kuufanyia kazi ipasavyo ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Hoja nambari 8.7.1.17: Upungufu wa vitendea kazi (computers) kwa watumiaji wa Mfumo (data entries).**

Kutokana na Mkataba kifungu 6.0 (ii) kinaitaka Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa vituo vyote vina vifaa vya kutosha. Hivyo ukaguzi umebaini kuwa watumiaji wa mfumo wa UVIKO 19 wanauhaba wa vifaa kama kompyuta zinazohitajika kwa ajili ya kuingizia taarifa za upimaji na majibu kwenye mfumo, wakati wa wimbi (wave) likiwa juu Maabara ilikua na waingiza taarifa 6 jambo ambalo kompyuta zilizokuwa zikitumika zilikua 2 pekee.

Hali hii ilichangia sana kucheleweshwa uingizaji wa taarifa hizi kwenye mfumo na hivyo kuchelesha upatikanaji wa majibu na taarifa sahihi kwa wakati kwa ajili ya kufanya maamuzi na kuchukua hatua stahiki za kupambana na janga la UVIKO 19. Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuweka vifaa vya kutosha katika vituo vyote vilivyopo Unguja na Pemba.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Ni kweli Wizara ilikuwa inakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi ikiwemo komputa. Kwa upande wa mahitaji ya vifaa hivyo yalikuwa kama yafuatayo:
Katika kukabiliana na changamoto hiii Wizara imefanikiwa kununua komputa ikiwemo; Desk top 8, laptop 13 na IPAD 31 na zimesambazwa maeneo mbalimbali kwa ajili ya kutoa huduma.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba ni kweli kasoro iliyoainishwa na Mkaguzi ilikuwepo. Hata hivyo, Kamati imeridhika na jitihada zilizochukuliwa na Wizara hasa ukizingatia vitendea kazi vya mifumo huo tayari vimeshapatikana.

**Hoja nambari 8.7.1.18: Vituo vya Afya kutokuwa na ufikiaji wa mfumo (system access) kwa ajili ya kuingiza taarifa za washukiwa.**

Ukaguzi umebaini kuwa miongoni mwa vituo vya Afya 35 ni kituo kimoja pekee cha Makunduchi ndicho kina ruhusa ya kuingiza taarifa za washukiwa wa UVIKO 19 moja kwa moja kwenye Mfumo wakati wa mahojiano (interview) na mshukiwa ambapo ni sawa na takribani asilimia 3 ya vituo vyote.

Kwa mfano, Kwa sasa Hospitali kama Mnazi Mmoja inayochukua sampuli na kupima UVIKO 19 kwa waliosamehewa na washukiwa ambao wanatokea katika Wodi na vitengo vingine mbalimbali kama 'Emergency' vyote havina uwezo wa kuingiza taarifa moja kwa moja kwenye Mfumo wa UVIKO 19 na badala yake wahusika wanachukua taarifa kwa kutumia fomu maalumu na kuandika kwa mikono (manually) na kuzipeleka kwa waingiza taarifa (data entries) ili ziingizwe kwenye mfumo.

Hali hii inachangia kwa sehemu kubwa kudhohofisha ubora na ucheleweshwaji wa taarifa sahihi za wagonjwa na washukiwa kwa wakati jambo ambalo linaathiri jitihada za mapambano dhidi ya UVIKO 19 hapa nchini kwa kushindwa kujua takwimu kamili za maambukizi na hali ya tatizo kwa wakati ili kuchukua hatua stahiki.

Ukaguzi uishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na mtoa huduma ya mfumo kutengeneza mpango kazi utakaoanzia na mambo yafuatayo:-

- Kuainisha maeneo yote ya Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na vituo vyote vinavyo chukua taarifa za wapimwaji ili kubaini wataalamu wa Afya kama vile madaktari, wataalamu wa Maabara na wengineo wanao hitaji ruhusa (access) ya mfumo wa UVIKO 19.
- Kuwapatia mafunzo hatua kwa hatua yatakayowawezesha kungiza taarifa sahihi kwa wakati.
- Kuwapa ruhusa ya kuingiza taarifa hizo kwa kuzingatia udhibiti (controls), usalama na ubora wa taarifa husika ili waweze kuingiza taaria hizo moja kwa moja (live data) wakati wakiwa na wapimwaji.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara ya Afya imefanya kazi ya kuainisha maeneo ya Mnazi mmoja pamoja na vituo vyote kubaini wataalamu wa afya kama ilivyoshauriwa na CAG na kuwatambua wale wote wanaohitaji ruhusa ya kuingia katika mfumo wa UVIKO 19.

Wizara imefanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa kwenye ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali kwa kuwapatia mafunzo wafanyakazi (32) wa sekta ya afya katika vituo mbalimbali Unguja na Pemba. Aidha Wizara imefanikiwa kuwapa ruhusa watumishi 15 ya kuingiza taarifa hizo kwa kuzingatia udhibiti (controls) na wengine 398 ambao tayari wamepata mafunzo wanasubiri kupatiwa ruhusa ya kuingia kwenye mfumo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC kwa kiasi kikubwa imeridhika na juhudi za Wizara katika kuhakikisha ushauri wa Mkaguzi unafanyiwa kazi.

**Maoni, Ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara uhakikishe wafanyakazi waliopatiwa mafunzo (398) wanapewa ruhusa ya kuingia katika Mfumo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa uahisi.

**Hoja nambari 8.7.1.19: Ucheleweshwaji wa vyeti vya chanjo ya UVIKO 19.**

Ukaguzi umebaini uwepo wa vituo 12 vilivyopo Pemba na 27 kwa upande wa Unguja vinavyotoa chanjo ya UVIKO 19, hata hivyo vituo vyote vinatumia fomu maalumu kuchukua taarifa za wachanjwaji kwa mkono (manually) kisha baada ya muda usiojulikana taarifa hizo huingizwa kwenye mfumo wa UVIKO 19 kupitia waingiza taarifa (Data entries) waliopo kwenye vitengo maalumu (data entry sections) kinyume na viwango bora vinavyokubalika (best practice) vya matumizi ya mifumo ya TEHAMA vinavyoelekeza uingizwaji wa taarifa kama hizi moja kwa moja kwenye mfumo wakati tukio linapotokea (live data entry).

Athari za ucheleweshwaji ya upatikanaji wa vyeti kwa wakati hili ni pamoja na usumbufu mkubwa kwa wananchi hususani kwa wale wanao hitaji vyeti kwa haraka ili kukidhi masharti ya kusafiri kwenda nchi za nje kwani pamoja na kuwa wameshakamilisha malipo ya vyeti hawawezi kupata vyeti kwa sababu taarifa zao mara nyingi zinakua hazijaingizwa kwenye mfumo. Ili kupata cheti cha chanjo kinachotengenezwa Wizarani pekee ni lazima aliyechanjwa asafiri kutoka aliko na kuja Wizarani kuwasilisha stakabadhi ya malipo ambayo itaingizwa kwenye mfumo na kisha kutengenezewa cheti, inapotokea taarifa zake hazijaingizwa kwenye mfumo maana yake ni kwamba hata taarifa za malipo haziwezi kuingizwa na hivyo basi hatopata cheti kwa wakati jambo ambalo linapelekea kuongezeka kwa gharama na muda kwa ajili ya kusafiri kuja kufuatilia vyeti Wizarani.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia, na Watoto mambo yafuatayo:-

- Kuweka utaratibu mzuri utakao hakikisha taarifa za wateja wake (Wananchi) zinaingizwa kwenye mfumo kabla au wakati wa kuchanja ili kwamba anapomaliza kuchanjwa taarifa zake ziwemo kwenye mfumo na awe tayari kuendelea na hatua nyingine bila kukwama kama vile kulipia huduma ya cheti na kupatiwa cheti chake bila kuchelewa.
- Wizara ifanye utaratibu wa kuziwezesha Hosipitali za Wilaya kuweza kupokea stakabadhi za malipo na kutoa vyeti ya chanjo ya UVIKO 19 ili kuwapunguzia gharama za usafiri na muda wananchi wanaokaa nje ya mji kwa kulazimika kwenda Wizarani (Mjini Unguja) kupeleka stakabadhi za malipo na kupatiwa vyeti vyao.
- Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba vituo vinavyo tumika kuingiza taarifa za chanjo kwa sasa vinapatiwa huduma ya mtandao (internet) bila kukoma ikiwa ni pamoja na kutenga bajeti na fedha kwa ajili ya huduma hiyo kulingana na mahitaji yaliyopo kwani pasipokua na mtandao uingizwaji wa taarifa kwenye mfumo pia unasimama jambo ambalo linakwamisha ufanisi wa Wizara katika kupata na kutunza taarifa za uchanjaji kielekitroniki kwa kutumia mfumo ulioigharimu Serikali pesa nyingi.
- Wizara ifanye maboresho au ihuwishe miongozo yake (Standard Operating Procedures –SOP) utaratibu unaojumuisha muda mfupi kwa kuzingatia mahitaji ya wasafiri kwenye kuchanja na kutoa vyeti vya chanjo mfano masaa 24 kila aliyechanja na kukamilisha malipo ya cheti apate cheti chake kwenye Hosipitali za Wilaya ama maeneo ya karibu zaidi na makazi yao.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Ni kweli awali kulikuwa na changamoto zilizozorotesha ushapishaji wa kadi za UVIKO-19 kama zifuatazo:

- kutokuwepo kwa vitendea kazi kama printer na wino.
- kutokuwepo kwa mkataba wa vaccine modules.

Wizara ya Afya imeandaa utaratibu ambao unahakikisha taarifa za wateja wake (Wananchi) zinaingizwa kwenye mfumo kabla ya kupata huduma ya uchanjaji jambo ambalo linarahisisha na kufanikisha hatua nyengine zinazofuata.

Wizara ya Afya imepokea pendekezo la kufanya utaratibu wa kuziwezesha Hosipitali za Wilaya kuweza kupokea stakabadhi za malipo na kutoa vyeti vya chanjo ya UVIKO 19 ili kuwapunguzia gharama za usafiri na muda wananchi wanaokaa nje ya mji kwa kulazimika kuja Wizarani (Mjini Unguja) kupeleka stakabadhi za malipo na kupatiwa vyeti vyao. Hata hivyo, kwakuwa jambo hili linahitaji rasilimali fedha, wataalamu wenye mafunzo na vitendea kazi, Wizara

inalifanyia kazi jambo hili lingalnifu na upatikanaji wa rasilimali kwani hadi sasa jumla ya maregister ….. yamechapishwa na watumishi 398 wamepatiwa mafunzo ya namna ya uchukuwaji wa taarifa na jinsi ya kujaza maregister ya chanjo ya UVIKO 19. Aidha hatua za ununuzi na usimikaji wa maprinter katika ofisi za Wilaya Wizara inalizingatia linganifu na upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka Serikalini ili kuanza utekelezaji.

Wizara inakubaliana na kufanya maboresho ya miongozo (Standard Operating Procedures - SOP) ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba cheti cha chanjo kinapatikana ndani ya masaa 24 pale mteja anapokamisha mahitaji yote ya huduma hii. Aidha upatikanaji wa huduma hii kwa Willaya itategemea na upatikanaji wa rasilimli fedha kama ilivyoainishwa katika majibu ya hapo juu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile kasoro hiyo imerekebishwa, Kamati ya PAC imeridhika na juhudi zilizochukuliwa na Wizara.

**Hoja nambari 8.7.1.20: Kutokuunganishwa kwa mfumo wa UVIKO - 19 na kanzi data za NIDA na benki ya PBZ.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba mfumo unakubali tarakimu zozote zinazoingizwa kwenye sehemu ya nambari ya risiti (receipt number) na nambari ya muamala (transaction number) kwa benki ya PBZ na vitambulisho vya NIDA.

Hali hii inaongeza mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali kwa kuwa hakuna udhibiti wa mfumo kwenye uingizaji wa namba sahihi za miamala na namba za stakabadhi zilizotoka Benki pekee jambo ambalo lingewezekana ikiwa pangekuwepo na kuunganishwa kwa mifumo hiyo miwili.

Ukaguzi unashauri Wizara Afya kushirikiana na Rahisi Solution Company, PBZ and NIDA ili kufanya uunganishwaji wa mfumo huu na kanzi data za NIDA na benki ya PBZ ili kuondosha mianya iliyopo ya upotevu mapato ya Serikali.

Kielelezo E: Kinaonesha kuwa namba ya NIDA sio sahihi imeingizwa kwenye mfumo.

Kielelezo F: Kinaonesha kuwa namba ya muamala na namba ya stakabadhi ni sawa hali ya kuwa hazikutakiwa kuwa sawa.

Kielelezo G: Kinaonesha kuwa nambari ya stakabadhi ya benki tayari imeshatumika lakini baada ya kuodosha sifuri ya mwanzo ya nambari ya stakabadhi imekubalika.

Kielelezo H: Kinaonesha kuwa mfumo unakubali tarakimu zozote licha ya kuwa si sahihi na hivyo kuonekana mwananchi ameshalipa.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kwa upande wa kuunganisha Mfumo wa UVIKO - 19 na kanzi data ya NIDA, Wizara imelipokea pendekezo hili baada ya ufuatiliaji imeonesha kwamba gharama kubwa inahitajika kufanikisha zoezi hili. Aidha, Kwa upande wa benki PBZ tayari limeshafanyiwa kazi tangu mwaka 2022 na kwa sasa watu hulipia kwa kutumia control number.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa ni kweli kulikuwa na kasoro ya kutounganishwa mfumo kulikosababishwa na udhibiti mbaya wa mfumo huo ambao umesababisha kupotea kwa fedha za Serikali.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati inaitaka Wizara kutoa ripoti inayoonesha kiasi cha fedha ambazo zimepotea kutokana na udhibiti mbovu wa mfumo huu.
2. Kwa vile kuna upotevu wa fedha za umma zimepotea, Kamati ya PAC inaitaka Wizara kuchukua hatua madhubuti kuwatafuta wote waliohusika na upotevu huo na kuwachukulia hatua za kisheria au kuwasilisha kadhia hiyo katika vyombo vya uchunguzi ili viweze kufuatilia na kuwabaini waliohusika.

**Hoja nambari 8.7.1.21: Udhaifu wa udhibiti wa kuingiza taarifa za malipo ya vipimo vya UVIKO 19 kwenye mfumo**

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Afya haina utaratibu mzuri wa kuingiza taarifa za malipo ya huduma za UVIKO 19 kwenye mfumo hususani kwa wateja wanaolipia kupitia kuweka fedha benki (bank deposits) ambao wanatakiwa kupeleka stakabadhi za malipo kwa watu walioruhusiwa kuingiza taarifa hizo kabla ya kupewa huduma. Hali ilivyo sasa ni kwamba kuna baadhi ya watu ambao sio wa kada ya uhasibu na wala sio watumishi wa Wizara ya Afya wanafanya kazi ya kuingiza taarifa za malipo kwenye mfumo wa UVIKO 19 na kuruhusu wateja kupewa huduma.

Hali hii inapunguza udhibiti wa mapato ya UVIKO 19 kwa Wizara ya Afya kwa kuwa Wizara imebakia kungojea kupewa taarifa za makusanyo yaliyopatikana pasipo Wizara yenyewe kushiriki ipasavyo ukusanyaji huo ili kuhakikisha kwamba mapato yanayoripotiwa Serikalini ni sahihi na halisi kwa mujibu wa huduma zilizotolewa. Mfano hai katika hili ni baadhi ya wafanyakazi wa Zanz Madicals wamepewa ruhusa ya kuingiza taarifa za malipo kwenye mfumo wa UVIKO 19 ambao kimsingi hawana dhamana ya kufanya kazi hii kwa upande wa Serikali.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuhakikisha inachukuwa jukumu la kuingiza taarifa zote za malipo ya huduma za UVIKO 19 kwenye mfumo wa UVIKO 19 na jukumu hili lipewe Idara ya Uhasibu wenye dhamana ya kazi hiyo ili kuweza kutumia taaluma zao kama inavyotarajiwa na kuwajibika pale wanapokwenda kinyume na Sheria, Sera na Miongozo kwenye jukumu hilo.

Aidha, watu wengine wote wasio kuwa kwenye Idara ya Uhasibu wa Wizara ya Afya watolewe ruhusa ya kuingiza taarifa za malipo ya huduma kwenye mfumo isipokuwa kwa viongozi wa Wizara wanaotakiwa kufahamu hali ya makusanyo ya fedha hizo wanaweza kupewa ruhusa ya kusoma pekee (read only access).

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara imepokea ushauri huu hata hivyo Wizara ya Afya imebinafsisha huduma hii ambapo mtoa huduma analazimika kuingiza taarifa zote zikiwemo za malipo na Wizara kwa kupitia Idara ya uhasibu wakiwa na jukumu la kufanya usuluhishi wa kila miamala inapofanyika.

Wizara imewaandikia benki ya PBZ barua yenye kumbukumbu namba AB.36/393/01 ya tarehe 10/05/2022 kuhusu suala hili na kuwataka kutoa maelezo juu kupokea fedha pungufu au kuingiza fedha pungufu za malipo ya UVIKO-19 ambazo ni kinyume na utaratibu wa malipo uliowekwa kisheria.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imeridhika na hatua zilizochukuliwa na Wizara na haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 8.7.1.22: Kutorejeshewa fedha kwa wakati kwa miamala iliyofanyika zaidi ya mara moja kupitia mtandao wa kibenki wa Visa/Master card wa benki ya CRDB**

Ukaguzi umebaini uwepo wa changamoto kwenye malipo yanayofanyika kupitia mtandao wa benki ya CRDB wa “Visa/ Master card”, changamoto hii hupelekea baadhi ya wateja kufanya malipo zaidi ya mara moja (double payments) kwa kuwa malipo ya awamu ya kwanza yanachelewa kuonekana

kwenye mtandao wa UVIKO 19 na kuzuia wateja kupewa huduma kwa wakati jambo ambalo hulazimisha wateja kufanya tena malipo kwa kuweka fedha benki (bank deposit) na kuwasilisha stakabadhi za malipo kwa watoa huduma ili kupewa huduma na kuweza kusafiri. Hali hii hupelekea migogoro na malalamiko kwa wateja kwenda kwa watoa huduma (Zanz Medicals) yanayotokana na kulipia huduma moja mara mbili kwa sababu wateja wanahitaji warejeshewe fedha zao za miamala ambayo wao walikatwa kwenye benki zao lakini miamala hiyo kuchelewa kuingia au kutoingia kwenye mfumo wa UVIKO 19 na kupelekea kuonekana kuwa hawajalipia huduma husika.

Ukaguzi unashauri yafuatayo:-

- Wizara ya Afya kuweka muwakilishi wake katika eneo la kufanyia vipimo vya UVIKO 19 atakayekuwa na mamlaka ya kusemea miamala yenye shida ili kwamba wateja wote wapeleke malalamiko yao kwa mtu huyu atakae yatolea ufafanuzi wakati wote bila kuathiri kazi za upimaji.
- Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Rahisi Solution Company na CRDB Bank kufanya tathmini ya utendaji kazi wa njia hii ya malipo ili kubaini chanzo cha changamoto hii ya kuipatia ufumbuzi wa kudumu.
- Kwa miamala inayokuwa imezuiliwa na benki ya mteja kwa sababu mbalimbali iwekewe utaratibu utakaoleta ujumbe kwa mteja kwamba muamala umezuiliwa kwa sababu “xyz” ili kupunguza malalamiko mengine ambayo hayana msingi.
- Wizara ya Afya kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi Solution Company kufanya tathmini ya miamala yote iliyolipia huduma moja zaidi ya mara moja na kuweka utaratibu wa kurejesha miamala hiyo kwa wahusika ili kulinda heshima ya Serikali kwa watalii na watanzania kwa ujumla.
- Miamala yote inayoshindwa kukamilika kwa sababu za mtandao pawekwe utaratibu kuibaini na kuirejesha miamala hiyo moja kwa moja (automatically) kila baada ya masaa 24, baada ya kujiridhisha kwamba huduma husika tayari zimeshalipiwa kwa njia nyengine kama vile kuweka fedha benki (bank deposit) n.k.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara ya Afya ilikuwa inafanya uhakiki wa malipo hayo ambao unafanyika mara mbili na baadae kupelekwa maombi ORFM kwa ajili ya malipo, ORFM wanajiridhisha na kufanya malipo husika. Hata hivyo, benki ya CRDB wanarejesha fedha hizo kwa wateja wao ndani ya siku 30.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Wizara kwa vile imefanikiwa kuufanyia kazi ushauri wa Mkaguzi. Hivyo, Kamati haikuwa na maelezo zaidi.

**Hoja nambari 8.7.1.23: Kukosekana kwa mpango wa kuendeleza biashara (Business Continuity Plan).**

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Afya na kampuni ya Rahisi hawana Mpango wa kuendeleza biashara baada ya maafa kinyume na Sera ya Wakala wa Serikali Mtandao kifungu cha 4.4.1.2.(d), ambapo Taasisi za Serikali zenye mifumo zinatakiwa kuanzisha mpango na miundombinu ya kuendeleza mfumo na taarifa zake zote baada ya maafa yoyote yanayoweza kujitokeza wakati wowote na kuathiri mifumo ya Taasisi.

Mpango huo unatarajiwa kuelezea hatua gani zitachukuliwa kabla ili kuweza kuzirudisha taarifa zote za mfumo yatakapotokea majanga kama udukuzi, majanga ya kimaubile au yanayosababishwa na binaadamu yatakayo haribu taarifa au miundombinu ya mfumo na kupelekea kupotea kwa taarifa hizo.

Kwa kuwa mfumo wa UVIKO 19 ni mali ya Wizara ya Afya na kwa kuwa mfumo huu unahudumiwa (hosting and administration) na kampuni ya Rahisi, ukaguzi unaishauri Wazara kuhakikisha kwamba inaandaa mpango wa kuendeleza biashara kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi na kuhakikisha kwamba Rahisi anapata nakala ya mpango huu ili kuwa tayari kuutumia mara yakitokea maafa kwenye chumba maalumu cha Seva katika kupunguza au kuepuka athari zinazoweza kujitokeza.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara tayari imeanza utaratibu wa kutayarisha mpango wa *Business Continuity Plan* wa Wizara. Mpango huo unatarajiwa kukamilika mwaka 2024.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC haijaridhishwa na kasi ndogo ya Wizara ya kuandaa mpango wa kuendeleza biashara “Business contuinity plan” jambo ambalo linaweza kupelekea kupoteza fedha za Serikali endapo janga lolote kwa mfumo litatokea. Hata hivyo, Wizara ilitaka kujua ni lini mpango huo umeanza kuandaliwa lakini haikupatiwa jibu lenye kutia moyo/matumaini yatakayoiwezesha Kamati kufanya tathmini kwamba ni kweli mwaka 2024 mpango utapatikana hasa ukizingatia ni muda mrefu umepita takriban miaka miwili tangu hoja hiyo kuainishwa na Mkaguzi lakini bado Mpango huo haujakamilika.

**Maoni, Ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ya Afya ihakikishe inaharakisha kukamilisha maandalizi ya Mpango wa Biashara ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi unaostahiki.

**Hoja nambari 8.7.1.24: Kukosekana kwa ushahidi wa kufanyiwa majaribio mfumo wa UVIKO 19.**

Kwa mujibu wa kifungu 2.1.6.1 cha mwongozo wa eGaz wa utengenezaji, upatikanaji, uendeshaji na utunzaji wa mifumo (eGAEXT/APA/005), Taasisi za umma zinatakiwa kufanya majaribio ya utendaji kazi wa mfumo na watumiaji wa mifumo hiyo ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mfumo unakidhi mahitaji ya mtumiaji.

Ukaguzi haukupata uthibitisho wowote wa kufanyiwa majaribio mfumo wa UVIKO 19 na watumiaji wa Wizara ya Afya kabla ya kuanza kutumika kukusanya, kuratibu na kusimamia taarifa za UVIKO 19 Zanzibar. Hali hii imepelekea uwepo wa maeneo yenye udhaifu katika mfumo ambayo yalitakiwa kubainika wakati wa kufanya majaribio ya mfumo, hili linajumuisha eneo la taarifa za washukiwa (suspects) ambalo halijakidhi mahitaji ya watumiaji wa mfumo. Kwa ujumla, kitendo cha mfumo kutokufanyiwa majaribio na watumiaji kunaweza kuwa na tafsiri mbalimbali ikiwemo, kutokuwa na mahitaji rasmi ya watumiaji wa mfumo ambayo ndio yanayojaribiwa kuhakikisha kwamba yamefanyiwa kazi kikamilifu na watengeneza mfumo, kutozingatiwa kwa miongozo ya kutengeneza mifumo n.k

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuzingatia Sera na Miongozo ya Wakala wa Serikali mtandao (eGaz) na Miongozo ya viwango bora vinavyokubalika katika utekelezaji na mifumo ya kielektroniki ili kuhakikisha kwamba mifumo hiyo inakidhi mahitaji ya watumiaji ya sasa na ya wakati ujao kulingana na maendeleo ya Teknologia ya TEHAMA ili kupunguza au kuondoa kabisa wingi wa maboresho yanayofanywa kwenye mfumo muda mfupi baada ya kuanza kutumika ambayo mara nyingi huwa na athari hasi zinazoweza kupunguza tija na ufanisi kwenye matumizi ya mfumo.

Kufanya majaribio ya mfumo mzima ili kubaini mapungufu yote yaliyopo sasa na kuyawasilisha kwa kampuni ya Rahisi ili yatatuliwe kwa pamoja kabla mfumo huu haujakabidhiwa Wizara ya Afya.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Nikweli mfumo haukufanyiwa majaribio wakati unaanzishwa kutokana na uharaka uliokuwepo kipindi hicho wa kurahisisha huduma za upimaji wa UVIKO-19.

Hata hivyo Wizara imekua inaendelea kufanya maboresho ya mfumo kwa kushirikiana na Kampuni ya Rahisi Solution ili kukidhi mahitaji ya watumiaji kadiri yanavyojitokeza.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa Wizara haikuwa na ushahidi wa kufanyiwa majaribio mfumo wa UVIKO 19 ulioandaliwa na kuendeshwa na kampuni ya Rahisi. Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC imesikitishwa na utekelezaji wa hoja hii kwa vile kutengenezewa Mfumo bila ya kufanyiwa majaribio kunapelekea kutumia mfumo ambao Wizara haitoweza kutambua kasoro zilizopo na vipi wataweza kupata njia ya kuzitatua iwapo kutajitokeza hitilafu yoyote. Aidha, ni kukiuka utaratibu na mwongozo wa uandaaji mifumo uliowekwa na e-Gaz.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha mifumo yote inayotengenezwa inafuata miongozo inayoandaliwa na e-GAZ na kama itatokea mifumo hiyo inahitajika kwa haraka, basi "best practice" ifuatwe baada ya kipindi cha haraka kumalizika.

**Hoja nambari 8.7.1.25: Mfumo kutotambua uhalali wa stakabadhi za benki za malipo ya UVIKO 19.**

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo unakubali tarakimu zozote zinazoingizwa sehemu ya namba ya stakabadhi (receipt number) na namba ya muamala (transaction number) ya benki ya PBZ. Baada ya kulipia huduma kupitia benki ya PBZ mteja anatakiwa kwenda kituoni na stakabadhi yake ili kuingizwa malipo hayo kwenye mfumo kabla ya kupewa huduma, mfumo hauna uwezo wa kutambuwa namba sahihi na halisi za stakabadhi za Malipo jambo linalo pelekea kukubali namba yoyote ile hata ambayo imekwishatumika na kuruhusu kuendelea na hatua inayofuata.

Udhaifu huu wa mfumo umekuwa ni miongoni mwa vyanzo vikuu vya uvujifu wa mapato ya Serikali kwa kutokuwa na udhibiti unaostahili na badala yake kutegemea uadilifu wa watu waliopewa ruhusa ya kuingiza taarifa za Malipo kwenye mfumo pekee.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi kufanya uunganishaji wa mfumo huu na kanzi data ya benki ya PBZ ili kuweka udhibiti wa namba za stakabadhi za malipo yote yaliyofanywa kupitia benki ya PBZ kuhakikisha kwamba mfumo unazigundua na kuzizuiya/kuzikataa stakabadhi ilizotumika na ambazo hazipo kwenye kanzidata ya PBZ.

Aidha, Wizara inashauriwa kuweka matumizi ya mfumo wa Zan Malipo unaotengeneza namba za ankala (Control Numbers) kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi na eGaz utakao unganishwa na mfumo wa UVIKO 19 ili kudhibiti mianya iliyopo kwa sasa na kuhakikisha kua unawekewa mkakati wa kuutekeleza kwa ufanisi na haraka.

Kielelezo l: Kinaonesha kuwa mfumo unakubali tarakimu zozote za stakabadhi za malipo za benki ya PBZ (bank deposit slip). *(mteja huyu hakulipa malipo lakini ziliandikwa nambari za kubuni na mfumo ukamtambua kama ameshalipa).*

**Majibu ya uongozi wa Kamati**

Kamati ya PAC imegundua kuwa ni kweli changamoto hiyo ilikuwepo wakati wa ukaguzi lakini kwa sasa mfumo huo umeunganishwa na mfumo wa malipo wa Benki ya PBZ na malipo yanafanyika kwa kutumia control number. Hivyo, Kamati imeridhika na majibu ya Wizara na haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 8.7.1.26: Udhaifu wa udhibiti wa uingizaji wa Malipo ya Vyeti vya Chanjo ya UVIKO 19**

Kulingana na udhibiti wa ndani ya Wizara ya Afya, malipo yote yaliyofanywa na wateja kupitia Benki yanatakiwa kuwasilishwa stakabadhi za malipo hayo Wizara ya Afya kwa ajili ya kuingizwa taarifa zake kwenye mfumo ili kutengenezewa cheti ambapo kwa sasa vyeti vyote hutengenezwa Wizarani pekee.

Katika kukagua eneo hili ukaguzi umebaini kwamba wapo baadhi ya wateja ambao wamekuwa wakienda Wizarani kupeleka stakabadhi za malipo ili ziingizwe kwenye mfumo kwa ajili ya kutengenezewa vyeti na kubainika kuwa stakabadhi hizo tayari zimekwisha ingizwa kwenye mfumo na watu wengine tofauti na waliopo Wizarani na kutakiwa kuendelea na hatua nyengine za kufuatilia vyeti kama inavyoonekana kwenye Kielelezo J, hii ina ashiria kwamba kuna watumiaji wengine zaidi ya wale waliopo Wizarani ambao wamepewa ruhusa ya kuingiza malipo ya vyeti kinyume na udhibiti wa ndani wa Wizara (internal control).

Hali hii inaondoa udhibiti wa mapato yatokanayo na vyeti vya chanjo ya UVIKO 19 na kuongeza mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali na kutengeneza mazingira ya rushwa kwani watu hawa wenye ruhusa ya kuingiza malipo wanaweza kuingiza malipo hewa kwenye mfumo kwa kua mfumo una udhaifu katika eneo hili kiasi cha kuruhusu nambari yoyote ile ya stakabadhi ya benki kutumika.

Ukaguzi unashauri yafuatayo:-

- Uongozi wa Wizara kwa kushirikiana na Kampuni ya Rahisi Solution kuhakikisha kuwa watumiaji wa mfumo wanaoingiza taarifa za malipo ya

vyeti vya chanjo za UVIKO 19 wanachujwa na kubakia wale wanaotambulika na wenye jukumu hilo kwa mujibu wa ajira zao Serikalini na kuwaondolea ruhusa wengine wote wasio stahili kufanya kazi hiyo.

- Wizara kuweka fomu maalum ya kuidhinisha watumiaji wa mfumo wa UVIKO 19 itakayo onesha majukumu ya kila mtu kwa kipindi husika ambayo itaidhinishwa na kiongozi wake wa kitengo au Idara ndani ya Wizara au taasisi yake kabla ya kuingizwa kwenye mfumo kama mtumiaji ili kuimarisha udhibiti wa watumiaji wa mfumo.
- Uongozi wa Wizara kuwaelimisha wanaoingiza taarifa za mapato juu ya athari za kughushi namba za stakabadhi za malipo za benki wakati wanaingiza taarifa hizo kwenye mfumo ikiwa ni pamoja na kufanya vitendo vya uhujumu wa uchumi, ubadhirifu wa fedha za Serikali pamoja na matumizi mabaya ya ofisi.
- Kuweka matumizi ya mfumo wa namba za bili (Control Number system) utakao unganishwa na mfumo wa UVIKO 19 ili kudhibiti mianya iliyopo kwa sasa na kuhakikisha kuwa mfumo unawekewa mkakati wa kutekeleza kwa ufanisi na haraka.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kweli kulikuwa na udhaifu wa udhibiti wa uingizwaji wa malipo ya vyeti vya chanjo ya UVIKO - 19. Kwasasa malipo yote yanafanyika kwa kutumia control number ambayo mteja analipa mwenyewe na kuleta risiti Wizarani kwa ajili ya kuchukuwa cheti chake. Wizara imepokea ushauri na kuufanyia kazi kwa kuwaondolea ruhusa waliokuwa hawahitajiki kuingia katika mfumo wa UVIKO 19.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Watendaji wa Wizara kukubaliana na hoja ya Mkaguzi na kurekebisha kasoro iliyokuwepo, lakini kwa vile kuna upotevu wa mapato ya Serikali uliosababishwa na uzembe wa kiutendaji wa baadhi ya wafanyakazi kwa kushindwa kudhibiti uingizwaji wa malipo ya vyeti vya chanjo ya UVIKO - 19 na kuisababishia Serikali kukosa mapato. Hivyo, Kamati ya PAC inaviomba vyombo vya utekelezaji au usimamizi wa sheria za nchi zifuatilie wale wote waliohusika ili wakithibitika hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaviomba vyomba vya uchunguzi na usimamizi wa Sheria ikiwemo ZAECA kufuatilia kwa karibu hoja hii na ikibaini kama kuna uzembe umetendeka, sheria ichukue mkondo wake.

**Hoja nambari 8.7.1.27: Udhaifu wa udhibiti wa msamaha wa upimaji UVIKO 19**

Ukaguzi ulibaini kwamba Wizara ya Afya inaudhaifu kwenye mchakato wa kutoa msamaha dhidi ya gharama za upimaji wa UVIKO 19 ambapo haijulikani vigezo rasmi vya kuzingatia ili kutolewa msamaha, utowaji na msamaha kufanywa na mtu mmoja badala ya kamati, kukosekana kwa azimio la Wizara la kutoa msamaha wa gharama za kupima UVIKO 19 kwa makundi mbalimbali ya watu.

Udhaifu huu umepelekea misamaha kutolewa kiholela Wizarani na kuikosesha Serikali mapato kwani baadhi ya waliopewa misamaha hii wanauwezo wa kulipia gharama husika. Aidha, udhaifu huu umepelekea manung'uniko kwa baadhi ya watumishi wanaonyimwa msamaha na kuathiri utendaji wa kazi.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kutengezea vigezo rasmi vitakavyotumika kutoa msamaha na kuviweka wazi kwa umma ili kila anayetimiza vigezo husika apatiwe msamaha husika. Pia, Wizara inashauriwa kwamba mchakato wa kutoa msamaha usifanywe na mtu mmoja badala yake iundwe kamati itakayokuwa na jukumu la kupitia maombi yote ya misamaha na kuyatolea maamuzi.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Ni kweli kulikuwa na udhaifu wa udhibiti wa msamaha wa upimaji. Kwa sasa tayari umeshatengenezwa muongozo rasmi ambao unaonesha vigezo vya nani anastahili kupatiwa msamaha wa upimaji wa UVIKO - 19 kama unavyoonekana katika kiambatanisho.

Kielelezo; (Muongozo *wa msamaha wa UVIKO -19.*)

**Uchuguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Wizara imekubaliana na hoja ya Mkaguzi na tayari imeshaufanyia kazi ushauri wa Mkaguzi, Kamati ya PAC haikuwa na maelezo zaidi kwani imebaini Wizara imeshaandaa muongozo huo ambapo watu wanaostahili kupewa msamaha ni kama ifuatavyo:-

- Wagonjwa wote wanaosafirishwa kwa ajili ya matibabu ni lazima matibabu ya muhusika yawe yamefadhiliwa na WAUJWJW pia ngudu anaeambatana na mgonjwa anahusika na msamaha huo.
- Wanafunzi wote wa kada za afya ambao ni wafanyakazi wa WAUJWJW na wanasoma nje ya nchi
- Wafanyakazi wa Wizara wanaosafiri nje ya nchi.

Aidha, Pamoja na sifa zilizotajwa hapo juu, muhusika atahitajika kuwasilisha barua maalum kutoka kwa Katibu Mkuu (WAUJWJW) kama uthibitisho wa kupatiwa vipimo hivyo.

**Hoja nambari 8.7.1.28: Kukosekana kwa muunganiko "Integration" baina ya Mfumo wa UVIKO 19 na Mfumo wa Vitambulisho vya Mzanzibari (Zan ID System).**

Katika ukaguzi uliofanyika ilibainika kuwa mfumo wa UVIKO 19 ulikua unatumika pasipo kuunganishwa na mfumo za vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi kwa kipindi kisichopungua miezi 10 ya mwaka 2021, jambo ambalo limechangia uingizwaji wa baadhi ya taarifa zisizo sahihi kwenye mfumo wa UVIKO 19.

Kwa kuwa kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi ni moja ya vitambulisho vilivyoenea zaidi miongoni mwa wazanzibari na kwa kua mfumo wa UVIKO 19 unahitaji utambulisho halisi wa anayepimwa au anayechanjwa na kwa kuzingatia ukweli kwamba moja ya malengo ya kuanzisha mfumo huu wa UVIKO 19 ni pamoja na kukusanya taarifa sahihi zinazohusu UVIKO 19 kwa wakati ili kurahisisha ufanyaji wa maamuzi sahihi na kwa haraka katika kukabiliana na janga hili, aidha ilitarajiwa uunganishwaji wa mifumo hii miwili iwe ni miongoni mwa vipaumbele katika utekelezaji wa mfumo wa UVIKO 19 kwani taarifa zao zote muhimu zinazohitajika kwenye mfumo wa UVIKO 19 zinapatikana kwenye mfumo wa Zan ID ukiachilia mbali kwa watu wachache ambao taarifa zao hazijakuwemo.

Hata hivyo mnamo mwezi wa Januari 2022, ukaguzi ulipata taarifa kutoka kwa uongozi wa Wizara ya Afya kwamba uunganishwaji wa mifumo hii miwili umefanyika kikamilifu ambapo katika kujiridhisha ukaguzi uligundua kwamba uwepo wa udhaifu kwenye mfumo katika hatua ya kuchagua kama mteja ana kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi au hana, na kama anacho kitambulisho bado mfumo ulikuwa unaruhusu kuingiza taarifa kwa mkono, mwanya huu umekuwa chanzo kikuu cha kuingiza taarifa tofauti na zilizopo kwenye mfumo wa Zan ID.

Uingizwaji wa taarifa zisizo sahihi kwenye mfumo wa UVIKO 19 unaashiria mambo mbalimbali yakiwemo yafuatayo:-

- Watumiaji wa mfumo kutopewa mafunzo ya mfumo kulingana na maboresho yaliyofanywa ikiwemo "integration" jambo ambalo hupelekea watumiaji kuutumia mfumo kama ilivyokua awali kabla ya kuunganishwa na kupelekea kufanya makosa mbalimbali.
- Mfumo kutokua na udhibiti toshelevu (insufficient controls) kulingana na mazingira yanayotumika hususani pale mteja anapokua na kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi, mfumo ulitakiwa usitoe mwanya

wa muingiza taarifa kuandika taarifa za mteja huyu badala yake taarifa zote zipatikane kutoka kwenye mfumo wa Zan ID ambao tayari umekwisha unganishwa na mfumo wa UVIKO 19. Kielelezo K Kinahusika.

- Kutokuonekana bayana kwa manufaa ya kazi kubwa iliyofanywa ya kuiunganisha mifumo hii miwili kwani lengo la kuhakikisha zinapatikana taarifa sahihi na kwa haraka kutoka kwenye kanzi data ya Zan ID bado halijafikiwa jambo ambalo pia linapunguza morali ya kazi kwa wafanyakazi, kupunguza utegemezi wa TEHAMA kwenye kurahisisha kazi na kuleta tija na ufanisi wa kuwahudumia wananchi.

**Ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi Solution kufanya yafuatayo:-**

- Kuandaa mpango kazi wa mafunzo kwa watumiaji wote wa mfumo na kutoa mafunzo yatakayo kuwa endelevu ili kukabiliana na mabadiliko mbali mbali yakiwemo ya mfumo au watumiaji wa mfumo angalau mara moja moja kila yanapotokea mabadiliko husika.
- Kuongeza udhibiti kwenye mfumo utakao hakikisha kwamba ikiwa kitambulisho kilichochaguliwa kutumika ni Zan ID basi mfumo usiruhusu uingizwaji wa taarifa kwa kuandika badala yake taarifa zote zipatikane kutoka kwenye kanzi data ya Zan ID. Utaratibu kama huu uzingatiwe pindi mfumo huu utakapounganishwa na kanzi data nyengine kama vile NIDA.
- Ikiwa mteja atakua na kitambulisho cha Zan ID ambacho taarifa zake hazijaonekana kwenye kanzi data ya Zan ID na kupelekea kutotambulika kwa kitambulisho chake au ikiwa hana kabisa kitambulisho cha Zan ID wala chengine chochote kile basi pawepo na mbadala 'Others' kwenye aina ya kitambulisho utakao toa ruhusa kwa muingiza taarifa kuweza kuingiza taarifa za mteja huyo kwa kuandika mpaka mwisho.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Tangu kuanza kwa huduma ya chanjo ya UVIKO - 19, mfumo wa ZAN ID uliunganishwa na mfumo wa UVIKO - 19, huku kukionekana kuwepo kwa kutofanya kazi ipasavyo (disfunctionality) ya mfumo ambapo baadhi ya vitambulisho vilikataa kuvuta taarifa hata kama namba ya kitambulisho ni sahihi. Hata hivyo, bado kuna changamoto ndogo ndogo na zinaendelea kufanyiwa kazi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa pamoja na mfumo wa Uviko – 19 kuunganishwa na mfumo wa vitambulisho lakini Mkaguzi amebaini kutooana kwa mifumo hiyo miwili jambo ambalo lilimwezesha kusema kwamba mifumo hiyo haijaunganishwa kwani ingelikuwa imeunganishwa taarifa zao zingekuwa zinaonana. Kamati pia imegundua kwamba sababu iliyosababisha kujitokeza kwa kasoro hii imesababishwa na Wizara kushindwa kuufanyia majaribio mfumo huo wa Uviko - 19 wakati wa uandaaji wake pamoja na kuufanyia "updates" kila baada ya muda.

Sambamba na hilo, Kamati ilitaka kujua ni kasoro gani ndogo ndogo zinazoukabili muunganiko huo na kuelezwa kwamba kuna baadhi ya watu wamebadilishwa jinsia ambapo mwanamke alikuwa akionekana kuwa mwanamme isipokuwa hivi sasa wamerekebisha kasoro hiyo.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inaishauri Wizara kuhakikisha inauendeleza mfumo huo ili kuweza kusomeka na mfumo wa vitambulisho na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za wanaopewa huduma.
2. Wizara ijikite katika utoaji wa mafunzo ya mara kwa mara kwa watendaji wa TEHAMA ili kuwawezesha kufanyakazi kwa ufanisi kwa maslahi ya Wizara na Serikali kwa ujumla.

### 8.7.2 Dosari zilizobainika katika kampuni ya Zanz Medical

Kwa kuzingatia mkataba wa upimaji wa UVIKO 19 kwa wasafiri ulioingiwa kati ya Wizara ya Afya na Kampuni ya Zanz Medicals kinyume na Sheria, Sera, Miongozo na taratibu zilizopo. Ukaguzi ulipitia majibu, majukumu na haki za kampuni ya Zanz Medicals ambapo mambo mbali mbali yalibainika kama ifuatavyo:-

**Hoja nambari 8.7.2.1: Kutokuendelea na upimaji kwa wasafiri waliopimwa mwanzo na kubainika kuwa na maambukizi ya UVIKO 19**

Kwa mujibu wa mkataba baina ya Wizara ya Afya na kampuni ya Zanz Medicals "Appendix A" kifungu cha 2(d) kinachosema "wasafiri waliopatikana na virusi wanapaswa kupimwa bila malipo hadi watakapothibitishwa kuwa hawana maambukizi". Hata hivyo ukaguzi ulibaini kwamba wasafiri wote wasiosamehewa wanalipia huduma ya kupima UVIKO 19 na baada ya kupimwa wanapobainika kuwa na maambukizi utaratibu unawataka kuahirisha safari na kurejea tena kupimwa baada ya siku saba (7) hata hivyo upimwaji huu haufanywi tena na Zan Medicals badala yake umehamishiwa

kwenye Maabara ya Mnazi Mmoja kinyume na matakwa ya mkataba uliopo baina ya Wizara na Zanz Medicals.

Ukaguzi unashauri kwamba Wizara ya Afya isimamie matakwa ya mkataba uliopo na kuhakikisha kwamba Zanz Medicals anatimiza wajibu wake kama ilivyoainishwa kwenye mkataba huu na kwamba wasafiri wote wanaolipia huduma ya upimaji wanapimwa na Zanz Medicals mpaka wanapokuwa tayari kusafiri kwa mujibu wa miongozo ya Afya kwenye UVIKO 19 na sio kuwahamishia kwenye Maabara ya Serikali huku wakikwepa jukumu lao la msingi.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wasafiri waliokutikana na maambukizi ya UVIKO 19 walikuwa wanapatiwa huduma za matibabu na Wizara ya Afya kama wagonjwa wengine na walikuwa wanatakiwa wajitenge katika hoteli maalum kwa ajili ya kufuatiliwa, hivyo upimaji wa marudio kwa wahusika ulikuwa unafanywa na Wizara kupitia hospitali ya Mnazi Mmoja. Aidha, Wizara pia ilimtaka Zanz Medics kufanya vipimo vya marudio kwa wasafiri waliokutwa na maambukizi na walikubali kufanya hivyo na utaratibu huo unaendelea mpaka sasa.

**Ushauri wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa kweli vifungu vya mkataba havikufuatwa ipasavyo, hilo lilifanywa na Wizara ili kuwanusuru wasafiri hao wasiweze kulipishwa na Kampuni kila wanapohitajika ili kuwapunguzia gharama za upimaji. Kamati imeridhika na majibu ya Wizara hasa ukizingatia kwamba tayari kasoro hiyo imesharekebishwa.

**Hoja nambari 8.7.2.2: Udhaifu katika kudhibiti ufikiaji wa mfumo wa UVIKO 19 (access control) kwenye kompyuta zinazotumiwa kuchakata taarifa na kufanya vipimo vya UVIKO 19 Maabara.**

Ukaguzi umebaini kuwa kompyuta zinazotumika kuingiza na kuchakata taarifa za UVIKO 19 kwenye Maabara ya Zanz Medicals hazina udhibiti wa ufukiaji (access control) na kwamba watumiaji wanaingia bila kutakiwa kuingiza nywila (password) zao jambo ambalo linahatarisha usalama wa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo.

Kwa kuzingatia hali halisi ya ugonjwa wa UVIKO 19 duniani na dhana zilizopo ambapo sehemu za jamii mbalimbali bado zinaamini kwamba ni ugonjwa uliotengenezwa na unakuzwa kwa malengo ya watu fulani hivyo kufanya mbinu mbalimbali za kurudisha nyuma jitihada za Serikali na wadau wengine katika kuidhibiti hali iliyopo jambo linalomaanisha kwamba taarifa za UVIKO 19 zinatakiwa kulindwa kwani zinaweza kuharibiwa na watu wenye nia mbaya

mara kama wakipata nafasi ya kufanya hivyo. Kuziacha bila ya kudhibiti kompyuta zinazotumika kuingiza taarifa za UVIKO 19 ni kuongeza hatari ya kuharibiwa kwa taarifa za UVIKO 19 ndani ya Maabara ya Zan Medicals.

Kufuatia hali hii, ukaguzi unaishauri Zanz Medicals kuweka udhibiti kwenye kompyuta zake zote zinazotumika kwenye Maabara yake katika kuingiza na kuchakata taarifa za UVIKO 19. Udhibiti huu unaweza kuwekwa kwa kutumia nywila, ambapo kila mtumiaji wa Kompyuta hizi atatakiwa kuwa na akaunti na nywila yake.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kompyuta zetu zote zinazotumika kuchakata na kuingiza taarifa za msafiri au Mteja wa UVIKO 19 zote zimewekewa udhibiti [Password] hamna mtu yoyote anaeweza kuzifikia taarifa za mteja, tulizingatia hali halisi ya Ugonjwa wa UVIKO 19 na kanuni za kimaabara na usiri kwa Mteja ili kuepuka kuleta athari katika jamii. Hata hivyo kazi ya kupima Uviko 19 kwa sasa inafanywa na kampuni ya Zanz Medics kwa niaba ya Serikali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake, ni kweli kulijitokeza kasoro zilizobainishwa. Hata hivyo, kasoro hiyo tayari imeshatatuliwa ambapo sasa kuna udhibiti wa kutosha kwa kompyuta hizo. Hivyo Kamati imeridhishwa na majibu ya Wizara na haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 8.7.2.3: Udhaifu wa udhibiti wa chumba cha Maabara cha Zanz Medicals.**

Ukaguzi umebaini kuwa Maabara ya Zanz Medicals inayopima UVIKO 19 haina udhibiti unaostahili kwa kukosa kamera za ulinzi (CCTV Camera) na kukosa udhibiti wa milango katika kuingia ndani ya chumba cha Maabara. Kwa mujibu wa "best practice guidelines" milango ya vyumba nyeti kama vile Maabara na chumba cha kuhifadhia vitu vya thamani inapaswa kuwa na udhibiti wa kuingia

ambapo vifaa maalumu huwekwa milangoni ili kuhakikisha kwamba wanaoingia kwenye vyumba hivi ni wahusika pekee au watu walioruhusiwa tu na kwamba watu wengine hawapati kuingia kwenye vyumba hivi. Kamera za ulinzi pia huwekwa ndani ya vyumba hivi ili kuongeza udhibiti na ulinzi wa maeneo haya.

Kutokana na kukosekana kwa udhibiti mzuri wa Maabara kunapelekea hatari ya kufanyiwa hujuma kirahisi na watu wenye nia mbaya na kutobainika kwa haraka jambo ambalo linaweza kusababisha athari za kijamii na kiuchumi kwa

kuwa upimaji wa UVIKO 19 unaohusisha watalii na wageni wengine wanaokuja nchini.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuwekwa udhibiti mzuri wa usalama katika Maabara ikiwa ni pamoja kuwa kamera za ulinzi sehemu ya kuingilia Maabara (main entrance) na ndani ya Maabara ili kuimalisha ulinzi na usalama wa taarifa za wateja wake kwa niaba ya Serikali ili kuziba mianya iliyopo sasa.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Jambo hili limefanyiwa kazi na kwasasa vyumba vya Maabara na Jengo zima la Zanz Medical limefungwa Camera kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa maabara ndani na nje ili kulinda nyaraka, sampuli na usiri wa wasafiri wa kutoka nchi mbalimbali walioingia nchini. Mlango wa maabara una ulinzi wa kuingia ndani kwa ajili ya wafanyakazi wanaofanya kazi ndani ya maabara tuu, mwingine hawezi kuingia kwa ajili ya mambo ya kiusalama.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli kulijitokeza kasoro zilizobainishwa na Mkaguzi. Hata hivyo, kasoro hizo tayari zimesharekebishwa ambapo sasa kuna udhibiti wa kutosha katika jengo hilo. Hivyo Kamati imeridhishwa na majibu ya Wizara na haikuwa na hoja zaidi kwani ilipata fursa ya kufika na kujionea kilichotekelezwa.

**Hoja nambari 8.7.2.4: Kutokufuatwa miongozo ya Wizara ya Afya (SOP) katika utekelezaji wa kazi za upimaji UVIKO 19.**

Ukaguzi umebaini kuwa Zanz Medicals hawana miongozo (SOP) kutoka Wizara ya Afya wanayoifuata katika kuendesha shughuli za Maabara Zanzibar. Aidha ukaguzi umebaini kwamba Maabara ya Mnazi Mmoja ina miongozo mbali mbali inayotakiwa kuzingatiwa na Maabara zinazofanya kazi hapa Zanzibar tofauti na hali halisi tuliyoikuta Zanz Medicals. Hali hii inatilia shaka ubora na viwango vya kazi za upimaji wa UVIKO 19 unaofanywa na Zanz Medicals kutokana na kutokufuata miongozo iliyopo kutoka Wizara ya Afya.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kufanya yafuatayo:-

- Kuipatia kampuni ya Zanz Medicals miongozo yote ya Maabara iliyopo nchini na kuisimamia kwa karibu ili kuhakikisha kwamba inafuata miongozo hiyo (SOP) kwa lengo la kupatikana tija na ufanisi.
- Kuhakikisha kuwa inaifanyia ukaguzi kampuni ya Zanz Medicals angalau mara mbili kwa mwaka katika jitihada za kupata utekelezaji wa

miongozo iliyowekwa na kubaini changamoto nyenginezo zilizopo ili kuzipatia ufumbuzi kwa haraka kwa kuwa mafanikio ya Zanz Medicals kwenye upimaji wa UVIKO 19 ni mafanikio ya Serikali kwa ujumla wake.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Miongozo ya upimaji ya uviko 19 inafuata taratibu za kimataifa kwa nchi zote (IHR 2005) na mwenendo wa mabadiliko hayo hutegemea hali ya nchi husika (Advisory Note) na taarifa hizo Wizara ya Afya imekuwa ikizisambaza kwa wadau wake wote

Wizara pia ina utaratibu wa kuweka Miongozo hiyo katika vituo vya Afya vilivyochaguliwa kwa shughuli hiyo ambapo Zanz Medics anazitumia kwa kazi za upimaji wa UVIKO 19. Aidha, kwa upande wa ukaguzi Zanz Medical amefanyiwa kaguzi zisizopungua tatu ambapo mara ya kwanza kabla ya kuanza kazi hii Wizara ilimkagua na kumpatia ushauri wa kitaalam pamoja na kumpatia access ya miongozo ya kufanyia kazi. Pia Wizara kwa kushirikiana na jumuiya ya afrika mashariki walifanyan ukaguzi mara mbili ili kuthibitisha ubora wa upumaji na utoaji wa majibu ya UVIKO 19 kwa tarehe 7 - 9 Aprili 2022.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa miongozo ambayo inatakiwa kutumiwa na Kampuni ya Zan Medics ilikuwepo kwa vile Kampuni ilikuwa ikufuata miongozo ya kimataifa "International Health Regulations" na sio miongozo ambayo inatolewa na Wizara ya Afya hasa ukizingatia virusi vya UVIKO - 19 lilikuwa ni janga la dunia na miongozo inatolewa kimataifa ili kampuni zote zinazojihusisha na upimaji wake kutoa huduma zinazofanana na katika mazingira yanayokubalika kimataifa.

Sambamba na hilo, Kamati imegundua kuwa Mkaguzi alikosa mashirikiano mazuri kutoka kwa Watendaji. Hili linatokana na ukweli kwamba Kamati imeweza kuoneshwa miongozo hiyo na kuridhika nayo isipokuwa Mkaguzi hakupatiwa.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ihakikishe Mkaguzi anapatiwa ushirikiano unaohitajika na iwapo atahitaji kupewa muongozo basi apatiwe ili kuepusha hoja za namna hii zisijitokeze.

**Hoja nambari 8.7.2.5 Kutokuwekwa vituo vya kupima UVIKO 19 kwenye Bandari za Mkokotoni na Kizimkazi.**

Kwa mujibu wa makubaliano baina ya Wizara ya Afya na Zanz Medicals, palitakiwa kufunguliwa vituo vya upimaji wa UVIKO 19 kwenye maeneo ya Mkototoni na Kizimkazi hata hivyo ukaguzi umebaini kuwa mpaka sasa maeneo hayo hayajaanzishwa. Kutoanzishwa kwa maeneo hayo ni kwenda kinyume na mkabata halali uliopo kati ya pande hizo mbili jambo ambalo linaongeza changamoto ya umbali kwa wasafiri wanaotumia Bandari hizo kuingia na kutoka nchini.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kusimamia utekelezaji wa mkataba huu na kuhakikisha kwamba Zanz Medicals inatimiza wajibu wake kwa mujibu wa makubaliano kama ilivyoainishwa kwenye mkataba husika. Aidha, vituo vya kupima UVIKO 19 vya Mkokotoni na Kizimkazi vianzishwe na kufanya kazi kwa haraka ili kuwafanyia wepesi wa kuchukuwa sampuli na kupimwa wasafiri wanatumia njia ya maji kuingia na kutoka nchini katika maeneo hayo.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wakati wa ukaguzi kiwango cha maambukizi ya UVIKO - 19 yalikuwa yanaanza kupungua Serikali ikafanya maamuzi ya:-

- Kupunguza vituo vya upimaji ikiwemo cha kizimkazi na mkokotoni
- Serikali ilianzisha utaratibu wa huduma mkoba (outreach servises) ili kuwafikia wananchi kwa uharaka zaidi
- Kwa vituo vilivyobaki sampuli zilikuwa zinakusanywa na kupelekwa kwenye maabara kuu ya migombani

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inakubaliana na hoja ya Mkaguzi kwa vile Wizara ya Afya na Zan Medics zilikiuka masharti ya ufunguaji wa vituo vya upimaji wa Uviko - 19 kwenye bandari za Mkokotoni na Kizimkazi. Hivyo, pamoja na kwamba maambukizi ya UVIKO - 19 hivi sasa yamepungua lakini Kamati haikuridhishwa na hatua za kushindwa kuweka vituo hivyo.

**Hoja nambari 8.7.2.6 Ucheleweshwaji wa vyeti vya uthibitisho wa malipo ya kodi ya zuio**

Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya pamoja na mabadiliko yake ya mwaka 2019 kifungu cha 85(2) kinaeleza kuhusu muda wa kupatiwa cheti cha kodi ya zuio kuwa ni ndani ya siku 30 baada ya mwisho wa mwezi ambamo kodi husika ilizuiwa. Ukaguzi umebaini kuwepo kwa ucheleweshwaji wa vyeti vya kodi ya zuio (Withholding Tax Certificate) unaofanywa na Wizara ya Afya dhidi ya Zanz Medicals kinyume na matakwa ya Sheria kwenye kodi iliyozuiwa

na Wizara ya Afya katika malipo ya kwanza ambayo Zanz Medicals ilipata kutoka Wizarani.

Kutokutolewa kwa vyeti vya kodi ya zuio kwa wakati kunapelekea Zanz Medicals kukosa ushahidi wa kufanyika kwa malipo ya kodi husika jambo ambalo linaiweka kwenye mazingira magumu ya kimahesabu na uwajibikaji kwa wamiliki na wawekezaji wake. Aidha, hali hii pia inatilia shaka utekelezwaji wa malipo ya kodi ya zuio kwa Bodi ya Mapato ambapo inawezekana kwamba Wizara ya Afya haijafanya malipo hayo na ndio maana haijapewa vyeti husika.

Ili kuboresha mazingira ya kufanyia biashara ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuhakikisha inatimiza masharititi ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 na kanuni zake kwenye kodi ya zuio ili kuwapa Zanz Medicals nafasi ya kufanya uwajibikaji kwa wamiliki na wawekezaji wake pasipo shaka, na kuongeza tija kwa upande wake.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Malipo yote kuhusu Zanz Medicals yalikuwa yakifanyika Wizara ya Fedha, hivyo Wizara ya Afya haikuhusika na ucheleweshaji huo, hata hivyo ushauri tumeuzingatia na tutashauriana na wenzetu wizara ya fedha kuona hili halitokei tena.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imeridhishwa na majibu ya Wizara kwa vile wahusika wa hoja hii walikuwa ni Wizara ya Fedha na Mipango kwani kwa muda huo ni kweli jukumu la mapato lilikuwa halisimamiwi na Wizara yao.

**Hoja nambari 8.7.2.7: Uwepo wa udanganyifu kwenye malipo ya upimaji wa UVIKO 19.**

Katika ukaguzi huu uliofanyika kwenye mfumo wa UVIKO 19 imebainika kuwepo kwa udanganyifu wa malipo ya huduma za upimaji unaofanywa na baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya PBZ kwa kushirikiana na baadhi ya wafanyakazi wa kampuni ya Zanz Medicals. Hali hii imejidhihirisha kwenye baadhi ya stakabadhi za malipo za PBZ zinazoonesha kuwa mteja amelipia kipimo cha UVIKO 19 cha PCR ambacho kimsingi bei yake ni Dola za Marekani 80.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana wakati wa ukaguzi huu zinasema kwamba wengi wa wasafiri wanaokumbwa kwenye tatizo hili ni wageni ambao wanakuwa hawana uelewa mzuri wa mfumo wa benki zetu jambo linalopelekea

kushindwa kuhoji kiwango kinachokuwa kimeandikwa kwenye stakabadhi za malipo wanazopewa na benki ya PBZ.

Kielelezo L: kinaonesha malipo ya shilingi za kitanzania Themanini (Tshs.80) na shilingi za kitanzania Elfu Tatu (Tshs. 80 and Tshs. 3,000) kupokelewa na benki ya PBZ kama malipo ya kipimo cha UVIKO 19 cha PCR jambo ambalo ni kinyume na bei zote za vipimo vya UVIKO 19 kama ilivyoelezewa kwenye utangulizi.

Kwa mujibu wa maelezo yaliyopatikana kupitia mahojiano (interview) na ukaguzi ulifahamishwa kwamba kwa nyakati tofauti wageni hawa walilipia USD 80 lakini stakabadhi za malipo hayo ziliandikwa Tshs. 80 na Tshs. 3,000 na Maafisa wa benki ya PBZ kwa sababu zao binafsi.

Aidha, stakabadhi hizi ilipofikishwa Zanz Medicals ambako ndiko inakopokelewa na kuingizwa kwenye mfumo kabla ya mteja kupewa huduma Zanz Medicals ilizipokea na kuziingiza kwenye mfumo bila kujali tofauti hiyo kubwa ya malipo iliyokuwa wazi kwenye stakabadhi hizo. Jambo hili limewezekana kufanikiwa kwa ushirikiano wa baadhi ya watumishi wasio waaminifu wa PBZ na Zanz Medicals. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 37: Baadhi ya Miamala ya USD 80 iliyoingizwa kwenye Hesabu ya TZS ya PBZ COVID RESCUE FUND TZS kama TZS 80 na baadhi ya Maafisa wa PBZ na kutumika kutoa huduma kwa wateja kupitia baadhi ya wahudumu wa Zan Medicals.**

| DATE | BANK NAME: THE PEOPLE'S BANK OF ZANZIBAR LIMITED<br><br>BANK ACCOUNT NAME: COVID-19 RESCUE FUND<br><br>BANK ACCOUNT NUMBER: 0748946001<br><br>BANK ACCOUNT CURRENCY: TZS<br><br>NB<br><br>COLUMN F9. 2= CREDIT, 1= DEBIT<br><br>EXPLANATION TEXT | VAL_DATE | TRANSACTION SEUENCE NO. | TRA_AMT | DEB_ CRE_IND |
|---|---|---|---|---|---|
| 23- | POS: M2050004: LUMUMBA | 23-01-21 | 15547 | 80.00 | 2 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 01-21 | ZANZIBAR Tanzania TZ TZ:102309887268: 01-23 09:21:27 | | | | |
| 25-01-21 | MOHAMED SADEGH SHAHI | 25-01-21 | 14279 | 80.00 | 2 |
| 28-01-21 | POS: M2050004: LUMUMBA ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:102810336665::01-28 10:18:56 | 28-01-21 | 17012 | 80.00 | 2 |
| 29-01-21 | POS:M2050004:LUMUMBA ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:102913228662::01-29 13:13:48 | 29-01-21 | 37757 | 80.00 | 2 |
| 05-02-21 | SANE NHAMBURO | 05-02-21 | 4960 | 80.00 | 2 |
| 06-02-21 | POS:M2050004:LUMUMBA ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:103709127607::02-06 09:15:27 | 06-02-21 | 10639 | 80.00 | 2 |
| 08-02-21 | dayer catherine | 08-02-21 | 10679 | 80.00 | 2 |
| 08-02-21 | DAYER GERALD | 08-02-21 | 10683 | 80.00 | 2 |
| 11-02-21 | POS:M2050004:LUMUMBA ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:104212352905::02-11 12:22:32 | 11-02-21 | 19520 | 80.00 | 2 |
| 24-03-21 | HASSAN ADEN | 24-03-21 | 2451 | 80.00 | 2 |
| 08-04-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:109714919467::04-07 14:45:19 | 08-04-21 | 23321 | 80.00 | 2 |
| 15-04-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:110509974676::04-15 09:42:54 | 15-04-21 | 7915 | 80.00 | 2 |
| 15-04-21 | TIAGO MANUEL | 15-04-21 | 5419 | 80.00 | 2 |
| 22-04-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:111209693344::04-22 09:24:53 | 22-04-21 | 7699 | 80.00 | 2 |
| 12-05-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:113213225709::05-12 13:10:25 | 12-05-21 | 36443 | 80.00 | 2 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 25-05-21 | MOHAMMED ISSA | 25-05-21 | 6880 | 80.00 | 2 |
| 03-06-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:115410993596::06-03 10:23:13 | 03-06-21 | 13507 | 80.00 | 2 |
| 04-06-21 | MARIE CHRISTINE GUINARD | 04-06-21 | 1725 | 80.00 | 2 |
| 05-06-21 | BIRHAN T ABRAH | 05-06-21 | 3954 | 80.00 | 2 |
| 07-06-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:115711422230::06-06 11:17:02 | 07-06-21 | 11128 | 80.00 | 2 |
| 07-06-21 | MARY GEORGIA BRUCE-JONES | 07-06-21 | 7133 | 80.00 | 2 |
| 15-06-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:116608242443::06-15 08:17:22 | 15-06-21 | 2244 | 80.00 | 2 |
| 22-06-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:117309713292::06-22 09:01:53 | 22-06-21 | 14274 | 80.00 | 2 |
| 28-06-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:117908495450::06-28 08:51:35 | 28-06-21 | 48586 | 80.00 | 2 |
| 16-07-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:119714264464::07-16 14:34:24 | 16-07-21 | 28607 | 80.00 | 2 |
| 09-08-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:122010210449::08-08 10:53:30 | 09-08-21 | 11054 | 80.00 | 2 |
| 03-09-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:124614942367::09-03 14:02:22 | 03-09-21 | 20420 | 80.00 | 2 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 20-09-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:126209013420::09-19 09:13:33 | 20-09-21 | 13189 | 80.00 | 2 |
| 25-09-21 | GREGORY ALLEN | 25-09-21 | 6173 | 80.00 | 2 |
| 06-10-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:127911830239::10-06 11:10:30 | 06-10-21 | 18292 | 80.00 | 2 |
| 07-10-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:128012509356::10-07 12:38:29 | 07-10-21 | 26326 | 80.00 | 2 |
| 08-10-21 | ALI MOHAMED MBARUK | 08-10-21 | 551 | 80.00 | 2 |
| 11-10-21 | TSUYOSHI SHIMAOKA | 11-10-21 | 14833 | 80.00 | 2 |
| 13-10-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:128613383765::10-13 13:19:43 | 13-10-21 | 23494 | 80.00 | 2 |
| 12-11-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:131609247468::11-12 09:24:07 | 12-11-21 | 13511 | 80.00 | 2 |
| 12-11-21 | POS:M2050004:MAZIZINI ZANZIBAR TanzaniaTZ TZ:131612184118::11-12 12:09:44 | 12-11-21 | 24325 | 80.00 | 2 |
| 18-11-21 | AKIDAH | 18-11-21 | 3399 | 80.00 | 2 |
| 21-12-21 | PAULA HERRAN BAIGORRA - 41791498R | 21-12-21 | 5784 | 80.00 | 2 |

Hali hii inapelekea kutokea kwa athari mbalimbali kwa Serikali zikiwemo zifuatazo:-

- Kuisababishia hasara Serikali kwa ubadhirifu wa fedha ambazo ilipaswa kuzipata.
- Kuchochea rushwa miongoni mwa jamii katika kupata huduma zinazotolewa na Serikali kupitia Mawakala wake.
- Kurudisha nyuma maendeleo ya nchi kwa kuhujumu uchumi wa Taifa na kuendeleza umaskini uliopo ambao Serikali inaweka jitihada za kuupunzua ama kuuondoa kabisa.
- Kukwamisha jitihada za uwekezaji na utegemezi wa TEHAMA katika kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii kwa kutumia mianya iliyopo kwa manufaa binafsi.

Kwa kuzingatia athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza kufuatia udanganyifu uliobainkika kwenye ukaguzi huu tunashauri mambo yafuatayo:-

- Vyombo vya ulinzi na usalama vinavyohusika na masuala ya rushwa na uhujumu uchumi kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini ukubwa wa tatizo hili na kuchukuwa hatua stahiki kwa wote waliohusika na udanganyifu huu kwa mujibu wa Sheria.
- Wizara ya Afya kuwaondolea ufikiaji wa mfumo kwenye eneo la kuingiza malipo watu wote wasio watumishi wa Wizara ya Afya Idara ya Uhasibu na kuirejesha kazi hii kwa wahasibu walioko chini ya Wizara ambapo inaweza kulazimu kuwapeleka kwenye vituo mbalimbali wahasibu hao kunakofanywa upimaji wa UVIKO 19 ili kufanyia kazi zao huko katika kurahisisha kazi ya kuwahudumia wasafiri kwa haraka.
- Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Zanz Medicals na Benki ya PBZ kufanya uchunguzi wa kubaini binu zilizotumika na kiwango cha fedha kilichopotea kwa kupitia udanganyifu wa aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na udanganyifu huu uliobainika kwenye ukaguzi na kuweka mikakati ya pamoja ya kuzuia hali hii kujirudia tena siku zijazo.
- Zanz Medicals kufanya uchunguzi kwa baadhi ya wafanyakzi wake wasio waaminifu na mabao wameshiriki kwa namna moja au nyengine kufanikisha udanganyifu huu na kuwachulia hatua za kinidhamu na kisheria ikiwa ni pamoja na kurejesha fedha zote zilizochepushwa.
- Benki ya PBZ kufanya uchunguzi kwa baadhi ya wafanyakazi wake wasio waaminifu na walioshiriki kutenda udanganyifu huu na kuwachukulia hatua za kinidhamu na za kisheria ikiwa ni pamoja na kurejesha fedha zote zilizochepushwa.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Udanganyifu wa mfumo wa malipo baada ya kufahamika Wizara kwa kushirikiana na Zanz Medics iliwahusisha benki ya PBZ na kampuni ya Rahisi Solution (ambayo ndio iliyotengeneza mfumo) na kuweza kutambua udhaifu huo, taasisi hizi kwa pamoja ziliboresha mfumo, wafanyakazi walioshutumiwa kuhusika na upotevu wa fedha walichukuliwa hatua na PBZ na Zanz Medics.

Mfumo uliorekebishwa umeonesha mafanikio na kupunguza uwezekano wa wizi wa kushirikiana.

Serikali ilianza baadae kutumia utaratibu wa control Number kwa kila mteja na account ya mteja ifunguke kwa ajili ya kuendelea na vipimo, mfumo huo ndio unaotumika hadi sasa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Wizara kukiri kwamba kulikuwa na udanganyifu uliofanywa na baadhi ya watendaji wa Wizara, Benki ya PBZ na Zanz Medics. Hata hivyo, Kamati haikuridhika na ufuatiliaji wa kasoro hiyo kwani imesababisha mapato mengi ya Serikali kukosekana. Kamati ilitegemea Wizara italifuatilia suala hilo huko lilipowasilishwa (ZAECA) ili iweze kubaini limefikia wapi. Kwa mnasaba huo, Kamati haijaridhishwa na majibu ya Wizara, hivyo hoja inaendelea kubakia.

Kamati iligundua kuwa kuna baadhi ya watendaji hususan wa Wizara ya Afya walichukuliwa hatua za kinidhamu lakini kamati ilipotaka vielelezo vya hatua zilizochukuliwa haikuweza kupatiwa. Kwa msingi huo, Kamati ilipata wasiwasi kwamba kuna uwezekano hatua zilizoelezwa hazikutekelezwa.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ihakikishe inawasilisha kwenye Kamati ya PAC vielelezo vya hatua za kunidhamu zilizochukuliwa dhidi ya wafanyakazi wake waliohusika kwa njia moja au nyengine na kadhia hiyo.
2. Kwa vile muda umekuwa mrefu na Wizara haifahamu chochote kuhusiana na kadhia ya upotevu wa fedha za mapato ya Serikali, Wizara ihakikishe inafuatilia ZAECA maendeleo ya suala hilo.

**Hoja nambari 8.7.2.8: Kubadilisha "Key experts" bila ya idhini ya Wizara ya Afya**

Kwa mujibu wa mkataba baina ya Wizara ya Afya na kampuni ya Zanz Medicals kipengele cha 30.1 kinachosema isipokuwa Mteja kukubali kwa maandishi, hapatakuwa na mabadiliko ya "Key Experts", key experts ni wataalamu muhimu katika zoezi la upimaji wa UVIKO 19 ambao wasifu wao uliambatishwa kwenye mkataba baina ya Wizara ya Afya na Zanz Medicals.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kwamba Zanz Medicals ilifanya mabadiliko kwenye baadhi ya key experts wake bila ya kupata idhini ya maandishi ya Wizara ya Afya jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya mkataba. Athari nyengine ni pamoja na kufanya udanganyifu kwa Serikali kwa kuweka

wataalamu wenye wasifu mkubwa ili kupata zabuni ambao wanahalalisha bei za juu za watoa huduma lakini inapokuja kwenye utekelezaji wa kazi husika wataalumu hawo hawaletwi kwenye maeneo ya kazi bila sababu za msingi.

Kwa kuwa Zanz Medicals imevunja moja ya mashariti ya mkataba huu Wizara ya Afya inashauriwa kuchukuwa hatua stahiki za kisheria kulingana na uvunjanji uliofanyika ikiwa ni pamoja na kuitaka Zanz Medicals kuandika barua na kujieleza ni kwanini isichukuliwe hatua kwa kisheria kwa kuvunja moja ya vipengele muhimu vya mkataba na mipango yake yake ya kuhakikisha kwamba wataalamu hao wote wanapatikana kazini kama ilivyotarajiwa na vinginevyo kuleta mbadala wa wafanyakazi hao kwa mujibu wa mkataba.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Baada ya kupokea taarifa hiyo timu ya Wizara ya Afya ilifika kwenye maabara ya Zanz Medics na ukaguzi ulibaini kwamba waliokuwepo hapo wana uwezo wa kufanya kazi hizo (credential), aidha Wizara ya Afya haikuweka masharti katika kubadilisha key expart kwani ilitambua kwamba jambo hili la upimaji linahitaji ujuzi, uzoefu na uweledi. Hivyo Wizara ilitoa mwanya kwa Zanz Medics kuajiri key expart linganifu na mahitaji ya utoaji wa huduma inagawa mkataba unasema pale anapobadilisha key expert basi aijuilishe Wizara.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba Wizara ilishindwa kufuata masharti ya kifungu 30.1 cha Mkataba baina ya Wizara ya Afya na Kampuni ya Zan Medics kwani Mkataba ulitaja majina ya madaktari ambao wanatakiwa kutoa huduma husika badala yake Wizara ilipanga madaktari kwa mujibu wa sifa na sio majina yaliyoainishwa ndani ya Mkataba na hatimae kupelekea kujitokeza kwa hoja hii.

Sambamba na hilo, Kamati imegundua kuwa Wizara haikumpatia ushirikiano wa karibu Mkaguzi kama ilivyopatiwa Kamati.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara inapoandaa mikataba yake ihakikishe inaweka sifa stahiki zinazotakiwa kuwa nazo daktari na sio majina ya madaktari.
2. Wizara impatie Mkaguzi mashirikiano ili aweze kutekeleza majukumu yake kwa wepesi zaidi.

**Hoja nambari 8.7.2.9: Kutokuwepo kwa udhibiti wa watu wanaoingia kwenye kituo cha kupima UVIKO 19 cha Migombani**

Ukaguzi umebaini kuwa kwenye kituo cha kupima UVIKO 19 cha Migombani hakuna utaratibu maalum wa kiudhibiti uliowekwa kwenye geti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba watu wanaoingia kwenye eneo hili ni wale wanaohusika na upimaji wa UVIKO 19 pekee. Kufuatia hali hii ukaguzi ulibaini uwepo wa baadhi ya watu wanaoingia kwenye vituo na kuwadanganya wasafiri hususani watalii namna ya kukwepa kulipia fedha halali za vipimo na kuwapa namna nyengine ambazo zinapelekea kutengenezewa vyeti feki. Athari nyengine ni pamoja na kusababisha mkusanyiko mkubwa wa watu kwenye eneo hili na kuongeza hatari za maambukizi ya UVIKO 19 kwa wasafiri.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Zanz Medicals kuweka utaratibu utakao hakikisha kwamba watu wanaoingia ndani ya geti la Maabara ya Migombani ni wale wanaohusika na upimaji wa UVIKO 19 pekee.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara ya afya kwa kushirikiana na Zanz Medical wameboresha na kuimarisha udhibiti wa wafanyakazi pamoja na wateja waliofuata huduma katika kituo hicho. Hii ni pamoja na kuimarishwa kwa ulinzi kwa kuajiri kampuni ya ulinzi pamoja na kuweka kamera katika maeneo yote muhimu ya jengo. Aidha, huduma kwa wateja ziliimarishwa kwa kuweka maofisa maalum ambao walihusika katika mapokezi, ukaguzi na kutoa maelezo kwa mteja ili kurahisisha upatikanaji wa huduma huku ikizingatiwa hali nzima ya usalama na afya za wateja.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Uchunguzi wa hoja hii unafanana na uchunguzi wa hoja nambari 8.7.2.3. Hivyo, Kamati ya PAC aikuwa na maelezo zaidi hasa ukizingatia kasoro hizo tayari zimesharekebishwa.

**8.7.2.10 Dosari kwa upande wa Kampuni ya Rahisi Solution**

Kwa kuwa Wizara Afya iliingia makubaliano na kampuni ya Rahisi katika utengenezaji wa mfumo unaotumika kusimamia na kuratibu taarifa za UVIKO 19 ukanguzi wa mifumo ya TEHAMA ulifanyika katika kuchambua wajibu, haki na majukumu ya Rahisi Solution kwa kuzingatia sheria, miongozo na sera mbalimbali zilizopo na kubaini dosari zifuatazo: -

**Hoja nambari 8.7.2.11: Kutokuwepo kwa eneo la kuendeleza mfumo baada maafa (Disaster recovery site/ offsite).**

Eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site) ni eneo mbadala maalum linalotengwa kwa lengo la kutumiwa wakati yanapotokea maafa au miundombinu kushindwa kufanya kazi kama inavyotakiwa (major

failures of the system) kwenye eneo la kazi la kila siku na kupelekea kuharibika kwa miundombinu ya TEHAMA na kushindwa kuzipata taarifa zilizomo ndani ya mfumo. Eneo hili hutengwa mbali na eneo la kila siku kwa angalau umbali wa Kilometa 50 ili kupunguza uwezekano wa kuathiriwa kwa maeneo yote mawili kwa wakati mmoja yanapotokea maafa.

Eneo hili linatakiwa kuwa na ukamilifu wote kama lilivyo eneo linalotumika kila siku kwa maana ya miundombinu yote na usalama kuzingatiwa kiasi kwamba wakati wowote eneo hili linaweza chukua nafasi ya eneo linalotumika kila siku.

Hata hivyo, ukaguzi umegundua kuwa kampuni ya Rahisi Solution pamoja na Wizara hazina eneo mbadala maalum lililoandaliwa kwa lengo la kuweka nakala za taarifa zote za mfumo moja kwa moja kulingana na matukio yanayoendelea kila wakati (real time events).

Kutokuwekwa eneo la kuendeleza utendaji kazi mfumo baada ya matatizo kutokea kunaweza kusababisha upotevu wa taarifa muhimu za Serikali na kuathiri utendaji kazi wa Wizara katika kuwahudumia wananchi jambo ambalo litakuwa na madhara mbalimbali kiuchumi na kijamii.

Kwa kuzingatia athari zinazoweza kujitokeza kwa kutokuwepo kwa “Disaster Recovery Site” ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na kapuni ya Rahisi kutengeneza eneo la kuendeleza mifumo baada ya maafa kulingana na miongozo ya TEHAMA ya kitaifa na kimataifa (best practice).

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Kwa hivi sasa Wizara inategemea eneo la ZICTIA kwa ajili ya kuendeleza mfumo baada ya maafa. Hata hivyo, kwa lengo la kuhakikisha usalama zaidi Wizara tayari imetenga eneo lake kwa madhumuni hayo, miongoni mwa mambo yaliyofanyika ni kutafuta eneo hilo ikiwemo Kitogani, kutafuta wafadhili wa kusaidia ukarabati wa eneo hilo pamoja na mifumo itakayo hitajika, kuandaa mpango wa TEHAMA kuhusiana na maafa. Mategemeo ya Wizara ni kuanza utekelezaji wake mnamo mwaka wa Fedha 2023/24.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya juhudi zilizochukuliwa na Wizara lakini Kamati ya PAC imebaini ni muda mrefu umepita takriban miaka miwili na Wizara bado inatafuta eneo. Hata hivyo, Kamati imegundua kuwa kwa kuhifadhi taarifa ZICTIA kama ndio eneo mbadala la kutusaidia iwapo majanga yatatokea bado Wizara itakuwa haijapata suluhisho la kudumu.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inashauri Wizara/Serikali kutengeneza eneo jengine la kuendeleza mifumo kwa upande wa Pemba ili mifumo yetu ipate kuhifadhiwa sehemu mbili tofauti endepo eneo moja litapata majanga.

**Hoja nambari 8.7.2.12 Kukosekana kwa mpango wa kupona maafa (Disaster Recovery Plan)**

Mpango wa kuendeleza mfumo baada ya maafa/ mpango wa kupona maafa (disaster recovery plan) unalenga kuikinga taasisi kuepuka madhara yatokanayo na mafuriko, tetemeko la ardhi, kimbunga, ajali, makosa ya kibinadamu, moto au mripuko, kukatika kwa umeme kwa muda mrefu, matatizo kwenye chumba cha seva na matatizo yasiyotarajiwa kwenye mifumo ya kielekitroniki. Mpango huu unatakiwa kuiwezesha taasisi kurejesha kazi/ huduma zake muhimu kwa haraka baada ya janga kutokea. Taasisi yoyote yenye mpango huu inakusudia kuendeleza huduma/ kazi zake kwamba hakuna tatizo lililotokea kwenye mifumo yake kwa kadri iwezekanavyo.

Aidha, kujiandaa kupona maafa kunahitaji kuzingatia vitu vingi kwa pamoja vinavyohitaji mbinu makini zinazojumuisha miundombinu ya TEHAMA, vifaa vya mtandao, programu, umeme, muunganiko (connectivity) na majaribio (testing) kuhakikisha kwamba kupona maafa kunawezekana. Vile vile, mpango huu una ainisha majukumu na wajibu wa kila mdau na huduma/ kazi muhimu zinazotakiwa kurejeshwa kwa haraka ikitokea majanga, pia unaelezea kwa namna gani taasisi inaweza kurejesha huduma mara tu baada ya kupatwa na maafa katika miundombinu ya utoaji wa huduma.

Ukaguzi umebaini kwamba kampuni ya Rahisi Solution pamoja na Wizara ya Afya hazina Mpango wa kupona maafa, kufanya hivyo ni kwenda kinyume "Best Practice Guidelines" ambazo zinasisitiza uwepo wa mpango huu kwa kuzingatia manufaa yake kama vile unafuu wa gharama katika kupona maafa ukilinganisha na gharama ambazo zingetumika kwenye mazingira ambayo hayana mpango.

Ukaguzi unashauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na kampuni ya Rahisi Solution kutengeneza mpango wa kupona maafa kwa kuzingatia miongozo ya ndani na ile ya kimataifa ili kuhakikisha mpango huo unakuwa wa kujitosheleza katika kukabiliana na maafa kama ilivyofafanuliwa hapo juu.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara tayari imeanza hatua za awali za utayarishaji mpango wa kupona maafa ikiwa ni pamoja na kutengeneza rasimu ya mpango huo ambao unatazamiwa kuwasilishwa kwa wadau kwa ajili ya michango yao tayari kwa kuidhinishwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC haikuridhishwa na majibu ya Wizara hasa ukizingatia ni muda mrefu ukilinganisha na kasi ndogo tangu Mkaguzi alipomaliza ukaguzi wake wakati Wizara ndio kwanza ipo katika hatua ya kuanza utayarishaji wa mpango wa kupona maafa (Disaster Recovery Plan). Aidha, Kamati imesikitishwa na kasi ndogo ya Wizara katika kuandaa mpango huo.

**Ushauri wa Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Serikali kuweka mkazo na msisitizo katika uandaaji wa mpango wa kupona maafa (Disaster Recovery Plan) ili endapo shambulio la aina yoyote litatokea dhidi ya mifumo yetu basi kuwepo na uhimili kutoka kwa mifumo hiyo.

**Hoja nambari 8.7.2.13: Kukosekana kwa nyaraka muhimu za mfumo wa UVIKO 19.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa mfumo wa UVIKO 19 hauna nyaraka zozote zinazohusiana na matumizi endelevu ya mfumo ambapo miongoni mwa nyaraka hizo ni kama zifuatazo: -

- System Operations Manual.
- System Architecture Document.
- System Configurations Manual.
- System Requirements Document.
- System Users Acceptance Testing.
- System Setups.

Aidha, imebainika kwamba mfumo huu muhimu katika kusimamia na kuratibu taarifa za UVIKO 19 nchini katika utengenezaji wake haukuzingatia miongozo na viwango bora vinavyokubalika (best practice) kuanzia hatua ya awali ya utengenezwaji hadi hatua ya mwisho ya ukamilishaji wa mfumo (System Development Life Cycle – SDLC).

Kutokuwepo kwa nyaraka zote zinazohitajika katika utengenezaji, usimamizi, uendeshaji na utaratibu wa mfumo kunaweza kupelekea athari mbalimbali ikiwamo zifuatazo: -

- Mfumo kuwa mali ya mtu/ watu wachache badala ya Taasisi, hii inatokana na ukweli kwamba aliyeutengeneza na wanaoutumia mfumo kwa sasa ndio wanafahamu kilichomo kwenye mfumo na namna kinavyofanya kazi kwa sababu hakijaandikwa kwenye nyaraka yoyote ile, mtu huyu au kikundi cha watu hawa ikitokea hawapo ofisini basi mfumo huu hautaweza kutumika katika namna ambayo ni endelevu na

kuinyima Taasisi haki ya kunufaika na uwekezaji uliofanywa katika namna endelevu.

- Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia mahitaji yote ya watumiaji ya sasa na ya wakati ujao katika usalama, udhibiti, ufikiaji, matumizi, urahisi wa kuutumia n.k.
- Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia hali halisi ya mabadiliko ya teknolojia na kusababisha mfumo husika kuwa kama kisiwa kwa kushindwa kuwasiliana na mifumo mingine kwa sababu ya utofauti wa teknolojia jambo linalorudisha nyuma urahisishaji wa kazi kwa kutumia TEHAMA.
- Taasisi kushindwa kufahamu uwekezaji halisi kwenye mfumo ikiwa ni pamoja na gharama, muda, juhudi na jitihada zilizotumika mpaka kuupata mfumo uliokamili, hili hutokea pale ambapo hakuna bajeti ya muda mfupi na mrefu kwa ajili ya kutengeneza mfumo wote.
- Taasisi kushindwa kufanya maboresho au mabadiliko kulingana na mahitaji kwenye mfumo kwa kuwa haifahamiki au haikumbukwi namna mfumo ulivyo sanifiwa na kutengenezwa.
- Kuendeleza utegemezi kwa mtoa huduma (system supplier) ikiwa mfumo umetengenezwa na mtoa huduma wa nje kwasababu Taasisi inakuwa haina kumbukumbu muhimu ambazo ingeliweza kuzitumia kujenga uwezo wa ndani na kupunguza utegemezi kwa mtoa huduma jambo ambalo linaokoa gharama na kuipunguzia mzigo Serikali.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kuisimamia kampuni ya Rahisi Solution na kuhakikisha kwamba inapata nyaraka zote muhimu za mfumo kama ilivyo ainishwa hapo juu, pia kuhakikisha kwamba nyaraka hizo zinakidhi vigezo vinavyokubalika.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Utengenezaji wa mfumo wa UVIKO - 19 ulikuwa ni wa dharura, jambo lililosababisha kutofuatwa kwa utaratibu wa kawaida wa kutegeneza mifumo ya TEHAMA (System Development Life Cycle). Hata hivyo Wizara ilifanya mawasiliano na Rahisi Solution na baadhi ya nyaraka hizo zilitengenezwa na nyengine zilizobakia zinaendelea kukamilishwa. Miongoni mwa nyaraka zilizotengenezwa ni kama zifuatazo;

- Modules distription
- Report manual
- User manual
- System permission
- Saver, hosting and System Configurations Manual. Imewasilishwa

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa Mfumo huo kweli ulitengenezwa bila kufuata miongozo na viwango bora vinavyokubalika (Best practices) jambo lililopelekea kupatikana hoja nyingi ambazo Mkaguzi amezibaini.

**Ushauri wa Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inapoandaa mifumo lazima ifuate miongozo na viwango bora ili mfumo ifanye kazi kwa ufanisi na ulete tija.

**Hoja nambari 8.7.2.14 Udhaifu wa udhibiti katika kuusimamia mfumo wa UVIKO 19**

Ukaguzi umebaini kuwa usimamizi wa watumiaji wa mfumo na miundombinu yake havina utaratibu rasmi wa kukagua shughuli zinazofanywa na watumiaji wenye haki zote za kwenye mfumo kwa kutumia akaunti za upendeleo (priviledge accounts). Pia, ukaguzi ulibaini udhaifu wa ubatilishwaji kwa haki za watumiaji ambapo hali iliyopelekea uwepo wa wafanyakazi waliokoma utumishi wao kuendelea kuwa na haki za kuingia katika mfumo wa UVIKO 19.

Aidha, ukaguzi ulibaini uwepo wa udhaifu katika eneo la mgawanyo wa majukumu kwa watumiaji wa mfumo kulingana na majukumu ya mtu husika kwa mujibu wa majukumu ya kazi katika mfumo huo.

Uwepo wa makundi ya watumiaji yasiyokuwa na ulazima kwenye mfumo huu ni miongoni mwa udhaifu uliobainika katika ukaguzi huu ambapo ni kinyume na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika.

**Ukaguzi unashauri mambo yafuatayo katika kukabiliana na udhaifu wa usimamizi wa mfumo huu:-**

- Jukumu la usimamizi wa mfumo wa UVIKO 19 lipewe Wizara ya Afya kwa kuzingatia hatua nyengine zote muhimu za makabidhiano ya mfumo huu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba inapewa nyaraka zote muhimu za mfumo na inajengewa uwezo unaostahili kufanya usimamizi huo.
- Kuwaondolea ruhusa watumiaji wengine wote wenye nguvu za super admin ili kuondoa muingiliano wa kazi zinazofanana kwa wakati mmoja.
- Kuhakikisha kuna mgawanyo wa majukumu katika utekelezaji wa kazi za kila siku kwenye mfumo.
- Kubatilisha akaunti zote za waliokuwa watumishi ambao kwa sasa utumishi wao umemaliza.

- Kufanya upitiaji wa mfumo wa mara kwa mara ili kubaini akaunti ambazo hazitumiki kila baada ya kipindi kisichozidi miezi 3 na kuziweka katika hali ya kutotumika (disabled).

Kielelezo M: kinaonesha kuwa mtumiaji bado yupo active hali ya kuwa kwasasa si mtumiaji wa mfumo.

Kielelezo N: kinaonesha uwepo wa Supper Admin zaidi ya mmoja wenye access sawa.

Kielelezo O: Kinaonesha uwepo wa Moh-fedha (muhasibu) katika mfumo ambae hajulikani na yupo active na wapo ambao hawatumii mfumo lakini katika mfumo wapo active, vile vile majina ya akaunti yamejirejea.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara ya Afya inakubaliana na ushauri wa CAG wa kupatiwa jukumu la usimamizi wa mfumo wa UVIKO 19 kwa kuzingatia hatua nyengine zote muhimu za makabidhiano ya mfumo huu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba inapewa nyaraka zote muhimu za mfumo na inajengewa uwezo unaostahili kufanya usimamizi huo. Kwa kutambua umuhimu wa penedezo hili wizara ilifanya maboresho na mabadiliko katika vipengele vya mkatabba wa kwanza (kipengele 7.0 (xi) na mkataba wa pili (kipengele 3.2 (xi)) cha umiliki pamoja na kuwataka rahisi solution kukabidhi mfumo kwa wizara viliingizwa ili kutoa uhalali wa makabidhiano hayo. Hata hivyo kutokana na kukabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo.

Uhaba wa wataalam (developers), vifaa na ujuzi katika usimamizi wa mfumo tajwa. Wizara imeanza kuyatekeleza haya kwa awamu ikiwa hadi sasa tayari tumepata “developer” 12, tumenunua sever kwa kushirikiana na CDC pamoja na ununuzi wa kompyuta. Wizara inaendelea kufanyia kazi jambo hili na tunatazamia kuwa na umiliki kamili ifikapo mwaka 2025.

Kwa upande wa kuwaondolea ruhusa watumiaji wengine wote wenye nguvu za super admin ili kuondoa muingiliano wa kazi zinazofanana kwa wakati mmoja Wizara kwa kushirikiana na rahisi solution imefanikisha zoezi la kuwaondolea ruhusa baadhi wa watumiaji wenye nguvu ya super admin ruhusa hiyo na bado wizara inashirikiana na rahisi katika kuiboresha orodha ya watumiaji tajwa hapo juu linganifu na mahitaji.

Kwa sasa mfumo wa Uviko 19 unalazimisha watumiaji kuwa na (credentials) ambazo ni tarakimu za kumtambua mtumiaji na neno siri ambavyo vinaimarisha udhibiti wa ufikiaji (access control) kuufikia mfumo wa Uviko 19.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imeridhishwa na majibu ya Wizara kwa vile kuna hatua nyingi ambazo Wizara imechukua. Hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara kufanya majaribio tofauti yanayohitajika kabla ya kuuleta mfumo "live" ili kuhakikisha mfumo huo unafanyakazi vizuri na mianya ambayo ingeweza kutumika na wadukuzi iweze kuzibwa.

**Hoja nambari 8.7.2.15 Mapungufu ya mfumo wa UVIKO 19 kwenye kuingiza taarifa za washukiwa wa UVIKO 19**

Ukaguzi umebaini mfumo wa UVIKO 19 haujakidhi haja ya mahitaji ya watumiaji wa mfumo (user requirements) kwenye eneo la kuingiza taarifa za washukiwa (suspects) ambapo mfumo unaruhusu kuingizwa baadhi ya taarifa zinazohitajika na watumiaji wa mfumo na kuacha sehemu ya taarifa ambazo ni muhimu katika usimamizi na uratibu wa masuala ya Afya nchini.

Kitendo cha mfumo wa UVIKO 19 kushindwa kupokea taarifa zote za washukiwa wa UVIKO 19 kwa mujibu wa mahitaji ya watumiaji wa mfumo (users requirements) kunapelekea mfumo huu usitumike ipasavyo katika kuingiza taarifa hizi na badala yake watumiaji kutafuta njia mbadala ya kutunza kumbukumbu za taarifa hizo ambapo kwa sasa Wizara ya Afya inatumia programu ya simu janja ijulikanayo kama "KoboCollect" jambo ambalo linasababisha taarifa za UVIKO 19 zisipatikane sehemu moja na kuweka ugumu wa kupata tathimini ya haraka ya hali ya UVIKO 19 ili kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati kwa kuwa baadhi ya taarifa ziko kwenye programuya simu janja na baadhi ziko kwenye mfumo wa UVIKO 19.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kumpatia mtoa huduma mahitaji yake yote ambayo hayakuzingatiwa wakati wa utengenezaji wa mfumo huu ikiwemo mahitaji ya taarifa za washukiwa "suspects" na kumsimamia kwa karibu kuhakikisha kwamba anakamilisha kazi yake kwa mujibu wa mkataba na Sheria za nchi.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara inakiri kuwepo kwa mapungufu ya kutokukamilika kwa mahitaji ya mtoa huduma ambayo hayakuzingatiwa wakati wa utengenezaji wa mfumo wa UVIKO 19 ikiwemo mahitaji ya taarifa za washukiwa "suspects". Hata hivyo, Wizara kwa kushirikiana na Kampuni ya Rahisi walifanya mabadiliko na maboresho ya mfumo kwa kuzingatia upatikanaji wa taarifa linganifu na zile zote zilizokuwa zikikusanywa na App ya Kobocollect ili kukidhi mahitaji. Aidha, "Quality Check" zilikuwekwa katika mfumo huu ili kudhibiti usahihi na ubora wa taarifa za washukiwa katika ukusanyaji wake.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na majibu ya Wizara na haikuwa na hoja zaidi kwa vile ushauri wa Mkaguzi umefanyiwa kazi ipasavyo.

**Hoja nambari 8.7.2.16 Kukatiwa huduma ya mtandao (internet) kwa vituo vinavyoingiza taarifa kwenye mfumo wa UVIKO 19.**

Mtandao (internet) unahitajika kwa ajili ya kuingiza taarifa za upimaji na majibu ya UVIKO 19 kwenye mfumo unaohifadhi na kutoa taarifa hizo. Mfumo huu ulianza kutumika tangu Mwezi Machi 2021, ukaguzi ulibaini kuwa Maabara ya Mnazi Mmoja ilipata mtandao kwa muda wa miezi mitatu pekee yaani, kuanzia mwezi Septemba mpaka Novemba 2021 na kwamba kwa kipindi cha takribani miezi mitano watumiaji wa mfumo walikuwa wanaingiza taarifa kwenye mfumo kwa kutumia "internet" ya simu zao za mkononi wakati kituo cha Lumumba (EOC) kilikuwa hakina huduma hii kwa Zaidi ya mwezi mmoja mpaka tunakamilisha ukaguzi wetu mwezi wa Disemba, 2021 ambapo ili kuingiza taarifa kwenye mtandao na wao pia walilazimika kutumia "internet" za simu zao za mkononi (Mobile Wi-Fi).

Katika kupitia mkataba baina ya Wizara ya Afya na kampuni ya Rahisi ukaguzi ulibaini kwamba kifungu 3.0 (i) kinaitaka kampuni ya Rahisi kutoa huduma ya mtandao kwenye vituo vyote vinavyoingiza taarifa za UVIKO 19 kwenye mfumo ambapo Rahisi ilikata huduma hiyo baada ya kinachodaiwa kucheleweshewa malipo kwenye huduma zake alizokuwa akizitoa kwa Serikali kupitia Wizara ya Afya.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kusimamia vyema utekelezaji wa mkataba huu kwa maslahi mapana ya Serikali kwani sababu iliyotolewa za Rahisi ya kucheleweshewa malipo na kupelekea kukata huduma ya mtandao ingeliweza kuepukika kama Wizara ingelikuwa na usimamizi mzuri wa mkataba huu.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Tatizo la kukatwa kwa huduma ya mtandao lilitokea kutokana na kucheleweshwa malipo kwa Rahisi Solution, baada ya kukamilisha malipo hayo huduma ilirejeshwa, hata hivyo Wizara kupitia kwa Wadau wa Maendeleo iliengeza nguvu ya kuunganisha huduma ya internet ambayo inaendelea kutumika hadi sasa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile kasoro iliyobainishwa na Mkaguzi imerekebishwa na ushauri wa Mkaguzi umetekelezwa ipasavyo. Kamati ya PAC imeridhishwa na majibu ya Wizara

**Hoja nambari 8.7.2.17: Udhaifu wa Mfumo katika kuoanisha huduma za upimaji wa UVIKO 19 na malipo yanayotakiwa kwa kila huduma**

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo UVIKO 19 hauna uwezo wa kuoanisha vipimo vya UVIKO 19 vilivyopo na bei ya kila kipimo, hali hii inapelekea mazingira ambayo mteja anaweza kulipia kipimo cha bei ndogo na kufanyiwa kipimo cha bei kubwa hususani kama muingiza taarifa za malipo hatakuwa na uadilifu na uzalendo kwa nchi yake kwa kuwa kila kipimo kina bei yake. Kutokana na dosari hizo mfumo unaweza kuisababishia hasara Serikali na kuchochea mazingira ya rushwa kwa watu wanaohusika na kuingiza taarifa za malipo ya vipimo mbalimbali vya UVIKO 19.

Kielelezo P: Kinaonesha kuwa mfumo hauna uwezo wa kuonesha na kulinganisha bei ya huduma.

Kielelezo Q: Kinaonesha mteja amepima kipimo cha RT-PCR (Polymerized Chain Reaction) ambacho ni USD 80 lakini amelipia USD 25 ambacho ni malipo ya kipimo cha "Antigen Rapid Test" bila ya mfumo kutambua.

Hivyo, ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya Serikali kufanya uchunguzi ili kuweza kubaini ukubwa wa tatizo hili na kujuwa chanzo chake ili kuweza kuchukuwa hatua stahiki.

Aidha, ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana ya kampuni ya Rahisi kufanya maboresho husika kwenye mfumo huu ili kuondoa udhaifu huu uliobainika kwa haraka iwezekanavyo.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Ni kweli hapo awali mfumo ulikuwa na udhaifu wa kuoanisha malipo na huduma iliyotolewa lakini baada ya kufanyika marekebisho ya kimfumo tatizo

hilo limesawazishwa. Kwa sasa kila huduma inayotolewa imefungamanishwa na gharama halisi ya huduma husika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile kasoro iliyobainishwa na Mkaguzi imerekebishwa na ushauri wa Mkaguzi umetekelezwa ipasavyo. Kamati ya PAC imeridhishwa na majibu ya Wizara

**Hoja nambari 8.7.2.18 Mfumo kutoruhusu usajili binafsi kwa waliosamehewa**

Ukaguzi umebaini kwamba wapimwaji waliosamehewa (exempts) ambao ni pamoja na wanafunzi wanaosoma nje ya nchi, madaktari wanaojitolea nchini, watumishi wa umma, na watu wengine wasiolipia upimaji wa UVIKO 19 hawajawekewa utaratibu wa kufanya usajili binafsi (self registration) kwenye mfumo wa UVIKO 19.

Hali hii inasababisa ucheleweshwaji wa uingizwaji wa taarifa za watu hawa kwa kua inalazimu muingiza taarifa (data entry) kuchukua taarifa za mpimwaji zilizojazwa kwenye fomu maalumu na mtabibu ili kuweza kuziingiza kwenye mfumo, pia taarifa kama vile umri, jinsia, makazi n.k zinaweza kuingizwa kwenye mfumo bila kuzingatia usahihi wake na kupoteza maana ya matumizi ya mfumo.

Ukaguzi unashauri kufanyike marekebisho kwenye mfumo huu ili wapimwaji wote walio samehewa wawekewe utaratibu maalum ili kuweza kufanya usajili binafsi (self registration) kwenye mfumo wa UVIKO 19 hii itasaidia kuingiza taarifa zilizo sahihi na kuondoa ucheleweshwaji wa kuingizwa taarifa zao kwenye mfumo kunakopelekea kucheleweshewa huduma.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Suala la msamaha juu ya huduma ya kupima UVIKO - 19 hapo awali halikuwa na miongozo rasmi hali iliyopelekea kutoingizwa mahitaji yake, aidha baada ya kuandaa muongozo wake Wizara imeona kutokuingiza sehemu ya kujisajili mteja mwenyewe baada ya kupatiwa msamaha kwa kuepusha mianya ya udanganyifu. Hata hivyo, Wizara ya Afya imeuchukuwa ushauri wa CAG wa kufanya marekebisho kwenye mfumo wa UVIKO 19 ili wapimwaji wote waliosamehewa wawekewe utaratibu maalum ili kuweza kufanya usajili binafsi (self registration) kwenye mfumo wa UVIKO 19.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kwa vile kasoro iliyobainishwa na Mkaguzi imerekebishwa na ushauri wa Mkaguzi umetekelezwa ipasavyo. Kamati ya PAC imeridhishwa na majibu ya Wizara

**Hoja nambari 8.7.2.19: Kutokutumika na 'Portal' ya usajili binafsi kwa ajili ya Chanjo za UVIKO 19.**

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa "Portal" maalumu iliyotengenezwa sambamba na moduli ya chanjo za UVIKO 19 yenye uwezo wa kuwaruhusu wanaotaka kuchanjwa kuingiza taarifa zao wenyewe (self registration) kabla ya kufika kwenye kituo kupata chanjo na kuomba nafasi (booking).

Hata hivyo ukaguzi umebaini "portal" hii haijawahi kutumika tangu kutengenezwa kwake.

Moja ya athari za kutotumika kwa portal hii ni pamoja na kucheleweshwa kwa upatikanaji wa vyeti vya chanjo kwa wakati kwa kua inachukua muda mwingi kuingiza taarifa za wachanjwaji kwenye mfumo na zikiingizwa mara kadhaa zinakua sio sahihi kama inavyotarajiwa.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kwa kuzingatia umuhimu wa upatikanaji wa chanjo za UVIKO 19 itoe elimu kwa wananchi na kuwahamasisha juu ya uwepo na matumizi ya "Portal" hii na namna ya kuitumia pamoja na mufaa yake ili ianze kutumika na kupunguza ugumu wa kazi za uingizwaji wa taarifa kama ilivyo sasa na tija kwenye taarifa zinazo kusanywa.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara ya Afya imepokea ushauri kutoka kwa CAG wa kuhamasisha jamii juu ya matumizi ya moduli ya chanjo ya UVIKO - 19 kwa mteja kujisajili mwenyewe kwenye mfumo. Aidha Mfumo huu bado unaendelea kuimarishwa ili kurahisisha usajili huo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Wizara kukubaliana kuwepo kwa hoja ya Mkaguzi. Hata hivyo, bado Wizara inakazi kubwa ya kufanya ili kuhakikisha 'portal' iliyopo inafanyiwa kazi kama ilivyokusudiwa.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kuendelea kuimarisha mfumo huo wa "portal" ili uweze kurahisisha utendaji.

**Hoja nambari 8.7.2.20: Udhaifu wa mfumo katika kuingiza tarehe za kufanya chanjo ya pili (Second Dose).**

Katika ukaguzi uliofanyika ilibainika kwamba Moduli ya chanjo ina udhaifu kwenye kuingiza tarehe ya chanjo ya pili wakati mchanjwaji amekwisha chanjwa ambapo mfumo unarudisha nyuma tarehe kwa siku moja. Kwa mfano, mtu amechanjwa tarehe 21/01/2022 ukiingiza kwenye mfumo tarehe hii unakupeleka tarehe 20/01/2022.

Hali hii inawalazimu waingiza taarifa za chanjo kwenye mfumo wawe wanaweka tarehe ya siku moja mbele ili kupata tarehe sahihi ya chanjo kwenye kumbukumbu za mchanjwaji.

Aidha, ukaguzi unaishauri Wizara kuisimamia kampuni ya Rahisi Solution katika kutatua changamoto hii ya mfumo mapema iwezekanavyo ili kuondoa usumbufu kwa waingiza taarifa na hatari ya kukosea kuingiza tarehe.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Mfumo wa UVIKO 19 haukuwa na uwezo wa kuingiza chanjo ya pili wakati ulipotengenezwa, lakini marekebisho yalifanyika na kwa sasa mfumo huo unaweza kuingiza chanjo ya pili kwa wateja wanaochanja dozi mbili, lakini pia (Booster dose).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC Iimeridhika na hatua zilizochukuliwa na Wizara zilizohakikisha kuwa mfumo unaweza kuingiza chanjo ya pili kwa wateja.

## 8.8.1 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI MFUMO MALARIA

Katika ukaguzi wa Mfumo wa Malaria unaosimamiwa na Programu ya Kudhibiti Malaria Zanzibar (Zanzibar Malaria Control Program) mambo mbali mbali yalibainika ikiwemo dosari zifuatazo: -

**Hoja nambari 8.8.1.1: Kutokuwepo kwa eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery site/offsite).**

Eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site) ni eneo mbadala maalum linalotengwa kwa lengo la kutumiwa wakati yanapotokea maafa au miundombinu kushindwa kufanya kazi kama inavyotakiwa (major failures of the system) kwenye eneo la kazi la kila siku na kupelekea kuharibika kwa miundombinu ya TEHAMA na kushindwa kuzipata taarifa zilizomo ndani ya mfumo. Eneo hili hutengwa mbali na eneo la kila siku kwa

angalau umbali wa Kilometa 50 ili kupunguza uwezekano wa kuathiriwa kwa maeneo yote mawili kwa wakati mmoja yanapotokea maafa.

Eneo hili linatakiwa kuwa na ukamilifu wote kama lilivyo eneo linalotumika kila siku kwa maana ya miundombinu yote na usalama kuzingatiwa kiasi kwamba wakati wowote eneo hili linaweza chukua nafasi ya eneo linalotumika kila siku.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa kampuni ya "Zanzibar Malaria Control Program (ZMCP) au Zanzibar Malaria Elimination Program (ZAMEP)" wala Wizara hazina eneo mbadala maalumu lililoandaliwa kwa lengo la kuweka nakala za taarifa zote za mfumo moja kwa moja kulingana na matukio yanayoendelea kila wakati (real time events).

Kutokuwekwa eneo la kuendeleza utendaji kazi mfumo baada ya matatizo kutokea kunaweza kusababisha upotevu wa taarifa muhimu za Serikali na kuathiri utendaji kazi wa Wizara katika kuwahudumia wananchi jambo ambalo litakuwa na madhara mbalimbali kiuchumi na kijamii.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kutengeneza eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa kulingana na miongozo ya TEHAMA ya kitaifa na kimataifa (best practice) kwa uharaka wa kutosha ili kuilinda taarifa mali (information asset) za Serikali ambazo kimsingi zimeigharimu Serikali fedha, muda na nguvu katika kuzikusanya, kuzichakata na kuzihifadhi.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Mfumo wa ukusanyaji taarifa kwa ajili ya ufuatiliaji wa ugonjwa wa malaria umewekwa katika Wakala wa miundombinu ya TEHAMA ya Serikali (ZICTIA) chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya, hata hivyo kutokana kukosekana eneo la kuendeleza mfumo ambalo linaendana na viwango vya kisheria. Wizara ya Afya imeandaa eneo la muda la kuendeleza mfumo (recovery data center) ndani ya Makao Makuu ya Wizara wakati ikisubiria Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA ya Serikali akamilishe eneo mbadala la kuendeleza mifumo yote ya Wizara ya Afya ikiwemo mifumo ya malaria. Hata hivyo, Wizara ya Afya imefanikisha ununuzi wa saver mbili pamoja na vifaa vya solar kwa ajili ya buckup ya umeme.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imeridhishwa na hatua za awali zilizochukuliwa na Wizara ya Afya na kusisitizwa kuhakikisha inafuatilia upatikanaji wa eneo husika kwa wakati.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara kuendelea kutafuta eneo mbadala la kuendeleza mfumo baada ya maafa kulingana na miongozo ya TEHAMA ya kitaifa na kimataifa (best practice).

**Hoja nambari 8.8.1.2: Kukosekana kwa mpango wa kuendeleza biashara (Business Continuity Plan).**

Kwa mujibu wa Sera za eGaz kifungu cha 4.4.1.2 (d) inazitaka taasisi za Serikali zenye mifumo kuanzisha mpango na miundo mbinu ya kuendeleza mfumo na taarifa zake zote baada ya maafa yoyote yatakayojitokeza dhidi ya mfumo husika. Mpango huo unatarajiwa kuelezea hatua gani zitachukuliwa kabla ili kuweza kuzirudisha taarifa za mfumo zote yatakapotokea majanga kama udukuzi, majanga ya kimaubile au yanayosababishwa na binaadamu yatakayo haribu taarifa au miundo mbinu ya mfumo na kupelekea kupotea kwa taarifa hizo.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa Wizara kupitia ZAMEP haina kabisa mpango huo unaotarajiwa kutoa muongozo ambao utafuatwa kabla na baada ya majanga kutokea ili kuokoa taarifa za mfumo

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Ushauri wa Mdhibiti tumeuchukua na tumeanza kuufanyia kazi kwa mifumo mengine ambayo ipo chini ya Programu ya kumaliza Malaria. Hivyo Wizara kupitia program ya Malaria kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imefanikiwa kupata Mshauri Elekezi kwa ajili ya kufanya maboresho ya mifumo iliopo chini ya program ya malaria pamoja na upatikanaji wa nyaraka muhimu ikiwemo “Business Continuity Plan”

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya juhudi ambazo Wizara imezichukua lakini Kamati haijaridhishwa kwa vile ni muda mrefu umepita tangu Mkaguzi awasilishe hoja hiyo (takriban miaka miwili) lakini ndio kwanza Wizara ipo kwenye mpango wa utekelezaji wakati hivi sasa ilitakiwa Mpango huo uwe unafanyakazi ipasavyo.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inakamilisha unapatikanaji wa Mpango wa Uendelezaji Biashara (Business Continuity Plan) ili uweze kutumika kwa maslahi ya Wizara na Taifa kwa ujumla.

**Hoja nambari 8.8.1.3: Kukosekana kwa mpango wa uhamishaji wa taarifa (Data Migration Plan)**

Uhamishaji wa Taarifa ni mchakato wa unaohakikisha kwamba taarifa zote zinazohitajika kwa kuzingatia "format" ya taarifa zinahamishwa kutoka kwenye kanzi data moja kwenda nyengine ambayo itaruhusu taarifa husika kutumika kwa mujibu wa matarajio ya watumiaji. Vitu vya kuzingatia kwenye zoezi la kuhamisha data ni pamoja na "data conversion" pale inapobidi ambayo inachangiwa na tofauti kwenye "field formats or sizes", miundo ya faili/kanzi data na "coding schemes".

Hata hivyo ukaguzi umebaini kuwa ZAMEP pamoja na Wizara ya Afya hakuna mpango wa kufanya uhamishaji wa taarifa za Malaria zilizomo kwenye mfumo wa Malaria ambao unatarajiwa kukoma kutumika ndani ya kipindi cha miezi michache kuanzia sasa.

Hali hii inaweza kupelekea kukosekana kwa taarifa zote muhimu wakati wa zoezi la kuhamisha taarifa kutoka kwenye mfumo wa awali kuja kwenye mfumo mpya, pia inaweza pelekea zoezi la kuhamisha taarifa kuonekana kuwa gumu na lisilo na tija kwa Serikali kwa sababu ya kukosekana kwa mpango sahihi.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na ZAMEP kuandaa mpango huu kabla ya kuanza zoezi la kuhamisha taarifa husika na kuutumia mpango huo wakati wa kutekeleza uhamishaji wa data hizo.

**Majibu ya uongozi wa Wizara**

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na ZAMEP na wadau wake imefanya "data migration" ambapo taarifa zetu zote zilizokuwa zinapatikana katika mfumo wa MEEDS sasa zinapatikana katika mfumo wa DHIS2.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imeridhishwa na majibu za Wizara za kuufanyika kazi ushauri wa Mkaguzi.

**UCHUNGUZI KUHUSU UKAGUZI WA RIPOTI YA TEHAMA KWA WAKALA WA SERIKALI MTANDAO (EGAZ) KWA MWAKA 2020/2021**

**MFUMO WA ZANMALIPO WA ZAMANI**

**Hoja nambari 12.8.1.1: Uwekezaji usiokuwa na tija kwenye kutengeneza mfumo shilingi 96,000,000**

Ukaguzi umebaini kufanyika kwa uwekezaji usiokuwa na tija wenye thamani ya zaidi ya shilingi 96,000,000 kwa ajili ya kutengeneza mfumo wa ZanMalipo wa zamani, kazi iliyofanywa na wataalamu wa ndani chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango mwaka 2021 ambapo mfumo huo haukuweza kukidhi mahitaji ya biashara (business requirements) na mahitaji ya watumiaji (users' requirements) ndani kipindi kifupi cha miezi 5 na kupelekea kusitishwa utekelezaji wake.

Hali hii imeisababishia Serikali hasara ya moja kwa moja isiyopungua shilingi 96,000,000 na hasara nyengine zisizo za moja kwa moja kama vile muda uliotumiwa na wataalamu wa Serikali kwenye utengenezaji wa mfumo husika, rasilimali nyengine kama vile umeme, mtandao na miundombinu ya TEHAMA iliyonunuliwa kwa ajili ya mfumo huo n.k. ambavyo havikuweza kuthaminishwa kwenye fedha kwa sababu ya kukosekana kwa kumbukumbu zake.

Ukaguzi unashauri kufanyika mambo yafuatayo: -

- eGAZ kuhakikisha inazingatia miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kama vile "Software Development Life Cycle" katika utengenezaji wa mifumo ya kielektroniki ili kuepusha hatari za kushindwa kukidhi matakwa ya kiusalama, usiri, tija na ufanisi kwa kuzingatia mahitaji ya biashara na watumiaji kwa kuwa miongozo hiyo imekwisha tumika kwenye sekta ya TEHAMA kwa muda mrefu na kuthibitika kuwa na ufanisi wa kutosha.

- Kuzingatiwa kwa weledi katika kazi zote za utengenezaji wa mifumo ya kielektroniki kwenye hatua mbali mbali bila kujali misukumo (pressures) inayokuwepo kutoka kwa wadau mbali mbali ambayo mara nyingi inakuwa haizingatii weledi, ukubwa na uzito wa kazi, na masuala mengine kama vile usalama, usiri, tija na ufanisi wa mifumo ya kielektroniki.

- eGAZ kufanya tathmini ya kina na kuandika ripoti kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwenye visababishi vilivyopelekea mfumo wa ZanMalipo wa zamani kushindwa kufikia malengo yake na kupelekea kusitiswa na kuanzisha mfumo mwengine ili kupata fundisho lililotokana na mazingira ya ndani ya nchi litakalo weza kutumika kama rejea

(reference) kwenye kuboresha utengenezaji wa mifumo ya kielekitroniki kwa kutumia wataalamu wa ndani.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Mfumo wa ZanMalipo wa zamani ulitengenezwa chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ambapo ilihusisha Msimamizi wa Mradi na Mratibu kutoka Ofisi hiyo pamoja na wataalamu wengine kutoka katika taasisi mbali mbali za umma. Wakala wa Serikali Mtandao ilishirikishwa kwa kutakiwa kutoa watendaji watatu (3) katika eneo la miundombinu (1), usanifu mifumo (1) na uchambuzi wa mifumo (1).

Kuhusu hoja ya ushirikishwaji wa wadau, Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) ilifuatilia na kubaini kuwa mahitaji ya mfumo yalikusanywa kutoka kwa wadau upande wa Pemba na Unguja, hali iliyopelekea kupatikana kwa nyaraka kuhusiana na mahitaji ya mfumo.

Aidha, eGAZ ilifuatilia matumizi ya shilingi 96,000,000 kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, fedha hizo zilitumika kwa manunuzi ya vifaa na vitendea kazi ambavyo vinaendelea kutumika katika mfumo wa ZanMalipo Mpya.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC haikuridhirishwa na Majibu ya Wakala kwa vile Wakala ulishindwa kumpatia Mkaguzi vielelezo vya matumizi ya shilingi 96,000,000 wakati wa ukaguzi unafanyika huku wakitambua kwamba Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma inaelekeza wazi kwamba vielelezo viambatanishwe na hati za malipo mara tu baada ya kukamilika kwa matumizi.

Sambamba na hilo, Kamati imebaini kuwa msimamizi wa mfumo huo hakuwa na uwezo wa kuusimamia ipasavyo.Aidha, Kamati imebaini kwamba wakati Mkaguzi anafanya kazi zake za ukaguzi, hakukuwa na ripoti ya tathmini inayoonesha kuwa mfumo huo haufai.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Wakala wahakikishe wanatoa ushirikiano wa kutosha kwa Mkaguzi ili aweze kupatiwa vielelezo anavyovihitaji na sio kusubiri hadi Kamati kufika katika Ofisi zao.

**Hoja nambari 12.8.1.2: Kutozingatiwa kwa miongozo ya Viwango bora vinavyokubalika katika utengenezaji wa mfumo "SDLC"**

"Software Development Life Cycle (SDLC)" ni mpangilio wa kimantiki (logical process) unaotumiwa na wachambuzi na wasaidizi wa mifumo ya kielektroniki (system analysts and developers) katika kutengeneza mifumo. "SDLC" inapelekea kupatikana kwa mifumo yenye ubora wa juu inayokidhi au kuzidi mahitaji ya biashara na yale ya watumiaji na kwamba mifumo husika inakamilika ndani ya wakati na bajeti na kuleta tija na ufanisi. Mifumo inayotenegenezwa kwa kuzingatia "SDLC" pia huwa na gharama nafuu za matengenezo na maboresho ambazo zinahakikisha matumizi endelevu ya mfumo (cost effective maintenance and enhancements).

Ukaguzi umebaini kwamba utengenezaji wa mfumo wa ZanMalipo wa zamani haukuzingatia miongozo ya "SDLC" jambo ambalo limepelekea mfumo huu kushindwa kukidhi haja za biashara na mahitaji ya watumiaji ndani ya kipindi cha miezi 5 tangu ulipoanza kutumika hali iliyopelekea kuisababishia Serikali hasara ya moja kwa moja kwenye gharama za uwekezaji wa kutengeneza mfumo zinazozidi shilingi 96,000,000 na hasara nyengine za kushindwa kudhibiti na kusimamia ukusanyaji wa mapato kama ilivyotarajiwa na kusababisha upotevu wa mapato.

Aidha, kurudisha nyuma jitihada za Serikali katika kutegemea TEHAMA ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi na kupunguza gharama kwa Serikali za kuwafi kiwa wananchi vimekwamishwa na udhaifu huu ambao ungeweza kuepukika kama miongozo ya "SDLC" ingezingatiwa tangu mwanzo wa utengenezaji wa mfumo huu.

Ukaguzi unaishauri Wakala wa Serikali mtandao kuzingatia "best practice guidelines" kama vile "SDLC" katika utengenezaji wa mifumo yote ya kielektroniki ili kuisaidia Serikali kuepuka hasara za aina mbali mbali kama zilivyojadiliwa hapo juu na kuongeza tija na ufanisi katika kuwahudumia wananchi na kuongeza makusanyo ya Serikali.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

eGAZ ilifuatilia hoja hiyo na kubaini kuwa utengenezaji wa mfumo huo ulizingatia viwango na miongozo bora ya utengenezaji wa mifumo (SDLC). Kutokana na uhitaji wa haraka wa kuwa na mfumo wa kudhibiti mapato ya Serikali ikizingatiwa kwamba Serikali ilikuwa imeshafanya mabadiliko na

kupitisha Sheria ya kutambua miamala ya kielektroniki na kuhitaji mfumo huo kuanza kutumika ifikapo Julai, 2020. Pamoja na uharaka wa utayarishaji mfumo huu, kipengele muhimu cha kukusanya mahitaji ya watumiaji kwa mujibu wa utaratibu na kuweka mfumo hewani kabla ya kufanyiwa majaribio ya uhakika kilizingatiwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kaatika kuthibitisha kilichoelezwa na Wakala, Kamati ilihitaji kupatiwa vielelezo lakini lakushangaza vielelezo vilivyoletwa ilibainika kuwa sio nyaraka kamili isipokuwa ilikuwa “draft document”. Aidha, ‘draft’ hiyo imefuata sehemu ya muongozo wa utengenezaji wa mfumo na sio kufuata viwango na miongozo bora ya kutengeneza mifumo. Kwa mnasaba huo, Kamati haikuridhika na majibu ya Wakala kwa vile uandaaji wa mfumo huo haukuzingatia miongozo bora ya utengenezaji.

**Ushauri wa Kamati ya PAC**

Mifumo ya TEHAMA inapoandaliwa ifuate miongozo ya kitaalamu ili kuepusha changamoto zinazoweza kujitokeza baadae.

**Hoja nambari 12.8.1.3: Kukosekana kwa nyaraka muhimu za usimamizi wa matumizi ya mfumo.**

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo wa ZanMalipo wa zamani hauna nyaraka zozote zinazohusiana na mfumo ikiwa ni pamoja na nyaraka muhimu katika matumizi ya mfumo inayoelezea namna mfumo unavyofanya kazi (system operations manual), nyaraka inayoelezea namna mfumo ulivyosanifi wa (system architecture document), nyaraka inayoelezea namna mfumo ulivyosanidiwa (system confi gurations manual), na nyaraka nyingine kama vile za mahitaji ya mfumo (system requirements document), na ile ya kuidhinisha matumizi ya mfumo baada ya kujaribiwa na kukidhi vigezo (Users Acceptance Certifi cate) n.k ambapo ni kinyume na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika katika utengenezaji wa mifumi ya kielektroniki kama vile SDLC. Kutokuwepo kwa nyaraka hizo kunaweza kutokezea athari zifuatazo:-

- Mfumo kuwa ni mali ya mtu/watu wachache badala ya taasisi, hali hii inatokana na ukweli kwamba aliyeutengeneza na wanaoutumia mfumo kwa sasa ndio wanafahamu kilichomo kwenye mfumo na namna kinavyofanya kazi kwa sababu hakijaandikwa kwenye nyaraka yoyote ile, mtu huyu au kikundi cha watu hawa ikitokea hawapo ofi sini basi mfumo

hautaweza kutumika katika namna ambayo ni endelevu na kuinyima taasisi haki ya kunufaika na uwekezaji uliofanywa na Serikali.

- Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia mahitaji yote ya watumiaji ya sasa na ya wakati ujao katika usalama, udhibiti, ufi kiaji, matumizi, urahisi wa kuutumia n.k kwani uandishi wa nyaraka mbalimbali za mfumo unawapa nafasi wadau mbali mbali wa mfumo kuchangia mawazo yao katika namna ambayo ni rasmi ikiwa ni pamoja na kutathmini na kuidhinisha nyaraka husika ili kuendelea na hatua nyengine jambo linalo changia kuboresha mfumo unaotengenezwa.
- Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia hali halisi ya mabadiliko ya teknolojia na kusababisha mfumo husika kuwa na upeo mdogo kwa kushindwa kuwasiliana na mifumo mengine kirahisi kwa sababu ya utofauti wa teknolojia jambo ambalo linarudisha nyuma urahisishaji wa kazi kwa kutumia TEHAMA.
- Tasisi kushindwa kufahamu uwekezaji halisi kwenye mfumo ikiwa ni pamoja na gharama, muda na jitihada zilizotumika hadi kukamilika kwa mfumo , jambo hili hutokea pale ambapo hakuna bajeti ya muda mfupi na mrefu kwa ajili ya kutengeneza mfumo wote.
- Taasisi kushindwa kudhibiti matumizi, muda na ubora wa mfumo husika kwa sababu hakuna mpango kazi ulioandikwa na kuidhinishwa na uongozi wa taasisi.
- Taasisi kushindwa kufanya maboresho au mabadiliko kulingana na mahitaji kwenye mfumo kwa kuwa haifahamiki au haikumbukwi namna mfumo ulivyo sanifi wa na kutengenezwa.

Kwa kuzingatia uhalisia uliopo kwamba, mfumo wa ZanMalipo wa zamani bado unatumika kwenye baadhi ya taasisi za umma na kwamba eGAZ haina mpango maalumu unao onesha muda ambao mfumo utakuwa umetolewa kwenye matumizi, ukaguzi unaishauri eGAZ kufanya yafuatayo: -

a) Kuchukuwa jitihada za makusudi za kuandaa nyaraka zote muhimu za matumizi, usimamizi na uendeshaji wa mfumo wa ZanMalipo wa zamani kwa kuzingatia miongozo ya viwango bora vinavyokubalika.
b) Kuhakikisha kwamba nyaraka husika zinapatikana kwa ajili ya matumizi ya ndani ya taasisi ikiwa ni pamoja na matumizi ya ukaguzi.
c) Kutatua changamoto mbali mbali zinazoukabili mfumo wa ZanMalipo wa zamani ili kuondoa udhaifu uliopo sasa unaosababisha Serikali kupoteza mapato kwa njia mbali mbali.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Katika utayarishaji wa Mfumo wa zamani wa ZanMalipo eGAZ ilitoa mtaalam katika eneo la uchambuzi wa mifumo. Mtaalam kutoka eGAZ aliweza kuandaa nyaraka zifuatazo; System Requirements Specification, System Design Document ambayo ndani yake imejumuisha System Architecture, System Operation Manual, na API Document.

Aidha, kutokana na uhitaji wa haraka wa mfumo huu baadhi ya nyaraka hazikuweza kukamilishwa kuandaliwa na baada ya kusitishwa kwa matumizi ya mfumo huu nyaraka hizo hazikuandaliwa ikiwemo "configuration manual". Kwa upande wa nyaraka ya "user Acceptance Scenario" iliandaliwa lakini hazikuwahi kutumika kwa watumiaji na kuweza kujiridhisha kuwa mahitaji ya mfumo yamekidhi mahitaji yao.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa nyaraka zote wakati wa ukaguzi hazikupatikana lakini hata nyaraka ambazo eGAZ wamewasilisha mbele ya Kamati ni nyaraka ambazo bado zipo katika hatua za maandalizi "draft version" na sio nyaraka ambazo tayari zimethibitishwa na uongozi wa eGAZ "approved version". Kwa mnasaba huo, Kamati haikuweza kuthibitisha uhalali na usahihi wa nyaraka hizo. Hivyo haikuridhika na majibu ya Wakala.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala ihakikishe inawasilisha nyaraka halisi (zilizopitishwa na uongozi wa Wakala) ili zikihitajika ziweze kuwa vielelezo vinavyokubaliwa kimatumizi.

**Hoja nambari 12.8.1.4: Kutofahamika kwa bajeti ya utekelezaji wa mfumo wa zamani wa ZanMalipo**

Kwa mujibu wa Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2016 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2021 kumewekwa utaratibu unaolazimisha taasisi za umma kuandaa bajeti kwa ajili ya kutekeleza mipango ya taasisi husika kabla ya kuanza utekelezaji wa kazi husika, bajeti hii hupaswa kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kabla ya kuanza kutumika. Pamoja na manufaa mengine yaliyopo kwa kuandaa bajeti ni udhibiti wa matumizi yanayofanywa na taasisi za umma pamoja na kuweka uwazi na uwajibikaji.

Hata hivyo, Wakala wa Serikali Mtandao imeshindwa kuupatia ukaguzi nyaraka za Bajeti ya utekezaji wa mfumo wa ZanMalipo wa zamani ambazo nyaraka hizo zilitarajiwa kuonesha kiwango cha makisio ya fedha yaliyotarajiwa kutumika kwa ajili ya utengenezaji, usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa mfumo huo.

Kutokuwepo kwa bajeti ya utekelezaji wa mfumo huo kunapelekea taasisi kushindwa kufanya tathmini ya ufanisi wa mipango yake kwa kulinganisha na gharama halisi kwenye utekelezaji (budget Vs actual costs), kunasababisha ugumu kwenye kazi za ukaguzi, ni kuvunja Sheria na Kanuni za Nchi zilizowekwa kwa nia njema ya kufanya usimamizi na matumizi bora ya rasilimali za Serikali. Uwepo wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali kwa jina la gharama za utengenezaji wa mfumo ni mojawapo ya athari zinazoweza kujitokeza kwa sababu ya kutokuwa na bajeti ambayo inaweka udhibiti wa matumizi hayo.

Ukaguzi unaishauri eGAZ kufanya yafuatayo: -

Kufanya mawasiliano na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba inapata bajeti iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mfumo wa ZanMalipo wa zamani kwa matumizi ya ndani ya taasisi kwa madhumuni kama ilivyoainishwa hapo juu.

Kwa manufaa ya siku zijazo, ukaguzi unashauri eGAZ kuhakikisha takwa la uwepo wa bajeti linazingatiwa kabla ya kutengeneza au kununua mfumo au miundombinu yoyote ya TEHAMA ili kuepuka kuvunja Sheria za nchi.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Kwa vile mfumo huu uliandaliwa na kusimamiwa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, eGAZ iliiandikia Wizara husika na kuomba kupatiwa bajeti iliotumika katika utayarishaji wa mfumo wa ZanMalipo wa zamani. Pia Wakala ilifanya ufuatailiaji na kupatiwa taarifa ya matumizi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati inakubaliana na hoja hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali licha ya juhudi za Wakala wa Serikali mtandao katika kuijibu hoja hii mbele ya Kamati.

**Hoja nambari 12.8.1.5: Udhaifu wa mfumo katika utengenezaji wa Nambari za Udhibiti (Control Numbers)**

Ukaguzi umebaini uwepo wa udhaifu katika hatua ya kuchakata taarifa (Data processing) katika Mfumo wa ZanMalipo wa zamani hali ambayo imepelekea kutolewa nambari za udhibiti zaidi ya moja zenye taarifa zinazofanana kwenye ombi moja la kutengeneza "control number" kwa wakati mmoja, kurudia namba za udhibiti lakini pamoja na kutoa nambari za udhibiti ambazo zikipelekwa benki ya PBZ kwa ajili ya kufanyiwa Malipo zinabainika kuwa hazifanyi kazi kunapelekea kujitokeza kwa usumbufu mkubwa kwa wananchi na kusababisha kuikosesha mapato Serikali. Ukaguzi unaishauri Wakala wa Serikali Mtandao kufanya yafuatayo:-

Kuhakikisha kuwa mfumo wa ZanMalipo mpya unafanyiwa majaribio kwa kina katika kuangalia changamoto za ZanMalipo ya zamani ili kuhakikisha kwamba hazijirudii kwenye ZanMalipo mpya.

Kufanya tathmini ya kina ili kubaini chanzo cha kutofanya kazi kwa baadhi ya nambari za udhibiti pindi zinapopelekwa benki ya PBZ kufanyiwa malipo kwa kushirikiana na wataalamu wa mfumo wa MUTM na Benki ya PBZ. Kutatua changamoto itakayobainika kwenye chanzo cha changamoto husika ili kundoa kabisa tatizo hili.

Kutekeleza mfumo wa ZanMalipo mpya kwa uharaka wa kukidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa ili kuona kama udhaifu wa nambari za udhibiti kutofanya kazi wakati wa kufanyiwa Malipo litatatulika.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

eGAZ baada ya kukabidhiwa mfumo huo ilifanya tathmni ya kiusalama na kuweza kugundua dosari mbali mbali zilitokana na uwezo mdogo wa utaalam wa kutengeza mifumo ya kifedha hali ilivyopelekea kuwepo na changamoto zifuatazo:-

- Usalama wa mifumo ya kifedha katika ukusanyaji mapato
- Upotevu wa mapato
- Udhaifu wa "control number" ambazo hazilipiki.
- Uwepo wa kujirudia rudia kwa namba za udhibiti

Kutokana na hilo, eGAZ ilichukua hatua ya kuusitisha mfumo wa ZanMalipo wa zamani na kuanza jitihada za kuandaa mfumo mpya ili kuweza kudhibiti mapato ya Serikali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini uwepo wa dosari kubwa kuhusiana na uimara na usalama wa mfumo wa zamani wa ZanMalipo kama alivyoeleza Mkaguzi. Hivyo, Kamati inaungana na hoja ya Mkaguzi kwa vile haikuridhika na majibu ya Wakala.

**Hoja nambari 12.8.1.6: Kutumika vibaya kwa mianya inayotokana na udhaifu wa mfumo**

Ukaguzi umebaini kuwa kuna mianya ambayo imekuwa ikitumika vibaya na baadhi ya watumiaji wa mfumo wa MUTM uliounganishwa na mfumo wa ZanMalipo wa zamani katika kutengeneza nambari za udhibiti kupitia POS zilizounganishwa na mfumo wa MUTM na kupeleka fedha benki ya PBZ.

Wakusanya mapato wanapewa Nambari ya udhibiti (Control Number) kila mwisho wa siku ya kazi kwenye maeneo yao, nambari hiyo inaendana na kiwango walichokusanya ili waweze kuzipeleka fedha hizo benki. Hata hivyo, ukaguzi umebaini baadhi ya wakusanya mapato hawaendi benki kwa wakati na kuziacha nambari za udhibiti kumaliza muda wake kwa makusudi (expire) au kuzungumza na mtu mwenye akaunti yenye uwezo wa kuzighairisha "Cancel" na kupanga kulipa siku anayoitaka mkusanya mapato, kama akiaumwa basi huomba atengenezewe "control number" nyengine na mtu mwenye uwezo wa kutengeneza namba hiyo ambapo anaweza kutengeneza nambari ya udhibiti na kuipa kiwango chengine ambacho sio halisi kama kilivyokusanywa katika siku husika.

Hali hii inaweza kusababisha wakusanya mapato kutumia fedha za Serikali kwa lengo la kuzirejesha siku nyengine lakini wakashindwa kuzilipa kwa uaminifu na kuisababishia upotevu wa mapato na kupelekea kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri Wakala kufanya tathmini ya mapungufu yaliyobainika kwenye matumizi ya mfumo wa ZanMalipo wa zamani uliounganishwa na mfumo wa MUTM na mifumo mengine ili kuchukuwa hatua za makusudi kuzuia upotevu wa fedha za Serikali kwenye mifumo yote miwili ya ZanMalipo (wa zamani na wa sasa)

Aidha, ukaguzi unaishauri Wakala kuhakikisha kwamba tatizo la kutofanya kazi kwa nambari za udhibiti zinapotakiwa kulipiwa Huduma ya benki ya PBZ

kunapatiwa ufumbuzi wa kudumu ili isitumike kama chanzo cha upotevu wa mapato ya Serikali.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

eGAZ ilifuatilia hoja hiyo na kuweza kubaini kuwa ni kweli Mfumo wa Zamani wa ZanMalipo ulikuwa na uhitaji (functionality) wa kutengeneza nambari ya udhibiti kwa watumiaji wa POS ambapo mkusanyaji wa mapato anaruhusiwa kukusanya mapato kuanzia asubuhi hadi mwisho wa siku na kutengeza control number moja ili waweze kulipa ya siku nzima.

Hata hivyo, utaratabu huu haukuwahi kutumika katika mfumo wa ZanMalipo wa zamani na eGAZ ilizuwia kutokutumika vibaya mianya hiyo ya udhaifu wa mfumo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imeridhika na hoja hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa vile Wakala haukuwa na majibu yenye kuiridhisha Kamati.

**Hoja nambari 12.8.1.7: Kukosekana kwa ripoti mbali mbali za mapato kutoka kwenye mfumo**

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo wa ZanMalipo wa zamani hauna uwezo wa kutoa ripoti mbali mbali za makusanyo ya mapato ya Serikali kwa lengo la kurahisisha ufanyaji wa Kimaamuzi kwa wakati. Aidha, Wakala wa Serikali Mtandao umeshindwa kuupatia ukaguzi ripoti mbali mbali za mapato zilizoombwa kwa ajili ya kazi za ukaguzi kutoka kwenye mfumo, ripoti hizo zilitarajiwa kuwa na uwezo wa kuonesha taarifa za makusanyo ya fedha za Serikali kwa kuzingatia “parameters” mbali mbali kama vile makusanyo kwa kila taasisi au taasisi zote za Serikali, kwa siku, wiki, mwezi, miezi mitatu, nusu mwaka na mwaka mzima, makusanyo kwa kuzingatia vyanzo mbali mbali vya mapato n.k.

Kukosekana kwa ripoti hizo kunauweka mfumo wa ZanMalipo kwenye kundi la mifumo isiyokuwa na ufanisi katika kuisaidia Serikali kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati jambo ambalo ni kinyume na matarajio ya uwepo wa mfumo husika na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa eGAZ kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba mfumo huu unakuwa na ripoti zote muhimu (basic reports) zinazoweza kuwasaidia maafisa masuuli na Serikali kwa ujumla kupata taarifa zilizochakatwa na kutafsiriwa ili kurahisisha ufanyaji wa maamuzi sahihi na kwa wkati ili kuleta tija na kuongeza ufanisi, uwazi, na uwajibikaji kwenye taasisi za umma.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Mahitaji ya ripoti mara nyingi huwa yanawekwa mwishoni katika utengenzaji wa mfumo. Katika kipindi cha ukaguzi mfumo huu ulikuwa katika hatua za majaribio (pilot) ili kuweza kugundua kasoro na kuzirekebisha kabla ya kwenda hewani kwa taasisi zote za Serikali. Hata hivyo, mfumo huo ulikuwa na "dashboard" ambayo ilikuwa inaonesha makusanyo ya mapato katika Taasisi ambazo zinatumia Mfumo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC kwa ujumla imebaini kuwa kwenye mfumo wa ZanMalipo wa Zamani kuna viashiria vingi vya kupotea kwa fedha za Serikali. Kwa mnasaba huo, Kamati haikuridhika na majibu ya Wakala na kuungana na hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaitaka Wakala wa Serikali Mtandao kutoa ripoti ya kina inayoeleza sababu za msingi za mfumo huo wa ZanMalipo kufeli.

**MFUMO ZANMALIPO MPYA**

**Hoja nambari 12.8.2.1: eGAZ Kutokuwa na Bajeti ya Utekelezaji wa Mfumo Mpya wa ZanMalipo**

Ukaguzi umebaini kwamba eGAZ inafanya utekelezaji wa mfumo mpya wa ZanMalipo ambao ulianza kufanya kazi mwishoni mwa mwaka 2021 pasipo kuwa na bajeti ya kufanya kazi hizo. Ukaguzi ulifahamishwa kwamba bajeti ya utekelezaji wa ZanMalipo mpya iko Ofisi ya Rais Fedha na Mipango (ORFM) na kwamba panapohitajika fedha kwa ajili ya kazi mbali mbali za utekelezaji wa mfumo huo eGAZ inaandaa mpango kazi kwa ajili ya kutekeleza kazi husika na kuuwasilisha ORFM kwa ajili ya kufanyiwa Malipo.

Hali hii inaweza kupelekea kutopatikana kwa ufanisi katika utekelezaji wa mfumo ikiwa ni pamoja na kazi za mbali mbali za mfumo kutofanyika kwa wakati na kukosa urahisi wa kubadilisha mipango kazi "flexibility" katika utekelezaji kwa sababu bajeti na fedha za utekelezaji huo zipo kwenye taasisi nyengine ambayo pia inaweza kuwa na vipaumbele tofauti katika majukumu yake ya kila siku na kuweka mipango kazi ya eGAZ kwenye umuhimu mdogo.

Aidha, hali hii inaongeza ugumu wa kutunza kumbu kumbu za bajeti dhidi ya gharama halisi, thamani kamili ya mfumo, kuongeza ugumu kwenye kazi za ukaguzi kwa kuwa inalazimisha ukaguzi wa mfumo mmoja kufanyika kwenye taasisi zaidi ya moja hali ambayo inachangia ukaguzi kuchukuwa muda mrefu tofauti na mpango wa ukaguzi ili kukamilika.

Ukaguzi unashauri kwamba, ili kuhakikisha eGAZ inatekeleza mifumo ya kielektroniki kwa ufanisi na tija, bajeti na fedha zinazohitajika kwa ajili ya kufanikisha kazi za utekelezaji wa mifumo hiyo zipewe eGAZ ili iweze kupanga na kutekeleza kazi hizo kwa kuzingatia rasilimali na vipaumbele vyake. Aidha, hatua hii itarahisisha utunzaji wa kumbukumbu za bajeti na gharama halisi zilizotumika katika kutengeneza mfumo husika, itahakikisha pia kwamba kazi za ukaguzi zinafanyika kwa kuzingatia mpango wa ukaguzi kwani nyaraka zote zinazo hitajika zitapatikana kwenye taasisi moja, thamani halisi ya mfumo itaweza kupatikana kiurahisi na kuingizwa kwenye daftari la mali (asset register) za taasisi.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

eGAZ iliendelea kutumia bajeti kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ambayo ilikuwa imetengwa kwa ajili ya utengenezaji wa mfumo wa ZanMalipo wa zamani. Hata hivyo eGAZ iliandaa dhana (Concept note) kwa ajili ya kuonesha umuhimu wa kutengeneza mfumo mpya, ambayo ilionesha gharama na mpango kazi wa mradi wa utayarishaji wa mfumo wa ZanMalipo mpya

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kujadili hoja hii, Kamati ilitaka kupatiwa kielelezo hicho na kuridhika nacho lakini Mkaguzi alipopita hakupatiwa. Kamati ilihoji na kubaini kwamba Wakala haukufuatiia upatikanaji wake wakati Mkaguzi alipokuwa akitekeleza majukumu yake.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala uhakikishe anapofika Mkaguzi katika Ofisi yao kutekeleza majukumu yake, anapatiwa vielelezo vyote anavyovihitaji ili kuepusha kasoro kama hii kujitokeza kwa mara nyengine.

**Hoja nambari 12.8.2.2: Kutokujulikana kwa Gharama zilizotumika kwenye utekelezaji wa mfumo mpya wa Zanmalipo.**

Ukaguzi umebaini kwamba eGAZ kama mtekelezaji wa mfumo wa ZanMalipo na msimamizi mkuu wa masuala yote ya Serikali Mtandao hapa nchini haina kumbukumbu za gharama halisi zilizotumika kwenye utekelezaji wa mfumo wa ZanMalipo mpya mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Februari, 2022 ambapo ni kinyume na matakwa ya Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 pamoja na kanuni zake za mwaka 2021.

Udhaifu kwenye utunzaji wa kumbu kumbu za gharama halisi za utekelezaji wa mfumo wa ZanMalipo unaweza kutumika kama mwanya wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali, aidha, hali hii ni chanzo kikuu cha mifumo inayotengenezwa na wataalamu wa ndani kutojulikana thamani yake na kushindwa kuingizwa kwenye daftari la mali za Serikali (Asset Register), pia kuinyima Serikali fursa ya kupata tathmini ya maamuzi iliyofanya ya kutengeneza mfumo husika kwa kutumia wataalamu wa ndani yakilinganishwa na maamuzi ya kununuwa mifumo.

Ukaguzi unashauri eGAZ kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba inakusanya taarifa zote za matumizi halisi (actual expenditures) yaliyowahi kufanyika na yanayoendelea kufanyika kwa ajili ya mfumo wa ZanMalipo mpya kuanzia kwenye kuandaa mikakati, mipango kazi, kutengeneza mahitaji ya biashara na watumiaji, kununua miundombinu (mtandao, vifaa na programu), utengenezaji wa mfumo, mafunzo, usaidizi wa kutumia mfumo (Go Live Support) na kuendelea kutoa msaada kwa watumiaji wa mfumo (implementation support) ili kuweza kujua thamani halisi ya mfumo huo na kulinganisha na bajeti yake ili kubaini ufanisi uliopatikana kwenye mipango na matumizi ya fedha za umma.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Gharama halisi za utengenezaji wa mfumo mpya wa ZanMalipo zinaonekana katika Kimbatanisho Nambari 9 ambacho Kamati ilipatiwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba uchunguzi wa hoja hii unafanana na uchunguzi wa Kamati ulioelezwa katika hoja iliyopita (Nambari 12.8.2.2) ambapo jumla ya shilingi 195,450,000 zilitumika kuutengeneza Mfumo mpya wa ZanMalipo.

**Hoja nambari 12.8.2.3: Kukosekana kwa Mpango kazi wa Utekelezaji wa Mfumo (Implementation Plan) wa Zanmalipo mpya uliojumuisha mafunzo, majaribio ya Mfumo na kuanza kutumika Mfumo kwenye taasisi za Umma.**

Ukaguzi umebaini kuwa eGAZ haina mpango kazi wa utekelezaji wa mfumo wa ZanMalipo mpya, mpango kazi huu ulitarajiwa kuonesha pamoja na mambo mengine ratiba jumuishi ya matukio yote yanayotarajiwa kufanyika ili kukamilisha utekelezaji wa mfumo huu. Matukio haya ni pamoja na ukusanyaji wa mahitaji ya biashara na watumiaji wa mfumo, uchambuzi wa mahitaji, kujenga mfumo (system customization), mafunzo ya mfumo, majaribio ya mfumo, usambazaji wa mfumo (system deployment), kuanza kutumia mfumo (Go Live), na kufunga mradi (project closure) kwa taasisi zote za umma.

Aidha, ukaguzi uliomba kupewa ripoti ya mafunzo ambayo yametolewa na eGAZ kwa taasisi za umma tangu kuanza utekelezaji wa mradi wa ZanMalipo mpya, hata hivyo ukaguzi haukupatiwa ripoti hiyo kwa majibu kwamba haipo.

Kukosekana kwa mpango kazi wa utekelezaji wa mradi mkubwa wa utengenezwaji wa mfumo wa ZanMalipo ambao unatarajiwa kuzifikia taasisi za umma zisizopungua 117 na watumiaji wasiopungua 250 na kwa kuzingatia umuhimu wa mfumo huu kwenye kusimamia mapato ya nchi ni udhaifu mkubwa kwenye usimamizi wa mradi wa TEHAMA chini ya uangalizi wa Wakala wenye dhamana ya kusimamia TEHAMA nchini.

Hali hii inaweza kusababisha kukosekana kwa ufanisi na tija ya mradi kwenye idadi ya taasisi za umma zilizotakiwa kufikiwa baada ya muda uliopangwa kwa sababu ya kukosekana kwa vigezo husika ambavyo vingekuwemo kwenye mpango kazi, muda unaotumika kukamilisha kazi husika ni eneo jengine ambalo limeachwa huru na linaweza pelekea mradi kutumia muda mrefu kukamilika na kupelekea kukosekana kwa tija, rasilimali zinazohitajika pia zimeachwa huru kwa kutoingizwa kwenye mpango kazi na inaweza kupelekea mradi kutumia rasilimali nyingi au chache na kukwamisha ufanisi wa mradi. Aidha, kukosekana kwa mpango kazi kunapelekea kuongeza ugumu kwenye

kazi ya ukaguzi hususani kwenye kufanya tathimini ya utekelezaji wa mradi kwa kukosa vigezo (benchmarks) vya kufanyia ulinganifu.

Hivyo, ukaguzi unashauri Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kuhakikisha kuwa inaandaa mpango kazi maalumu wa utekelezaji wa mradi huu utakao jumuisha vigezo (parameters) mbali mbali kama vile taasisi zinazotakiwa kufikiwa, watumiaji wanaotarajiwa kufundishwa, na matukio mengine yote yaliyomo kwenye mradi kama vile kufanya majaribio ya mfumo (Uers Acceptance Testing), kuanza kutumia kwa mfumo kwenye taasisi moja moja (Go Live), n.k. Mpango kazi huu unatakiwa uidhinishwe na Menejimenti ya eGAZ kabla ya kuanza kutumika.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Mpango kazi wa Utekelezaji wa Mfumo (Implementation Plan) wa Zanmalipo mpya uliojumuisha mafunzo, majaribio ya Mfumo na kuanza kutumika Mfumo kwenye taasisi za Umma.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba kielelezo kinachohusiana na hoja hii imepatiwa lakini imeshindwa kukiubali kwa vile kinatia shaka juu ya uhalali na uhalisia wake hasa ukizingatia kwmba Mkaguzi hakupatiwa wakati wa ukaguzi.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala uhakikishe anapofika Mkaguzi katika Ofisi yao kutekeleza majukumu yake, anapatiwa vielelezo vyote anavyovihitaji ili kuepusha kasoro ndogo kama hii kujitokeza kwa mara nyengine.

**Hoja nambari 12.8.2.4: Kasi Ndogo ya Usajili wa Taasisi za Umma Kwenye Mfumo wa ZanMalipo Mpya.**

Katika ukaguzi uliofanyika wa Mfumo mpya wa ZanMalipo kwa Wakala wa Serikali Mtandao imebainika kwamba hadi sasa asilimia 26 pekee ya taasisi zote za umma ndio ambazo zilizosajiliwa kwenye mfumo tangu utekelezaji wa mfumo huu ulipoanza miezi mitano iliyopita kuanzia mwezi wa Novemba, 2021. Hata hivyo ni asilimia 18 ya taasisi za umma zilizosajiliwa ndizo ambazo zimeanza kutumia mfumo wa ZanMalipo mpya hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi Machi, 2022.

Kiujumla hali hii ni sawa na usajili wa wastani wa asilimia 5 ya taasisi za umma kwa mwezi ambapo kwa kasi hii inaashiria kwamba eGAZ itachukuwa wastani wa miezi 20 ili kukamilisha usajili wa taasisi zote za umma.

Kuwepo kwa kasi ndogo ya usajili wa taasisi za umma katika mfumo mpya wa ZanMalipo kunaweza kupelekea kukosa udhibiti wa mapato jambo ambalo litapelekea kutitokeza kwa upotevu wa mapato na hatimae kucheleweshа maendeleo kwenye Jamii. Matumizi ya rasilimali nyingi zaidi kwenye utekelezaji wa mradi iliyosababishwa na muda wa utekelezaji kuongezeka.

Ukaguzi inaishauri eGAZ kufanya tathmini ya kasi ya utekelezaji wa mradi huu ili kubaini vikwazo vinavyopelekea kutumia muda mwingi kwa kaisi kilichoainishwa hapo juu na kuchukuwa hatua za kutatua vikwazo hivyo kwa haraka ili kunusuru hasara kwa Serikali inayotokana na upotevu wa mapato kwa kukosa udhibiti madhubuti unaotarajiwa kupatikana kupitia matumizi ya mfumo wa ZanMalipo mpya.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Wakala ilianza kuruhusu kutumika kwa mfumo wa ZanMalipo mpya mnamo tarehe 21 December, 2021 ambapo Wizara tano (5) na taasisi zake zilichaguliwa kutumia mfumo kama ni 'Pilot' kwa dhumuni la kuibua changamoto zitakazojitokeza na kuweza kuzidhibiti kabla ya kuanza kutumiwa rasmi na Taasisi zote za Serikali.

Kipindi cha majaribio kilidumu kwa muda wa mwezi mmoja na baada ya mafanikio kuonekana Taasisi nyengine ziliendelea kupewa mafunzo na kuungwa katika mfumo kwa utaratibu uliowekwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba kwa wakati Mkaguzi anafanya ukaguzi wake ni kweli kwamba kasi ya usajili wa Taasisi za Umma Kwenye Mfumo wa ZanMalipo Mpya ilikuwa ndogo lakini kwasasa Kamati imeridhishwa na juhudi ambayo Wakala umechukua na kuwasisitiza wazidi kuongeza juhudi.

**Hoja nambari 12.8.2.5:Kusokekana Kwa Ripoti Mbali Mbali za Mapato Kwenye Mfumo wa zanMalipo.**

ZanMalipo ni mfumo wa usimamiaji ukusanyaji wa mapato ya Serikali ambao unalengo la kurahisisha ulipaji wa huduma za umma kwa kumuwezesha mlipaji kupata njia mbalimbali na rafiki za kufanya malipo kama vile kulipa kwa kutumia simu za kiganjani, Benki na Mawakala wa malipo. Hivyo, mfumo huu unatarajiwa kuwa na kumbukumbu zote za mapato yote ya Serikali yaliyopita katika mfumo huo kwa utaratibu wa kutumia nambari za udhibiti (Control Numbers) zilizotumika kulipia huduma kwenye taasisi za umma.

Hata hivyo, ukaguzi uliomba ripoti mbali mbali za mapato kutoka kwenye mfumo lakini ripoti hizo hazikupatikana kwa ajili ya ukaguzi, miongoni mwa ripoti zilizoombwa ni pamoja na ripoti ya mapato ya taasisi moja moja kwa kila mwezi wa ukusanyaji, ripoti ya jumla ya ukusanyaji wa mapato, n.k. Kwa kuzingatia matarajio yaliyopo ya mfumo wa ZanMalipo mpya kwa watumiaji na wadau mbali mbali mfumo huu unatarajiwa kutoa taarifa toshelezi kubaini makusanyo kwa taasisi moja moja, kwa ngazi ya Wizara nzima, kwa Serikali yote kwa kila wakati (real time collections), kwa siku, wiki, mwezi, robo mwaka, nusu mwaka, mwaka n.k taarifa ambazo ni za msingi kuwepo kwenye mfumo ili kupata tija na udhibiti kwenye makusanyo.

Kitendo cha mfumo wa ZanMalipo kukosa ripoti hizo ni udhaifu wa mkubwa kwenye mfumo kwani matarajio ya watumiaji, Serikali na wadau mbali mbali hayajafikiwa na kuashiria kutopatikana kwa tija na ufanisi wa mfumo kwa hatua uliyofikia.

Kwa kuwa ripoti hizi zinatarajiwa kurahisisha kuonekana (visibilty) kwa picha kamili ya mapato kuanzia ngazi ya taasisi mpaka kwenye ngazi ya Serikali nzima ukaguzi inaishauri eGAZ kuhakikisha ripoti hizo zinatangenezwa na kuwekwa kwenye mfumo na kwamba zinapatikana kwa ajili ya matumizi ya wadau mbali mbali wa mfumo huo kulingana na nafasi zao.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Mfumo wa ZanMalipo wa sasa ni mfumo ambao umeweza kukidhi mahitaji ya ripoti zinazohitajika kupitia “Generic portal”. Mfumo huo unaweza kutoa ripoti za aina 26. Aidha, kwa Taasisi ambazo zinatumia mifumo ya ndani zinaweza kutengeneza ripoti kwa mujibu wa mahitaji yao.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba kipindi cha ukaguzi mfumo huo ulikuwa unaweza kuonesha ripoti kwenye "dashboard" pekee na hauwezi kuzibadilisha kwenda kwenye mifumo ya excel au PDF. Lakini kamati imejiridhisha kuwa hali hiyo imetatuliwa na sasa ripoti zote zinaweza kupatikana kwa mfumo ambao taasisi husika itaona inafaa.

**Hoja nambari 12.8.2.6:Kukosekana kwa Nyaraka za Watumiaji na Majukumu yao Kwenye Mfumo (System User Matrix).**

"System user's matrix" ni nyaraka inayofafanua majukumu ya makundi mbali mbali yanayotumia mfumo ikiwa ni pamoja na wasimamizi wa mfumo, nyaraka hii huandaliwa kwa kuzingatia mgawanyo wa majukumu na udhibiti wa ndani wa taasisi (internal controls) na kuhakikisha kwamba mtumiaji mmoja hawezi kufanya kazi kwenye mfumo zinazomuwezesha kukamilisha mzunguko mzima peke yake, hususani kwenye maeneo yenye hatari. Hivyo nyaraka hii ni muhimu ili kuweza kutambua watumiaji wa mfumo wanafanya kazi kulingana na majukumu yao ya kazi za kila siku na kuweza kuwazuia kufanya vitendo nje ya majukumu na mamlaka yao.

Msingi wa nyaraka hii ni "Segregation of Duties (SoD)" kama ilivyo ainishwa kwenye miongozo

ya viwango bora vinavyokubalika (best practice guidelines) ya ISACA. Hata hivyo, ukaguzi umeshindwa kupata nyaraka ya watumiaji na majukumu yao kwenye mfumo mpya wa ZanMalipo.

Kutokuwepo na hati hii kunaweza kupelekea mtumiaji wa mfumo kupewa ruhusa ya kufanya kazi kinyume na majukumu yake pamoja na mipaka yake jambo ambalo linaweza kusababisha kujitokeza kwa mianya ya upotevu wa mapato na kuingiza hasara Serikali wa kufanya ubadhirifu wa fedha za umma, kubadilisha taarifa za mapato kwenye taasisi kwa manufaa binafsi, chanzo cha rushwa n.k.

Hivyo, ukaguzi unashauri kuwa itengenezwe nyaraka ya watumiaji na majukumu yao kwenye mfumo kwa nafasi zao kama vile Muhasibu, Muhasibu Msaidizi, Afisa TEHAMA, n.k ili kuweza kubainisha wazi majumu ya watumiaji wa mfumo na kuona kama kuna uwiyano na kazi zao za kila siku pia kuweza kuhakikisha kuwa mtumiaji wa mfumo anapata taarifa kutoka katika mfumo kulingana na majukumu yake.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Uwepo wa Nyaraka za Watuamiaji na majukumu yao (User Matrix Documents) ni suala muhimu katika kudhibiti na kuzingatia mgawanyo wa majukumu ya kimfumo. Mfumo huu umeweka bayana ugawaji wa majukumu kwa kutumia utaratibu maalumu wa kuleta maombi eGAZ kwa kujaza fomu kwa watumiaji wote wa mfumo. Utaratibu uliowekwa unahitaji mkuu wa Taasisi kuthibitisha majukumu yaliyoombwa na mtumishi wa Taasisi hiyo. Fomu hiyo inawasilishwa eGAZ kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Kwa utaratibu huo unaotumika ni vigumu kuweza kumpa mtumiaji jukumu ambalo halihusiani na kazi yake.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Document ambayo Wakala imeleta ni sehemu ya "User Matrix" wakati document inayotakiwa ni 'document' ambayo ina aina ya watumiaji na majukumu yao kwenye mfumo huo. Kwa hiyo Kamati haikuridhika na majibu ya Wakala na kusisitiza kwamba ni vyema Wakala ukawa na utaratibu mzuri wa kuhifadhi kumbukumbu zake ili ziweze kupatikana kwa haraka. Aidha, Wakala uwe na mashirikiano ya karibu na Mkaguzi ili akihitaji nyaraka ampatie.

### 12.8.2.7 Kukosekana kwa Nyaraka Muhimu za Mfumo Mpya wa ZanMalipo.

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo mpya wa ZanMalipo hauna nyaraka muhimu zinazohusiana na mfumo ikiwa ni pamoja na nyaraka za mahitaji ya mfumo (system requirements document), nyaraka ya kujaribu na kuidhinisha matumizi ya mfumo (Test Cases and Users Acceptance Certificate) n.k ambapo ni kinyume na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika katika utengenezaji wa mifumi ya kielektroniki kama vile SDLC. Miongoni mwa athari zinzoweza kutokea kwa kukosekana kwa nyaraka hizo muhimu ni pamoja na zifuatazo:-

- Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia mahitaji yote ya mfumo ya sasa na ya wakati ujao katika upande wa biashara, watumiaji, usalama, udhibiti, ufikiaji, urahisi wa matumizi n.k.
- Mfumo kutengenezwa bila kuzingatia hali halisi ya mabadiliko ya teknolojia na kusababisha mfumo husiska kukosa sifa ya kuingilianan "interoperability" na mifumo mengine kwa sababu ya utofauti wa teknolojia.

- Kusababisha hasara kwa Serikali kwa kutengeneza mfumo ambao haujakidhi matakwa ya biashara na mahitaji ya watumiajai wa mfumo na kusababisha mfumo kutokuendelea kutumika.

Kwa kuzingatia uhalisia uliopo kwamba, mfumo wa ZanMalipo mpya ndo kwanza unaanza utekelezwaji wake na kwamba Serikali bado ina kumbu kumbu za kutofanikiwa kwa mfumo wa ZanMalipo wa zamani. Ukaguzi unashauri eGAZ kufanya yafuatayo: -

- Kuchukuwa jitihada za makusudi za kuandaa nyaraka ya mahitaji ya mfumo ya mfumo ili kuhakikisha kwamba mfumo unaotekelezwa unaweza kupimwa ufanisi na tija yake.
- Kuandaa nyaraka ya vigezo vya majaribio ya mfumo (test cases document) na kuhakikisha kuwa inatumiwa kuujaribu na kudhibitisha ufanisi wa mfumo kabla haujaendelea kutumika kwenye taasisi zote za umma ili kuhakikisha kwamba mahitaji yote muhimu ya watumiaji nay ale ya biashara yamezingatiwa na kama kuna mapungufu yawekewe utaratibu wa kuyapatia ufumbuzi.
- Kuhakikisha kwamba nyaraka husika zinapatikana kwa ajili ya matumizi ukaguzi.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Nyaraka Muhimu za Mfumo Mpya wa ZanMalipo zipo na ambapo Matayarisho ya mfumo wa ZanMalipo mpya yalitumia nyaraka zile zile za ZanMalipo ya zamani.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwepo kwa baadhi ya nyaraka hizo na kukabidhiwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini nyaraka hizo bado zipo katika hatua ya "draft version" na sio nyaraka zilizothibitishwa na uongozi wa Wakala wa Serikali mtandao. Hivyo, Kamati haikuweza kuridhika nazo kwa vile ilishindwa kutambua juu ya usahihi na uhalisia wake.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala uhakikishe anapofika Mkaguzi katika Ofisi yao kutekeleza majukumu yake, anapatiwa vielelezo halisi (original) anavyovihitaji ili kuepusha kasoro ndogo kama hii kujitokeza kwa mara nyengine.

### 12.8.3 DOSARI KWENYE UDHIBITI WA JUMLA WA UENDESHAJI WA TEHAMA

**Hoja nambari 12.8.3.1:Kukosekana kwa Mpango wa Uendeshaji wa TEHAMA kwa Ngazi ya eGAZ na Ngazi ya Nchi (ICT Governance Framework)**

Mpango wa uongozaji wa TEHAMA kwa ujumla unatoa muongozo kwa taasisi za Umma katika kutengeneza sera, viwango na taratibu bora zinazokubalika katika uongozaji na usimamizi wa rasilimali za TEHAMA ili kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yanaongeza tija na ufanisi katika kufanikisha taasisi kufikia malengo waliyojiwekea.

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Serikali Mtandao bado haijatoa Mpango wa Uongozaji wa TEHAMA katika sekta za Umma. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 5(e) cha Sheria Nambari 12 ya mwaka 2019 ambapo Wakala imetakiwa kuandaa na kuendeleza sera, viwango na taratibu nyengine za kwa ajili ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa Umma Zanzibar.

Athari za kukosekana kwa "ICT Governance Framework" inajumuisha: -

- Taasisi za umma kukosa muongozo rasmi wa kufuatwa katika uendeshaji wa TEHAMA nchini jambo linalopelekea ugumu kwenye kupima tija na ufanisi wa uendeshaji wa TEHAMA nchini.
- Kukosekana kwa udhibiti madhubuti wa TEHAMA kwa taasisi za umma kwa kuwa kila taasisi inakuwa huru kufuata au kutofuata framework yoyote ile.
- Kuhatarisha usalama wa mifumo ya TEHAMA nchini.

Ukaguzi unashauri Wakala wa Serikali Mtandao, kuhakikisha wanaandaa na kutoa mpango wa uongozaji wa TEHAMA kwa taasisi za Umma ili kuenda sambamba na madhumuni ya uanzishwaji wa Wakala kama ilivyoelekezwa katika kifungu nambari 5 (e) cha sheria nambari 12 ya mwaka 2019.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

eGAZ imepokea hoja ya mkaguzi na inaendelea na jitihada za kutayarisha nyaraka hizo ambapo mwezi wa Mei, 2023 tulizindua "Mpango wa Kitaifa wa Muelekeo wa Uchumi wa 2023 - 2027 na mwezi wa Julai, 2023 ulizinduliwa Mkakati wa Kidigitali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa 2023 - 2027.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhishwa na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Wakala wa Serikali Mtandao na haikuwa na hoja zaidi.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri eGAZ kuhakikisha mpango huo unakamilika na kupatikana ndani ya wakati uliokusudiwa.

**Hoja nambari 12.8.3.2: Kukosekana kwa Sera na Miongozo Toshelevu ya Usimamizi na Matumizi ya TEHAMA Katika Ngazi ya eGAZ na Taifa Kwa Ujumla**

Sera, Miongozo na Kanuni za matumizi, usimamizi na wendeshaji wa TEHAMA ni nyenzo muhimu sana katika kufikia adhima ya Serikali Mtandao ambayo inalenga kuwezesha utoaji wa huduma na upatikanaji wa taarifa mbali mbali kwa umma kwa gharama nafuu na kwa uharaka zaidi ili kuleta tija na ufanisi Serikalini kupitia TEHAMA. Taasisi za umma zinatarajia kupata Sera, Miongozo na Kanuni mbali mbali za matumizi sahihi, salama, na endelevu ya TEHAMA kutoka kwa eGAZ ili kuhakikisha kwamba uwekezaji kwenye TEHAMA unakwenda sambamba na thamani ya fedha, manufaa ya uwekezaji husika (Return on Investiments), miradi inakamilika kwa wakati, inakidhi malengo na dira ya taifa n.k.

Katika ukaguzi uliofanyika wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar imebainika kuwepo kwa udhaifu mkubwa katika eneo la kutengeneza Sera, Mingongozo na Kanuni zinazojitosheleza ambazo zitatumika kwenye usimamizi, uendeshaji, na matumizi ya TEHAMA nchini, hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na Wakala kujikita zaidi kwenye utengenezaji, utekelezaji (implementation), usimamizi (administration) wa mifumo ya TEHAMA, kazi ambayo inahitaji uzingatiaji na muda mwingi ili kuzifanikisha na kupelekea kudorora kwa utengenezaji wa Sera, Miongozo na Kanuni za TEHAMA.

Aidha, uchache wa rasilimali watu wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha kwenye eneo la kutengeneza Sera na Miongozo ni sababu nyengine iliyochangia kutokea kwa udhaifu katika utengenezaji wa sera na miongozo ambapo linapelekea athari hususan linapokuja suala la usimamizi, uendeshaji na matumizi sahihi ya TEHAMA yenye kuleta tija na ufanisi katika utumishi wa umma.

Miongozo kama vile Mikakati ya TEHAMA ya taifa iliyoimarishwa (updated) ni chanzo muhimu kwa taasisi za umma kutengeneza mikakati yao kwa

kuzingatia muelekeo wa taifa ambapo linashajihisha matumizi ya rasilimali za umma kwenye njia na malengo yaliyopangwa kuanzia ngazi ya taifa.

Kwa mara ya mwisho Sera ya TEHAMA ilitengenezwa mwaka 2012, hata hivyo Sera hii haijaelezea kwa undani namna ya utekelezaji wake, na hakuna sera nyengine yoyote iliyoelezea miongozo na viwango vya kufuata mpaka mwaka mnamo mwaka 2021 ambapo eGAZ ilipotoa toleo la manunuzi na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA.

Kukosekana kwa Sera, Miongozo na Viwango toshelevu vya TEHAMA ni kwenda kinyume na kifungu nambari 5 (e) cha sheria Nambari 12 ya mwaka 2019 ambapo Wakala imetakiwa kuandaa na kuendeleza sera, viwango na taratibu nyengine za kwa ajili ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa Umma Zanzibar.

Aidha, hali hii inachelewesha kupatikana kwa manufaa yaliyotarajiwa ya uwekezaji unaofanywa na taasisi mbali mbali za umma kwenye TEHAMA kwa sababu ya kukosa uangalizi na usimamizi wa karibu kupitia Sera, Miongozo na Viwango vya TEHAMA. Uwepo wa mifumo zaidi ya mmoja ambayo kwa sehemu kubwa inafanya kazi zinazofanana ndani ya taasisi moja ni mojawapo ya athari za mdororo wa usimamizi wa TEHAMA katika ngazi ya nchi.

Ukaguzi unashauri mabo yafuatayo:-

- Wakala wa Serikali Mtandao iwekeze muda na jitihada zake nyingi zaidi kwenye kutengeneza Sera, Miongozo na Viwango toshelevu kwa ajili ya matumizi, usimamizi na wendeshaji wa TEHAMA kwenye taasisi za umma ili kuziwezesha taasisi hizo kujiongoza kwa kufuata miongozo hiyo na kuleta tija kwa wingi na kwa mara moja.
- Ili kwenda na kasi ya mabadiliko yanayotokea kwenye TEHAMA katika kubaini mabadiliko ya teknolojia zilizopo, mpya na hatari (risks) zinazoambatana nazo na kuzitengenezea Miongozo na Viwango toshelevu vya kukabiliana nazo Wakala inashauriwa kuweka utaratibu na mazingira wezeshi ya kukutana na wadau wa kimkakati muhimu kwenye TEHAMA wanaojumuisha sekta za umma na binafsi ili kuchukuwa mawazo yao na kuyaratibu katika utekelezaji angalau mara moja kwa mwaka.
- Kufanya mapitio ya Sera, Miongozo na Viwango vya TEHAMA angalau kila baada ya miaka 3 ili kubaini mapungufu na kuyafanyia kazi katika kuhakikisha kwamba miongozo husika inabakia hai na yenye tija.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

eGAZ imepokea hoja ya mkaguzi na inaendelea na jitihada za kutayarisha nyaraka hizo ambapo hadi sasa jumla ya miongozo 18 imeshaandaliwa. Aidha, Sera ya Serikali Mtandao ya mwaka 2012 ipo katika hatua za kufanyiwa mapitio baada ya kuvuka kipindi cha miaka 10 ya utekelezaji wake. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa rasimu ya awali ambayo imepangwa kuwasilishwa kwa wadau tarehe 15 Agosti, 2023.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa Sera na miongozo wakati wa ukaguzi vilikuwa havipo. Hata hivyo, Kamati imeona na kuridhika na juhudi zinazochukuliwa na eGAZ katika kuhakikisha Sera na Miongozo hiyo inapatikana.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri eGAZ kuhakikisha Sera na Miongozo inakamilika na kupatikana ndani ya wakati uliokusudiwa.

### 12.8.3.3 Kukosekana kwa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya TEHAMA Kwa Ngazi ya Taifa na Kwa Ngazi ya eGAZ

Mpango mkakati wa TEHAMA hufafanua maono ya taifa/taasisi ya TEHAMA na kuunda ramani ya kimkakati ya kutumia TEHAMA, rasilimali za kidijitali na maarifa ya kiufundi ili kuunda thamani ya taifa/taasisi husika.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 6(a) cha Sheria ya kuanzisha Wakala wa Serikali Mtandao kinaelezea kuwa moja katika kazi za Wakala wa Serikali mtandao ni kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera za TEHAMA, kanuni na miongozo katika utumishi wa umma. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Serikali Mtandao haijaandaa mpango mkakati wa maendeleo ya TEHAMA kwa ngazi ya Taifa ikiwa ni moja kati ya majukumu yake kwa mujibu ya sheria. Aidha, Wakala wa Serikali mtandao imebainika kutokuwa na Mpango mkakati wa maendeleo ya TEHAMA katika ngazi ya Wakala yenyewe.

Kukosekana kwa mkakati wa mendeleo ya TEHAMA kunaweza kupelekea taifa kutokuwa na muelekeo mzuri wa TEHAMA utakofahamika kwa wadau na taasisi za umma jambo ambalo linaweza kupelekea taasisi za umma kushindwa kutegemea, kupanga na kufuata ipasavyo mikakati na malengo endelevu ya Taifa na kupelekea kutopatiakana kwa ufanisi na kupungua kwa kasi ya maendeleo ya Nchi kwa ujumla.

Hivyo, ukaguzi unaishauri Wakala wa Serikali Mtandao kufanya jitihada za makusudi za kuandaa Mpango Mkakati wa maendeleo ya TEHAMA kwa kuzingatia dira na mwelekeo wa nchi kwa ngazi ya Wakala na ngazi ya Taifa, na kuhakikisha kwamba mpango mkakati wa maendeleo ya TEHAMA kwa ngazi ya Taifa unawafikia wadau mbali mbali pamoja na taasisi zote za umma.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

eGAZ tayari imeshandaa Mkakati wa Kidigitali wa Serikali ambao ulizinduliwa tarehe 29 Julai, 2023. Aidha, Mpango Mkakati wa eGAZ umeshaandaliwa ambapo tarehe 17 Agosti 2023 utawasilishwa kwa wadau.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhishwa na maelezo ya Wakala wa Serikali Mtandao kwa kuhakikisha Mpango Mkakati wa Maendeleo ya TEHAMA kwa ngazi ya Taifa na ngazi ya TEHAMA umekamilika. Hata hivyo, Kamati ya PAC imesisitiza kwamba Mkaguzi anapopita awe anapatiwa vielelezo hivyo anapovihitaji.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala uhakikishe anapofika Mkaguzi katika Ofisi yao kutekeleza majukumu yake, anapatiwa vielelezo anavyovihitaji ili kuepusha kasoro ndogo kama hii kujitokeza kwa mara nyengine.

**Hoja nambari 12.8.3.4:Kutokuwepo kwa Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) kati ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar na Wakala wa Serikali Mtandao Tanzania Bara**

Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar inafanya mashirikiano na Wakala wa Serikali Mtandao Tanzania bara katika kupatiwa huduma na rasilimali mbali mbali za TEHAMA. Hadi ukaguzi unakamilika, Wakala wa Serikali Mtandao umeshindwa kutoa Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) baina ya taasisi hizo mbili.

Kutokuwepo kwa makubaliano rasmi baina ya pande hizi mbili zinazofanya kazi za kusimamia mifumo, kushirikiana katika kazi za mifumo ikiwa ni pamoja na kuchangia wataalamu na rasilimali nyengine za TEHAMA kunaweza kupelekea athari mbali mbali kwenye mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika maeneo ya usalama, matumizi endelevu ya mifumo na hali ya umiliki wa mifumo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kuzingatia miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kwa kuweka makubaliano ya ushirikiano (Memorundum of Understanding) ambapo kimsingi makubaliano hayo yatatoa ufafanuzi wa haki na wajibu wa kila upande na kuelezea matarajio ya kiwango cha huduma kitakachotolewa ili kuhakikisha kwamba muda na rasilimali nyengine zilizotumika kutengeneza mifumo iliyokamilika na inayoendelea kutengenezwa zinalindwa kwa makubaliano rasmi.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) kati ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar na Wakala wa Serikali Mtandao Tanzania Bara yapo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na eGAZ katika kuhakikisha nyaraka hiyo ya makubaliano ya ushirikiano inapatikana. Aidha, Kamati imebaini kulikuwa na uzembe wa watendaji uliopelekea kushindwa kumpatia Mkaguzi kielelezo hicho wakati wa ukaguzi.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala uhakikishe anapofika Mkaguzi katika Ofisi yao kutekeleza majukumu yake, anapatiwa vielelezo anavyovihitaji ili kuepusha kasoro ndogo kama hii kujitokeza kwa mara nyengine.

**Hoja nambari 12.8.3.5:Udhaifu Katika Uelewa na Mipango Endelevu ya Usalama wa Mfumo wa ZanMalipo**

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Serikali Mtandao hawana uwelewa wa kutosha kuhusiana na masuala ya usalama wa mfumo "System Security" kwa mfano, hawana uwelewa wa namna ya kuhakikisha taarifa za Serikali zinazohifadhiwa kwenye miundombinu ya eGA na kubakia salama kwa muda wote. Usalama wa mfumo huelezea vidhibiti na ulinzi ambao taasisi huhakikisha mfumo na miundombinu mengine iko salama dhidi ya kuingiliwa kwa nia mbaya. Hivyo lengo kuu la usalama wa mfumo ni ulinzi wa taarifa na miundombinu dhidi ya wizi, na uharibifu wa aina nyengine, huku ukiruhusu taarifa na miundombinu kupatikana wakati wote inapohitajika na kuleta tija.

Kutokana na kuwa Wakala wa Serikali Mtandao ina uelewa duni wa masuala ya usalama wa mfumo wa ZanMalipo katika masuala ya usalama kunaweza kupelekea kutofahamu njia zinazofaa kutumika kwa ajili ya kuendelea kuuweka mfumo salama pale ambapo utakapokuwa chini ya uangalizi wa Serikalini ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ukaguzi unashauri, wakala Serikali mtandao Zanzibar (eGAZ ) kushirikiana na Mamlaka ya Serikali mtandao Tanzania (e-GA) ili kupata uwelewa mpana na taaluma juu ya masuala ya usalama wa mfumo wa ZanMalipo kwa upana wake ambapo itasaidia katika kupunguza au kumaliza kabisa utegemezi kwenye eneo hili.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Hakuna udhaifu katika Uelewa na Mipango Endelevu ya Usalama wa Mfumo wa ZanMalipo, ambapo hadi sasa mfumo wa ZanMalipo umeshatumika zaidi ya miaka mitatu na kila mwaka unaonyesha ongezeko la mapato ya Serikali. Aidha eGAZ inaendelea na kutoa mafunzo katika taasisi kwa lengo la kuongeza uelewa na kuleta ufanisi katika utumiaji wake.

eGAZ inaendelea kuboresha mfumo wa ZanMalipo ambapo hivi karibu ilizundua mkakati wa miaka mitano wa kidigitali ambapo ndani yake ZanMalipo itaboreshwa zaidi na kuenda kwa wananchi wa kawaida kwa lengo la kuongeza mapato.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa katika kipindi cha ukaguzi, Mkaguzi aliwafanyia “interview” watendaji wa eGAZ na kuuliza masuala mbali mbali yanayohusiana na usalama wa mifumo na kupata majibu yasioridhisha. Aidha, licha ya majibu hao, Kamati imejiridhisha na kasi ya Wakala wa Serikali Mtandao katika kuengeza uelewa wa usalama wa mifumo kwa njia tofauti ikiwemo kufanya mafunzo kwa watendaji.

Hata hivyo, kamati inasisitiza uongozi wa eGaz utoe mafunzo ya mara kwa mara kwa watedaji wa TEHAMA yatakayosaidia kuwafanya watendaji hao kuendana na kasi kubwa ya TEHAMA kwa wakati.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Taasisi ya Wakala wa Serikali Mtandao kuwa na utamaduni wa kuwafanyia mafunzo ya muda mfupi "refresher courses" watendaji wa taasisi hiyo hususani wale wanaohusika na masuala ya kuhakikisha mifumo hiyo ipo salama na haidukuliwi.

**Hoja nambari 12.8.3.6: Kutofahamika kwa Hali ya Umiliki wa Mifumo**

Katika mapitio ya mfumo wa ZanMalipo, ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Serikali Mtandao haina uelewa kamili juu ya hali ya umiliki wa mfumo husika, hadi ukaguzi unakamilika haikuweza kujulikana bayana mfumo wa ZanMalipo ni mali ya SMZ kwa kupewa kama zawadi (grant), umekodishwa au kupewa na kwamba SMZ inautumia kama huduma tu.

Hivyo, kutofahamika kwa hali ya umiliki wa mfumo huo kunapelekea kutishia uendelevu wa mfumo (system sustainability) kwa sababu inakuwa ni vigumu kufahamu mipaka iliyopo baina ya pande mbili hizo. Ama kuwekeza kwenye mfumo, kununua miundombinu inayohitajika kwa ajili ya kuusimamia mfumo ipasavyo au la.

Ukaguzi unashauri kuwa, Wakala wa Serikali Mtandao ifanye mazungumzo yaliyo bayana na eGA tangu mwanzo kuhusu hali ya umiliki wa mfumo huo na mifumo mengine iliyokuwa katika hali hiyo mapema iwezekanavyo na kuyaweka kwenye "MoU" makubaliano hayo ili yapatikane kwa matumizi ya ndani ya ofisi pamoja na kazi za ukaguzi na kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na utata wa hali ya umiliki.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Umiliki wa mifumo unaeleweka kwa kuwa eGAZ ina makubaliano na eGA katika usimamizi na uendeshaji wa mifumo ambapo wataalam kutoka Taasisi zote wanashirikiana katika kubadilisha utaalamu, mafunzo na uzoefu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC haijaridhishwa na kitendo cha "Servers" kuwepo nje ya Zanzibar hali ambayo inaweza kupelekea kuvuja kwa siri za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaushauri Wakala kutengeneza "Data centre" kwenye eneo la Zanzibar kwa usalama zaidi ili taarifa zote ziwe zinapatikana hapo na kuepusha udukuzi kufanyika kwa wepesi.

**Hoja nambari 12.8.3.7: Kukosekana kwa kumbukumbu za taasisi za umma zilizopeleka maombi ya kufanyiwa tathimini, kuidhinisha ama kupatiwa ushauri wa kitaalamu na eGAZ kwenye masuala ya TEHAMA**

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala hauna kumbu kumbu za taasisi za umma zilizowahi kupeleka maombi ya kufanyiwa tathimini, kupewa ushauri wa kitaalamu na kuidhinishiwa mipango ya miradi ya TEHAMA kwa mujibu wa Toleo la Wakala la Manunuzi na Ufungaji wa vifaa vya TEHAMA kwenye Sekta za Umma la mwaka Julai, 2021.

Kwa mujibu wa toleo la manunuzi na ufungaji vifaa vya TEHAMA katika sekta za umma lililotolewa na Wakala wa Serikali Mtandao 13, julai 2021 kipengele nambari 1(a) – (g) kinazitaka taasisi kupeleka maombi mbali mbali kwa ajili ya kupitiwa, kushauriwa na kuidhinishwa kabla ya utekelezaji (implementation), uimarishaji (upgrade) au ununuzi wa mfumo.

Kukosekana kwa kumbu kumbu hizo kunaashiria udhaifu wa Wakala katika kutimiza majukumu yake yaliyopo kisheria na kinyume na miongozo yake yenyewe, udhaifu wa Wakala katika kutunza kumbu kumbu, Wakala kutofanya tathmini ya utekelezaji wa miongozo na matoleo yake aidha, hali hii inaweza kupelekea athari mbali mbali zikiwemo zifuatazo:-

- Kukwamisha ufanyaji wa tathmini ya kupima ufanisi wa Wakala katika kuzihudumia taasisi za umma kwa mujibu wa miongozo yake.
- Ucheleweshwaji wa majibu ya mapitio, idhini, na ushauri wa kitaalamu kwa taasisi za umma.
- Kushindwa kupima ufanisi wa utekelezaji wa toleo/ miongozo kwa upande wa taasisi za Serikali.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

kumbukumbu za taasisi za umma zilizopeleka maombi ya kufanyiwa tathimini, kuidhinishwa ama kupatiwa ushauri wa kitaalamu na eGAZ kwenye masuala ya TEHAMA zinapatikana. Taasisi huwasilisha kwa njia ya barua pepe au kwa kuwasilisha barua rasmi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba Wakala ulikuwanavyo vielelezo isipokuwa kutokana na uzembe wa watendaji walishindwa kumpatia Mkaguzi na kupelekea hoja hii nyepesi kuingizwa katika kitabu. Kwa mnasaba huo, Kamati baada ya kuvipitia vielelezo hivyo, imeridhishwa navyo.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala uhakikishe anapofika Mkaguzi katika Ofisi yao kutekeleza majukumu yake, anapatiwa vielelezo anavyovihitaji ili kuepusha kasoro ndogo kama hii kujitokeza kwa mara nyengine.

**Hoja nambari 12.8.3.8: Kutopitishwa kwa Wakati Rasimu ya Sera za TEHAMA na Bodi ya Washauri ya eGAZ**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 12(2) cha Sheria Nambari 12 ya Wakala wa Serikali mtandao ya mwaka 2019 kinaitaka Bodi kukaa vikao vyake kila robo mwaka na kuwasilisha ripoti yake kwa Waziri. Hata hivyo ukaguzi umebaini kwamba kwa kipindi cha miaka miwili 2020 na 2021 Bodi imekaa vikao 2 pekee kati ya vikao 8 ambavyo vilitakiwa kukaa.

Kwa mujibu wa kifungu 12(1)(b) Bodi ina jukumu la "kumshauri Waziri katika masuala ya maendeleo ya kisera na mikakati ya Serikali Mtandao".

Kupitia majadiliano na wakaguliwa ukaguzi ulifahamishwa kwamba Wakala iliandaa Rasimu ya Sera za uendeshaji na usimamizi wa TEHAMA ambayo haijakamilika kwa ajili ya matumizi kwasababu ilitakiwa ipitie kwenye vikao vya Bodi ili kuweza kumshauri Waziri kwa mujibu wa kifungu 12(1) jambo ambalo limechukua muda mrefu kufanyika kwa sababu ya uchache wa vikao vya Bodi kama ilivyoainishwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri Wakala kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba Bodi inakaa vikao vyake kwa mujibu wa Sheria na kwamba Rasimu za Sera zinawasilishwa kwenye Bodi kwa ajili ya kupitiwa na kumshauri Waziri kama watakavyoona inafaa ili kupata Sera imara na kwa wakati kwani mabadiliko na vihatarishi vinavyojitokeza kwenye TEHAMA hayaangalii changamoto za ndani ya nchi.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Rasimu ya Sera ya TEHAMA iliandaliwa kabla ya kuanzishwa kwa Bodi ya Ushauri ya Wakala. Sera ya TEHAMA ilianzishwa mwaka 2012 ambapo kipindi hicho eGAZ ilikuwa ni Idara.

**Uchunguzi wa kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa ni kweli wakati wa ukaguzi Sera ya TEHAMA haikutekelezwa kutokana na Sera hiyo kuanzishwa kabla ya kuanzishwa kwa Bodi yake. Kwa sasa Sera hiyo inafanyiwa kazi vizuri.

**Hoja nambari 12.8.3.9: Kukosekana kwa Mkataba wa Huduma kwa Wateja Wanaohudumiwa na Wakala wa Serikali Mtandao (Taasisi za Umma).**

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Serikali Mtandao haina mkataba wa Huduma kwa wateja kinyume na Sheria na Miongozo iliyopo Zanzibar, inayoelekeza kwamba taasisi za umma zinatakiwa kuwa na mkataba wa Huduma kwa wateja, ambapo pamoja na mambo mengine mkataba huu unatarajiwa kuonesha muda ambao eGAZ itachukuwa kuweza kukamilisha utoaji huduma zake kwa wateja mbalimbali na taratibu nyengine za kufuatwa na wateja ili kupatikana huduma kwa haraka na kwa ufanisi.

Kukosekana kwa mkataba wa Huduma kwa wateja kunaweza kupelekea kuzorota kwa utoaji wa huduma kwa wateja kwa kuwa Wakala anajuwa kwamba wateja wake hawana misingi ya vipimo vya ubora wa huduma zinazotakiwa kutolewa ikiwa ni pamoja na muda na Huduma kwa wateja. Aidha, hali hii inaweza kusababisha kuongeza ugumu kwenye ufanyaji wa tathmini za ufanisi wa taasisi hususani wakati wa ukaguzi.

Hivyo basi, ukaguzi unaishauri Wakala wa Serikali mtandao kuandaa na kuutumia mkataba wa Huduma kwa wateja kwa kuzingatia miongozo ya ndani na viwango bora vinavyokubalika kwenye eneo hilo.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Mkataba wa Huduma kwa Wateja wanaohudumiwa na Wakala wa Serikali Mtandao (Taasisi za Umma) tayari upo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba Mkataba wa huduma kwa Wateja ulikuwepo isipokuwa kutokana na uzembe wa Watendaji walishindwa kumpatia Mkaguzi na kupelekea kujitokeza kwa hoja hii.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala uhakikishe unampatia Mkaguzi vielelezo vyote anavyovihitaji ili aweze kujiridhisha na kuepusha kuwepo kwa hoja zisizokuwa za ulazima.

**Hoja nambari 12.8.3.10: Kukosekana kwa Mpango wa kuendeleza huduma/biashara baada ya kutokea maafa (Business Continuity Plan)**

Kwa mujibu wa Sera za Wakala wa Serikali Mtandao ya mwaka 2012 kifungu cha 4.4.1.2.(d) kinazitaka taasisi za Serikali zenye mifumo kuanzisha mpango na kuweka miundombinu ya kuendeleza huduma za mfumo na taarifa zake baada ya kutekezea maafa dhidi ya mfumo husika. Mpango huo unatarajiwa kuelezea ni kwa utaratibu gani huduma zitaendelea wakati wa majanga na hatua gani zitachukuliwa kabla ili kuweza kuzirudisha taarifa za mfumo wakati yatakapotokea majanga kama kwa mfano udukuzi, majanga ya kimaubile, yanayosababishwa na binaadamu yatakayo haribu taarifa au miundombinu ya mfumo na kupelekea kupotea kwa taarifa hizo.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa Wakala haina mpango huo unaotarajiwa kuwa ni muongozo ambao utafuatwa kabla na baada ya majanga kutokea ili kuokoa taarifa za mfumo kupotea na kubainisha utaratibu wa kufanyika baada ya majanga kutokezea.

Kukosekana kwa mpango huo kunaweza kupelekea kupoteza taarifa muhimu zilizomo ndani ya mfumo kwa sababu Wakala kupitia taasisi mbali mbali za umma zinazotumia mifumo inayosimamiwa na Wakala kutojua nini kifanyike, hatua gani zichukuliwe na nani na wakati gani ili kupata matokeo tarajiwa kabla, wakati na baada ya tukio linaloweza sababisha upotevu mkubwa wa taarifa kama vile moto, mafuriko, tetemeko la ardhi, wizi, uharibifu wa miundombinu, matumizi mabaya n.k.

Ukaguzi unaishauri Wakala kuandaa mpango huu kwa mujibu wa miongozo na sera za Wakala wa Serikali mtandao na kwa kuzingatia miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kimataifa, aidha Wakala ijiwekee utaratibu wa kufanya majaribio angalau mara moja kwa mwaka mipango yote inayolenga kulinda taarifa pamoja na miundombinu ya TEHAMA ambayo imeigharimu Serikali fedha nyingi, muda na juhudi kubwa kuziandaa, kuzichakata na kuzitunza.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Kamati ya PAC haikupokea majibu ya maandishi kutoka kwa Wakala. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa Wakala hauna Mpango wa kuendeleza

huduma/biashara baada ya kutokea maafa (Business Continuity Plan). Kutokuwepo kwa mpango huo, kunaweza kusababisha kuwepo na udhibiti mdogo wa taarifa za Wakala hususan wakati wa kutokea kwa majanga.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wakala uandae mpango wa kuendeleza huduma/biashara baada ya kutokea maafa kwa mujibu wa miongozo na sera za Wakala wa Serikali Mtandao na kwa kuzingatia miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kimataifa.

2. Wakala ijiwekee utaratibu wa kufanya majaribio angalau mara moja kwa mwaka mipango yote inayolenga kulinda taarifa pamoja na miundombinu ya TEHAMA ambayo imeigharimu Serikali fedha nyingi, muda na juhudi kubwa kuziandaa, kuzichakata na kuzitunza.

**Hoja nambari 12.8.3.11: Kutokuwepo Kwa Mpango wa Kupona Maafa (Disaster Recovery Plan)**

Mpango wa kupona maafa (disaster recovery plan) ni mpango ambao unalenga kuikinga taasisi kuepuka madhara yatokanayo na mafuriko, tetemeko la ardhi, kimbunga, ajali, makosa ya kibinadamu, moto au mlipuko, kukatika kwa umeme kwa muda mrefu, matatizo kwenye chumba cha seva na matatizo yasiyotarajiwa kwenye mifumo ya kielekitroniki. Mpango huu unatakiwa kuiwezesha taasisi kurejesha kazi/ huduma zake muhimu kwa haraka baada ya janga kutokea. Taasisi yoyote yenye mpango huu inakusudia kuendeleza huduma/ kazi zake bila ya kutambua kwamba hakuna tatizo lililotokea kwenye mifumo yake mikuu kwa kadri iwezekanavyo.

Aidha, kujiandaa kupona maafa kunahitaji kuzingatia vitu vingi kwa pamoja vinavyohitaji mbinu makini zinazojumuisha miundombinu ya TEHAMA, vifaa vya mtandao, programu, umeme, muunganiko (connectivity) na majaribio (testing) kuhakikisha kwamba kupona maafa kunawezekana. Aidha, mpango huu una ainisha majukumu na wajibu wa kila mdau na huduma/ kazi muhimu zinazotakiwa kurejeshwa kwa haraka ikitokea majanga, pia unaelezea kwa namna gani taasisi inaweza kurejesha huduma mara tu baada ya kupatwa na maafa katika miundombinu ya utoaji wa huduma.

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Serikali mtandao haina Mpango wa kupona maafa ambapo kufanya hivyo ni kwenda kinyume na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kimataifa vinavyosisitiza uwepo wa mpango huu kwa kuzingatia manufaa yake kama vile unafuu wa gharama katika kupona

maafa ukilinganisha na gharama ambazo zingetumika kwenye mazingira ambayo hayana mpango, kuongeza tija kwa wafanyakazi kwa kuwa wanakuwa wanafahamu nini cha kufanya na kinafanywa na nani kwa wakati gani, kuelewa ukubwa wa kazi zinazotakiwa kufanyika na kuendelea kuwahudumia wateja wa taasisi husika.

Athari zinazoweza kujitokeza ikiwa eGAZ haina mpango wa kupona maafa na pindi itakapofikwa na maafa hayo ni pamoja na kusababisha hasara kwa kushindwa kuendelea na kutoa huduma ya ukusanyaji wa mapato kwa taasisi za umma zinazotumia mfumo wa ZanMalipo au kushindwa kufanya kazi kwenye mifumo mengine ya Serikali kama vile “e-Office”, mfumo wa “Government Mail”, kupoteza muelekeo kwa wafanyakazi kwa kutofahamu nini kifanyike na afanye nani kwa wakati gani na kupoteza tija na ufanisi kazini, kupoteza sifa ya Wakala katika kutegemewa kutoka huduma wakati wote.

Ukaguzi unashauri kutengenezwe mpango wa kupona maafa kwa kuzingatia miongozo ya ndani na miongozo ya viwango bora vinavyokubalika kitaifa na kimataifa ili kuhakikisha mpango huo unakuwa wa kujitosheleza kukabiliana na maafa kama ilivyofafanuliwa hapo juu.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

Mpango wa Kupona Maafa kwa taasisi upo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imejiridhishwa kwa kuwepo kwa Mpango huo wa kupona maafa (Disaster Recovery Plan). Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kwamba wakati wa ukaguzi kulikuwa hakuna Mpango huo.

**Hoja nambari 2.8.3.12: Kutokuwepo Kwa Mpango wa Usimamizi na Uratibu wa Kufanya Mabadiliko Kwenye Mfumo (System Change Management Plan).**

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Serikali Mtandao haina mpango rasmi wa kufanya mabadiliko kwenye mfumo. Kukosekana kwa mpango huo kunaweza kupelekea mifumo inayosimamiwa na Wakala kukosa muendelezo wa ubora (consistence of good quality) kwani inaweza kuwepo baadhi ya mabadiliko yanayofanywa kwenye mfumo ambayo madhara yake ni makubwa na kusababisha kushuka kwa ubora wa mfumo. Kwa sababu hiyo, ni muhimu sana kuhakikisha kwamba mabadiliko yoyote yale yanaratibiwa vyema, yanafanyiwa tathimini kwa kina kwenye faida na hasara zake, gharama na muda unaohitajika ili kuyafanya pamoja na yanaidhinishwa na mtu mwenye

uwezo (capacity) wa kubaini uchambuzi ulofanyika na kuwa na uhakika kwamba mabadiliko husika yanapelekea uimarikaji wa mfumo.

Ukaguzi unaishauri Wakala wa Serikali mtandao kuhakikisha kwamba inaandaa na kuutumia mpango rasmi wa kufanya mabadiliko kwenye mfumo kwa kuzingatia miongozo ya viwango bora vinavyokubalika.

**Majibu ya uongozi wa Wakala**

eGAZ ipo katika hatua za awali za kuandaa Mpango wa Usimamizi na Uratibu wa Kufanya Mabadiliko Kwenye Mfumo (System Change Management Plan).

**Uchunguzi wa kamati ya PAC**

Kamati haikuridhishwa na utendaji wa Wakala hasa ukizingatia kwamba ni muda mrefu umepita lakini bado Wakala haijakamilisha uandaaji wa mpango huo muhimu.

**Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaushauri Wakala uhakikishe mpango wa usimamizi na uratibu wa kufanya mabadiliko kwenye mfumo (System Change Management Plan) unapatikana ndani ya muda uliopangwa.

**UKAGUZI MAALUM WA DAWA NA VIFAA TIBA KWA WIZARA YA AFYA USTAWI WA JAMII, WAZEE, JINSIA NA WATOTO**

**1.5.2 HADIDU REJEA NAMBA 1**

**Kupitiwa kwa mchakato mzima wa Zabuni zote zinazohusiana na ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai 2018 mpaka Septemba 2021.**

Katika hadidu rejea hii ukaguzi ulibaini mambo yafuatayo:-

**Hoja nambari1 5.2.1: Kutokujuulishwa kwa Wazabuni kuhusiana na Mshindi wa Zabuni.**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 141 cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinamtaka Afisa Masuuli ndani ya siku 30 baada ya kusaini mkataba kuwajulisha wazabuni walioshindwa kuhusiana na jina la mshindi wa Zabuni na thamani ya mkataba wa aliyoshinda.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto imeshindwa kutekeleza matakwa ya kifungu nambari 141 cha Kanuni

ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ambapo wazabuni walioshindwa hawakupatiwa maelezo na sababu zilizopelekea kushindwa katika zabuni waliyoiomba.

Wazabuni ambao wameshindwa na hawakujulishwa katika mchakato wa zabuni ya dawa na vifaa tiba kwa mujibu wa mkataba wenye kumbukumbu nambari SMZ/H0I/G/2018/2019/07 wenye thamani ya shilingi 5,009,832,500 ni kama wafuatao:-

- M/s In Depth Scientific Ltd.
- M/s Salama Pharmaceutical Ltd.

Aidha Wizara iliweza kumjulisha na kumpitisha mzabuni M/s Kat Med Group Limited bila ya kuzingatia matakwa ya kifungu nambari 141 cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**
Wizara inathibitisha kwamba wazabuni wote walioshiriki katika mchakato huu walijulishwa kuhusu kupata au kushindwa kupata kazi hii. Mzabuni Salama Pharmaceutical limited alibahatika kupata lot na barua ya kujulishwa ilitolewa tarehe 22/05/2019 Yenye kumb namba AB/42/333/92.

Indepth Scientific Ltd hakubahatika kupata kazi hii na alijulishwa kukosa kazi kwa barua yenye kumb namba AB/42/333/113 ya tarehe 19 Julai 2019.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Watendaji wa Wizara kutokubaliana na hoja ya Mkaguzi na kutaka kuviwasilisha mbele ya Kamati vielelezo vya barua husika, Kamati ya PAC ilitaka kujua kwanini vielelezo hivyo hakupatiwa Mkaguzi wakati anatekeleza majukumu yake Ofisini hapo na kujibiwa kwamba vielelezo vilikuwepo isipokuwa vilikuwa havijaonekana. Kutokana na sababu hiyo, Kamati ya PAC ilivikataa vielelezo na kukubaliana na hoja ya Mkaguzi. Kamati imefikia maamuzi hayo kwa vile Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma inaelekeza kwamba matumizi ya fedha husika lazima yaambatanishwe na hati za malipo ili kuhalalisha thamani halisi ya matumizi yaiyofanyika.

Sambamba na hilo, Sheria ya Mkaguzi inaruhusu kutoa fursa ya mwezi mmoja iwapo kuwasilisha vielelezo. Kiufupi, Kamati imebaini kulikuwa na ukiukwaji mkubwa wa taratibu za ununuzi na matumizi ya fedha za umma.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ihakikishe inawasimamia kwa karibu watendaji wake hususan katika uandaaji na uhifadhi wa nyaraka zake ili ziweze kuhalalisha matumizi ya fedha zaumma.
2. Wizara pamoja na watendaji wake watoe mashirikiano ya hali ya juu kwa Mdhibiti wakati wa ukaguzi.

**Hoja nambari 1.5.2.2: Kukosekana kwa barua ya uthibitisho wa kukubali Zabuni**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 139 (1) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinamtaka Mzabuni alieshinda kuthibitisha kwa maandishi kukubali kuwa mshindi mara baada ya kupokea barua ya kujulishwa kuwa mshindi katika zabuni hiyo.

Ukaguzi umeshindwa kupata barua ya uthibitisho wa ushindi wa zabuni kutoka kwa Mzabuni aliyeshinda. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na matakwa ya kifungu nambari 139 (1) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Orodha ya Wazabuni ambao barua zao za uthibitisho wa zabuni hazikupatikana kwa ukaguzi ni kama ifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 1: Wazabuni walioshindwa kuwasilisha barua za uthibitisho wa kukubali zabuni walizopatiwa**

| Namba | Nambari ya Zabuni | Maelezo | Jumla ya Fedha (Tshs.) | Jina la Mzabuni | Hoja ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SMZ/H0I/G/2018/2019/07 | Ununuzi wa vifaa vya maabara | 1,278,700,000 | M & D Chemical and Surgical Limited | Ukaguzi umeshindwa kupata barua ya uthibitisho |
| 2. | SMZ/RBID/G/2018/2019/17 | Ununuzi wa Dawa na Vifaa Tiba | 884,427,500 | Kat Med Group | |

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wazabuni wote wawili walikubali zabuni kupitia barua zao kama ifuatavyo:

(i) M&D Surgical and Surgical Ltd barua yenye kumbukumbu nambari MD/OFFL/VOL.026/2019 ya tarehe 29 Mei 2019.

(ii) KAT MED Group (T) Limited barua yenye kumbukumbu nambari AB/42/333/115 ya tarehe 18 Juni 2019.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba Mkaguzi hakupatiwa vielelezo hivyo, hali hiyo ilisababishwa na kukosekana ushirikiano kwa watendaji wa kitengo cha Manunuzi pamoja na uwepo wa uhifadhi mbaya wa kumbukumbu za Ofisi. Hivyo, Kamati nayo haikuweza kuvikubali vielelezo hivyo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ichukue juhudi za makusudi kuimarisha kitengo cha uwekaji kumbukumbu pamoja na kitengo cha uhasibu.
2. Watendaji wa Wizara wanatakiwa kutoa ushirikiano wa karibu anapofika Mkaguzi kutekeleza majukumu yake ili kusaidia hoja kupata majibu sahihi.

**Hoja nambari 1.5.2.3: Kutokufuatwa kwa ushauri elekezi wa Mwanasheria Mkuu.**

Kwa mujibu wa Kifungu nambari 27(3) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 na kifungu Nambari 47(1) cha Kanuni za Manunuzi kinaelezea kwamba, "Makubaliano yoyote yanayohusiana na ununuzi ambayo thamani yake ni kubwa kuweza kutumia njia ya ununuzi wa zabuni zenye thamani ndogo kwa mujibu wa njia za ununuzi zilizoelezwa ni lazima mkataba huo upate ridhaa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla kusainiwa kwa mkataba huo".

Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto iliingia makubaliano ya mkataba Nambari SMZ/HOI/G/RCB/2020/2021/06 na Kat Media Group limited wenye thamani ya shilingi 21,600,000 kwa ajili ya ununuzi wa filter tips kwa ajili ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Afya haikuweza kuufanyia kazi ushauri kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu ambao ulitaka kufanyike marekebisho katika baadhi ya vifungu vilivyokua na dosari katika mkataba ikiwemo kifungu nambari 17.2 cha masharti ya mkataba (GCC 17.2) cha rasimu ya mkataba ambacho kilitakiwa kufanyiwe marekebisho na Wizara kabla ya mkataba huo kutiwa saini kwa ajili ya utekelezaji.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Wizara imefuata ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kufanya marekebisho kwenye vifungu kwa Mkataba wa Kat Medical Group. Barua ya Mwanasheria na Mkataba uliosainiwa upo kwa kuthibitisha.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imegundua majibu yaliyotolewa hayakuwa na ukweli wowote kwani ilipoulizia kuhusu kupatiwa kielelezo cha barua ambayo Watendaji wa Wizara wameisema haikuweza kupatikana na kuelezwa kwamba ipo Wizarani wakati Kamati imeelekeza kupitia barua yake ya kazi za Kamati kwamba vielelezo vyote vinatakiwa viwepo wakati wa ukaguzi lakini maekelezo hayo Wizara haikuyatekeleza.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara inapotoa majibu ya hoja za Mkaguzi inatakiwa kutoa majibu yaliyo sahihi na yenye vielelezo madhubuti.

**Hoja nambari 1.5.2.4: Kutokufuatwa kwa utaratibu wa kumpata Mzabuni shilingi 701,126,850**

Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto ilitoa zabuni ya ununuzi wa dawa muhimu za kensa na vitendanishi vya damu salama kwa msambazaji ambaye ni Salama Pharmaceutical LTD yenye thamani ya shilingi 701,126,850

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokufuatwa kwa utaratibu wa kumpata Mzabuni wa usambazaji dawa na vitendanishi jambo ambalo limetia shaka juu ya uhalali wa thamani ya fedha iliyotumika ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya Uongozi wa Kamati ya PAC**

Wizara iliingia mkataba (frame work contract) na mzabuni Salama Pharmaceutical Ltd wa kusambaza dawa za kensa na vitendanishi vyenye thamani ya Tsh. 6,417,851,711/= kwa muda wa mwaka mmoja. Manunuzi yake yalikuwa ya ushindani wa wazi na taratibu zote za manunuzi zilifuatwa. Jumla ya Tsh. **701,126,850** zilitokana na malipo ya oda iliyotolewa na Wizara

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na majibu yaliyowasilishwa na Wizara, Kamati imebaini ni kweli taratibu za kumpata Mzabuni zilifanyika kwa Zabuni ya Lot Nam. 2. Kamati imedhubutu kusema hivyo kwa vile imehbahatika kuoneshwa tangazo la Zabuni hiyo iliyotangazwa kupitia gazeti la 'the Guardian" la tarehe 28/1/2019 kwa Zabuni nambari SMZ/HOI/G/1CB/2018/2019 pamoja na gazeti la siku ya Alhamis tarehe 31/1/2019 pamoja na gazeti la 'Zanzibar leo' la tarehe

31/1/2019. Hata hivyo, Watendaji wa Wizara hawakumpatia Mkaguzi vielelezo hivyo na kupelekea hoja hii kuingizwa kwenye kitabu. Kwa mnasaba huo, watendaji wa Wizara hawakutekeleza wajibu wao kutokana na uzembe waliouonesha wakati wa ukaguzi.

Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC
Watendaji wa Wizara wahakikishe hoja zisizo za msingi kama hizi hazijitokezi katika kitabu cha Mkaguzi iwapo watakuwa wakitekeleza majukumu ya kuhifadhi vielelezo vizuri na kumpatia mkaguzi wakati wa ukaguzi.

### 1.5.3 HADIDU REJEA NAMBA 2

**Kupitia mikataba yote ya ununuzi wa dawa ikiambatanishwa na idhini kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai 2018 - Septemba 2021.**

Katika hadidu rejea hii ukaguzi ulibaini mambo yafuatayo:-

**Hoja nambari 1.5.3.1: Kukosekana kwa idhini ya Mwanasheria Mkuu katika Mikataba shilingi 18,408,698,263**

Kwa mujibu wa Kifungu nambari 27(3) Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na kifungu nambari 47(1) cha kanuni za Manunuzi kinaelezea kwamba, “Makubaliano yoyote yanayohusiana na manunuzi ambayo thamani yake ni kubwa kuweza kutumia njia ya manunuzi ya zabuni zenye thamani ndogo kwa mujibu wa njia za ununuzi zilizoelezwa ni lazima mkataba huo upate ridhaa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla kusainiwa kwa mkataba huo”.

Ukaguzi umebaini kwamba, Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto ilisaini mikataba na wasambazaji wa dawa na vifaa tiba mbali mbali kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai 2018 hadi Septemba 2021 ambapo uthibitisho wa idhini na ushauri elekezi kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali haukuweza kupatikana kwa ukaguzi jambo ambalo limetia shaka juu ya uhalali wa matumizi ya fedha ya shilingi 18,408,698,263 zilizotumika kupitia mikataba hiyo.

Mikataba ambayo ukaguzi ameshindwa kupatiwa idhini ya Mwanasheria Mkuu ni kama inavyoonekana kwenye jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 2: Mikataba iliyokosa idhini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

| Namba | Jina la Msambazaji wa dawa | Nambari ya Mkataba | Tarehe | Kiasi (Shs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Salama Pharmaceutical LTD | RGZ/MOH/PMU/ FC/G/01/2020/2021 | 06/01/2021 | 6,417,851,711 | Ununuzi wa dawa na Vifaa Tiba (LOT 1- 6 inahusika) |
| 2. | | RGZ/MOH/PMU/ FC/G/01/2017/2018 | 3/01/2018 | 5,746,801,386.12 | Ununuzi wa dawa na Vifaa Tiba (LOT 1- 4 na LOT 6 zinahusika). |
| 3. | Anudha Limited | SMZ/HO1/ SBID/G/2019/2020/01 | 03/01/2020 | 406,750,000 | Ununuzi wa reagents for Parasitology |
| 4. | Pacific Diagnostics | SMZ/HO1/G/ NCB/2019/2021/83 | 12/04/2021 | 300,400,000.009 | Kufanya services ya 4 maintenance ya mashine ya MRI |
| 5. | Crown Health Care (T) Ltd | RGZ/MOH/PMU/TDR/ SG/05/2017/18 | 08/06/2018 | 90,775,300 | Ununuzi wa mashine Bio Chemistry analyzer na hematology Analyzer |
| 6. | Harsh Pharmaceutical Ltd | RGZ/MOH/PMU/ FC/G/02/2017/2018 | 08/02/2018 | 593,850,000 | Ununuzi wa haemo dialysis Kits & maintenance yahaemo dialysis pamoja na water |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | treatment machine |
| 7. | Crown Health Care Ltd | RGZ/MOH/PMU/ RBID/G/03/2016/2 017 | 13/04/20 18 | 196,259,400 | Ununuzi wa hematolo- gy reagents ,control na Calibrator (MINDRAY) |
| 8. | Kat Med Group Ltd | SMZ/HOI/G/OQ/20 18- 19/01 | 13/12/20 18 | 50,000,000 | Ununuzi wa MRDT kwa ajili ya Kitengo cha Kum- aliza Malaria |
| 9. | Royal Mart Co.Ltd | SMZ/HO1/PMU/ RBID/G/2018/2019 /05 | 31/12/20 18 | 129,800,000 | Ununuzi wa Stabilizer 2 kwa ajili ya Hospital ya Abdallah Mzee |
| 10. | Biotech Prod- ucts Ltd | SMZ/HO1/G/ SS/2020/2021/84 | 14/07/20 21 | 67,257,980 | Ununuzi wa biolarvi- cides- Bactive (BTI) |
| 11. | Indepth Scien- tific Ltd | SMZ/HO1/PMU/G/ RCB/2020/2021/72 | - | 150,000,000 | Ununuzi wa VTM kwa ajili ya kituo cha huduma za dharura |
| 12. | Kat Med Group Ltd | SMZ/H01/G/ NCB/2020/2021/05 | 05/01/20 21 | 1,003,620,00 0 | Ununuzi wa mashine za hospital kwa ajili |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ya Hospital ya Kivunge |
| 13. | Immunolabs Medical Supplies | RGZ/MOH/PMU/ FC/G/01/2017/2018 | 03/01/2018 | 228,205,736 | Ununuzi wa reagents za microbiology |
| 14. | Nebula Health Care Ltd | SMZ/HO1/G/ RCB/2020/2021/86 | 23/09/2021 | 2,316,000,000 | Ununuzi wa reagents za VTM |
| 15. | Nebula Health Care Ltd | SMZ/HO1/G/ NCB/2020/2021/08 | 29/07/2021 | 658,134,750 | Ununuzi wa vifaa vya Mifupa |
| 16. | Lab Equip Limited | SMZ/H01/PMU/ SS-BID/G/2018/2019/ 18 | 04/04/2019 | 52,992,000 | Ununuzi wa reagent za electrolyte analyser |
| **Jumla** | | | | **18,408,698,263** | |

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Kama ilivyo utaratibu mikataba yote hupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kupata ushauri wa kisheria. Barua kutoka kwa Mwanasheria Mkuu zinapatikana kwa uthibitisho.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC haiukukubaliana na majibu ya Wizara kwa vile hakuna vielelezo vilivyoweka wazi upatikanaji wa idhini ya Mwanasheria Mkuu.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ihakikishe inatunza vielelezo vizuri ili vitakapohitajika viweze kupatikana kwa urahisi.
2. Wizara ihakikishe inapoingia mikataba na watoa huduma, inawasilisha mikataba yake Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Hoja nambari 1.5.3.2: Kutokurikodiwa kwa baadhi ya mikataba kwenye "Contract Register" shilingi 7,112,535,191**

Ukaguzi umebaini kwamba, baadhi ya taarifa za mikataba ya manunuzi hazikuorodheshwa kwenye daftari la kurikodia taarifa za mikataba ambayo inafungwa baina ya taasisi na mtoa huduma yenye thamani ya shilingi 7,112,535,191 jambo ambalo limepelekea uwepo wa changamoto ya kufahamu idadi ya mikataba halali iliyofungwa na Wizara kwa mujibu wa mwaka wa fedha husika kupitia wasambazaji mbali mbali walioshinda zabuni na kusababisha kuathiri upeo wa ukaguzi.

## Jadweli Nambari 3: Mikataba iliyokuwa haikurikodiwa kwenye "Contract Register"

| Na | Aina ya Mkataba | Nambari ya Mkataba | Mzabuni Husika | Nambari ya LOT | Thamani ya Mkataba (Shs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ununuzi wa biolarvicides - Bactive(BTI) | SMZ/HO1/G/SS/2020/2021/84 | Biotech Products Ltd | N/A | 67,257,980 |
| 2. | Ununuzi wa filter tips na sterile filter 96 tips. | SMZ/HO1/G/RCB/2020/2021/06 | Kat Med Group (T) Limited | N/A | 21,600,000 |
| 3. | Ununuzi wa Vifaa tiba. | SMZ/HO1/G/NCB/2020/2021/06 | Lab Equip Ltd | LOT 2 | 107,026,500 |
| 4. | Ununuzi wa VTM. | SMZ/HO1/PMU/G/RCB/2020/2021 | Indepth Scientific Ltd | N/A | 150,000,000 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | /72 | | | |
| 5. | Ununuzi wa dawa. | SMZ/HO1/G/ OQ/2020/2021/ 06 | Life Care Pharmacy | N/A | 48,399,000 |
| 6. | Kufanya matengenezo ya mashine ya MRI | SMZ/HO1/G/ NCB/2019/2021 /83 | Pacific Diagnostics | N/A | 300,400,000 |
| 7. | Ununuzi wa dawa, vifaa tiba, na vitendanishi | RGZ/MOH/PMU / FC/G/01/2020/ 2021 | Salama Pharmaceutical Ltd | LOT 1-6 | 6,417,851,711 |
| **Jumla** | | | | | **7,112,535,191** |

**Majibu ya Uingozi wa WIizara**

Ushauri unapokelewa na umeshaanza kufanyiwa kazi. Mikataba yote inarikodiwa kwenye daftari maalum

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imegundua kuwa Ofisi ya Mkaguzi haikupaswa kuiainisha hoja kama hii katika kitabu cha Ripoti kwa vile haijahusisha matumizi ya fedha au ukiukwaji wa sheria yoyote au ufungaji mbaya wa hesabu za mwisho wa mwaka. Hoja hii haikupaswa kujitokeza kwa vile daftari lililoelezwa lilitumiwa na watendaji kuwarahisisishia kutekeleza majukumu yao na sio kama lilikuwa kielelezo cha kumbukumbu za mikataba kama ilivyojitokeza katika Kamati. Sam amba na hilo Kamati imeweza kujiridhisha kwamba taarifa zilizoainishwa na Mkaguzi zilikuwa zimesharekebishwa. Kwa mnasaba huo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

**HADIDU REJEA NAMBA 3:**

**Kuhakiki upya madeni ya dawa na vifaa tiba.**

Katika hadidu rejea hii ukaguzi ulibaini mambo yafuatayo:-

**Hoja nambari 1.5.4.1: Kukosekana kwa taarifa za madeni katika kitengo cha Uhasibu.**

Kwa mujibu wa uhakiki wa madeni uliofanyika imebainika msambazaji wa dawa na vifaa tiba huwasilisha dawa na vifaa tiba pamoja na ankara za malipo Bohari Kuu ya Dawa kwa kuzingatia makubaliano ya Wizara.

Aidha baadhi ya wasambazaji huwasilisha dawa na vifaa tiba kwa watumiaji bila ya uwepo wa taarifa za mapokezi Boharia Kuu ya Dawa na kupelekea kujitokeza kwa athari zifuatazo:-

- Kutokuwepo kwa baadhi ya taarifa za ankara za malipo ya madeni katika Kitengo cha Uhasibu.
- Kutokuwepo kwa taarifa sahihi za dawa zilizopokelewa na kusambazwa na Bohari Kuu ya Dawa katika mfumo wa usimamizi wa taarifa za dawa na vifaa tiba "mSupply".
- Kukosekana kwa daftari la kurikodia ankara za malipo ya madeni "Invoice Register" ya dawa na vifaa tiba zilizopokelewa na Bohari Kuu.
- Kuongeza hatari ya kuingiza dawa zilizokaribia/zilizoisha muda wa matumizi.
- Kupelekea kutokujua mahitaji sahihi ya dawa na vifaa tiba yanayohitajika kwa miaka ijayo.
- Uwezekano wa kuwepo kwa madeni hewa na kufanya malipo zaidi ya mara moja kwa ankara moja.
- Kuwepo kwa taarifa za madeni zinazotofautiana juu ya madeni yaliyoripotiwa Bohari Kuu ya Dawa, Mfamasia Mkuu na Mhasibu Mkuu.
- Kutokurikodiwa kwa madeni ya dawa zilizopokelewa Bohari kwenye Mfumo wa malipo wa IFMIS uliopo Wizara ya Afya.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Kitengo cha uhasibu hakina mfumo wa kuweka rekodi za madeni. Hata hivyo Wizara ipo katika hatua ya kuanzisha mfumo utakaowahusisha kitengo cha uhasibu, ofisi ya mfamasia, bohari kuu ya dawa na kitengo cha manunuzi kuweza kufuatilia madeni hayo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba kulikuwa na taarifa za akara ambazo Mkaguzi hakuzipata alipokuwa kitengo cha uhasibu jambo ambalo limesababishwa na kutokuwepo kwa Mfumo wa pamoja kwani Kitengo pekee bila ya kuzishirikisha taasisi nyengine (Bohari Kuu na kitengo cha Manunuzi) hakitoweza kufanikiwa kutengeza mfumo wake hasa ukizingatia Taasisi hizo huwa zinajitegemea., Aidha, Kamati imebaini kuwa ni kweli kulikuwa na changamoto ya kutokuwepo kwa taarifa sahihi za dawa zilizopokelewa na kusambazwa na Bohari Kuu ya Dawa katika mfumo wa usimamizi wa taarifa za dawa na vifaa tiba “mSupply”. Hilil lmebainika kutokana na ukaguzi ulionyinywa na Mkaguzi katika mifumo ya Taasisi hizo.

Katika mpango mzima wa kuzuia upotevu wa mapato ya Serikali, Kamati ya PAC ilitaka kujua uanadaaji wa mfumo umefikia hatua gani na kuelezwa kwamba bado mfumo huo haujaanza kutayarishwa tofauti na ilivyoelezwa na Majibu ya Wizara. Kamati pia ilitaka kujua kuhusu kuwepo kwa daftari la kurikodia ankara za malipo ya madeni “Invoice Register” ya dawa na vifaa tiba zilizopokelewa na Bohari Kuu na kubaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake ya kiukaguzi katika Bohari Kuu kulikuwa hakuna daftari hilo ila hivi sasa Kamati imejiridhisha kwamba daftari lipo na linafanyakazi zake ipasavyo.

Kuhusiana na taarifa za madeni ya Wizara ya Afya, Kamati imebaini haitumii Mfumo wa IFIMS isipokuwa fedha zake huwa zinapitia moja kwa moja Benki na sio WIzara ya Fedha na Mipango. Hata hivyo, taarifa za madeni ya nunuzi wa dawa na vifaa tiba haziingizwi katika hesabu ya mwisho wa mwaka (Financial Statement) ya Wizara. Hali ambayo imepelekea kutokuwa na Hesabu yenye sura halisi na sahihi kwa wakaguzi na watumiaji wa hesabu hizo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

1. Wizara iandae mfumo utakaozishirikisha Taasisi zote muhimu za Bohari ili kurahisisha utoaji w huduma na kupungunguza kama sio kumaliza ubadhirifu wa mali za umma.
2. Wizara inapoandaa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka, ihakikishe inaingiza na madeni ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba ili taarifa hiyo iweze kukamilika na kueleweka na mtumiaji.

**Hoja nambari 1.5.4.2: Kukosekana kwa uhalisia wa deni la dawa na vifaa tiba linalodaiwa**

**(a) Tofauti ya deni baina ya Mfamasia Mkuu na Msambazaji shilingi 1,636,059,059 na USD 503,317.98**

Kutokuwepo kwa baadhi ya taarifa za ankara za malipo ya madeni katika Kitengo cha Uhasibu kumepelekea kukosekana kwa uhalisia wa deni la dawa na vifaa tiba linalodaiwa na kupelekea kila kitengo kuripoti deni lake jambo ambalo hupelekea kujitokeza kwa uwezekano mkubwa wa Serikali kulipa deni lisilokuwa halisi au kulipa ziada ya deni husika.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kitengo cha Mfamasia Mkuu kimeripoti uwepo wa deni la shilingi 9,190,613,214 ambapo ukaguzi umebaini uwepo wa deni la shilingi 7,554,554,155 ambalo limewasilishwa na wasambazaji wa dawa na vifaa tiba katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kupelekea uwepo wa ziada ya deni hewa la shilingi 1,636,059,059 pamoja na USD 503,317.98 lililobainika katika ukaguzi.

Hali halisi ya taarifa za deni hilo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 4: Tofauti ya madeni iliyobainika kwa wasambazaji wa dawa na vifaa tiba**

| Namba | Jina la Msambazaji | Taarifa ya Deni Kutoka Kwa Mfamasia Mkuu (Tshs) | Taarifa ya Deni kutoka kwa Msambazaji (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Salama Pharmaceutical Ltd | 2,975,312,008 | 2,978,522,007 |
| 2. | Kat Medics Group | 2,121,838,500 | 1,980,650,500 |
| 3. | Lab Equip | 107,026,500 | 107,026,500 |
| 4. | Nebula | 465,297,500 | 715,689,150 |
| 5. | MSD | 1,446,141,606 | 992,984,129 |
| 6. | Harsh Pharmaceutial | 135,582,800 | 199,522,500 |
| 7. | Indepth Scientific | 21,022,000 | 134,099,363.42 |
| 8. | Kas Med | 57,710,000 | 94,873,005.81 |
| 9. | Anudha | 12,715,000 | 42,573,000 |
| 10. | Amini Pharmacy | 39,120,000 | 44,274,000 |
| 11. | Bahari Pharmacy | 16,932,000 | 159,575,000 |
| 12. | Ghareeb Nawaz | 21,876,000 | 24,126,000.00 |
| 13. | Life Care | 14,700,000 | 80,639,000.00 |
| 14. | Abbott | 1,755,339,300 | |
| | **Jumla** | **9,190,613,214** | **7,554,554,155** |
| 15. | Abbott (USD) | | **USD 503,317.98** |

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Taarifa rasmi ya madeni ya Wizara ni ile iliyotolewa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Wizara ambayo inaonesha madeni hadi kufikia Septemba 2021. Kwa kutatua changamoto hii isijirejee Wizara imeanzisha kamati ya kuratibu madeni yote yakiwemo ya dawa na vifaa tiba.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kutathmini majibu ya hoja hii, Kamati imebaini kwamba Wizara haikuwa na majibu ya kutosheleza kwani taarifa zilizoibuliwa katika hoja ya Mkaguzi zilipatikana baada ya kufuatilia mifumo ya malipo ya Kampuni husika na kubaini kwamba kuna tofauti ya madeni ambapo baadhi ya madeni yaligundulika kuwa tayari yameshalipwa na yanaombewa tena kulipwa. Jambo ambalo ni ubadhirifu na uhujumu wa mali za umma. Kwa mnasaba huo, Kamati imebaini utaratibu uliokuwa ukitumika wa uandaaji, ulipwaji na uhifadhi kumbukumbu za madeni haukuwa katika mpango unaoeleweka. Vile vile, Kamati imepata wasiwasi kwamba utaratibu huo ulikuwa unatoa mwanya kwa baadhi ya watendaji kunufaika na fedha za ununuzi wa dawa na vifaa tiba kinyume na utaratibu (kulikuwa na harufu ya wizi wa fedha za Serikali).

Kamati imepata mashaka zaidi kwamba majibu ya Wizara yaliegemea katika Ripoti ya mwaka ya Mkaguzi wa Ndani ambayo haikuwa na ukweli wowote wala haikupelekwa kwa Mdhibiti a Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyoelekezwa na Sheria ya Kuanzishwa Ofisi ya hiyo nambari 11 ya mwaka 2003. Hali hiyo imepelekea uwepo wa ziada ya deni hewa la shilingi 1,636,059,059 pamoja na USD 503,317.98 lililobainika katika ukaguzi.

Katika hoja hii, Kamati ya PAC inakubaliana na maelezo yaliyoelezwa na Mkaguzi kwani ilipotaka vielelezo juu ya uhalali wa uwepo kwa fedha hizo, Kamati haikupata majibu hayo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Vyombo vyengine vya uchunguzi ikiwemo ZAECA vihakikishe vinalifuatilia kwa karibu suala hili kwa kuwaita, kuwahoji na kuwachukulia hatua wote wanaohusika na kadhia ya udanganyifu kwa lengo la kutaka kuhujumu uchumi wa Wazanzibari ambao ndio walipakodi.

2. Afisa Masuul ahakikishe anatumia mbinu mbadala kuwasimamia watendaji wake wasiokuwa waaminifu na kuwachukulia hatua za kinidhamu wote waliohusika.

3. Afisa Masuul aandae mfumo maalum wa malipo ya wasambazaji bidhaa ili kuepusha wajanja wengine kutaka kujinufaisha na rasilimali za umma kinyume na sheria.

**(b) Tofauti ya deni iliyobainika baina ya Bohari Kuu ya Dawa na Msambazaji shilingi 1,121,935,897.79 na USD 503,317.98**

Aidha, Bohari Kuu ya Dawa imeripoti uwepo wa deni la shilingi 6,280,203,983.21 pamoja na USD 503,317.98 kwa mujibu wa ankara za malipo zilizopo, ukaguzi umebaini uwepo wa deni la shilingi 7,402,139,881 pamoja na USD 503,317.98 lililowasilishwa na wasambazaji wa dawa na vifaa tiba katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupelekea uwepo wa ziada ya tofauti ya shilingi 1,121,935,897.79 baina ya taarifa ya deni kutoka Bohari Kuu ya Dawa na taarifa ya deni kutoka kwa Wasambazaji (Wadai).

Pamoja na uwepo wa ziada ya taarifa ya deni lilioripotiwa na Wasambazaji wa dawa na vifaa tiba ambalo deni hilo linatofautiana na deni halisi lililowasilishwa na Bohari Kuu ya Dawa kwa ajili ya ukaguzi kama linavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 1** ambalo linatokana na kutokuwepo kwa daftari la kurikodia ankara za malipo ya madeni “Invoice Register” ya dawa na vifaa tiba zilizopokelewa na Bohari Kuu.

Kutokuwepo kwa daftari hilo kunaweza kupelekea Serikali kulipa madeni ambayo hayakuwepo (madeni hewa). Hali halisi ya taarifa za deni hilo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 5: Tofauti ya madeni iliyobainika baina ya Bohari Kuu ya Dawa na Wasambazaji wa dawa na vifaa tiba**

| Nam. | Jina la Msambazaji | Taarifa ya Deni Kutoka Bohari Kuu ya Dawa (Tshs) | Taarifa ya Deni kutoka kwa Msambazaji (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Salama Pharmaceutical Ltd | 2,692,013,090.98 | 2,700,877,733 |
| 2. | Kat Medics Group | 1,890,150,000 | 1,980,650,500 |
| 3. | Lab Equip | 107,026,500 | 107,026,500 |
| 4. | Nebula | 715,689,150 | 715,689,150 |
| 5. | MSD | 992,984,12 | 992,984,129 |
| 6. | Harsh Pharmaceutial | 104,839,500 | 199,522,500 |
| 7. | Indepth Scientific | 134,099,363.42 | 134,099,363.42 |
| 8. | Kas Med | 78,959,650.81 | 94,873,005.81 |
| 9. | Anudha | 42,573,000 | 42,573,000 |
| 10. | Amini Pharmacy | 44,274,000 | 44,274,000 |
| 11. | Bahari Pharmacy | 159,575,000 | 159,575,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 12. | Ghareeb Nawaz | 24,126,000.00 | 24,126,000.00 |
| 13. | Life Care | 80,384,000 | 80,639,000.00 |
| 14. | M&D Chemical And Surgical Limited | 206,494,728 | 125,230,000 |
| **Jumla (Tshs.)** | | **6,280,203,983.21** | **7,402,139,881** |
| 15. | Abbott | USD 503,317.98 | USD 503,317.98 |
| **Jumla (USD)** | | **USD 503,317.98** | **USD 503,317.98** |

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Bohari kuu ya dawa ilithibitisha invoice 2 tofauti kutoka Abbot GMBH INVOICE 13-03536734 na invoice no. 13-03536763 kwa thamani ya USD 503,317.98. Aidha tofauti ya deni 1,121,935,897.79 ni mjumuisho wa invoice kutoka wasambazaji tofauti na imebainika kuwa kupitia deni la MSD kuna tofauti ya tarakimu zilizowasilishwa na Mkaguzi wa Hesabu. Deni halisi ni shilingi 992,984,129 na sio shilingi 99,298,412. (Kiambatanisho barua ya uthibitisho ya tarehe 20.12.2021. Kumbukumbu nambari WAUJUJW/CMS/CW/27/2021).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katikaka kufuatilia majibu ya hoja hii, Kamati ya PAC ilihoji kwamba kwanini majibu na kielelezo hicho hakupatiwa Mkaguzi wakati alipofika katika Ofisi zao kwa ukaguzi na wakati wa kuwasilisha barua kwa Uongozi yenye mapendekezo ya hoja (management letter) na Kamati kubaini kwamba Mkaguzi hakupatiwa vielelezo hivyo kwa vile vilikosa alama ya uthibiitisho wa ukaguzi wake. Kwa mnasaba huo, Kamati nayo haikuvikubali kutokana na kuwepo shaka juu ya usahihi wake.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara iwapatie ushirikiano wa kutosha Wsksguzi wanaofika katika maeneo yao kwa kazi za Ukaguzi ili aweze kupata majibu na vielelezo vitakavyorahisisha utekelezaji wa kazi zake.
2. Taasisi za kiuchunguzi zifuatilie wale wote wanaohusika na udanganyifu uliofanyika na kuwachukulia hatua za kisheria hususan watendaji waliokuwa wakihusika na masuala ya manunuzi na uhasibu.

**Hoja nambari 1.5.4.3: Makato ya Kodi ya Ongezeko la thamani yaliyokatwa kimakosa shilingi 325,990,201.95**

Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) namba 4 ya mwaka 1998, Jadweli nambari 2, sehemu ya 10, kifungu nambari 2 (c) inatoa ruhusa ya kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwa uingizaji wa madawa na vifaa tiba.

Ukaguzi umebaini uwepo wa wasambazaji ambao wamekatwa kodi ya Ongezeko la Thamani kinyume na mazingatio ya sheria iliyonakiliwa hapo juu na kupelekea uwepo wa malalamiko ambayo yamepelekea malimbikizo ya deni la shilingi 325,990,201.95 yanayodaiwa na wasambazaji.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba M & D Chemical na Salama Pharmaceutical LTD waliandika barua za kuomba kurejeshewa gharama za fedha zao zilizokatwa kimakosa kwa mujibu wa Kiambatisho Nambari 2 pamoja na jitihada zilizochukuliwa na Wizara ukaguzi haukuthibitisha uwepo wa marejesho ya fedha hizo kufanyika.Mchanganuo wa wasambazaji hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 6: Fedha za makato ya kodi iliyokatwa kimakosa**

| **Nam** | **Jina la Mdai** | **Fedha Iliyolipwa (Tshs)** | **Fedha ya Kodi Iliyolipwa Kimakosa (VAT - 18%) A (Tshs)** | **Fedha ya Kodi ya Zuio (Withholding Tax - 3%) B (Tshs)** | **Fedha Anayodai (A– B ) (Tshs)** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | M & D Chemical | 719,231,000 | 109,713,203.39 | 20,948,475.73 | 88,764,727.66 |
| 2. | KAS Medics | 24,426,480 | 3,726,073.22 | 711,450.87 | 3,014,622.35 |
| | | 77,620,000 | 11,840,338.98 | 2,260,776.70 | 9,579,562.28 |
| | **Jumla Ndogo** | **102,046,480** | **15,566,412.20** | **2,972,227.57** | **12,594,184.63** |
| 3. | SALAMA Pharmaceutical | 213,111,400 | 32,508,518.64 | 6,207,128.16 | 26,301,390.49 |
| | | 244,285,789 | 37,263,933.92 | 7,115,120.07 | 30,148,813.85 |
| | | 528,258,965 | 80,581,876.02 | 15,386,183.45 | 65,195,692.57 |
| | | 131,518,816 | 20,062,192.27 | 3,830,645.13 | 16,231,547.14 |
| | | 3,450,000 | 526,271.19 | 100,485.44 | 425,785.75 |
| | | 68,187,762 | 10,401,523.02 | 1,986,051.32 | 8,415,471.70 |
| | | 11,926,434 | 1,819,286.54 | 347,371.86 | 1,471,914.68 |
| | | 288,000 | 43,932.20 | 8,388.35 | 35,543.85 |
| | | 13,649,284 | 2,082,094.17 | 397,551.96 | 1,684,542.21 |
| | | 260,000,000 | 39,661,016.95 | 7,572,815.53 | 32,088,201.42 |
| | | 84,573,720 | 12,901,075.93 | 2,463,312.23 | 10,437,763.70 |
| | | 7,286,245 | 1,111,461.10 | 212,220.73 | 899,240.37 |
| | | 103,060,000 | 15,721,016.95 | 3,001,747.57 | 12,719,269.38 |
| | | 38,161,598 | 5,821,260.71 | 1,111,502.85 | 4,709,757.86 |
| | | 3,450,000 | 526,271.19 | 100,485.44 | 425,785.75 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 108,154,450 | 16,498,136.44 | 3,150,129.61 | 13,348,006.83 |
| | | 750,000 | 114,406.78 | 21,844.66 | 92,562.12 |
| **Jumla Ndogo** | | **1,820,112,463** | **277,644,274.02** | **53,012,984.36** | **224,631,289.66** |
| **JUMLA KUU** | | | | | **325,990,201.95** |

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Hizi fedha ni kweli zilikatwa kimakosa, ila fedha zote zilipelekwa moja kwa moja ZRA, pamoja na hayo barua ilipelekwa ya kuomba kurejeshwa fedha hizo kwa ajili ya kulipwa wahusika, hata hivyo ZRA walijibu kuwa fedha hizo hazistahiki kurejeshwa kwa wahusika kwa mujibu wa sheria nambari 9 ya 2009 ya Usimamizi wa Kodi ya kifungu nambari 37. (Kiambatisho; Barua kumbu. ZRB/WH.2/VOL.II/52 YA TAREHE 09/03/2021).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kutafuta ukweli wa hoja hii, Kamati ilihoji kwanini Wasambazaji bidhaa hao walikatwa kimakosa kodi hizo na kutokea shida katika urudishwaji wake na kuelezwa kwamba awali waliwakata kodi ya asilimia 18 ya VAT wakati walistahiki kulipa asilimia 3 ikiwa ni kodi ya Stempu kwa mwaka huo. Kwa vile Wasambazaji wanaodai wanastahiki kurudishiwa kodi hiyo. Ni busara kwa Taasisi ya kodi irekebishe changamoto iliyojitokeza.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ya Afya ikutane na uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ili kuitafutia ufumbuzi changamoto ya Wasambazaji wa bidhaa zetu ili kama wana haki basi wapatiwe haki zao kwa kuwalipa deni husika kupitis huduma wanazozitoa hapa Zanzibar..

**1.5.5: Hadidu Rejea Namba 4**

**Kuhakiki deni la msambazaji wa dawa "Salama Pharmaceutical ltd" kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu.**

Katika Ufatiliaji wa deni la shilingi 2,972,535,555 lililoripotiwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na Salama Pharmaceutical ikiwa ni deni kuanzia tarehe 17 Septemba 2019 hadi tarehe 11 Januari 2022, Kamati imebaini yafuatayo:-

- Mfumo wa "SAP Business One" ndio mfumo mkuu unaotumiwa na Salama Pharmaceutical kwa ajili ya uwekaji wa kumbukumbu za upokeaji wa fedha, thamani za Ankara zilizotolewa, taarifa za urejeshwaji

wa bidhaa (Credit Note), pamoja na Jumla ya bakaa la deni linalodaiwa baina ya Wizara ya Afya na mzabuni huyo.

- Uwepo wa deni la shilingi 2,990,368,539 linaloonekana kwenye mfumo wa SAP Business One unaomilikiwa na Salama Pharmaceutical Ltd ambapo deni hilo limebainishwa kwenye ripoti inayoitwa "Customer Statement" ya Wizara ya Afya Zanzibar kuanzia 01 Aprili 2011 hadi 01 Februari 2022, Kielelezo Nambari 1 Kinahusika.
- Uwepo wa deni jengine la shilingi 4,543,646,729 linaloonekana kwenye mfumo wa SAP Business One unaomilikiwa na Salama Pharmaceutical Ltd ambapo deni hilo limebainishwa kwenye ripoti inayoitwa "Customer Statement ya Wizara ya Afya Zanzibar kuanzia 17 Septemba 2019 hadi 01 Februari 2022, Kielelezo Nambari 2 Kinahusika**.**
- Taarifa iliyopatiwa Kamati ni kwamba Ankara za malipo hutolewa kutoka ndani ya mfumo wa SAP Business One, lakini mfumo huo haujaunganishwa moja kwa moja na Benki ya CRDB inayotumiwa kwa malipo na badala yake fedha zinazopokelewa kwa malipo ya dawa kutoka Wizara ya Afya taarifa zake huingizwa katika mfumo wa SAP kwa njia ya kawaida "manually" jambo ambalo huwenda likapelekea kujitokeza kwa makosa ya kibinaadamu "human error" katika uingizaji wa taarifa hizo.
- Kamati ilipatiwa taarifa za mikataba kuanzia mwaka 2018 hadi 2021, ankara zote zilizofanyiwa malipo kuanzia mwaka 2017 hadi mwaka 2022, hati za uthibitisho wa mapokezi ya bidhaa (Delivery Notes) pamoja na ankara zilizowasilishwa kwa ajili ya madai kuanzia tarehe 8 Aprili 2021 hadi tarehe 25 Agosti 2021, Kielelezo Nambari 3 Kinahusika. Aidha katika kuhakiki ankara zote zilizowasilishwa na mzabuni Salama Pharmaceutical Ltd kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu SPL/ZNZ/03/2022 ya tarehe 28 Machi 2022, kamati imebaini jumla ya shilingi 5,158,570,761 zimelipwa kuanzia mwaka 2017 hadi mwaka 2022 kwa ankara zilizowasilishwa na Salama Pharmaceutical Ltd ambapo jumla ya shilingi 13,024,251,232.87 zimelipwa na Wizara ya Afya kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2022 kwa mujibu wa hati za malipo pamoja na ankara zake zilizowasilishwa, taarifa za kibenki (bank statements) na kubainika uwepo wa ziada ya malipo ya shilingi 7,865,680,471.87 aliyolipwa Salama Pharmaceutical Ltd ambapo malipo hayo hayakuweza kujulikana kutokana na ankara zipi alizoziwasilisha hadi kufanyiwa malipo hayo, Kielelezo Nambari 4 na Kielelezo Nambari 5 kinahusika.
- Kamati imebaini uwepo wa malipo yaliyolipwa kwa mzabuni Salama Pharmaceutical Ltd yenye thamani ya jumla ya shilingi 801,137,232 ambayo yamelipwa tarehe 25 Februari 2019 yenye thamani ya shilingi 684,742,632 na tarehe 24 Aprili 2019 yenye thamani ya shilingi 116,394,600 malipo hayo yamebainika kulipwa kupitia taarifa za kibenki lakini kamati imeshindwa kujiridhisha kutokana na kukosekana kwa hati za malipo kutoka Wizara ya Afya, hata hivyo jitihada mbali mbali zimechukuliwa za kuwasiliana na watendaji wa Wizara ya Afya

waliohama na walioko kazini kwa lengo la kutupatia hati za malipo hayo pamoja na ankara zilizohusika na malipo hayo, pia kamati ilitumia jitihada ya kuwasiliana na Mkurugenzi Kinga pamoja na Mhasibu Mkuu wa Serikali na kuwataka watusaidie kufanya mawasiliano na wahasibu waliohama na waliopo kazini kwa kutoa ushirikiano kwa kamati lakini hadi tunakamilisha uhakiki wa madai hayo kamati haijapatiwa taarifa hizo.

- Kamati imefanya uhakiki wa kina kupitia ripoti ya mfumo wa mapokezi ya fedha wa mzabuni Salama Pharmaceutical Ltd na kubaini uwepo wa jumla ya shilingi 5,670,008,088 zilizopokelewa kutoka Wizara ya Afya kwa ajili ya malipo ya usambazaji wa dawa, hata hivyo kutokana na utaratibu uliokuwa ukitumiwa na Wizara wa kulipa malipo ya dawa kutoka katika hesabu ya Katibu Mkuu Wizara ya Afya – Madawa kamati imeshindwa kujiridhisha uhalali wa uwepo wa malipo hayo kutokana na kutokupatiwa hati za malipo kutoka Wizara ya Afya, ankara za malipo zilizofanyiwa malipo hayo, kutokuonekana kwa miamala hiyo ya kifedha katika taarifa za kibenki (bank statements) za hesabu ya Katibu Mkuu Wizara ya Afya - Madawa iliyofungwa na inayotumika sasa pamoja na kutokupatiwa kwa taarifa za hesabu za benki (bank statements) za mzabuni Salama Pharmaceutical Ltd ili kuweza kujiridhisha uhalali wa malipo aliyokiri kulipwa kutoka Wizara ya Afya, Kielelezo Nambari 6 Kinahusika.
- Kamati ilifanya kikao cha awali na kampuni ya Salama Pharmaceutical Ltd tarehe 23 Machi 2022 katika ofisi yake iliyopo Dar es Salaam ambapo katika kikao hicho mambo mbali mbali yalijadiliwa ikiwemo kupatiwa taarifa za kibenki (bank statements) kwa ajili ya kupitia miamala yote ya malipo yaliyolipwa na Wizara ya Afya kwa kampuni hiyo, kampuni ya Salama Pharmaceutical Ltd iliieleza Kamati kwamba haiwezi kutupatia taarifa tuliyoiomba kutokana na kwamba taarifa hiyo imekusanya miamala ya fedha ya kampuni nyengine, vyenginevyo wanaweza kutupatia taarifa watakayoiandaa kupitia CRDB Online Banking System jambo ambalo halikuwa sahihi kutokana na uchunguzi uliokuwa unafanywa na kupelekea kukwaza upeo (limitation of scope) wa uhakiki wa madai hayo. Aidha Kamati ilirudi kwa Kampuni ya Salama kwa mara ya pili na kuibembeleza kampuni hiyo iweze kutupatia taarifa hizo kutokana na umuhimu wa utekelezaji wa maagizo ambayo yatapelekea Serikali kuchukuwa hatua ndipo kampuni ya Salama ilipoandika barua na kuipeleka benki ya CRDB yenye kumbukumbu namba SPL/CORR/ISC/05/2022 ya tarehe 24 Machi 2022 ya kuitaka Benki imuwasilishie taarifa zake za hesabu za kibenki (Bank statements), Kielelezo Nambari 7 Kinahusika.
- Kamati ilikutana tena kwa mara ya tatu na kampuni ya Salama na kuwataka watuwasilishie taarifa za kibenki (bank statements) jambo ambalo limepelekea kamati kuongozana na watendaji wa kampuni hadi kwa Meneja wa benki ya CRDB tawi la Lumumba, Dar es Salaam na

kumueleza umuhimu wa jambo tunalolifanya kwa maslahi ya taifa na kumtaka atusaidie upatikanaji wa taarifa hizo.

- Hata hivyo, kutokana na muda wa uhakiki wa madai kuendelea kuwa mkubwa bila ya mafanikio ya taarifa tulizokuwa tunaziomba kupatikana, Kamati ilikutana na watendaji wa Kampuni ya Salama katika Ofisi yake na kufanya kikao cha tarehe 28 Machi 2022 baada ya kupatiwa taarifa na wasamaria wema ambao walikuwa na nia ya kuisaidia kamati juu ya upatikanaji wa taarifa kutoka benki ya CRDB na kutuamuru njia bora ya kuishauri kampuni ya Salama kutokana na taarifa tunazozitaka zitumwe moja kwa moja kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa njia ya barua pepe ili kuondoa khofu ya kubadilishwa kwa taarifa hizo kabla ya kufika kwa Kamati, Kampuni ya Salama Pharmaceutical Ltd iliiandikia barua Benki ya CRDB yenye kumbu kumbu nambari SPL/ CORR/ISC/06/2022 ya tarehe 28 Machi 2022 Kielelezo Nambari 8 Kinahusika, hata hivyo hadi tunakamilisha uhakiki wa madai hayo Kamati haijapatiwa taarifa za kibenki ya miamala ya kifedha (bank statements) iliyolipwa na Wizara ya Afya katika Kampuni ya Salama Pharmaceutical Ltd.
- Kamati imebaini uwepo wa dawa zilizosambazwa na mzabuni Salama Pharmaceutical ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba ZFDA/OTC&MDA.D/3VOL.II ya tarehe 30 Januari 2020 iliyotoka ZFDA na kwenda Bohari Kuu ya Dawa imebainisha matokeo ya uchunguzi wa kimaabara uliofanywa na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar umeonesha kuwa mzabuni aliwasilisha dawa aina ya PHENYTOIN SODIUM (PHENHIR) toleo nambari H18037 na METHYLDOPA (HIRDOPA-250) toleo nambari H19045 ambazo si salama kwa matumizi ya binadamu. Kwa mujibu wa barua hiyo Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar ilitoa taarifa ya kuzuwia matumizi ya dawa zilizotajwa hapo juu kufuatia malalamiko kutoka Hospitali na Vituo vya Afya kwa Unguja na Pemba na kumtaka Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa kufuata taratibu za urejeshaji wa dawa hizo pamoja na kumuambatanishia nakala ya barua kutoka kwa kampuni ya Salama Pharmaceutical yenye kumbukumbu nambari ZFDA/001/2020 ya tarehe 29 Januari 2020 inayokubali kufanya kosa la kusambaza dawa zisizo salama kwa matumizi ya binaadamu na kutamka ya kwamba “We regret the inconvenience caused and assure you that we shall make maximum amends in the future”. Kielelezo Nambari 9 Kinahusika. Kutokana na dosari iliyobainika hapo juu Kamati imesikitishwa na kitendo cha mzabuni huyo kuendelea kutumiwa kusambaza dawa na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto. Hata hivyo Kamati imepatwa na shaka juu ya uwepo wa kitengo cha Bohari Kuu ya Dawa kupokea dawa zisizokuwa salama kwa matumizi ya binaadamu na kuendelea kuzigawa katika Hospitali na Vituo mbali mbali vya Afya hali ya kuwa walithibitisha mapokezi yake na kubainisha ya kwamba dawa hizo ni salama kwa matumizi na zipo

katika hali ya ubora hadi pale wananchi walivyopaza sauti zao na hatua stahiki zikachukuliwa na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi kwa mujibu wa barua niliyoinakili hapo juu.

- Kamati katika kufanya majadiliano na msambazaji wa dawa Salama Pharmaceutical Ltd juu ya taratibu anazozipokea kutoka Wizara ya Afya za usambazaji wa dawa aliieleza kamati ya kwamba kikawaida hupokea taarifa za uagizwaji wa dawa kutoka Bohari Kuu ya Dawa na baadae dawa hizo huzikabidhisha Bohari Kuu ya dawa jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.
- Kamati imebaini uwepo wa baadhi ya taarifa kuombewa malipo mara mbili tofauti kwa ankara za aina moja kwa mujibu wa barua yenye kumbu kumbu namba WA/CMS/83/2018 ya tarehe 16 Julai 2018 iliyoombwa kufanyiwa malipo yenye thamani ya shilingi 554,320,110 ambapo ndani ya malipo hayo kuna malipo ya shilingi 365,737,525 yaliyoombewa kwa barua yenye kumbu kumbu namba WA/CMS/91/2018 ya tarehe 3 Agosti 2018, Kielelezo Nambari 10 Kinahusika.

Kutokana na taarifa hizo kamati imeshindwa kutoa ithibati juu ya uhalali wa uwepo wa dai hilo la shilingi 2,972,535,555 kwa mzabuni Salama Pharmaceutical Ltd kutokana na uwepo wa taarifa za dai zenye kukinzana na uhalisia wa dai linalobainika kwenye mfumo wa SAP Business One anaoutumia na hatimae kuilazimisha kamati ikubaliane na deni aliloliwasilisha ambapo ni kinyume na uwepo wa uhalisia wa deni aliloliripoti kwenye mfumo huo anaoutumia kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za Ankara za malipo na madai zinazohusiana na Wizara ya Afya, kubainika uwepo wa miamala ya fedha aliyolipwa ambayo imeonesha ziada ya fedha aliyolipwa kinyume na huduma aliyotoa msambazaji huyo, kubainika kwa miamala ya fedha aliyolipwa ambayo imeshindwa kuthibitika uhalali wa malipo hayo kutokana na kukosekana kwa ankara halisi zilizopelekea uwepo wa malipo hayo pamoja na kuwepo kwa miamala ya fedha iliyolipwa ambayo hati za malipo pamoja na ankara za malipo hayo kukosekana wakati wa uhakiki wa madai hayo.

Aidha Kamati imebaini uwepo wa malipo yaliyofanyika kwa mwaka 2021 ambayo ndani ya mfumo ameyathibitisha kuyapokea lakini hayakubainisha kwamba ni Ankara zipi zilizofanyiwa malipo na kupelekea kutoa taarifa ya kwamba malipo hayo yalikuwa ya mwaka 2018 ambapo Kamati haikuoneshwa katika mfumo Ankara zilizolipia malipo hayo jambo ambalo lilipelekea kutoa ripoti ya awali iliyobainisha uwepo wa ziada ya shilingi bilioni 3.8 aliyolipwa Salama Pharmaceutical Ltd awali.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Vielelezo vya malipo ya sh. 801,137,232 hayo vipo Wizarani kwa kujiridhisha (*Voucher no. V2/5 ya mwaka 2019 (116,394,600/) na Voucher no. V3/3 ya mwaka 2019 (684,742,632)*)

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati haikurudhika na majibu mepesi ya Wizara hasa ukizingatia huu ulikuwa ni ukaguzi maalum ulioombwa kufanyika na Wizara yenyewe ili iweze kujitathmini ufanisi wake. Vile vile, Kamati imebaini kwamba kulikuwepo ujanja kwa baadhi ya watendaji kutaka kutumia udhaifu uliopo ili kunufaisha nafsi zao. Kamati imegundua hilo baada ya kujiridhisha na maelezo ya Mkaguzi kwamba madeni hayo hayakuonekana katika mifumo ya Wasambazaji wakati walipoenda Dar es Salaam kufanya ukaguzi wa madeni hayo. Na kwa vile Watendaji wa Wizara walielezwa mapema (kupitia barua ya kazi za Kamati) kwamba vielelezo vyote wawe navyo wakati wa kikao na kueleza kwamba vielelezo husika vipo Wizarani halioneshi uwepo wa vielelezo hivyo na utayari wa kuviwasilisha. Sambamba na hilo, vielelezo hivyo hakupatiwa Mkaguzi wakati wa ukaguzi au ndani ya mwezi mmoja baada ya ukaguzi kukamilika kama inavyoelekeza Sheria ya Kuanzishwa Ofisi ya Mdhibiti a mwaka 2003.

Kiujumla, Kamati haikukubaliana na majibu ya Wizara na hoja inaendelea kubakia. Majibu zaidi ya hoja hii yanapatikana katika majibu ya hoja nambari Hoja nambari 1.5.4.1.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ihifadhi vizuri kumbukumbu zake na itoe mashirikiano kwa Mkaguzi.
2. Vyombo vinavyohusika na uchunguzi wa makosa mbali mbali kwa watumishi wa umma ifuatilie suala hili na ikibainika kuna watu wamechangia katika udanganyifu uliofanyika wa kuongeza au kuainisha deni la jumla ya shilingi 2,990,368,539 lililokuwa lishalipwa, sheria ichukue mkondo wake.

**Hoja nambari 1.5.5.1 Ufuatiliaji wa kurejesha vifaa vyenye thamani ya shilingi 7,500,000 kwa M&D Chemical and Surgical**

Katika ufatiliaji wa taarifa hiyo, kamati imebaini kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya ametekeleza agizo la kumuandikia Mkurugenzi wa M&D Chemical and

Surgical barua ya kurejesha vifaa vyenye thamani ya shilingi 7,500,000 kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba EC.255/477/01 ya tarehe 21 Machi, 2022, Kielelezo Nambari 11 Kinahusika.

Aidha, Mkurugenzi wa M&D Chemical and Surgical amethibitisha kupokea barua hiyo na kuwa tayari kupokea vifaa hivyo kwa mujibu wa barua MD/TZ/MOH/2022/56 ya tarehe 22 Machi 2022, Kielelezo Nambari 12 Kinahusika.

Kutokana na deni alililoliwasilisha la shilingi 125,230,000 kwa mujibu wa ankara namba 0747, 0602 na 0609 hivyo dai halisi liliopo sasa ni shilingi 117,730,000 ambalo linatokana na ankara namba 0747 yenye thamani ya shilingi 80,740,000 ya tarehe 2/6/2021 na ankara namba 0609 yenye thamani ya shilingi 36,990,000 ya tarehe 24/08/2021 baada ya kurejesha mzigo wenye thamani ya shilingi 7,500,000 kwa ankara namba 0602 ya tarehe 28/06/2021.

Kutokana na taarifa hiyo kamati imethibitisha uwepo wa dai hilo la shilingi 117,730,000 kwa mzabuni M&D Chemical and Surgical kwa mujibu wa vielelezo vilivyoonekana, hata hivyo kamati imeshindwa kuthibitisha uwepo wa deni hilo kwa kukosekana uthibitisho kutoka kwa Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba kutoa ankara za kuthibitisha na kuliombea kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya kwa hatua stahiki.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Vifaa tiba vilivyoletwa kupitia Ankara 0602 yenye thamani ya TZS 7,500,000 vilishindwa kupokelewa kutokana na kutokidhi viwango (Specification) na kurejeshwa kwa Mzabuni (Supplier), hivyo Bohari kuu haiwezi kutoa uthibitisho wa mapokezi ya vifaa hivyo.

Vifaa tiba vilivyoletwa kupitia Ankara namba 0747 yenye thamani ya TZS, 80,740,000 na 0609 yenye thamaniya TZS 36,990,000 tayari zimeshathibitishwa kwa barua. (Barua ya kuthibitisha ya tarehe 23/09/2021 kumbukumbu number WAUJWJW/CMS/122/21)

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kutokana na juhudi ambayo Wizara imechukua katika kushughulikia hoja hii, Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Wizara na haikuwa na hoja zaidi. Hata hivyo, Kamati imebaini watendaji wa Wizara hawakutoa ushirikiano mzuri kwa Mkaguzi maana hawakumpatia vielelezo hivyo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ihakikishe inakuwa na mashirikiano mazuri na Mkaguzi ili hoja kama hizi zisiweze kujitokeza.

**Hoja nambari 1.5.6: Kuthibitisha vifaa vilivyopokelewa vyenye thamani ya shilingi 791,320,000 kutoka kwa mzabuni Kat Med Group (T) Limited.**

Kwa mujibu wa dai alililoliwasilisha mzabuni Kat Med Group lenye jumla ya shilingi 1,355,007,500 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Nambari 13, kati ya dai hilo vifaa vyenye thamani ya shilingi 791,320,000 kwa mujibu wa ankra namba 0213 ya tarehe 02/07/2021 kamati imebaini kwamba vifaa tiba vilivyotolewa na kampuni ya Kat Med Group havikuthibitishwa kupokelewa kutokana na taratibu za kiufundi kutokuweza kukamilika na kushindwa kujiridhisha kwa Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa, Kielelezo Nambari 14 Kinahusika.

Hivyo, kunapelekea uwepo wa dai la shilingi 563,687,500. Hata hivyo Kamati imebaini kufanyika kwa malipo ya shilingi 100,000,000 kwa mujibu wa ankara namba 0247 ya tarehe 12 Novemba 2021 kwa ajili ya manunuzi ya MUREX kwa matumizi ya kitengo cha Damu Salama. Aidha Kamati imethibitisha kupokelewa na kurikodiwa katika kitengo cha Bohari Kuu ya Dawa ambapo haijulikani mgao wake ulivyofanyika kutokana na kitengo cha Damu Salama kutokuthibitisha usahihi wa mapokezi kwa mujibu wa kiwango cha MUREX kilivyonunuliwa kutokana na thamani ya fedha iliyotumika, ingawa imebainika mgao wa MUREX uliofanyika ulitumia ankara nambari 0236 ya tarehe 30 Agosti 2021 na sio ankara nambari 0247 ya tarehe 12 Novemba 2021 kwa mujibu wa malipo ya fedha yalivyofanyika.

Kutokana na malipo ya shilingi 100,000,000 yaliyofanyika kumepelekea kushindwa kujiridhisha kutokana na malipo hayo kuwa yanapunguza dai lililowasilishwa na mzabuni au ni malipo mapya ambayo hayahusiani na dai la awali. Kutokana na taarifa hiyo kamati imeshindwa kuthibitisha uwepo wa deni hilo kwa kukosekana uthibitisho kutoka kwa Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba kutoa ankara za kuthibitisha kiasi halisi cha deni kinachodaiwa na mzabuni huyo kutokana na kushindwa kuthibithisha na kuliombea kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya kwa hatua stahiki.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

1. Vifaa tiba vilivyopokelewa venye thamani ya TZS 791,320,000 kupitia Ankara 0213 tayari vimeshathibitishwa baada ya ripoti ya makubaliano ya uongozi wa Hospitali ya kivunge kupitia Biomedical engineer, na msambazaji

2. Madai yenye thamani ya TZS 563,687,500 ni mjumuisho wa Ankara tofauti za uletaji vifaa tiba kutoka Kampuni ya Kat med ambazo nyengine tayari zimeshathibishwa
3. Mzabuni hakuandika barua ya kuomba kulipwa fedha za Vifaa tiba vilivyopokelewa venye thamani ya TZS 100,000,000 kupitia Ankara 0247, hivyo Bohari haikuweza kuthitisha dai hilo.

(***Kumbukumbu nabari; WA/CMS/124/2022/23 ya tarehe 02/05/2023***)

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ilitaka kujua dai la milioni 100,000,000 lililolipwa bila kuwa na vielelezo lilitokea wapi na kubaini kwamba Msambazaji alipatiwa malipo ya shilingi 100,000,000 kabla ya kupokelewa, jambo ambalo ni kwenda kinyume na utaratibu wa malipo ya fedha za Serikali. Kwa mnasaba huo, Watendaji wa Wizara walifanya uzembe mkubwa uliosababisha kuitia Serikali hasara.

Kamati imegundua kwamba kwenye Hadudi rejea namba 4, Kamati haikupatiwa vielelezo vianvyothibitisha uklali wa matumizi hayo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ihakikishe inafuata taratibu za fedha kama inavyoelekezwa na Sheria na kanunui zake ili kuepusha kasoro zilizojitokeza.
2. Watendaji waliohusika na uzembe katika utekelezaji wa majukumu yao, vyombo vya uchunguzi viwachukulie hatua za kinidhamu.

**Hoja nambari 1.5.7.1: Kuchelewa kuchukuliwa hatua za urejeshwaji wa vifaa vyenye thamani ya shilingi 791,320,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wizara ya Afya ilifunga mkataba wenye kumbukumbu namba SMZ/H01/G/NCB/2020/2021/05 wa tarehe 1 Januari 2020 kwa ajili ya kusambaza vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali ya Kivunge (Lot 1) wenye thamani ya shilingi 1,003,620,000.

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba AB/42/333/243 ya tarehe 25 Machi 2022 ilibainisha vifaa hivyo viliwasilishwa na kupokelewa Bohari kuu ya dawa siku ya tarehe 2 Julai 2021 hata hivyo ilibainika baadhi ya vifaa vilipokelewa na kukubalika na baadhi kutokukubaliwa kutokana na kutokukidhi kwa vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa zabuni. Ukaguzi umebaini vifaa vyenye thamani ya shilingi 212,300,000 ndivyo vilivyokubalika na kupokelewa kwa mujibu wa zabuni iliyotolewa na kupelekea uwepo wa vifaa

vyenye thamani ya shilingi 791,320,000 ambavyo havikukidhi vigezo na masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa zabuni iliyotolewa na kutakiwa vifaa hivyo kurejeshewa mzabuni huyo.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni ucheleweshwaji wa kuchukua maamuzi ya kufanya urejeshwaji wa vifaa hivyo kwa mzabuni jambao ambalo limepelekea vifaa hivyokuhifadhiwa katika ghala la Hospitali ya kivunge kwa zaidi ya mwaka mmoja bila ya kutolewa kwa maamuzi yeyote.

Aidha mnamo tarehe 18 Machi 2022 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilimshauri Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa kutekeleza maagizo yaliyotolewa katika kikao cha pamoja na Makamo wa Pili wa rais Mheshmiwa Hemed Suleiman Abdulla pamoja na Mzabuni Kat Med Group (T) Ltd chenye lengo la kumtaka Mkurugenzi wa Bohari kuchukua hatua ya haraka ya kumuandikia Katibu Mkuu Wizara ya Afya barua ya kuthibitisha kutokuwa na ubora uliotakiwa wa vifaa hivyo ili hatua za haraka za kukabidhiwa Mzabuni huyo zichukuliwe.

Hata hivyo, hadi Mzabuni anaandika barua niliyoinakili hapo juu pamoja na kupitiwa kwa zaidi ya mwaka bila ya kukabidhiwa Mzabuni huyo maamuzi ya kuvirejesha vifaa hivyo bado hayajaweza kuchukuliwa jambo ambalo linaweza kupelekea kuitia hasara Serikali kwa kuendelea kushikilia vifaa ambavyo havihitajiki kwa ajili ya matumizi na kuingia gharama za utunzaji wa vifaa hivyo.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unatekeleza maagizo yanayotolewa na Viongozi Wakuu kwa lengo la kuepusha kuja kujitokeza kuitia hasara Serikali kutokana na uwepo wa vitendo vya urasimu na uzembe wa kuchelewa kufanya maamuzi kwa wakati. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama unavyoonekana katika Jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 7: Vifaa vilivyochelewa kurejeshwa kwa Msambazaji**

| Namba | Aina ya Kifaa | Idadi ya Vifaa |
|---|---|---|
| 1. | Incubator | 3 |
| 2. | Anesthesia machine WATO 65 | 1 |
| 3. | Suction Machine | 3 |
| 4. | Nebulizer | 1 |

**Hoja nambari 1.5.7.1: MZABUNI KAS MEDICS LTD**

Mzabuni KAS MEDICS LTD aliwasilisha dai lenye jumla ya shilingi 82,266,480 linalotokana na Ankara nambari 1072 ya tarehe 02/07/2018 yenye thamani ya shilingi 24,426,480, Ankara nambari 597 ya tarehe 12/03/2021 yenye

thamani ya shilingi 57,710,000 pamoja na Ankara nambari 610 ya tarehe 16/03/2021 yenye thamani ya shilingi 130,000 ambapo kamati imethibitisha uwepo wa dai hilo kwa mzabuni.

Kutokana na taarifa hiyo kamati imethibitisha uwepo wa dai hilo la shilingi 82,266,480 kwa mzabuni KAS MEDICS LTD kwa mujibu wa vielelezo vilivyoonekana, hata hivyo kamati imeshindwa kuthibitisha uwepo wa dai hilo kwa kukosekana uthibitisho kutoka kwa Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba kushindwa kuthibitisha ankara za madai hayo na kuziombea malipo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya kwa hatua stahiki.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Bohari Kuu ya Dawa tayari imeshaandika barua ya uthibitisho wa mapokezi wa vitendanishi zenye thamani ya TZS 57,710,000 kupitia Ankara namba 597 kutoka kwa kampuni ya Kas Medics LTD. Aidha, Bohari kuu haijapokea vitendanishi zinazodaiwa na kampuni ya Kas Medics kupitia Ankara 610. (***Barua ya Bohari yenye kumbukumbu ya namba WAUJWJW/CMS/98/21 ya tarehe 20/7/2021***)

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kutokana na kukosekana kwa uthibitisho wa barua kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Bohari, Kamati ilitaka kujua utaratibu wa kupokea na kuthibitisha dawa wanazohidha katika maeneo yao na kuelezwa kwamba dawa zinapopelekwa Bohsri kuu, watendaji huwa wanazipokea kwa kuzithibitisha kama ndio dawa zilizomo kwenye orodha ya dawa zinazotakiwa kuletwa zimo katika muda wa matumizi unaotakiwa au laa, baada ya kujiridhisha ndio hutoa barua ya vifaa au dawa halisi walizozipokea. Hivyo hutokezea baadhi ya wakati dawa au vifaa kupokelewa Bohari kuu lakini zisithibitishwe na huambiwa muhusika kuja kuvichukua vifaa vyake vilivyokuwa havijakidhi vigezo.

Kamati imebaini tofauti ya maelezo imejitokeza katika mazingira hayo na kupelekea kutolewa ankara za malipo zilizokuwa hazitambuliwi au hazijathibitishwa na Mkurugenzi wa Bohari Kuu. Hili linmeonekana na Kamati kwamba hujitokeza kutokana na kutokuwepo kwa mfumo au mawasilisano ya karibu baina ya Wizara na watendaji wa Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Watedaji wa Wizara na Bohari Kuu ya Madawa wafanye kazi kwa mashirikiano ya karibu ili kuepusha kujitokeza madeni yasiyothibitishwa.
2. Wizara ihakikishe inaweka mfumo maalum utakaokuwa unaziunganisha Taasisi hizo ili kurahisisha utoaji huduma na kuepusha malalamiko kutoka kwa Wazabuni.

**Hoja nambari 1.5.7.2: Mzabuni Bahari Pharmacy Ltd**

Mzabuni Bahari Pharmacy Ltd aliwasilisha deni lenye jumla ya shilingi 159,575,000 linalotokana na Ankara nambari 6685 ya tarehe 10/06/2021 yenye thamani ya shilingi 16,932,000, Ankara nambari 8061 ya tarehe 20/07/2021 yenye thamani ya shilingi 17,000,000, Ankara nambari 2046805 ya tarehe 16/08/2021 yenye thamani ya shilingi 31,960,000 pamoja na Ankara nambari 2046905 ya tarehe 01/09/2021 yenye thamani ya shilingi 52,683,000 pamoja na Ankara nambari OOS092101 ya tarehe 17/09/2021 yenye thamani ya shilingi 41,000,000.

Kamati imebaini kati ya deni la shilingi 159,575,000 Wizara ya Afya imefanya malipo yenye thamani ya shilingi 118,575,000 na kupelekea uwepo wa dai la shilingi 41,000,000 ambalo halikuthibitishwa uwepo wake na Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba kutokana na bidhaa hizo kutokupokelewa na kukosekana kumbu kumbu za mapokezi yake katika Bohari Kuu ya Dawa, hata hivyo katika kufuatilia na kutaka kujiridhisha Kamati ilifanya kikao cha pamoja na Kampuni ya Bahari Pharmacy tarehe 24 Machi 2022 katika Ofisi yake iliyopo Dar - es - Salaam ambapo Afisa masoko aliileza Kamati kwamba bidhaa hizo ziliwasilishwa Kitengo cha Damu Salama jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa mapokezi ya Dawa na Vifaa Tiba na kupelekea kukosekana kwa kurikodiwa katika Mfumo wa dawa na Vifaa Tiba uliopo Bohari Kuu ya Dawa na hatimae kukosekana kwa taarifa za mapokezi yake.

Aidha, Kamati imebaini mapungufu ya kiutendaji yaliyopelekea ukiukwaji wa Sheria nambari 11 ya ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 ambapo mapungufu hayo yalipelekea mzabuni kusambaza dawa kwa kutumia Local Puchase Order (LPO) yenye nambari 35876 ya tarehe 27 Juni 2021 kwa dawa zenye thamani ya shilingi 118,575,000 pamoja na LPO yenye nambari 46910 ya tarehe 3 Septemba 2021 yenye thamani ya shilingi 41,000,000 ambapo taratibu za manunuzi zinaelekeza kufanyike kwa zabuni ya wazi kwa lengo la kuwepo kwa ushindani wa bei kwa wazabuni.

Kutokana na taarifa hiyo pamoja na uwepo wa dai la shilingi 41,000,000 Kamati imeshindwa kuthibitisha uwepo wa dai hilo kwa kukosekana uthibitisho kutoka kwa Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba

kushindwa kuthibitisha ankara za madai hayo na kuziombea malipo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya kwa hatua stahiki.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Bohari kuu ya Dawa tayari imeshathibitisha mapokezo ya vifaa yenye thamani ya sh. 118,575,000/ kupitia ankara 6685, 8061 na 20469OS. Hata hivyo vifaa vyenye thamani ya sh 41,000,000/- ambavyo Mkaguzi amezitaja havijapokelewa Bohari. (*WAUWJWW/CMS/123/21 ya tarehe 23.09.2021*)

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile Wizara imekiri kwamba vielelezo vya shilingi milioni 41,000,000 havijathibitishwa na Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba kutokana na kukiuka taratibu za manunuzi na kwa vile hakuna malipo yaliyofanyika, Kamati haikuwa na maelezo zaidi isipokuwa imewasisitiza Watendaji wa Wizara na Bohari Kuu kuwa makini na matumizi ya fedha za Serikali kwa kufanya matumizi kama zinavyoelekeza Sheria za Manunuzi na Fedha.

**Hoja nambari 1.5.7.3: Mzabuni Anudha Ltd.**

Mzabuni Anudha Ltd. aliwasilisha deni lenye jumla ya shilingi 49,923,000 linalotokana na ankara nambari 74903 ya tarehe 08/05/2020 yenye thamani ya shilingi 4,255,000, ankara nambari 75358 ya tarehe 05/06/2020 yenye thamani ya shilingi 9,078,000, ankara nambari 76911 ya tarehe 03/09/2020 yenye thamani ya shilingi 2,250,000, ankara nambari 78352 ya tarehe 24/11/2020 yenye thamani ya shilingi 8,525,000, ankara nambari 78408 ya tarehe 24/11/2020 yenye thamani ya shilingi 3,150,000, ankara nambari 81752 ya tarehe 26/05/2021 yenye thamani ya shilingi 8,965,000, ankara nambari 81862 ya tarehe 31/05/2021 yenye thamani ya shilingi 3,750,000, pamoja na Ankara nambari 84064 ya tarehe 16/09/2021 yenye thamani ya shilingi 9,950,000.

Kutokana na taarifa hiyo pamoja na uwepo wa dai la shilingi 49,923,000 Kamati imeshindwa kuthibitisha uwepo wa dai hilo kwa kukosekana uthibitisho kutoka kwa Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba kushindwa kuthibitisha ankara za madai hayo na kuziombea malipo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya kwa hatua stahiki.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Bohari kuu ya Dawa huthibitisha huandika barua ya uthibitisho pale inapopata barua ya maombi ya fedha kutoka kwa Kampuni husika ambayo

inayohitaji uthibitisho wa mapokezi. Hivyo kuhusu Kampuni ya Anudha LTD. Bohari haijapokea barua inayohitaji uthibitisho wa mapokezi ya dawa au vifaa tiba kutoka Anudha LTD.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile hakuna uthibitisho wowote wa maombi ya barua yaliyowasilishwa Bohari Kuu ambapo na Kamati ya PAC haikupatiwa uthibitisho huo, na kwa vile hakuna fedha yoyote iliyolipwa au kupotea. Kamati inaungana na Mkaguzi kwamba malipo ya maombi hayo hayana mashiko kulipwa.

**Hoja nambari 1.5.7.4: Mzabuni Life Care Pharmacy**

Mzabuni Life Care Pharmacy aliwasilisha deni lenye jumla ya shilingi 32,240,000 linalotokana na ankara nambari 0028 ya tarehe 18/06/2021 yenye thamani ya shilingi 14,700,000, ankara nambari 0115 ya tarehe 15/08/2021 yenye thamani ya shilingi 13,530,000, ankara nambari 0039 ya tarehe 03/09/2021 yenye thamani ya shilingi 510,000 , pamoja na ankara nambari 0043 ya tarehe 19/09/2021 yenye thamani ya shilingi 3,500,000.

Kutokana na taarifa hiyo pamoja na uwepo wa dai la shilingi 32,240,000 Kamati imeshindwa kuthibitisha uwepo wa dai hilo kwa kukosekana uthibitisho kutoka kwa Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba kushindwa kuthibitisha ankara za madai hayo na kuziombea malipo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya kwa hatua stahiki.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Bohari Kuu ya Dawa haikuweza kuthibitisha mapokezi ya dawa kutoka Life Care Pharmacy kwa sababu kwamba baada ya mapokezi ya dawa na Vifaa tiba kutoka life care Pharmacy ankara halisi (Original Invoice) zilichukuliwa na Kitengo cha Ununuzi kwa ajili ya kufanyiwa malipo hivyo Bohari haikuweza kuthibitisha mapokezi hayo kupitia copy ya ankara kwa kuchelewa kufanyika malipo mara mbili.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile uthibitisho wa vielelezo vilivyowasilishwa vilikuwa nakala (copies) na Kamati ya PAC haikupatiwa uthibitisho halisi (original), na kwa vile hakuna fedha yoyote iliyolipwa au kupotea. Kamati inaungana na Mkaguzi kwamba malipo ya maombi hayo hayana mashiko kulipwa.

**Hoja nambari 1.5.7.5: Mzabuni Nebula Health Care Ltd.**

Mzabuni Nebula Health Care Ltd. aliwasilisha dai lenye jumla ya shilingi 124,897,650 linalotokana na ankara za malipo kama inavyoonekana katika Kielelezo Nambari 15.

Kati ya ankara hizo, jumla ya shilingi 34,062,000 ni dai linalotokana na ankara nambari 0642 ya tarehe 10/04/2021 yenye thamani ya shilingi 33,300,000 na ankara nambari 0127 ya tarehe 05/07/2021 yenye jumla ya shilingi 762,000 ambazo hazikuthibitishwa kupokelewa na Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba.

Aidha, Kamati ilibaini ankara nambari 0128 ya tarehe 05/07/2021 yenye thamani ya shilingi 4,400,000 haikuwa sahihi taarifa ya fedha iliyoainishwa na badala yake ilisomeka shilingi 762,800 hivyo kupekelea dai la mzabuni huyo kuwa na jumla ya shilingi 121,260,450.

Kutokana na taarifa ya uwepo wa dai la shilingi 121,260,450 kwa Mzabuni Nebula Health Care Ltd. Kamati imeshindwa kuthibitisha uhalali wa uwepo wa deni hilo kutokana na kikao kilichofanyika tarehe 29 Machi 2022 baina ya kamati na Nebulla Health Care na kumtaka awasilishe vielelezo vya madai yake ikiwemo taarifa za kibenki, ankara zote alizolipwa, pamoja na uthibitisho wa mikataba yake kwa vile ukaguzi wa awali ulibaini Nebulla Health Care alilipwa ziada ya malipo ya shilingi 727,427,350 kwa ajili ya kujiridhisha usahihi wa ziada ya malipo hayo kwa mujibu wa miamala ya fedha itayobainika katika taarifa zake za kibenki. Hata hivyo, hadi uhakiki unakamilika Nebulla Health Care ameshindwa kuiwasilishia kamati vielelezo alivyotakiwa kuwasilisha.

Aidha, imebainika Ankara nambari 0642 ya tarehe 10/04/2021 yenye thamani ya shilingi 33,300,000 hazikuweza kuthibitishwa mapokezi ya vitendanishi vilivyotumika kwa upimaji wa UVIKO - 19 vilivyowasilishwa na Mzabuni huyo kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu nambari WA/CMS/30/22 ya tarehe 30 Machi 2022 kutoka kwa Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa kwa mujibu wa Kielelezo Nambari 16.

Kutokana na taarifa hiyo pamoja na kushindwa kuwasilisha vielelezo husika mbele ya Kamati na kukosekana uthibitisho kutoka kwa Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba kushindwa kuthibitisha ankara za madai hayo na kuziombea malipo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya kwa hatua stahiki, Kamati haikuweza kujiridhisha kuhusiana na uwepo wa madai husika.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Bohari kuu ya Dawa imepokea vifaa tiba kutoka kwa Mzabuni. Hata hivyo, haijafanya uthibitisho kwa sababu Mzabuni hajawasilisha maombi ya malipo ya vifaa hivyo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuna uhujumu wa fedha za Serikali ambazo hazijathibitishwa matumizi yake. Lakushangaza zaidi Mzabuni ameelekezwa na Mkaguzi kuwasilisha taarifa zake za kibenki zinazohusiana na malipo yaliofanyika lakini ameshindwa kutekeleza hili ya kwamba kuna jumla ya malipo ya ziada ya shilingi shilingi 727,427,350 alizolipwa ambayo fedha za Serikali. Hivyo, kuna haja kwa suala hilo kufuatiliwa kwa karibu ili kuweza kubainika fedha halali ni ipi na isiyohalali ni ipi.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Vyombo vinavyohusika na uchunguzi wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali kuchukua hatua za makusudi kulifuatilia suala hili ili kutambua fedha ya Serikali iliyopotea na wahusika kuchukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria za Zanzibar.
2. Wizara ihakikishe haifanyi malipo ya aina yoyote ambayo yametiliwa mashaka na Mkaguzi pasi na Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kujiridhisha na malipo hayo kwa kutoa idhini ya kulipwa fedha za dai husika.

**Hoja nambari 1.5.7.6: Mzabuni Indepth Scientific**

Mzabuni Indepth Scientific aliwasilisha dai lenye jumla ya shilingi 21,027,200 kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba ISL/SVPZ/VOL.001/2022 ya tarehe 7 Februari 2022 ambapo kati ya dai hilo shilingi 13,250,000 kwa ajili ya ununuzi wa VTMS na shilingi 7,777,200 kwa ajili ya ununuzi wa GLOVES.

Katika ufuatiliaji wa uhakiki wa deni hilo kamati ilifanya kikao cha awali kilichoitishwa na Makamo wa Pili wa Rais, Ofisini kwake Vuga tarehe 18 Machi, 2022 na kumtaka Mzabuni huyo kutoa taarifa za uhalali wa dai lake ikiwemo kuwasilisha taarifa za kiasi anachokidai Serikali, Mzabuni alieleza kwenye kikao kwamba hakujiandaa na taarifa alizoulizwa hivyo apewe muda kwa ajili ya kuwasiliana na watendaji kuhusiana na upatikanaji wa taarifa hizo. Pamoja na kupatiwa muda aliouomba Mzabuni alishindwa kuthibitisha dai halisi analoidai Serikali.

Mwenyekiti wa kikao hicho ambae ni Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alitoa agizo la kukaa na Mzabuni ili kuweza kujiridhisha kiasi halisi cha fedha anachoidai Serikali. Aidha kamati ilifanya jitihada za kuwasiliana nae na kutaka kukutana nae katika kikao cha pamoja bila ya mafanikio. Hata hivyo, kamati ilifanya jitihada za kuwasiliana na Wazabuni wenzake katika kupatiwa msaada kwa lengo la kufahamu Ofisi zake zilipo, na kufanikiwa kufika katika Ofisi yake iliyopo maeneo ya Chukwani lakini kamati haikufanikiwa kukutana na Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo na kufanya mawasiliano kwa njia ya simu na

kumtaka kutuwasilishia taarifa za uwepo wa dai lake kwa vile ukaguzi wa awali ulibaini malipo ya ziada aliyolipwa yenye jumla ya shilingi 115,702,746.

Hadi tunakamilisha taratibu za uandishi wa ripoti kamati haikupata taarifa za kibenki za miamala ya kifedha (bank statements), mkataba tangu alipoanza biashara na Wizara ya Afya pamoja na ankara zilizofanyiwa malipo ili kuweza kujiridhisha juu ya uhalali wa uwepo wa dai linalodaiwa. Hata hivyo, Mzabuni huyo hakuweza kujitokeza kukutana na kamati pamoja na jitihada zilizochukuliwa za kumtaka kukutana nae katika kikao cha pamoja ili kuweza kujiridhisha juu ya uwepo wa deni alililoliwasilisha la kuidai Serikali.

Kutokana na taarifa hiyo pamoja na kushindwa kuwasilisha vielelezo husika mbele ya Kamati na kukosekana uthibitisho kutoka kwa Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa na Vifaa Tiba kushindwa kuthibitisha ankara za madai hayo na kuziombea malipo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya kwa hatua stahiki, Kamati haikuweza kujiridhisha kuhusiana na uwepo wa madai husika.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Bohari imethibitisha mapokezi ya vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi 7,772,000 kupitia ankara namba 075, ankara namba 144 haijathibitishwa kwa sababu haijawasilisha maombi. Barua ya Bohari kumbukumbu namba WAUJWJW/CMS/94/21 ya tarehe 20/07/2021

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imegundua kwamba kuna ubabaishaji wa deni linalodaiwa. Hii inatokana na ukosefu wa vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa malipo hayo. Kwa msingi huo, Wizara inatakiwa kuwa makini kabla ya kufikia maamuzi ya kulipa madeni ya namna hii.

Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Vyombo vinavyohusika na uchunguzi wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali kuchukua hatua za makusudi kulifuatilia suala hili ili kutambua fedha halali ya Serikali inatakiwa kulipwa na kama kuna malipo ya ziada yaliyofanywa Kampuni ifanye utaratibu wa kuzirudisha fedha hizo.
2. Wizara ihakikishe haifanyi malipo ya aina yoyote ambayo yametiliwa mashaka na Mkaguzi pasi na Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kujiridhisha na malipo hayo kwa kutoa idhini ya kulipwa fedha za dai husika.

### 1.5.8 HADIDU REJEA NAMBA 5

**Kuhakiki mahitaji ya dawa "Quantification of drugs" kwa mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai 2018 hadi Juni 2021.**

Katika Hadidu rejea hii yamebainika mambo yafuatayo:-

**Hoja nambari 1.5.8.1: Maoteo (Quantification) ya Bajeti na Mahitaji ya Dawa**

Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kupitia Mfamasia Mkuu wa Dawa imeendelea na kuandaa mahitaji ya dawa na vifaa tiba kwa mujibu wa maagizo na taratibu zilizopo kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai 2018 hadi Juni 2021.

Ukaguzi umebaini uandaaji wa mahitaji ya dawa na vifaa tiba hushirikishwa wadau wote wa Wizara wakiwemo Hospitali za Rufaa pamoja na vituo vya afya mbali mbali Unguja na Pemba ambapo bajeti ya fedha za dawa na vifaa tiba huhusisha fedha za Serikali kuu pamoja na Washirika wa Maendeleo.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha Julai 2018 hadi Juni 2021, Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto ilikuwa na mahitaji ya dawa na vifaa tiba kwa mujibu wa maoteo ni kama ifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 8: Maoteo ya Bajeti na Mahitaji ya dawa**

| **Nam.** | **Mwaka wa fedha** | **Bajeti**<br>**A**<br>**(Shs "000")** | **Fedha kutoka SMZ**<br>**B**<br>**(Shs "000")** | **Fedha kutoka Washirika wa Maendeleo**<br>**C**<br>**(Shs "000")** | **Jumla ya Fedha**<br>**B+C (Shs "000")** | **Tofauti ya Fedha**<br>**A - (B+C)**<br>**(Shs "000")** | **Asilimia Pungufu (%)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 2018/2019 | 12,700,000 | 10,350,000 | 1,000,000 | 11,350,000 | 1,350,000 | 11 |
| 2. | 2019/2020 | 15,760,000 | 13,400,000 | 1,030,615 | 14,430,615 | 1,329,385 | 8 |
| 3. | 2020/2021 | 17,000,000 | 8,400,000 | 664,131 | 9,064,131 | 7,935,869 | 47 |
| **Jumla Kuu** | | **45,460,000** | **32,150,000** | **2,694,746** | **34,844,746** | **10,615,254** | |

Kutokana na Jadweli hapo juu imebainika kwamba maoteo ya ununuzi wa dawa yanaongezeka mwaka hadi mwaka, kwa mwaka 2019/2020 kumekuwa na ongezeko la shilingi Bilioni 3.06 ukilinganisha na mwaka 2018/2019. Aidha kwa mwaka 2020/2021 maoteo ya ununuzi wa dawa yameonekana kuongezeka kwa shilingi Bilioni 2.76 ukilinganisha na mwaka 2019/2020.

Pamoja na kuongezeka kwa maoteo ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba imebainika upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mahitaji ya ununuzi wa dawa umeshuka kwa asilimia 47 kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Hii inatokana na upatikanaji wa fedha kutoka Wizara ya Fedha kutofautiana na mahitaji halisi ya maoteo yanayofanywa. Maoteo ya dawa kwa mwaka 2018/2019 Shilingi 17,687,970,901/- na 2020/2021 Shilingi 61,192,512,907/-.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imegundua kuwa ni kweli kuna ongezeko kubwa la watoto na wanaozaliwa ambalo halilingani na uhalisia wa upatikanaji wa bajeti ya Wizara inayopangwa na kuingizwa. Hata hivyo, Wizara inatakiwa kufanya utafiti ili iweze kubaini wastani wa ongezeko la maoteo kwa kipindi cha miaka mitatu au mitano. Kufanya hivyo kutaisaidia Wizara kujua mahitaji kamili ya bajeti wanayohitaji.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iongeze bajeti ili iendane na ongezeko la watu nchini.

**Hoja nambari 1.5.8.2: MSD kutokuwa na uwezo wa usambazaji Dawa na Vifaa Tiba**

Katika kipindi cha miaka mitatu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kupitia Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar iliingia mikataba ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba ili kuweza kurahisisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo mbali mbali vya Afya Unguja na Pemba. Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto ilifanya makubaliano (MoU) ya kusambaziwa dawa na vifaa tiba kwa vipindi mbali mbali kutoka kwa MSD, ukaguzi umebaini kwamba taasisi hiyo inayojishughulisha na usambazaji wa dawa na vifaa tiba haina uwezo wa kuisambazia dawa na vifaa tiba kwa asilimia mia moja (100%) Kiambatisho 4(A) kinahusika.

Aidha Wizara ilifanya jitihada za upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa wasambazaji mbali mbali wa ndani na nje ya nchi ili kuweza kuondoa uhaba wa upatikanaji wa dawa.

Ukaguzi umebaini kutokana na kuwatumia wasambazaji hao kumepelekea kuongezeka kwa gharama za ununuzi wa dawa na vifaa tiba ukilinganisha na

gharama zinazotozwa na MSD jambo ambalo ni ukiukwaji wa maagizo ya Baraza la Mapinduzi kupitia kikao cha tarehe 16/07/2020 Kiambatisho Nambari 4(B) kinahusika.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Agizo la Baraza la Mapinduzi ni kuwa Wizara inunue dawa kwa MSD na si kwa Wazabuni wengine, pia makubaliano ya usambazaji dawa baina ya Wizara na MSD yalitiwa saini.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilitaka kujua kwamba hivi sasa Wizara inasambaziwa dawa na vifaa tiba na MSD lakini wanaweza kununua kwa wasambazaji dawa wakubwa na sio wadogo wadogo. Kadhalika, Kamati ilihoji kwamba lile agizo la Baraza la Mapinduzi limefutwa hata Wizara iwe inasambaziwa dawa na vifaa tiba na MSD wakati ilibainika ilikuwa na majukumu mengi ya kusambaza dawa na vifaa tiba katika Wilaya za Tanzania Bara.

Aidha, iligundulika MSD walikuwa wakinunua dawa na vifaa tiba vyengine kwenye Kampuni nyengine kwa vile walikuwa wakinunua dawa hizo kwa Serikali yote.hivi sasa kumetoka agizo jengine (Baraza la Mapinduzi) kwamba dawa na vifaa tiba ziendelee kununuliwa na MSD na Kampuni nyengine kubwa lakini Kamati ilipotaka uthibitisho wa barua hiyo haikuweza kupatikana. Hivyo, Kamati imeagiza kupatiwa kielelezo hicho.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ichukue juhudi kuhakikisha Sheria ya Bohari Kuu inafanyiwa marekebisho ili iruhusu na kuipa uwezo Bohari Kuu kuweza kusambaza dwa navifaa tiba nchini. Kufanya hivyo, kutapunguza kwa kiasi kikubwa uwezekano wa kuletewa dawa zilizohitajika au zilizopitwa na wakati.
2. Wizara ihakikishe inatekeleza majukumu yake kwa kufuata maagizo yanayotolewa na Serikali.

**Hoja nambari 1.5.8.3: Upungufu wa Baadhi ya Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi katika Bohari Kuu ya Dawa - Zanzibar**

Katika uhakiki wa mahitaji ya dawa na vifaa tiba ukaguzi umebaini uwepo kwa upungufu wa baadhi ya dawa na vifaa tiba pamoja na vitendanishi katika Bohari Kuu ya Dawa kwa kipindi cha mwaka 2019/2020 na 2020/2021. Upungufu huo umetokana na uwepo wa deni kubwa la fedha linalodaiwa na Wasambazaji ambalo linaathiri makubaliano ya mkataba uliofungwa baina ya Wizara ya Afya na Wasambazaji.

Baadhi ya taarifa za upungufu wa dawa zilizobainika kwa baadhi ya hospitali na vituo vya afya ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 9: Taarifa za upungufu wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi**

| Namba | UNGUJA | PEMBA |
|---|---|---|
| 1. | Hospitali ya Mnazi Mmoja | Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani |
| 2. | Hospitali ya Makunduchi | Hospitali ya Chake Chake |
| 3. | Hospitali ya Kivunge | Hospitali ya Wete |
| 4. | Hospitali ya Kidongo Chekundu | Hospitali ya Micheweni |
| 5. | Kituo cha Afya Magogoni | Hospitali ya Vitongoji |
| 6. | Kituo cha Afya Mpendae | - |

Aidha kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu nambari WAUJWJW/CMS/118/21 ya tarehe 10/09/2021 ilibainisha uwepo wa upungufu mkubwa wa dawa katika Bohari Kuu ya Dawa ambapo kwa mujubu wa maombi ya dawa na vifaa tiba ya robo mwaka ya Julai - Septemba yenye thamani ya shilingi Bilioni Nne hadi kufikia tarehe 10/09/2021. Wizara imepokea vifaa vyenye thamani ya shilingi Milioni Mia Nne sawa na asilimia 10 ya mahitaji jambo ambalo limepelekea kufanyika kwa maombi ya dharura juu ya upatikanaji wa dawa hizo ili kuweza kuepusha maafa ambayo yanaweza kutokezea kwa kukosekana kwa baadhi ya dawa muhimu katika vituo vya afya na kupelekea Bohari Kuu kutokuwa na uwezo wa kusambaza dawa kwa mujibu wa mahitaji halisi kutoka katika vituo vya afya. Hali halisi ya mahitaji ya dharura yaliyofanyika ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho Nambari 5.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Hii inatokana na bajeti ndogo ikilinganishwa na fedha halisi inayopatikana.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba ni kweli Wizara inakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na bajeti ya kutosha. Hata hivyo, Wizara ijitahidi kulipa madeni yaliyopo ili iweze kuwapa hamasa wasambazaji wa huduma hiyo.

### 1.5.9 HADIDU REJEA NAMBA 6

**Kuhakiki usahihi wa bei za dawa "Actual Price" kutokana na bei za sokoni "Market price".**

Katika Hadidu Rejea hii mambo yafuatayo yamebainika:-

Ukaguzi umebaini uwepo na utofauti wa bei za dawa na vifaa tiba katika soko la ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa Kampuni tofauti zinazotoa huduma za usambazaji katika Wizara ya Afya,Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.

Hata hivyo, ukaguzi umeangalia baadhi ya dawa na vifaa tiba kupitia kwa wasambazaji mbali mbali na kubaini kuwepo kwa tofauti kubwa ya bei kwa baadhi ya dawa na vifaa tiba zinazosambazwa na wasambazaji hao kupitia Bohari Kuu ya dawa ukilinganisha na uhalisia wa upatikanaji wa dawa hizo sokoni. Jadweli lifuatalo linaonesha orodha ya dawa na vifaa tiba kwa baadhi ya maduka ya madawa na tofauti ya bei kwa mujibu wa soko.

**Jadweli Nambari 10: Tofauti wa bei za dawa na vifaa tiba katika soko la ununuzi wa dawa na vifaa tiba**

| Na. | Aina ya dawa | Bei kwa mujibu wa Soko | | Bei kwa mujibu wa Wasambazaji | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Mwembeladu Pharmacy | Unguja Pharmacy | MSD | Salama Pharmaceutical LTD |
| | | Bei ya dawa (Tshs) | Bei ya dawa (Tshs) | Bei ya dawa (Tshs) | Bei ya dawa (Tshs) |
| 1. | Acetazolamide 250mg tabs (pack of 100) | 18,000 | 18,550 | 22,987 | 14,406 |
| 2. | Acetylsalicylic acid 75mg tabs (pack of 100) | 8,500 | 8,000 | 3,867 | 8,440.74 |
| 3. | Amoxiclav powder for injection(vial) | 8,550 | 8,000 | 7,115 | 5,955.00 |
| 4. | Amoxicillin 250mg caps (pack of 100) | 5,000 | 4,000 | 3,214 | 6,000.00 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 5. | Amoxicillin 500mg inj. (vial) | 1,550 | 1,825 | 2,752 | 900.00 |
| 6. | Ampiclox 500mg inj. (pack of 100) | 2,000 | 1,800 | 1,985 | 9,277.54 |
| 7. | Anti-toxictetanus 1,500 iu/ ml-iml (ATs) inj.Ampoule | 3,800 | 4,150 | 4,413 | 4,850.00 |
| 8. | Captopril 25mg tabs | 7,625 | 7,725 | 5,442 | 9,015.00 |
| 9. | Carbinazole 5mg tabs | 18,000 | 19,500 | 14,000 | 18,464.10 |
| 10. | Hyoscine- N-butylbromide 10mg tabs | 22,500 | 21,600 | 20,500 | 33,607.60 |
| 11. | Tranexamic acid 100mg inj. 5ml | 160,550 | 166,350 | 143,500 | 210,000.00 |
| 12. | Tranexamic acid 500mg tabs (pack of 100) | 30,000 | 29,550 | 27,850 | 32500.00 |
| 13. | Haloperidol 1.5mg tabs (pack of 100) | 10,000 | 11,250 | 15,000 | 17,000.00 |
| 14. | Metronidazole 200mg tabs | 2,0150 | 2,155 | 1,267 | 1,250 |
| 15 | Misoprostol 200mg tabs (pack of 100) | 3,500 | 3,755 | 3,740 | 2,315 |
| 16. | Syringe disposable with needle, 5cc (pack of 100) | 9,550 | 10,500 | 8,900 | - |
| 17. | Tramadol 50mg/ml -2ml. | 30,755 | 31,255 | 29,333 | - |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | inj. | | | | |
| 18. | Tramadol 50mg capsule. | 3,655 | 3,875 | 2,623 | 3,300 |

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Kwa kawaida bidhaa zilizoko sokoni bei zake (market price) zinahusisha bidhaa yenyewe tu. Bei za mikataba ambazo zilitokana na zabuni zimejumuisha gharama za bidhaa yenyewe, bima, forodha na usafiri mpaka eneo husika (Bohari Kuu ya Dawa). Aidha, mikataba hii ya dawa ni ya muda wa miaka 3 (Framework contracts), hivyo mzabuni anakabiliana na gharama hizo kwa zaidi ya mara moja kulingana na oda zinazotolewa na Wizara hali ambayo Mzabuni anaingiza gharama zote hizo katika bei zake. Pia mchakato wa zabuni ulikuwa wa ushindani wazi (international competitive tendering) na bei za mikataba hiyo zilitokana na ushindani huo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeridhika na majibu ya hoja kwani Kamati imebaini kuwa mfumo wa ushindani wa zabuni unaongeza sana fedha ukilinganisha na ununuzi wa kawaida. Hata hivyo, bei zilizoinishwa zinaoenaka zimezidi maradufu.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Serikali kupitia Bohari Kuu ya Dawa zifanye utaratibu wa kuagiza dawa wenyewe kutoka viwanda vya dawa ili kuzuia upotevu wa fedha na watu wachache kunufaika kwa fedha za wengi.

## 1.5.10 HADIDU REJEA NAMBA 7

**Hoja nambari 1.5.10.1: Kuhakiki muda wa kuishi kwa dawa zinazonunuliwa "Duration of Expiry"**

Katika Hadidu Rejea hii mambo yamebainika mambo yafuatayo:-

Ukaguzi umebaini Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto inaendelea na ununuzi wa dawa na vifaa tiba kutoka kwa makampuni mbali mbali yanayouza dawa na vifaa tiba kwa ajili ya matumizi ya hospitali na vituo vya afya Unguja na Pemba.

Katika uhakiki uliofanyika imebainika dawa na vifaa tiba vyenye gharama ya shilingi 2,535,425,720.33 vimeishiwa na muda wa matumizi na kupelekea

kusababisha hasara kubwa kwa Serikali. Hasara hiyo imetokana na kukosekana kwa mfumo mzuri wa uwekaji wa taarifa za dawa zinazoingia, zinazotumika, zinazokaribia kuharibika na kupelekea kutokujua kwa aina ya dawa ambazo zimekaribia muda wake wa kumalizika ili ziweze kutolewa na kutumika haraka kabla ya kufikia muda wa kuharibika kwake.

Ukaguzi unashauri mfumo uliopo utumike ipasavyo ili kunusuru uwepo wa upotevu mkubwa wa fedha za umma pamoja na uandaaji wa sera, miongozo na taratibu nzuri za kuhakikisha kuziteketeza dawa na vifaa tiba vilivyoharibika ambavyo havitumiki na vimerundikana katika hospitali na vituo vya afya Unguja na Pemba jambo ambalo linatia hofu kuwepo kwake katika maeneo hayo ili kuweza kunusuru kuja kutumika kwa matumizi ya binadamu. Orodha ya dawa na vifaa tiba vilivyoishiwa muda kwa matumizi ya binaadamu ni kama inavyoonekana katika Kiambatisho Nambari 6.

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

Uongozi wa Bohari umeandaa miongozo mbalimbali ya kazi (SOP), moja katika miongozo hiyo ni "Muongozo wa Upokeaji wa dawa." Kwenye muongozo huo, kuna timu ya mapokezi inayojumuisha Afisa Mapokezi wa Bohari, Msambazaji wa Dawa, Afisa Manunuzi wa Wizara na mtumiaji kwa bidhaa maalumu. Timu hii huhakiki shehena ya dawa pale inapoletwa Bohari. Vile vile "custodian" huwa wanafanya hesabu za mkono za kila mwezi, wafanyakazi wote hushiriki katika zoezi la hesabu ya mkono wa kila mwaka na mfumo unatumia utaratibu wa kuelekeza kutoa dawa zinazomaliza muda wa matumizi mwanzo

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba changamoto ya kuwepo dawa katika Bohari kuu haliwezi kuepukika kwani kuna baadhi ya dawa huwa ni za msaada ambazo huingizwa kwa maradhi maalum na wingi maalum. Dawa kama vile za kifua kikuu, malaria, ukoma na ukimwi ni jamii ya dawa hizo. Aidha, kuna dawa zinanunuliwa na kuhifadhiwa ghalani lakini matumizi yake ni ya nadra sana lakini lazima zipatikane maana likitokea tatizo ndio umuhimu wake unajitokeza, kwa mfano dawa za kichocho na kichaa.

Mbali na sababu iliyoelezwa na Wizara lakini kubainika kutumika kwa shilingi 2,535,425,720.33 kwa kununulia dawa na vifaa tiba vilivyopitwa na muda ambazo nyengine ni dawa zilizoagizwa na Wizara wala sio dawa za misaada ni jambo la kuhuzunisha na linarudisha nyuma juhudi za Serikali za kujikwamua na wimbi la upungufu wa dawa na vifaa tiba katika haspitali zetu.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Bohari iandae utaratibu wa kufanya kinachoitwa 'stock taking' kila mwaka ili kuzihakiki dawa na vifaa tiba walivyokuwa navyo, vilivyopitwa na muda pamoja na kujua mahitaji yao.

### 1.5.11 Hadidu Rejea Namba 8:Kujua idadi ya wasambazaji wa dawa na vifaa tiba

**Hoja nambari 1.5.11.1: Kutokutumika kwa Mfumo wa Usambazaji wa Dawa na Vifaa Tiba**

Katika Hadidu Rejea hii ukaguzi umebaini kuwepo kwa idadi ya wasambazaji 24 wa Dawa na Vifaa Tiba ambao wamefanya biashara ya usambazaji wa dawa na vifaa tiba nje ya mfumo. Aidha imebainika uwepo wa msambazaji mmoja ambae amefanya biashara ya usambazaji dawa na vifaa tiba kwa kutumia mfumo wake ambapo ametoa ruhusa ya matumizi ya mfumo wake kwa kuagizia na kununua dawa na vifaa tiba vinavyohitajika na Bohari Kuu ya Dawa. Hivyo kupelekea ukaguzi kubaini jumla ya wasambazaji 25 waliotumika kufanya biashara ya usambazaji wa dawa na vifaa tiba kwa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa kipindi cha miaka mitatu. Mchanganuo wa Wasambazaji hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 11**: **Wasambazaji ambao hufanya manunuzi na Bohari Kuu ya Dawa bila ya kutumia Mfumo**

| Namba | Jina la Msambazaji Dawa/Vifaa Tiba | Huduma anayoitoa |
|---|---|---|
| **WASAMBAZAJI WALIOPO NCHINI (LOCAL SUPPLIERS)** | | |
| | Salama Pharmaceuticals | Dawa na Vifaa Tiba |
| 1. | KAT Med Group (T) LTD | Vitendanishi "Reagents" za Maabara na Huduma za za Damu Salama |
| 2. | KAS Medics | Vitendanishi "Reagents" za Maabara |
| 3. | Abbott Diagnosis | Vitendanishi "Reagents" za Mashine ya PCR (UVIKO -19) |
| 4. | Nebula Health Care LTD | Vifaa vya Mfupa na Vipimo vya UVIKO -19 |
| 5. | LAB Equip LTD | Vifaa Tiba |
| 6. | Bahari Pharmacy | Mikoba ya Vifaa vya Uzazi |
| 7. | Indepth Scientific | Vitendanishi "Reagents" za Maabara |
| 8. | Anudha LTD | Vitendanishi "Reagents" za Maabara |
| 9. | M&D Chemicals | Consumables za Maabara |

| | | |
|---|---|---|
| 10. | IDA Foundation – Nertherland | Dawa Muhimu |
| 11. | DAWA Arus | Dawa na vifaa tiba |
| 12. | Life Care | Dawa na vifaa tiba |
| **WASHIRIKA WA MAENDELEO (DONORS)** | | |
| 13. | UNICEF | Virutubisho vya Watoto na Vifaa vya Kipindupindu |
| 14. | Global Fund | Dawa za Mradi wa UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria |
| 15. | WHO | Vifaa vya UVIKO – 19 |
| 16. | UNFPA | Dawa na Vifaa vya Uzazi |
| 17. | GLOBAL LIFE SHARING – SOUL, KOREA | Dawa na Vifaa Tiba |
| 18. | CHINA GOVERNMENT | Dawa za Kichina |
| 19. | USAID | Vifaa vya UVIKO – 19 |
| 20. | HILL LIFECARE – INDIA | Dawa Muhimu |
| 21. | UNDP | Vifaa Tiba |
| 22. | ENGEDER HEALTH | Vifaa Tiba |
| 23. | SD BIOSENSOR - KOREA | Test kit za Kupima UVIKO – 19 |

**Majibu ya Uongozi wa Wizara**

MSD, huwa anatumia mfumo wake wa maombi ya dawa (eLMIS) kwa wateja wake wote, ikiwemo Bohari. Hata hivyo, manunuzi yote ya dawa kwa sasa yanafanywa na kitengo cha manunuzi cha Wizara kupitia mfumo wa kidijitali(e-procurement). Halikadhalika, Bohari inao mfumo wake ambao una uwezo wa kufanya manunuzi ambao unaweza kutumika baada ya Bohari kuwa na Sheria yake.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini hatari kubwa iliyopo kwa afya za wananchi kupatiwa dawa zilizopitwa na muda pamoja na kuwepo kwa ubadhirifu wa fedha za Serikali kwa vile Makampuni ya usambazaji dawa hufanya usambazaji wa dawa pasi na kutumia Mfumo.

**Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Vyombo vya uchunguzi vifuatilie kadhia hii kwa kuzichunguza Kampuni zote 24 zilizokuwa zikitumika kusambaza dawa na vifaa tiba pasi na kutumia mfumo.

2. Vyombo vya uchunguzi pia viwachunguze na kuwafikisha katika vyombo vya kisheria watendaji wote waliohusika na ukiukwaji wa sheria ziliopo za kuruhusu Makampuni ya usambazaji dawa na vifaa tiba kusambaza bidhaa hizo pasi na kutumia mifimo uliopo.

## HITIMISHO

Kamati ya PAC kama zilivyo Kamati nyengine zinazosimamia masuala ya kifedha, hufanya kazi zake za ukaguzi kwa kupitia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuchunguza hoja mbali mbali zilizojitokeza katika Ripoti hizo pamoja na kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa mambo yote yanayohusu Hesabu za Mawizara kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Toleo la 2020.

Katika kutekeleza hayo, Kamati ya PAC ilieleza mambo ambayo imeyabaini kupitia majibu ya Watendaji na kutoa Mapendekezo kwa Wahusika kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Taasisi za Umma. Kwa mnasaba huo, Kamati hii inaliomba Baraza la Wawakilishi, kuipitia, kuijadili na hatimaye kuiridhia Ripoti hii kwa lengo la kufanyiwa kazi na Serikali.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati ya PAC inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Mawizara na Taasisi zake kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati hii wakati inatekeleza majukumu yake ya kikatiba. Shukurani pia ziwafikie Watendaji wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mashirikiano yao kwa Kamati hii.

Kwa umuhimu wa pekee, tunatoa shukurani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza pamoja na Watendaji wote wa Afisi ya Baraza hilo kwa mashirikiano yao ya dhati waliyoyaonesha katika muda wote ambao Kamati hii ilipokuwa ikiwajibika.

****Mwisho****